Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 11 Agosti, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Musa Z. Azzan) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji na Hesabu Zilizokaguliwa za Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2011*(The Annual Report and Audited Accounts of The National Environment Management Council (NEMC) for the Year ended 30th June, 2011).*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Randama za makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa 2012/2013
### Wizara ya Maliasili na Utalii

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala huu wa Maliasili na Utalii na sasa mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kwanza ninaomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri ambayo mmewasilisha na ambayo inatoa matumaini kwa wana Mazingira.

Ninaomba niende moja kwa moja kwenye Hoja ya Hifadhi ya Misitu. Kila mtu anafahamu umuhimu wa misitu. Misitu ndiyo vyanzo vya maji na ukizingatia kule kwetu Urambo ambako tuna karibia 80% ya Hifadhi ya Misitu ya Mkoa wa Tabora ni kama Hifadhi ya maji ya

Mkoa wa Tabora. Ni hifadhi ya maji yanayokwenda katika mto Malagarasi na katika ziwa Tanganyika ambayo ni 30%. Lakini pia misitu hii ndiyo inatengeneza hewa tunayovuta, misitu hii hutupa chakula, misitu hii ni vitega uchumi kwetu kwa sababu tunaitumia kuweka mizinga yetu ili tuweze kupata fedha, misitu hii vilevile ni kivutio kikubwa cha Watalii kwa hiyo, misitu ni kitu muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linakuja kwenye *Management* ya hifadhi za misitu na matatizo yenyewe tunaweza kuyagawa katika sehemu mbili. Tatizo la kisiasa na tatizo la uongozi. Hifadhi zimekuwepo toka wakati wa Mkoloni na wala zilikuwa hazina matatizo wakati tunapata Uhuru Watanganyika tulikuwa milioni sita na baadaye tukafika milioni tisa na sasa hivi tuna karibia milioni 45 kama itakavyokuja kuthibitishwa baadaye na sensa, kutokana na kuongezeka kwa watu kumekuwa na utaratibu unaoeleweka na Serikali watu wanapeleka maombi kupitia taratibu zinazoeleweka na maeneo yamekuwa yakiongezwa kupitia taratibu hizi.

Pia taratibu zinazoeleweka ndiyo vinazaliwa vijiji kama Luyembe, Sungimlole, Kangeme, Kumbisiganga, Lumbe, Kakoko, Msinga na Ndiga katika Tarafa ya Kumbisiganga hivi ni vijiji ambavyo vimezaliwa kiutaratibu kabisa, lakini tatizo lilikuja kuzuka pale ambapo baadhi ya Wanasiasa tulianza kuona mapori haya kama vile tunaweza kuyatumia kama mtaji wa kisiasa hapo ndiyo tatizo kubwa lilikuja kuzuka.

Kwamba kumbe kuna mapori yamekaa mtu anaweza kushawishi watu wakahamia pale wakajaa ili hatimaye baadae aje awatumie katika kumpigia kura na hili liko katika ngazi mbalimbali kazi za vitongoji, ngazi za vijiji na hata ngazi za Ubunge hili ndiyo limeleta sokomoko kubwa.

Vijiji hivi ambavyo nimezungumza vilikuwa vinatambua kabisa kuwa jirani yetu ni msitu, jirani zetu ni wanyama pori hivyo waliishi kwa tahadhari hiyo lakini leo vurugu zimejaa katika misitu ya Urambo kwa sababu wavamizi wamejaa kwa kushawishiwa kisingizio kikubwa kinachotumika hapa wakishajazana katika misitu ile kwamba sisi hatujui mipaka, siyo kweli kabisa kuwa mipaka haijulikani kwa sababu ingekuwa mipaka haijulikani huko wanakokaa ingekuwa tumechanganyika na sisi wakazi wa zamani, wakazi asilia lakini ukienda katika maeneo hayo utakuta wamejaa wageni tena kuanzia mwaka 2000 mpaka 2010 hapa katikakati hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wageni wa aina moja kazi yao ni moja ya ufugaji kabila lao ni moja na Chama chao ni kimoja kwamba wewe ukihamia huku na kuingia katika Chama hiki mimi nitakuwa mlinzi wako kuhakikisha kuwa unakaa hapa bila kubughudhiwa.

Hii imeleta kasheshe kweli mtu anaposimama na kusema mipaka ni tatizo siyo kweli kwa mfano; pale Igagala tumeanzisha WMA inaitwa ISAWIMA kwenye jiwe la ISAWIMA lenyewe kuna mtu kaenda kujenga mji hivi ni kweli hajui mpaka kwa sababu jiwe liko pale

linaonyesha kuwa hapa ndiyo mwanzo wa WMA lakini yeye kajenga pale hifadhi kwa hiyo, hili ukilinganisha na udhaifu wa uongozi na hapa ninazungumzia uongozi wa Serikali Kuu tunalo tatizo kubwa. *(Makofi)*

Hifadhi hizi zilikuwepo toka wakati wa Mkoloni, Mkoloni alikuwa na utaratibu wa kuhakikisha kuwa kila baada ya miezi fulani anapita kukagua hivi sasa Hifadhi hizi hakuna anaye kagua watu wanakaa miaka 10, 12 mpaka 15 baadaye inakuja kuwa ni kero kubwa.

Sasa hivi kwa kuwa tatizo limekuwa kubwa ndiyo Serikali imeanza kuzinduka ilikuwa imeachiwa Halmashauri, Halmashauri haiwezi, fedha ni kidogo na utalaam ni kidogo nguvu za maaskari ni kidogo matokeo yake ni kuwa misitu inakwisha na misitu inapokwisha athari zake hujitokeza moja kwa moja katika Wilaya yetu ya Urambo na katika Mkoa wetu wa Tabora mvua kwa sasa zimepungua karibia 50%, kulikuwa na mvua za milimita 1500, mpaka 1600 hivi sasa tunaishia milimita 800 tu, maji ya kunywa yamekuwa haba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika Urambo mwaka 1995 mpaka 2000 kuna eneo linaitwa Maboha na kuna eneo linaitwa Shela pale kulikuwa na Ziwa kubwa na watu walikuwa wakipita eneo lile kwa mitumbwi ndiyo maana 1997 tulipata ajali ya watu kupinduka na mtumbwi na watu karibia 30 walipoteza maisha. Ilikuwa ni kwaya inatoka sehemu moja ya eneo kwenda kuwatembelea waumini wenzao leo hii ukienda na kwa kuwa ardhi yetu ni tambarare unaweza kucheza mpira tu hakuna chochote ni vumbi tupu.

Ninaishukuru sana Kamati ya Maliasili na Mazingira walipata nafasi kwenda kuangalia na wakathibitisha mambo mawili la kwanza, kwamba kumbe ni kweli katika vijiji hivi kuna eneo ambalo ni halali na eneo ambalo ni haramu. Kwa hiyo, hata *operation* ya kuchoma nyumba ilipokuja waliochomewa walikuwa ni wale ambao wako katika Shela haramu, Shela halali wananchi hawakuguswa kabisa.

Lakini vilevile wakathibitisha kuwa zile *propaganda* za watu waliouawa karibia ishirini siyo kweli walitoa taarifa waliambiwa onyesheni makaburi lakini kaburi hata moja halikuonekana hili ni tatizo. Kwa sababu ya udhaifu huu Halmashauri ambayo inajitahidi inabidi itumie rasilimali zake tunaishiwa. Lakini pia kwa sababu watu hawa wameshajizatiti kule porini wanatuua sana na kututukana sana tarehe 4 Februari, 2011 kulikuwa na watu na ninaomba kwa idhini yako nisome ambao walikwenda kutoa taarifa kuwa eneo hili la *North Lugala* siyo halali ni msitu wa Hifadhi tunaomba muhame na *operation* inakuja badala ya kuwasilikiliza walichokifanya watu wale walioenda kutoa taarifa walipigwa na kuuawa kikatili na wafuatao waliuawa Ndugu Yasini Nyembe - *VEO,* Ndugu Makenzi Magida - Mwenyekiti wa Kitongoji, Ndugu Emmanuel Gabriel - Mgambo na Ndugu Ayo Ramadhani - Mgambo. Walionusurika kwa baraka za Mwenyezi Mungu walikuwa ni Ndugu Miraji Selemani, Ndugu Yasin Kapaya, Ndugu Ramadhani Amani, Ndugu Bahati Mlangila na Ndugu Nuhu Philipo. Hawa wote walikuwa wamekwenda kutoa elimu na kuwaasa wale watu watoke katika misitu ya Hifadhi, wakauawa kikatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotuuma tumejitahidi sana sisi na Halmashauri, tumejitahidi sana na *DC* wetu kuieleza Serikali angalau wapate kifuta machozi familia za watu hawa mpaka leo hakuna hata senti tano, inauma na inasikitisha.

Ninamwomba Mheshimkiwa Waziri wakati atakapokuwa anafanya majumuisho anielezee kuwa anakwenda kuzieleza nini familia hizi za watu hawa waliouawa na watu waliofanya mauaji mpaka leo hawajakamatwa. Ukiuliza Serikali unaambiwa utaratibu unafanyika inauma sana sisi ambao tumejitolea kulinda misitu hii na kulinda wanyama hawa hatutendewi haki ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri hili unisaidie.

Ushauri wangu ni kuwa Serikali hii Kuu iandae *operation* kabambe na katika *operation* hii wakawaondoe wavamizi walio katika misitu hii. Wakawaondoe wavamizi walio katika njia ya kupitia wanyama kutoka Ugala kuja Moyovozi ili uoto ule wa asili urudi katika hali yake ya asili. Ikisha fanya hivyo isiwe kama zimamoto waendelee kuwa wanasimamia kama ni suala la mipaka wachonge barabara kama ilivyokuwa zamani mimi nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri azingatie haya,lingine ni kuwa tunayo kampuni ya uwindaji inaitwa *Robin Heart Safaris.* Kampuni hii kule kwetu ukizungumzia misaada kwa wananchi kampuni hii haifanyi chochote kusaidia wananchi tunajiuliza hivi sisi faida yetu ni nini ukisikia wanayoyafanya kule Arusha wanafanya makubwa sana. Lakini huku ukiwaeleza shida wanakwambia

mwaka 1995 tulitoa mabati na kukarabati madarasa mawili hivi toka mwaka 1995 mpaka leo 2012 hayo madarasa mawili ndiyo mwisho?

Mheshimiwa Mkwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri kuwa mkataba wao utakapokwisha watu hawa usiwarudishe kwetu tena waelekee huko huko Arusha tutafutie wawekezaji wengine waje tukae nao. *(Makofi/ Vicheko)*

Ndiyo, maana na sisi tunahitaji misaada kama wanavyohitaji wengine hizi *Corporate Social Responsibilities* lazima ziwepo katika maeneo yote na nilipokuwa nikizungumza suala la vijiji, vijiji kama hivi viko katika Kata ya Seleli, Kata ya Sasu na Kata ya Kashihi.

Hawa nao vilevile kuna vijiji ambavyo vilikuwa vimezingatiwa kwa taratibu za Serikali navyo vilevile mnapoanza *operation* kubwa hii isiwe mtego wa panya kuingia asiyekuwemo na aliyemo wako watu ambao wamekaa pale kihalali kufuatana na taratibu za kiserikali. Wako watu ambao ni wavamizi na sisi tunawajua na mipaka inajulikana tusaidiane, tushirikiane tumalize tatizo hili. Ahsante sana ninaunga mkono hoja.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii. Lingine nimpongeze au niipongeze safu mpya ya Wizara hii na kwa mwelekeo wanaonekana wanaweza, ninawapongeza sana.

Kwanza ningetanguliza kuomba kama kuna tathimini yoyote ya misitu iliyofanywa ni vyema tukajulishwa kwa kuwa hali ya uharibifu wa ukataji wa misitu umekithiri umekuwa ni mkubwa mno kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu. Kwa hiyo, kama kuna tathimini yoyote ambayo Wizara imefanya na imekamilika ni vyema Bunge hili likajulishwa ili tujue kinachoendelea katika mazingira yetu.

Lingine ilikuwa nizungumzie kuhusu migongano ya Kisera. Nimepata wasiwasi mkubwa na Sera ya Kilimo Kwanza.

Sera ya Kilimo Kwanza kwa kiasi kikubwa inapingana na uhifadhi. Tatizo ni kwamba Sera hii imeletwa yaani imeibuliwa lakini taaluma kwa jamii na wananchi ni ndogo sana. Kwa maana hiyo watu walihamasishwa kulima wanasaidiwa nyenzo za kulima lakini jinsi ya kulima ili kwenda sambamba na mazingira au uhifadhi hilo limekosekana kwa maana hiyo uharibifu ni mkubwa wa mazingira. Ukataji wa misitu umekuwa ni mkubwa sana na hasa upande wa Kusini, ufyekaji wa mapori kwa ajili ya kilimo cha ufuta umekuwa ni mkubwa sana na tatizo ni kuwa ni ukulima wa kuhamahama watu wanakata miti wakijua mwaka wa kwanza na wa pili watavuna vizuri, mwaka wa tatu na wa nne kunakuwa hakuna mazao mazuri wanaacha wanakwenda mbele hivyo maeneo yanabakia matupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukulima wa namna hii au Sera ya Kilimo Kwanza cha namna hii kinaweza kutuletea athari kubwa ikawa ni jangwa baadaye.

Lakini pia Kilimo Kwanza, kinakaribisha *investors* wengi wanakuja na kulima. Mfano Lindi kuna *investors* walikwenda wakafyeka pori kwa ajili ya kupanda mibono karibia hekta 30 mibono haikupandwa na baada ya kufyeka walihamisha magogo na Mbao wakafanya biashara lakini hakuna mbono ambao ulipandwa na eneo limeachwa tupu, hili ni tatizo na baadaye tunaweza kuja kulia kilio cha Mbwa mgeni kwa sababu tumeleta Sera ambayo imepokelewa vibaya. Mimi ninafikiri kuna haja kubwa kuwa Wizara ya Maliasili ikae pamoja na Wizara ya Kilimo iweze kuangalia ni jinsi gani tunaweza kutekeleza Sera ya Kilimo Kwanza na wakati huohuo tukatunza mazingira yetu.

Ninashauri pia Wizara hizo mbili zikae pamoja ili ziweze kufanya kazi kwa sababu tunaweza kuelimisha watu wetu wakaweza ku-*practice* kilimo cha *Conversation Agricuture* ingekuwa ni vizuri zaidi kwa kuwa tutatumia eneo dogo, kwa kutumia kilimo cha kisasa, teknolojia ya kisasa kwa maana hiyo tunalima padogo, tunavuna sana na tunapunguza uharibifu au ukataji wa misitu hovyo. Ninashauri Wizara hizi mbili zikae pamoja ili tuweze kuepukana na janga ambalo linaweza likatupata hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ilikuwa nizungumzie kwa kifupi kuhusu hii *participatory forest Management*. Ushirikishwaji wa wananchi au jamii kwenye ulinzi wa misitu lilikuwa ni jambo zuri sana na ni jambo ambalo lilipata ufadhili na kwa kiasi fulani lilionekana kufanya vizuri lakini tatizo lilifanywa katika *pilot areas* tu na wananchi walilikubali na kulipokea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hatujui kulitokea nini, lakini utendaji wa *PFM* kwa kweli sasa hivi ni mbovu, wananchi wameshavunjika moyo, jamii imeshakata tamaa na kwa kweli hawataki tena kusikia habari ya ushirikishwaji wa ulinzi wa misitu kwa sababu mikataba inaonekana haitoki Wizarani.

Sasa sijui kuna tatizo gani, kwamba mikataba imeshindwa kusainiwa na jamii wakapata kushiriki katika ulinzi huo, kwa sababu inawezekana pengine watendaji wa Wizara wanafaidika zaidi ikiwa hakuna ushirikishwaji, lakini wakiwashirikisha jamii inaonekana kwamba itakuwa ni kigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iliangalie vizuri suala hili, ili kama kuna mikataba ambayo tayari wameshazungumza na jamii isainiwe na jamii iweze kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni mgao wa *Tanzania Forestry Services* kwa jamii ambayo ina *manage* yale maeneo ya misitu. Jambo hili nalo pia utendaji wake hauridhishi na inasemekana

kwamba Wizara ya Fedha ndiyo ambao wamezuia huu mgao.

Naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze tatizo ni nini. Je ni kwa nini mgao huu haufanyiki kawaida. Tujue tu kwamba duniani kote hakuna jamii ambayo iko tayari kushiriki katika kuhifadhi kama haifaidiki, hilo halipo. Kwa hivyo kama jamii hawafaidiki na kama Serikali imezuia kuwapa mgao wao, kwa hivyo uhifadhi au ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi huo hauna faida kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hayo, nakushukuru sana.(*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. Mimi niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pongezi za dhati kwa Waziri na Naibu wake na timu nzima ya Wizara hii kwa kuonesha mwelekeo mzuri toka waanze kuingia katika Wizara hiyo, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu waendelee vizuri kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sheria ya hifadhi ya wanyamapori ya mwaka 2009 nikinukuu vifungu mbalimbali. Kwa mfano kifungu Na. 15 (1) nikiisoma kwa tafsiri ya Kiswahili ambayo siyo rasmi inasema kwamba mtu yeyote ukiondoa wale wanaosafiri kwenye barabara kuu inayokatisha kwenye hifadhi hataruhusiwa kukatiza kwenye hifadhi labda awe na kibali cha maandishi kutoka kwa Afisa anayetambuliwa na uongozi wa hifadhi. Lakini kipengele cha pili vile vile kinasema kwamba mtu

yeyote atakayehalifu kifungu cha hapo juu, atakuwa amevunja sheria na atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja, lakini isiyozidi laki tano au kifungu kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sheria hiyo katika kifungu Na. 17 (1) kinasema kwamba mtu hataruhusiwa kuingia kwenye hifadhi na bunduki, upinde, mishale au silaha yeyote na atakayekwenda kinyume na kifungu hicho, basi atakuwa amehalifu na atawajibika kulipa faini isiyozidi laki mbili, au jela miaka isiyozidi mitatu au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelazimika kuvisoma vifungu hivi kwa sababu ya mazingira yaliyojitokeza katika Jimbo langu la Tunduru Kusini. Jimbo hili miaka ya nyuma Serikali ilichukua maeneo ya vijiji vya ujamaa na ikafanya maeneo ya uwindaji ambao kwa kweli sasa hivi unaleta kero sana kwa wananchi wa Tunduru. Sisi watu wa Tunduru tuna jamaa zetu wengi sana Msumbiji, tunalazimika kwenda kusalimiana na Ndugu zetu, lakini vile vile chanzo pekee cha kitoweo Tunduru ni mto Ruvuma.

Ili uweze kwenda Tunduru na uweze kwenda Msumbiji ni lazima ukatishe msitu ule wa Mwambesi ambao kwanza ni mali ya vijiji vya ujamaa, na kwa mujibu wa sheria ya hifadhi ya wanyamapori tuliyoipitisha mwaka 2009 tulieleza kwamba maeneo yote ambayo yamechukuliwa na Serikali yatarudishwa kweney vijiji vya ujamaa ili wapange matumizi wavyoyataka wao wenyewe. Hadi leo tunazungumzia

mwaka 2012 sheria hii bado haijatekelezwa ya kurudisha maeneo yale ili wananchi wapange matumizi yao wenyewe wanavyoamua.

Aidha kuendelea kufuga wanyama au kubadilisha matumizi kwa namna nyingine yeyote. Naiomba sana Serikali irudishe ardhi hii kwa wananchi wenyewe waamue nini cha kufanya juu ya ardhi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika sasa hivi, nashangaa wenzangu wengi wamezungumzia kwamba wana faida, wanapata manufaa kutokana na hifadhi, lakini sisi kule faida tunayoipata ni kupigwa makofi na askari walinzi wa makampuni ya wawindaji. Laiti makofi yale tungekuwa tunapigwa na askari wa Serikali ingekuwa rahisi kwangu kwenda kuwadhibiti, wananchi wanapigwa na askari wa makampuni ya wawindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tunduru ni wavumilivu, wasikivu, lakini adha hii wanayoipata itafikia siku uvumilivu huu utavunjika kwa wananchi wale. Uvunjifu ukiisha na amani inaweza ikatoweka. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kupitia Waziri na Naibu wake wajaribu kufuatilia jambo hili, ardhi ya Msitu wa Mwambesi irudishwe kwa vijiji vya Kata mbalimbali ambazo zinahusika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataja hapa Kata mbalimbali na vijiji vyake ambavyo ardhi yake ilichukuliwa, Kata ya Mtina maeneo ambayo vijiji vilimegwa ili kuandaa msitu huu wa Mwambesi ni Kijiji cha Ngalia, Namatuli, Mtina, pamoja na Kijiji cha

Semeni. Kata ya Tuwemacho ni Kijiji cha Nasia, Kata ya Mchesi ni Vijiji vya Mwenge, Vyundeni na Mchesi.

Kata ya Lukumbule ni Vijiji vya Lukumbule, Kazamoyo, Imani, Mitana, Makande na kitongoji cha Mkandanguo. Kata ya Masakata ni kijiji cha Amani, Masakata, pamoja na Mjendamoto. Kata ya Misechela ni Meya Mtwaro, Chiungo na kitongaji kimoja kinaitwa Nkarachani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalazimika kusema haya kwa sababu kila ninapowatembelea wananchi hawa kilio chao ni hicho, kwamba sheria imeshapitishwa ardhi yetu tunaomba turudishiwe na sisi wenyewe tupange matumizi ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya yote yanatokea kutokana na matokeo ya hapo nyuma, kumekuwa na mshambulizi makubwa sana ya tembo ambao wamekuwa wakishambulia wananchi, askari wa wanayamapori na hadi leo hii kipindi naingia Bungeni mwaka 2007 mwezi ule ule baada ya kuapishwa nimerudi nyumbani nimekutana na tukio la kuuwawa kwa askari wanyamapori anaitwa Sadick. Familia ya Sadick haijapewa fidia mpaka leo. Fidia ya shilingi laki mbili tu maana yake ni kifuta machozi cha kipindi hicho laki mbili mpaka leo hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Ngalia kuna tembo walivamia wakavunja maghala wakala vyakula kiangazi lakini hadi leo wananchi wale hawajalipwa fidia. Mwaka huu vijiji vya Misechela tembo waliingia,

wakala mpunga katika mashamba ya wananchi lakini hadi leo fidia haijalipwa.

Kwa hiyo kuna tabia ya wananchi kujenga chuki na hawa wanyama. Hili ni jambo baya lisije likatokea, ni bora misitu hii warudishiwe wananchi. Tunayo maeneo mengi sana ya kuweza kufuga wanyama *Seleou i*meingia Tunduru na mwananchi yeyote hajawahi kugusa lakini wanalazimika kufuatilia ardhi hii kwa sababu ni mali ya vijiji vya ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tutafanya sensa. Sensa hii dhamira yake ni kujua idadi ya watu, lakini watu wamekuwa wakiongezeka toka Uhuru.

Tunaambiwa kwamba baada ya uhuru Watanzania walikuwa takribani milioni 6 na 9. Leo tunategemea watu wawe zaidi ya milioni 50. Lakini watu hawa jinsi wanavyoongezeka haijawahi kutokea hata siku moja tukasema wananchi wavunwe kwa sababu wameongezeka. Lakini wanyama wanapoongezeka ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wanayama hao wanavunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni matarajio yangu kwamba maeneo ya vijiji vya ujamaa hayatapunguzwa kwa sababu idadi ya watu wanaongezeka. Lakini sitarajii kwamba maeneo ya kuhifadhi wanyama yapanuliwe kwa sababu wanyama wakiongezeka wanavunwa. Kuna haja gani ya kuongeza maeneo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali tabia ya kuchukua maeneo ya wananchi kuongeza kwa ajili ya kufuga wanyama naomba tabia hii iishe kwa sababu watu wanaongezeka na hawavunwi, lakini wanyama wanapoongezeka na wanavunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa asubuhi ya leo na mimi kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Waziri, Balozi Kagasheki, Naibu Waziri, katibu Mkuu Mama Tarishi na Naibu Katibu Mkuu Mama Nuru Milao kwa kazi nzuri wanayoifanya, naomba Mwenyezi Mungu aendele kuwapa nguvu waendelee kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kupitia mchango wangu wa hotuba ya Wizara hii mwaka jana nilichangia na kuiomba Serikali baada ya kutokea tatizo katika maeneo ya *Delta* Wilaya ya Rufiji ya wananchi kuhamishwa katika maeneo yao, ambayo kimsingi walikuwa hawana ardhi kabisa, lakini Serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Wizara hii, walitembelea maeneo yale wakawashauri wakulima wa maeneo hayo ya *Delta* ili waweze kulima Mpunga pamoja na ilimo cha mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kusema hali sasa hivi *Delta* ni shwari na nawaomba wakazi wa Mfisini, Nchinga, Kiomboni, Salale, Kiongoroni, Mbuchi, Mbwara waendelee kutimiza mmwlekeo waliyopewa na Serikali hii, na kwa kweli Serikali ni sikivu iliwasaidia, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika mchango wangu wa mwaka jana nilizungumzia migogoro ya mipaka baina ya vijiji vinavyozunguka hifadhi, katika Mkoa wetu wa Pwani. Tunayo hifadhi ya Saadani, *Seleou* na tunayo hifadhi ya Wami Mbiki. Tukianzia Saadani kuna mgogoro mkubwa kati ya vijiji vya Mkange, Matipwili, Saadani yenyewe na kuna kitongoji cha Uvinje kimeambiwa kitoke ndani ya maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali ilileta Wahifadhi pale, wananchi wa Mkange walikaa vikao kupitia Serikali zao za vijiji nilivyovitaja, kupitia Halmashauri Kuu ya Serikali na kupitia mikutano ya vijiji, tulikubaliana mipaka na kutoa mapendekezo katika mikutano hiyo.

Naomba Wizara izingatie makubaliano haya ambayo tuliyafanya tangu mwaka 2011 kupitia aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo tukatoa mapendekezo lakini mpaka sasa hivi hayajafanyiwa kazi. Naiomba Wizara ijitahidi kuyafanyiakazi kwa sababu mgogoro ni mkubwa.

Wananchi wa kitongoji cha Uvunje wameambiwa wahame na wao kwa kweli wanaona kama hawajatendewa haki. Lakini pia sambamba na hilo kuna mgogoro kijiji cha Mloka, Nyaminywili na mbuga ya *Selou.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wananchi wa maeneo yale rasilimali pekee waliyopewa na Mwenyezi Mungu ni hiyo hifadhi lakini pia ni kweli kwamba wananchi wa maeneo yale kama alivyochangia Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Pwani Kurthumu Mchuchuli, hamna namna ambavyo wanaweza wakaboresha au wakapata kipato na wakasaidia kujikwamua kiuchumi ni shughuli ambazo wanaweza kufanya katika mazingira yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa hifadhi hizi lakini naomba Wizara kama alivyoomba Mbunge mwenzangu watembelee katika maeneo yale ili wananchi wa maeneo yale hususani wa Nyaminywili wapate fursa ya kufanya shughuli ambazo walikuwa wanafanya kwenye mabwawa yao ya asili. Mabwawa yale yalianza kabla hata ya *Seleou* haijawa hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya kutokana na migogoro hii baina ya wananchi na askari wa kampuni za uwindaji mara kwa mara inatokea mauaji.

Katika eneo la Wami Mbiki Kata ya Ubena vijana wawili mmoja amepoteza maisha na mmoja yupo Ndugu Miraji yupo hoi kitandani lakini mwenzake amepoteza maisha. Lakini pia huko Mloka miezi mitatu

iliyopita vijana wawili wa familia moja walipoteza maisha. Hii imeleta mgogoro mkubwa sana na wanakijiji wamewapiga marufuku wale askari wa kampuni za uwindaji wasikanyage kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri baada ya Bunge hili kwa kuwa Mkoa wa Pwani ni karibu, basi atembelee aone athari na asikilize maoni ya wananchi imekuwa ni tatizo kubwa. Lakini pia hata mwaka jana Wilaya ya Kisarawe maeneo ya Vikumbui tulipoteza vijana wawili na Mbunge wa Kisarawe alilieleza hapa, mmojawao alikuwa hoi hospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema hapa ni kuiomba Wizara kwa kweli kama kuna vipaumbele walivyonavyo, basi kipaumbele cha kushughulikia migogoro baina ya vijiji vinavyozunguka hifadhi iwe kipaumbele namba moja kwa sababu wanaopata madhara wengine ni wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo kuna miradi ya ujirani mwema katika maeneo ambayo nimeyataja. Kwa mfano maeneo ya hifadhi ya Saadani zipo kampuni zinatusaidia kwa mfano Saadani *Safari Lodge, Century T. Limited*, ukilinganisha na namna ambavyo shirika la Hifadhi la *TANAPA* linavyotusaidia. Kwa kweli ni kiasi kidogo sana, naiomba *TANAPA* itusaidie katika maeneo haya kuchangia huduma za jamii.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, lakini pia zile kampuni za uwindaji *Selou* Rufiji hawajachangia chochote, nakuomba Waziri na wao kwa kuwa sasa wanatuzuia

kuvua vitoweo, basi watusaidie kuchangia huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichangie suala la misitu. Misitu katika Mkoa wa Pwani inaisha sana, na mikoa ya jirani yetu kwa mfano Tanga hali ni mbaya. Hapa nimpongeze Mkurugenzi wa Misitu Dkt. Kilahama, nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mkuu wa Wilaya ya Handeni kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia misitu.

Imekuwa ni mchakamchaka wanaingia kwenye maeneo hayo pamoja na *DC* wa Kilindi pia kukagua na wanafanya doria wao, na hata mimi mwenyewe nimekamata mbao mia mbili katika kijiji cha Mtiti Muheza. Nawaomba sana wananchi wa maeneo ya Pwani na Tanga, tunalo tatizo kubwa la misitu kuvunwa.

Tumeshaanza kuona athari za tabianchi, hakuna mvua inayonyesha katika maeneo haya kama ilivyokuwa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ituongezee nguvu ya doria, ukiongea na ofisi za misitu za Wilaya zetu wanasema hawana wafanyakazi wa kutosha. Kwa hiyo, inamlazimu *DC* na kamati yake ya ulinzi na usalama kuanza kulinda na kukimbizana na wakataji misitu na kufanya doria za usiku ili aweze kuwakamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri atuunge mkono katika kampeni hii ambayo pia Mkoa

wa Tanga tunatekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa kupiga marufuku vibali vipya. Lakini tunakuomba utuunge mkono kwa kutuongezea nguvukazi na uwezeshaji kwa sababu doria hizi ni gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia limejitokeza suala la uchimbaji wa madini ndani ya Hifadhi zetu, kuna hifadhi ya amani, msitu ni mkubwa, gharama kubwa zimetumika, wananchi walihamishwa kupisha msitu wa Derema lakini wamejitokeza watu wanachimba madini, naomba Waziri uje uangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mgalu kwa mchango wako, sasa namwita Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Lucy Owenya ajiandaye na Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye mada kwa sababu muda ni mfupi ni kwamba namwomba Waziri katika Jimbo la Mufindi Kusini kuna matatizo makubwa sana ya mipaka kati ya Maliasili na wanakijiji. Kwa mfano kijiji cha Ihomasa, Kitasengwa, Iyegea, Mkalala, Kihanga na Nyololo, sehemu kubwa ilichukuliwa na Maliasili na wananchi

kule wanakosa hata sehemu ya kulima ili kuweza kupata mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri aliyepita Mheshimiwa Maige ambaye alifika kule na kuongea na wanakijiji, alifanya mkutano katika Kijiji cha Ihomasa na alifanya mkutano kule Kibengu aliona moja kwa moja jinsi wananchi wanavyopata shida kule, wameshindwa kupata maeneo ya kulima.

Waziri Maige alifika kule akaongea na wanakijiji alifanya mkutano pale Ihomasa na alifanya mkutano pale Kibengu aliona moja kwa moja wananchi kule jinsi wanavyopata shida, wameshindwa kupata maeneo ya kulima. Mwaka 1974 ulifanyika uhamisho. Sasa kuna maeneo makubwa yalichukuliwa na maliasili, yale maeneo yamebaki. Sasa wananchi walikuwa wanatumia kwa kilimo. Kwa hiyo, sasa hivi wanashindwa kulima pale na maliasili waliweka mipaka ambayo haiendelezwi.Kwa hiyo, nakuomba Waziri pale alipoachia Waziri Maige na wewe uweze kuendeleza pale kwa sababu walishakubaliana na wananchi kwamba mwaka huu wataweza kuendelea na kilimo chao kama kawaida. Wanakijiji wa Ihomasa na wanakijiji wa Kilolo mpaka Udumuka wanapata shida sana. Hatuwezi kukaribisha njaa wakati maeneo yao ya kulima yapo sisi tumeweka tu tumesema ni hifadhi. Bahati nzuri sisi kule hatuna wanyama kwanza. Kwa hiyo, tunaomba kule sisi tuendelee na kilimo kama kawaida Mheshimiwa Waziri kama hatutaruhusu kulima mwaka huu inaweza ikatokea matatizo kwa sababu hatuwezi kufa na njaa wakati maeneo yetu tunayo. (*Makofi*)

Suala jingine ambalo la msingi naliona katika Wilaya ya Mufindi, sisi tuna masuala ya misitu, ukizungumzia misitu katika Tanzania, misitu mikubwa iko Mufindi. Sasa ukiangalia uwiano wa uvunaji wa misitu mimi bado sijaufurahia vizuri. Kwanza kabisa nianze na *system,* nakumbuka mwaka mmeanzisha ujazaji wa fomu ambayo ile fomu iko *very complicated* kwa mtu wa kawaida akiiona anaweza akaona ni ngumu sana.

Lakini *anyway* ni *system* tunaweza tukasema kwa *supervision* ni *system* nzuri. Lakini kwa wale wavunaji wa kawaida sisi katika msitu ule kuna wavunaji wa aina mbili. Kuna wavunaji wakubwa na wavunaji wadogo wadogo. Sasa tatizo kubwa linakuja kwa wavunaji wadogo wadogo. Wavunaji wadogo wadogo wanafanyiwa *assessment* kila mwaka, lakini wavunaji wakubwa wanaendelea kila mwaka wanavuna tu. Mheshimiwa Waziri kwanza nakupongeza kwa mpango ulioanzisha sasa hivi wa ukaguzi wa misitu kwa sababu sasa hivi kuna watu wanafanya ukaguzi ile hatua nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Lakini nataka nikuambie kwamba sasa hivi wananchi wale wavunaji wadogo wadogo wameanza kula hata mitaji yao kwa sababu wamesimama tangu mwezi wa tano mpaka sasa hivi hawafanyi kazi. Wale watu wanategemea sana kuvuna mbao ili waweze kuishi.

Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri tunapoanza mwakani hii ya kusimamisha wavunaji wadogo wadogo naomba labda uangalie mfumo mpya

wasisimame wavune moja kwa moja wapewe vibali kama ni kuvuna mitano, wavune miaka mitano. Sasa hivi kule hata ujambazi umeanza watu wanaanza kupiga nondo kwa sababu vijana hawafanyi kazi kwenye upasuaji mbao. Ukiangalia wale wavunaji wadogo wadogo ndio wanaojenga Mji wa Mafinga, wanajenga Mji wa Igowole, wanajenga Mji wa Igowole, wanajenga mji wa Nyololo na Mji wa Mtwango. Ni wavunaji wadogo wadogo. Ukienda kwa wavunaji wakubwa hawajengi mji wale wanaajiri tu watu na kusafirisha kwenda nje. Lakini hawa wanauzia humu humu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hilo uliangalie kwa makini kwa wavunaji wadogo wadogo. (*Makofi*)

Katika ukaguzi ule ulisema kwamba wakusanye mashine za uvunaji mbao. Sasa sijui utafanyaje kwa sababu mashine zimefika karibu 2000 na zaidi, wavunaji sijui utafanyaje, kwa sababu katika fomu ile mlisema watu wapeleke mashine na watu wameshanunua mashine tayari. Sisi sielewi kwa sababu mtu kama amenunua mashine halafu akakosa kibali na wewe umemwambia anunue mashine ametuma hela kwa kununua mashine akakosa kibali inaweza ikaleta tatizo sana katika Wilaya ya Mufindi. *(Makofi)*

Halafu suala jingine ambalo nimeliona ni kwamba kuna wavunaji wapya. Kuna watu wengine wanaomba kuvuna ana-apply kupata kibali miaka mitatu mfululizo hapati kibali. Lakini utashangaa katikati ya mgao kuna vibali vingine vinakuja vinakotoka havieleweki. Sasa nakuomba uangalie sana kwa sababu vibali vyenyewe vinatoka Dar es salaam

utakuta order zinatoka Dar es Salaam. Kwanza nawashukuru sana viongozi wale watendaji wa pale *Sao Hill* ambao wako ofisini pale sijawahi sikia tatizo kama hilo. Lakini vibali vingi fake, mimi naita vibali fake, vinatoka Dar es Salaam sasa utashangaa kuna wenyeji pale wanaomba miaka mitatu hawapati vibali. Sasa nakuomba Mheshimwia Waziri hilo ulizingatie. Suala jingine ambalo nataka nipongeze kwa mgao wa mwaka jana, naomba ule uendelezwe kwamba wanavijiji pale ni muhimu sana kupewa vibali. Vijiji vinavyozunguka msitu kwa sababu wale ndio wanaopanda msitu, wale ndio wanaolinda moto, usipotoa vibali kwa vijiji italeta tatizo kubwa sana. Ukiangalia katika Wilaya ya Mufindi mimi huwa nashangaa, huwa tunakosa hata madawati. Sasa vile vibali ukitoa kwenye vijiji maana yake zile fedha zinatumika hata kuchonga madawati na kujenga shule pamoja na kumalizia zahanati ambazo zimebaki. *(Makofi)*

Mwaka jana umetoa vibali kwa vijiji 14 mwaka huu usitoe vibali kwa vijiji 14 toa kwa vijiji zaidi ya 30 kwa sababu kule kuna vibali vinakwenda mpaka 600 sasa wewe ukitoa vibali 30 kwa vijijij kuna ubaya gani. Nakuomba sana hasa hasa vijiji vile ambavyo vinazunguka pale, naomba nikutajia haraka haraka ili nikusaidie. Ukianza unakwenda Matanana ni kijiji ambacho kiko jirani, unakwenda Bumilainga, unakwenda Kisada, unakwenda Nyololo, unakwenda Nzivi, unakwenda Igowole, unakwenda Kihanga, unakwenda Mninga, unakwenda Mkalala, unakwenda Kibao, unakwenda Sawala, unakwenda Kijiji cha Kalinga, unakwenda Itimbo, unakwenda na vijiji vingine

viko jimbo la Kaskazini nadhani Mbunge mwenzangu atakupa. Hivyo vijiji ni msingi, viweze kupewa vibali. *(Makofi)*

Sasa nataka nikuambie kitu kimoja, ukitoa kibali kimoja bado hakisaidii toa vibali viwili utakuwa umeshamaliza hata maendeleo ya Wilaya yetu itasonga mbele. Sasa ukitoa kibali kimoja bado hakisaidii sana. Lakini *anyway* kwa mwaka jana mlifanya vizuri kwa sababu mlitoa kibali kimoja kimoja kwa vijiji 14 imeleta *impact* kubwa sana. Kwa hilo nakupongeza. Lakini kwa mwaka huu nakuomba Mheshimiwa Waziri utoe vibali viwili. Hiyo italeta *impact* kubwa kwa wanavijiji kule. Wanavijiji ndio wanaofanya maendeleo kule, usije ukafikiri labda wavunaji wakubwa wanafanya maendeleo ni wanavijiji. Tunashukuru sana kwa hilo kwa mpango wa kutoa vibali kwenye vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo ni la msingi naomba niongelee kwenye masuala ya wanyamapori. Sisi katika Wilaya ya Mufindi hatuna Wanyamapori. Kuna sehemu fulani kwa mfano vijiji vya Iyegea kuna kijiji cha Kwatwanga na vijiji vingine tumeweka tumesema game reserve. Sisi hatuna game reserve. Kule wanyama hawapo tunakaa kule ni binadamu tunakaa kule tunalima. Sasa naomba vile vijiji ambavyo unaweka *game reserve* kwa mfano Iyegea pale naomba sehemu wakabidhiwa wanavijiji waweze kuendelea na kufanyakazi zao za kila siku. Halafu mwaka jana nakumbuka kuna sehemu ya………..

*(Hapa Kengele ililia kuashiria Muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD LUTENGANO KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza napenda ni-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri wa Wizara hii lakini Wizara hii ina changamoto nyingi, ushauri wangu kwao wamuweke Mungu mbele na yote watayaweza hakuna linaloshindikana kwa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Utalii ni kati ya sekta ambayo inaliingizia taifa fedha nyingi sana. Kutokana na kitabu cha hali ya uchumi kinaonyesha mwaka jana sekta hii iliingiza dola milioni 1.34. Lakini tunaweza tukaingiza fedha nyingi zaidi kama tukiwa na mipango mizuri na tukaweza kujitangaza zaidi. Lakini suala la *marketing* linahitaji fedha. Tukiangalia shughuli zinazofanywa kwa ajili ya *marketing* ni *Tanzania Tourist*

*Board* wanafanya. Lakini kuna wachangiaji wengine wamekuwa wakiilalamikia *Tanzania Tourist Board.*

*Tanzania Tourist Board* wanapewa fedha kidogo sana. Mwaka huu wamepewa bilioni 4.6 ukizingatia tangazo moja tu *CNN* ni dola 800,000 sawa na bilioni 1.8. maskini wa Mungu hawa watafanyaje kazi? Wenzetu wa Kenya wametoa shilingi bilioni 16 kwa ajili ya utangazaji, *South Africa* wametoa bilioni 70. Sasa tunategemea *TTB* watafanyakazi kwa kutumia fedha kidogo namna hii? Kwa hiyo, mimi ningeomba Serikali na Wabunge, tuombe Wizara ya Fedha waongeze fedha kwa ajili ya *Tanzania Tourist Board* ili nao waweze kuwa washindani. *(Makofi)*

Siyo hilo tu, wenzetu wa Kenya na *South Africa* tayari wana ndege zao kwa hiyo wanatushinda sisi kwenye suala hili. Wageni wengi wakija *Africa package* yao ina-*include* tiketi.

Sisi kama Tanzania tumepoteza zaidi ya asilimia 60 kwenye watalii, ni kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 2.2 sababu tu hatuna ndege yetu wenyewe. Kwa hiyo, naomba Serikali ijitahidi basi Waziri wa Uchukuzi alisema wananunua ndege nyingine wafanye basi haraka ili na sisi tuweze kuwa na ndege yetu tuweze kuwa *competitive.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu *Local Tour Operators.* Inabidi Serikali iangalie jinsi ya kuwalinda *Operators* wa ndani. Sasa hivi soko hili linashikiliwa zaidi na wageni kutoka nje. Unakuta *Local Tour Operator* akitaka kufungua kampuni

anatakiwa awe na magari matano mapya. Magari matano mapya kwa mzawa ina maana gari imeshakata *roof* kwa ajili ya kwenda kufanya *tours* kwenye *National Parks* siyo chini ya shilingi milioni 120. Sasa magari matano unaongelea milioni 750 bado hajalipa *taller license* na kodi nyingine. Lakini wenzetu wanaotoka nje wakija hapa wanatakiwa walete magari 10 mapya. Mimi napenda kuuliza Je, ni nani anayecheki kama wameleta magari hayo, kwa sababu kule kwao tayari riba kwenye mabenki yao ni ndogo, lakini riba kwetu sisi ni kubwa. Kwa hiyo, hatuwezi kushindana na wageni kutoka nje. Tukumbuke kwamba wageni wakitoka nje fedha wanazozileta hapa ni zile kulipia ma-*potter* na *park fee.* Fedha nyingi zinabaki kule kule nje. Lakini mkimlinda mzawa ina maana pato la taifa litaongezeka na fedha zao ziko hapa hapa. *(Makofi)*

Naomba niongelee kidogo kuhusu *karibu fair* iliyoko Arusha. Sasa hivi matangazo mengi ya utalii wa ndani yameongezeka. Napenda nipongeze Wizara wanatangaza kwenye *TV,* lakini *karibu fair* inaweza kuwa ndio chanzo kizuri cha kuweza ku-*promote local tourism.* Lakini pale wanakofanyia maonyesho Arusha ardhi ile ni mali ya Magereza. Kwa hiyo wako kwa muda tu. Sasa ningependa kwa sababu Serikali ni moja wapewe *TTB* ile ardhi au Wizara ili waweze kujenga mabanda ya kudumu. Kuwe na *restaurant*, vyoo na kadhalika, hii itawavutia watu wengi kutoka nje waweze kuja na waifanye iwe nzuri kama ile ya Indaba iliyoko *South Africa.* Nina hakika tutapata watu wengi na uchumi wetu utakuwa na Jiji la Arusha litazidi kuvutia watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo naomba nizungumzie Mlima Kilimanjaro. *Park* hii ni kati ya *park* ambayo inaliingiza Taifa fedha nyingi sana. Kwa mwaka jana imeingiza shilingi bilioni 20 na tunaweza tukaingiza fedha zaidi kama tutaweza kupata mbinu mpya zaidi. Kwa mfano, katika Mlima Kilimanjaro kwa sasa hivi kuna njia sita za kupanda, *Marangu route, Machame Route, Ungwe Route, Rongai Route, Lemosho great* na ile Rondorosi. Lakini kuna njia ambazo zipo zinaweza zikatumika kwa ajili ya kupanda mfano barabara ya Kilema Kaskazini, barabara ya Kilema Kaskazini tayari miundombinu ipo ni kiasi tu cha kuruhusu ile njia ianze. Kuna barabara ya *Old Moshi,* barabara ile ilikuwa zamani inatumika kwa ajili ya *emergency,* lakini sasa hivi tayari zile *camps* zipo na njia ile ni fupi sana. Tunaweza tukaitumia kwa ajili ya ku-*acclimatize* wakaenda hata kwa siku mbili au wakaenda kwa *day trip* na inachukua siku tatu tu kufika kwenye mlima. Kuna watu wengine wanakuja wana muda mfupi. Kwa hiyo, tukifungua njia ile watalii wengi wanaweza wakaja wakaitumia na tukapata watalii zaidi.

Lakini cha kusikitisha pale *Kilimanjaro National Park* kuna ukiritimba mbaya sana. Sasa hivi tukilipia wageni kwenda kupanda mlima tunalipa kwa kadi za aidha *CRDB au Exim.* Wageni hawa unakuta *well in advance* sasa wakija wakitaka kupanda mlima wakitaka kupanda mlima wanataka wakifika *gate* waondoke, lakini kuna matatizo ya *system* kuwa *down* benki. Unakuta wale maafisa pale kwenye *National Park* wanawazuia wageni wanaweza wakakaa pale *gate*

hata zaidi ya masaa manne wakisubiri mtandao uwe sawa. Mimi ningeshauri kwa sababu kuna *Tour Operators* ambao wamekuwa wakipandisha milima zaidi ya miaka 30 zaidi ya miaka 20 kwa nini wasiruhusu wageni waende halafu baadaye waje wamwambie hata Yule dereva abaki pale mpaka wakati *system* itakapokuwa sawa? Badala yake wanawaweka wageni wanakaa kwa muda mrefu na hii inaleta *bad image* kwa nchi yetu wanafikiri kwamba wale ma-*tours operators* ni matapeli. Lakini kumbe ni *system* tu mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu kwenye *booking* katika *gate* la Marangu ni baya sana. Kawaida inabidi watu wapeleke *booking* halafu watoe *deposit* kwa wale watu ambao wamewa-*book.* Lakini unakuta maafisa pale *Marangu Gate* wana *block book* wale watu hawapeleki *deposit* unakuta mtu ka-*book* watu 52 *the end of the day* wale watu hawaji, Yule mtu ambaye alikuwa na wageni wa uhakika wa kuja wanawanyima wana-*cancel* tayari unakuta na wale ma-*tours operators* ambao walikuwa na wageni wa uhakika wana-*cancel* zile *booking* na taifa na wananchi na ma-*potters* kila mtu anakosa pato katika *booking* ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo utalii mwingine zaidi ya ……..

*(Hapa Kengele ililia kuashiria Muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Wamenipunja muda wangu.

**MWENYEKITI:** Hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MUSTAPHA BOAY AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia mimi niwe hapa. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, tatu natuma salaam zangu kwa Waislam wote Ulimwenguni waliofunga Mwenyezi Mungu atie kibali funga yao pamoja na yangu. Nne, Mwenyezi Mungu pia awape nguvu Mawaziri wawili, Waziri Balozi Kagasheki na Mheshimiwa Nyalandu ambao wameteuliwa upya. Nawapongeza zaidi kwa kuanza kazi kwa kukutana na wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ni sekta muhimu sana katika uchumi wa Tanzania na inatakiwa pia katika Bajeti hii itazamwe kwa jinsi hivyo. Jana Mheshimiwa Zakia Megji alitoa takwimu za umuhimu wa sekta hii katika uchumi wetu sitazirudia. Pili, pia naungana na Mbunge mwenzangu Lucy Owenya kwa *data* pia alizotoa. Sasa mimi ninaanza na vivutio vya nchi hii nikivilinganisha na sehemu ambazo Tanzania inashindana navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vivutio ambavyo Tanzania inavyo duniani Tanzania ni namba mbili. Lakini katika ushindani ni namba 110. Afrika Kusini kwa ranking ya vivutio ni namba 14 katika ushindani ni namba 66

Mauritius *ranking y*ake katika vivutio ni namba 13 nafasi yake katika ushindani ni namba 53 na Kenya ambayo ni jirani yetu ambayo sisi na wao na tunauza *product* zinazofanana *ranking* yake katika vivutio ni 28 lakini katika *ranking* yenyewe ni 103. Sasa hiii ina maana gani? Kwa kifupi hii ina maana kwamba katika ushindani sisi tuko chini sana. Sababu inayotufanya tuwe chini sana ziko sababu nyingi nitazitaja chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba nitamke kwamba mimi ni mfanyakazi katika sekta hii kwa miaka zaidi ya 20 kwa hiyo, nazungumza hapa kisomo na utalaam na uzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linalokumba sekta ya utalii hapa Tanzania ni upungufu wa watalaam na upungufu wa mafunzo yaani *training* wa sekta mbalimbali ukianzia sekta ya hoteli, sekta ya *tour guiding,* sekta ya ofisini katika *operations* na sekta ya umma ofisini hasa kule kwa Waziri.

Sasa mambo mengi hapa yanazungumzwa madongo yakitupwa kwa Waziri lakini haya mambo yanatokana na utendaji ofisini. Kwa hiyo, tutazame ndani ya ofisi kwanza utendaji ni vipi.

Kwanza napongeza Serikali imeshaona kwamba kuna haja ya kupitia upya sera. Kwa hiyo, niipongeze Serikali kwa jambo hili lakini naishauri kwamba sera yote pamoja na sheria pamoja na kanuni zote zinazohusiana na biashara ya utalii itazame upya ndio itaondoa tatizo alilotamka Mheshimiwa Owenya hapa

kwamba gari zinatakiwa 5 ili mtu aanze biashara ya utalii.

Sasa ijulikane maana ya *tour operator* ni nini tofauti yake ni nini. Je, ni lazima mtu awe na gari awe *tour operator?* Je, hawezi mtu akakaa ofisini akaleta nchi za nje wageni 10,000 lakini hana gari na wageni wakaenda porini wakaleta hela Tanzania wakaongeza ajira, wakaongeza kodi ya Serikali? Kwa hiyo, hii itaangaliwa iwapo sera itapitiwa na kanuni zitapitiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona haya sasa hii baada ya kutengeneza upya ndio itafanya kitu kinaitwa *branding* kwa upya yaani *product* zetu zitengenezwe upya. Mheshimiwa Zakia Megji jana alitamka juu ya *branding* kwa bahati mbaya sana *branding* ya Tanzania imechezewa sana kama mdoli. Kwa sababu mwaka huu inakuwa na jina hili, mwaka mwingine jina lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi ilikuwa inaitwa *Tanzania Land of Kilimanjaro* and Zanzibar, ilikuwa ni nzuri sana kwa sababu ilikuwa inaonyesha Tanzania Bara yaani yenye wanyama, mlima Kilimanjaro, yenye fukwe za Zanzibar yaani *beaches,* sasa inapotaka kujaribiwa kuondolewa, inapungua thamani yake na hii ni kwa sababu ya upungufu wa kutowasiliana na sekta binafsi. Ile zana ya Serikali ya *PPP* imepungua na hii pia imedhahirishwa jana na Mheshimiwa Telele alipokuwa analalamikia juu ya uwongozi wa Ngorongoro. Laiti kungekuwa na *Public*

*Private Sector participation* hata hayo maugomvi ya Ngorongoro hayangekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka pia kuungana na wenzangu kwamba branding ikiwa nzuri, basi marketing bajeti yake iongezwe sitarudia *data* iliyotolewa na wenzetu ambao wana bajeti kubwa. Sasa Bajeti ya *TTB* ni ndogo, tufanye nini? Bajeti ya Serikali hapa ni bilioni 77 pesa nyingine haitapatikana.

Kwa hiyo, ninaishauri Serikali ile *tools and development levy* basi ianze mara moja ili *TTB* ipate pesa ya kufanya hiyo *marketing.* Naipongeza zaidi Serikali vile vile kwa kukubali ya *destination marketing strategy* ambayo imeundwa na *private sector* na Serikali. Ile ikitazamwa upya kuwe na soko maalum ambayo nchi yetu itakuwa ime-*focus* labda tutapata sasa wageni ambao ni fursa maalum kuliko kusambaza fedha nyingi katika *market* za sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia *destination marketing,* kwa haraka haraka nimegusia *PPP* naomba sasa niangalie sehemu za Jimboni kwangu kuhusu mipaka ya wanyama waliohifadhiwa na wananchi. Hii imekuwa ni tatizo kubwa na wananchi wengi, mazao yao yanaliwa, wao wameuliwa, fidia ni ndogo, rangers ni wakatili sana wanapiga risasi wanyama na binadamu.

Sasa napendekeza kwamba eneo lile ambalo wanyama wanawaingilia sana wananchi, basi ziwe fenced, ziwekewe zuiyo, fence zimefanyika sehemu nyingi duniani kama Kenya, Afrika ya Kusini na

Botswana kwa maeneo kama Lake Manyara na Tarangire, maeneo ambayo wananchi wamesumbuliwa, napendekeza zifanywe *fence, fence* mbili ambayo wananchi mazao yao yatapona na wanyama wa pori watapona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii wanyamapori wananchi hawafaidi nao sana kwa sababu Sheria hairuhusu wauwawe, halafu wawekwe kwenye ma-*butcheries* wauzwe kama kitowewo pia nishauri Kanuni zitazamwe upya ili wanyama hao wauzwe kwenye *butcher* kwa sababu wawindaji wanakuja wanawinda nyama zinaharibika hovyo, wanatumiwa kama *bate* ya kuuwa wanyama wengine na sisi wengine tunaotumia wanyamapori, tunawatizama.

Kule Kenya kuna kitu kinaitwa *carnival centre,* nyamapori inachomwa na watu wanaifurahia. Sasa hapa nchini kuna wawekezaji wanataka kuanzisha vitu kama hivyo, lakini Kanuni hairuhusu, tunaomba Sheria itazamwe upya kama mwananchi anaruhusiwa kufanya *ranching,* basi aruhusiwe kuuza labda nyumbu, nyumbu huyo aonekane kwenye *butcher.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka haraka pia kwa ajili ya muda nizungumzie *domestic tourism.* Watu wengi wanaelewa *domestic tourism* kama kutembelea mbuga za wanayama. Utalii wa ndani maana yake ni kutembelea au kutumia vivutio vilivyoko nchini kwetu, inawezekana ikawa ni vya kihistoria, mtu wa Mwanza kwenda kutembelea Dar es Salaam, wa Dar es Salaam kwenye mpaka Mbulu kuona huko Mbulu watu wanaishi namna gani ikiwa ni

pamoja na kuhudhuria *cultural tourism* za eneo mbalimbali. Kwa hiyo, ninazishauri Halmashauri mbalimbali kuanzisha sehemu za utalii kama huo ili uunganishwe katika *main tourism products.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni juu ya zile fedha za *TANAPA* asilimia 10 inayopelekwa kwenye Serikali, ile fedha kama alivyosema Mbunge mmoja wapo ni kwamba inadidimisha uwezo wa *TANAPA* kufanya kazi zake, zile pesa *TANAPA* wangerudishiwa fedha zao ziweze kutumika kwa Bajeti yao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitazungumzia sana juu ya biashara ya uwindaji, lakini ni sehemu kubwa ya malalamiko nayo pia kama Sera na Sheria yake na Kanuni yake ikatazamwe upya, pengine Serikali itagundua kama kuna matatizo yalitokana na kubadilishwa kwa Sera ama kuboreshwa ambayo sasa hivi inatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante sana.*(Makofi)*

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii iliyoko mezani ya maliasili na utalii. Awali ya yote napenda nitoe shukurani ya hali ya juu kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara kubwa aliyoitumia, macho ya makini kabisa aliyotumia kuchangua Mawaziri mahiri katika Wizara hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri ambayo ameianza na *speed* hiyo aliyonayo, wasije wakaingia katika ule msemo wa Kiswahili kwamba nguvu ya soda. Waendelee na *speed* hiyo, hiyo nidyo italeta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pongezi kwa hali ya juu kwa Waziri wa Maliasi na Utalii na Waziri wa Mambo ya Ndani katika tukio ambalo lilitokea Wilayani Serengeti la mauwaji katika *camp* ya *Ekoma Bush Tented Camp* ambapo *Manager* Msaidizi aliuwawa pamoja na mtalii wa kutoka Uholanzi. Usiku ule nilipopata taarifa, ilikuwa ni saa sita usiku tarehe 20 mwezi wa sita, nilimpigia Waziri wa Mambo ya Ndani asubuhi yake wote walikwenda Wilaya ya Serengeti.

Nawashukuru sana, nawapongeza na pia kwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe pamoja na Mheshimiwa Waziri Kagasheki kwa kutoa kibali cha Serikali kujenga uwanja wa ndege Wilayani Serengeti, uwanja wa pale Mugumu eneo la Bulunga. *(Makofi)*

Naomba hali hii ya mtazamo wa kuinua uchumi wan chi, iwe kwa kweli ni Sera na mawazo mazuri na Mawaziri wengine watumie mfano huu. Ni njia ya kuinua uchumi na vitu kama hivi ndivyo ambavyo vitasaidia kupunguza ujangili katika mbunga ya Serengeti, kwa sababu hakuna mtu ambaye yuko tayari kwa kweli ku-*risk* maisha yake kwenda katika mazingira hatari ya ujangili. Lakini kama kuna vitega uchumi, ukiwemo uwanja wa ndege, barabara ya lami ndiyo njia pekee ya kupatia wananchi kipato hususani

vijana ambao sehemu kubwa hawana ajira ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala zima la kero ambazo ziko katika Wilaya ya Serengeti. Ziko kero nyingi lakini suala la mipaka katika Sheria hii Utalii ya mwaka 1959 ni vizuri itazamwe upya, mara kadhaa Wizara wametuambia hapa Bungeni kwamba mipaka ilivyo, haitabugudhiwa, haitabadilishwa.

Lakini tunachokiona wananchi hawa wa Serengeti ambao kwa kweli wamefanya kazi kubwa kupitia uwindaji wa asili, ndiyo sababu wanyama hawa bado tuko nao na kwa sehemu kubwa wamesaidia sana kulinda wanyama hawa la sivyo tusingekuwa nao tunajivunia. Sasa badala yake imegeuka ile ya Kiswahili kwamba kumbe shukurani ya punda mateke.

Aidha hii ambayo wananchi wa Serengeti wanaipata katika historia hiyo ya uwindaji mzuri, uwindaji wa asili, wanyama hawa leo wanapata fursa nzuri kusaidia uchumi wa Kitaifa. Asilimia 17 hii ambayo pato la Kitaifa linatokana na utalii, ni pamoja na mchango mkubwa wa Wanaserengeti.

Lakini kero hii ya mipaka ardhi, pamoja na mifugo masuala ya malisho, naomba hili Mheshimiwa Waziri ulitazame kwa macho mawili. Kupitia nafasi hii kwa niaba ya Wanaserengeti naomba nikupe mwaliko rasmi baada ya Bunge hili, tuongozane kwenda Serengeti ujionee mwenyewe. *(Makofi)*

Maana yake Kiswahili wanasema wenzetu kwamba *to see is to believe,* ukiona unaamini. Na ukisikia vile vile utaamini. Katika kazi uliyoifanya nzuri Mheshimiwa Waziri, kwa bahati nzuri umetembelea Wilaya ya Serengeti mara mbili baada ya kuwa umeingia ofisini katika uteuzi wa juzi, naomba hii iwe ni sehemu ya kukufungua macho, yako mengi, naomba uje, tukae vizuri, tuzungumze ndani ya Wilaya na kutembelea wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo kuna kuainisha mipaka, mwaka 2008 tumejionea, kulikuwa na tathmini, kulikuwa na kusema wanapitia mpaka 2010 na mwaka huu zoezi hilo linaendelea, lakini hii haishirikishi wananchi.

Kwa mfano zoezi ambalo lipo kuna timu ya Wizara inazunguka hivi ninavyozungumza katika maeneo ya Bisarara kule Bonchugu, Mbirikiri, Machochwe, Nyamakendo, kule Natambiso pamoja na Ekwaromobada hapa Kinyigoti. Kwa kweli kuna kero kubwa Mheshimiwa Waziri, kama inawezekana naomba zoezi hili lisimame, utaratibu ufuatwe. Wananchi washirikishwe ili kusudi hiyo ndiyo ushirikishi na utawala bora wa Kisheria.

Lakini suala la kwenda wataalam halafu wanatoa maagizo na maelekezo, hiyo haina tija na inakuwa ni sehemu ya uhusiano ambao ni hafifu. Sasa kuishi kwa kunyoosheana vidole haijengi, kikubwa ni kujenga uhusiano na kuishi vizuri na jamii iweze kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa *National Parks.*

Suala kwa mfano la kuanzia tarehe 27 mpaka 29 ambapo ng'ombe wa Mzee mmoja anaitwa Mzee Mwita Temaha, hawa walikamatwa lakini akalipishwa shilingi milioni 2,340,000. Fedha zile kwa ushuhuda huu nilionao mimi nina mashaka na nakala za risiti hizi ambazo ninazo na hata ukipiga thamani ambayo ni milioni 2,340,000 hailingani na mifugo 97 ambayo ilikamatwa wakiwemo mbuzi 18, kondoo 16 pamoja na ng'ombe 58.

Suala hili kuna giza naomba baada ya hapa nimkabidhi Mheshimiwa Waziri afuatilie suala hili kwa umakini na pia jambo la msingi, Tume ya Wizara kulingana na michango ambayo ilitolewa na Waheshimiwa Wabunge mwaka jana. Wizara iliahidi kwamba inaunda Tume, Tume imekwenda kule mpaka sasa taarifa ile hatuna na pamoja na Bodi ya *TANAPA* ambayo wametembelea katika mazingira yale ni vizuri tupate taarifa kamili ni kitu gani ambacho kimejiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijaribu kuangalia kero nyingine ambayo ipo katika Wilaya ya Serengeti, haiwezekani kule tunao wafanyabiashara wazuri wakubwa na wana uwezo wa kifedha.

Kwa nini manunuzi haya mpaka leo hii tunazungumza katika Idara zingine za *TANAPA,* mahoteli yaliyoko mbugani, manunuzi yanafanyikia Arusha ambako ni zaidi ya kilomita 400 na wakati mwingine yanafanyikia Mwanza, pale Serengeti haiwezekani? Narudia neno hili, mwaka jana nilisema kwamba hata *toilet paper* hivi ni mpaka zitoke Arusha, Nairobi au Mwanza?

Hawa ambao wana uwezo kwa Serengeti wapewe kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, hivi juzi umefanya ziara nzuri ya kikazi pale Ekwamarobanda kufuatilia mgogoro wa WMA. Hivi WMA's ni vizuri ziangaliwe upya na zisimamiwe katika *Management* zake kwa sababu inafika mahala hata katika kuchagua uwongozi wa *WMA's* unakuta kampeni inapigwa kuliko hata ya kuchangua Mwenyekiti wa Kijiji wakati *WMA's* hizi zinapaswa ziwe chini ya Kijiji, zitoe taarifa ya fedha katika Kijiji pamoja na Halmashauri.

Kwa hiyo, mimi nashukuru kwamba ufuatiliaji ambao umefanywa juzi, isiishie hapo, suala hili lifuatiliwe kwa umakini. Kero ya ajira, ni vizuri Serikali iangalie itazame upya kuwe na *quarter* ya mgao kwa watumishi wale ambao wanatoka jirani na maeneo ya hifadhi. Kwa mfano mwaka 2008 nakumbuka Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Edward Lowassa alitembelea Wilaya ya Serengeti.

Waziri Mkuu aliulizwa hivi kwa mfano katika hii *Brass Band* ile ya *TANAPA* kuna watumishi wangapi ambao wanatoka Serengeti? Kulikuwa na mtumishi mmoja tu kitu ambacho ni aibu na ni kero kwa wananchi. Ni vizuri kuwe na *statement* ambayo ipo Kisheria kwa ajili ya kuweka mgao mzuri na kujenga moyo na imani kwa hawa wananchi wa Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la tembo na wanyama wengine waharibifu wanaingia sana katika maeneo ya makazi. Kwa mfano mwaka juzi aliuwawa Kijana mmoja Marehemu Mataiga, mwaka jana nilileta taarifa zake kwa Waziri mpaka leo imekuwa kimya. Lakini hawa wanyama wanavyoingia katika maeneo ya makazi, adhabu inayotolewa kwa mfano kwa wananchi ambao wanajipatia mboga kidogo ni kubwa kuliko ambavyo Serikali inalipa kifuta jasho na kifuta machozi. Kwa hiyo, suala hili ni vizuri litazamwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya mwisho ni suala la mapato. Nilijaribu kuangalia katika kiambatanisho ambacho kiko katika ukurasa wa 60 na 61 juu ya mapato kutokana na uwindaji wa utalii. Utashangaa kuona kwamba Wilaya ya Serengeti mwaka juzi walipangiwa milioni 42, mwaka jana milioni 29 na mwaka huu oteo la milioni 51. Ukijaribu kuangalia hakuna mtiririko mzuri pamoja na kwamba inategemea na *projection* ya wawindaji, lakini je Wizara imejipanga vipi kwamba hii milioni 51 itapatikana na kupelekwa Wilaya ya Serengeti.

Lakini ukilinganisha na maeneo mengine ambayo yana eneo dogo la Hifadhi, mapato yale ni makubwa kuliko Wilaya ya Serengeti, napenda wakati wa kujumuisha Mheshimiwa Waziri nipate maelezo ya kina.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Dkt. Kebwe nakushukuru.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mengine nitawasilisha kwa maandishi na nashukuru sana napongeza Mawaziri, karibuni sana Serengeti nashukuru.*(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uhai na uzima, kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu, lakini la pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unachangia asilimia 17.2 ya pato la Taifa na utalii huu huu ndiyo unaingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni katika nchi yetu. Kwa hivyo, kwa vyovyote utalii una umuhimu wa pekee katika nchi yetu. Uko aina nyingi ya utalii, kuna utalii wa fukwe, kutembelea wanyamapori, kwa maana ya uwindaji na kupiga picha, kuna utalii wa kwenda katika maeneo ya mali kale, lakini zaidi nijikite katika utalii wa picha.

Katika hali ya kawaida, Serikali inapata fedha katika utalii wa picha kutakuwa na aidha kukodisha vitalu kwa ajili ya wale ambao watawakaribisha wanaokuja kupiga picha na kutoa leseni za wale ambao wanakwenda kupiga picha za utalii.

Mimi nadhani umefika sasa wakati sasa Wizara iangalie hawa watalii ambao wanapiga picha. Inavyoonekana ni kuwa watalii wengine wanakuja kibiashara, licha wa wale ambao wanakuja kujifurahisha na kuona wanyama wetu na maandhari

yetu, lakini inaonekana kuwa watalii wengine wanakuja, wanapiga picha zile, wanataharisha filamu zile, wanaziuza huko duniani. Inavyoonekana Serikali yetu haipati chochote kuhusiana na suala lile. *(Makofi)*

Kwa mfano hai ni kama huu; imetaharishwa filamu inayojulikana Lion King, filamu hii imetayarishwa katika mbuga ya Serengeti na eneo hasa au mazingira ambayo au maandhari ambayo imepigwa filamu hii ni katika eneo ambalo linajulikana kwa jina la Nyasirori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, filamu hii baada ya kutaharishwa, hao waliopiga picha hii, pekee yao walilipwa dola milioni 36 za Kimarekani. Hapa Serikali inaonekana pengine haielewi, haikupata chochote. Vinginevyo labda Waziri atakapokuja kutujulisha labda anieleze kuwa Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi Serikali imepata.

Lakini picha hii, *Lion King* ambayo inaonyesha suala zima la wanyama mpaka sasa duniani imefikia mauzo ya dola za Kimarekani bilioni 4. Ni fedha nyingi hizi, Serikali yetu nadhani haijapata wala pengine haielewi. Sasa nadhani Wizara hii iendelee kukusanya kutokana na vitalu, leseni, lakini ipo haja ya kuona kwa njia gani watapata fedha kutokana na watu wanaokuja wanaotumia wanyama wetu, maandhari yetu katika kupata filamu ambazo zinavutia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile imegundulika kuwa si maandhari za mbuga zetu, lakini zimeonekana ziko filamu nyingine, maadhari yao ni maporomoko ya Kalambo ambayo yako Mkoa wa Rukwa. Maporomoko haya ni ya pili katika Afrika baada ya maporomoko ya Victoria. Kwa hivyo, wako watu wamechukua picha pale, wanaziuza duniani, wanapata fedha nyingi lakini Serikali, naamini haipati chochote kuhusiana na suala hili.

Kwa hivyo, nadhani imefika wakati Wizara ione kuwa Rwanda, wao wamebahatika kuwa na wanapata fedha. Walitayarisha *Lion King,* picha kama hii kwa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiri wake ni nini? Usiri ni kuwa, kunafanyika mambo mawili. Kwanza, inatakiwa eneo husika lifanyiwe thamani, *value,* tuseme Serengeti, lionekane wanyama waliomo kiwastani, ardhi yake, halafu inajulikana kuwa Serengeti, ina thamani kiasi kadhaa. Halafu, inatolewa Hatimiliki. Sio kwa sababu *TANAPA* ipo tu Kisheria, lakini haitoshelezi. Ukifanya hayo mambo mawili, hapo tena unaweza kupata fedha kutokana na picha au filamu ambazo zinauzwa nje.

Kwa hiyo, mimi nadhani hili naona Wizara waliangalie, walifanyie kazi, walitafiti na ionekane kuwa, Serikali yetu, haipotezi mapato kutokana na watalii wanaokuja kupiga picha, ambao wanaziuza nchi za nje na wanapata mapato makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la ujangili wa wanyamapori. Hili ni suala kubwa na ni suala ambalo linaleta tishioo kubwa kwa kutoweka wanyama wetu. Licha ya tembo ambao meno yake yamekuwa ghali au yamepata bei kubwa katika soko haramu dunia katika nchi za Asia ya Mbali, kwa sababu, mwaka 1990 kilo moja ya meno ya tembo ilikuwa ni dola 100, hii leo, kilo moja ni dola baina ya 1,200 mpaka 1,500. Kwa hivyo, hii ni kazi ambayo…

*(Hapa Kengele ililia kuashiria Muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** ......... itakuwa inafanywa na wengi wanaoifanya na itakuwa na mtandao mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo ninaloliona kubwa ukiachana na pengine mmomonyoko wa maadili, licha ya kuwa hiyo meno ya tembo yana bei kubwa, licha ya kuwa kesi za uhujumu uchumi zinazohusiana na maliasili hii zinahujumiwa, lakini naona tatizo kubwa mimi liko katika Bajeti. Ni tatizo la kibajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii, Bajeti yake hii ambayo tunaijadili leo ni bilioni 77.24 kwa sekta zote kwa kweli. Leo, Idara ya Wanyamapori peke yake, ili iweze kudhibiti ujangili na kuendeleza uhifadhi katika mapori ya akiba, inahitaji bilioni 31. Karibu nusu ya Bajeti ya Wizara nzima. Ina maana iende katika Idara ya Wanyamapori, ambayo haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuliachia suala hilo Wizara ya Maliasili na Utalii peke yake, ni kujidanganya. Kwa sababu, Bajeti ni *ceiling,* maduhuli yanayokusanywa yanapelekwa Serikali Kuu, karibu bilioni 124 wanayapeleka katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo, haiwezekani wao kuhudumia Idara hii kwa matatizo yake yote, ili waweze kulinda wanyamapori wetu hawa. Kwa hivyo, ni wajibu wa Serikali kubadilika kibajeti. Kwa kweli, vinginevyo itakuwa ni hadithi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuone tu katika sehemu moja. Kuna matatizo hawana vitendeakazi hawana magari, wafanyakazi wachache wako 1,044 tu na wanaotakiwa ni wafanyakazi 4,588, yote hii ninayoizungumzia ni Bajeti.

Kwa hivyo, nadhani karibu 70% ya matatizo ya Wizara hii, kwa kweli, katika suala la ujangili kuzuia, basi yanatokana na ufinyu wa Bajeti. Hayo mengine tena 30%, ikishapatikana Bajeti inawezekana yakarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kama Serikali Kuu kama yenyewe haitakushiriki kikamilifu katika kuongeza bajeti. Aidha kwa kuwapatia fedha inayotosheleza…

*(Hapa Kengele ililia kuashiria Muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:**…au kuachia mapato wanayokusanya ...........

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Sasa namwita Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, ajiandaye Mheshimiwa John Paul Lwanji.

Hayupo? Mheshimiwa John Paul Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsantesana. Mimi naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii na ninaelewa shughuli muhimu tatu za Wizara hii. Mojawapo ikiwa ni kuhakikisha kwamba, rasilimali za nchi yetu zinalindwa na kuwanufaisha Watanzania wote. Halafu ni kuhakikisha kwamba, jamii zinazozunguka maeneo ya Hifadhi, zinanufaika na rasilimali za wanyamapori na misitu. Halafu kuboresha mazingira na makazi ya watumishi wa Wizara hiyo, hasa Idara ya Wanyamapori, wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi langu, nusu ya Jimbo langu ni mbuga za wanyamapori. Karibu kilometa za mraba 9,000 ni mbuga ya Rungwa, Kizigo, Muhesi na Chaya. Sasa na vijiji vyote hivyo vilivyopo vinategemeana na rasiliamli hizo. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi Jimbo hili lilivyo muhimu sana na linavyoambatana na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi rai yangu ni kuwaomba hawa Mawaziri wapya, watembelee eneo langu. Nitashukuru sana Mheshimiwa Kagasheki na Mheshimiwa Nyalandu, kama mtafanya jitihada za

makusudi mtembelee Kizigo, mtembelee Rungwa, mtembelee Muhesi, mtembelee mbuga za Chaya. Nadhani hiyo, itatusaidia sana kuweza kubaini ni nini mfanye kuweza kutusaidia kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Tunachangia kikubwa sana kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa, takribani shilingi bilioni 2 kwa mwezi zinapatikana kutokana na rasilimali hizo. Tuna wawindaji lukuki wako kule, lakini vijiji vyetu vingi bado ni duni kwa maendeleo. Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara hii, wajaribu kuna maeneo haya, wasiendelee kutembelea maeneo ya hifadhi tu zile za Taifa, Serengeti, Ngorongoro, Tarangire, ningeomba hizi mbuga nazo waweze kuzitembelea. Ninakumbusha lile ombi ambalo tuliomba kwamba, iwepo basi Mamlaka ya kusimamia hizi Hifadhi hizi za wanyamapori, badala ya kutegemea Idara. Tunaomba siku nyingi na sijui inaishia wapi? Toka 2007/2008 tumekuwa tukipiga kelele, toka enzi za Mheshimiwa Mama Mwangunga na wengine, tukaahidiwa kwamba, Serikali ingekuja na utaratibu wa kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori, lakini hakuna. Hii Idara hii iko *chopped,* hakuna kitu kinachorudishwa. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi walivyokuwa na mazingira magumu katika kuendesha hifadhi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliomba toka mwaka juzi wananchi wetu walipokabiliwa na ukame mkubwa sana. Tuliomba mabwawa haya ya Itwaga, Makengelebhe katika Kata ya Ipande yafunguliwe. Bahati nzuri Wataalamu walitumwa kwa ngazi ya

Wilaya, Mkoa, wakaenda wakafanya *assessment,* ikaonekana kwamba, ingewezekana sana mabwawa haya yangeweza kuwasaidia wananchi wetu.

Lakini maombi yako Wizarani pale, yamekaa mwaka, miaka miwili, hakuna jibu. Ni vizuri basi hata majibu yangekuwa yanatoka kusema tu walao basi haiwezekani, basi watu wakajua kuliko maombi yanakaa pale, hakuna majibu yoyote yanayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi huwa tunashangaa kwa sababu, maeneo mengine, jamii nyingine zinaruhusiwa kutumia mabwawa kama hayo, lakini jamii nyingine katika nchi hii hii hawaruhusiwi. Sasa hapo ndipo tunapopata kigugumizi, tunashindwa kuelewa jinsi tunavyogawana rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana hata juzi hapa tulikuwa tunazungumza tukasema kwamba, bwana kwa nini, watu wa maeneo mengine wafidiwe mifugo iliyokufa na watu wa maeneo mengine wasifidiwe? Sasa hii *discrimination* ya aina hii ningeomba hii Wizara, ijaribu kuangalia. Nina uhakika kabisa kuna jamii nyingine ambazo ni sawasawa kabisa na hizo jamii zinazoruhusiwa. Kwa mfano, kama jamii yangu ni mwiko kula wanyamapori. Mpaka leo bado watu, ukifanya hivyo, wewe unaonekana ni mtu ambaye sio wa kawaida. Ni karibuni tu watu wameanza kula, lakini miaka yote ilikuwa ni mwiko na tulia-*associate* na wanyama kama kawaida na mabwawa haya tulikuwa tunayatumia kama kawaida. Sasa ningeliomba suala hili liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni kwamba, tuliomba Vijiji kadhaa. Kwa mfano kijiji cha Lulanga, Kata ya Mganda, hiki Kijiji kilikuwa Kitongoji kikapewa hadhi ya kuwa Kijiji. Kiko ukingoni kabisa na mpaka wa Hifadhi hii ya Rungwa, lakini sasa Kijiji hiki kimepanuka, kinashindwa kufanya shughuli zake kwa sababu, kiko mpakani na tuliomba siku nyingi. Tuliwahi kuomba Kijiji cha Poroto, Kijiji cha Poroto kikawa kimeangaliwa wakapanua mpaka na hatuoni sababu kwa nini, Rungwa wasiweze kufikiriwa katika utaratibu huo huo. Ninaomba hayo maombi yaliyoko katika hiyo Wizara, Mheshimiwa Kagasheki, muyashughulikie, ili wananchi waweze kupanua shughuli zao na waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Rungwa, ni kitendawili. Bwawa hili lilivunjwa na mafuriko ya maji mwaka 2004, 2005/2006, tukaomba katika ile *Tanzania Wildlife Protection Fund,* wakatupa shilingi milioni 200 kwa ajili ya kulikarabati hili bwawa. Mpaka leo lile bwawa limeshindikana, ni kujenga kuta tu. Visingizio vingi, milioni 200 wakati huo zilitosha, lakini kwa kuwa kazi haikufanyika, ina-*accumulate,* imezidi, ongezeko limezidi la pesa hizi. Sasa tungeliomba Serikali, iweze kuona uwezekano wa kuongeza fedha watu waweze kuishi kama walivyokuwa wanaishi nyakati zile na bwawa hilo. Bwawa hilo, lilikuwa ni sehemu ya maisha ya wananchi pamoja na wanyama walioko karibu pale, walikuwa wanaishi vizuri. *(Makofi)*

Sasa bwawa hilo hakuna, ningeliomba Serikali, i-*revisit* suala hilo, ombi hilo ili liweze kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kupuuza juhudi za makusudi ambazo zimefanywa na Wizara, katika kuboresha hiki kiwango cha kifuta machozi kwa ile familia, mtu anapouwawa. Katika nyaraka zake ambazo imekuwa ikileta, tulianza na 50,000/=, lakini sasa hivi wanalipa 2,000,000/=. Hilo niwapongeze ndugu zangu mkwa jitihada hizo na muendelee kuboresha, ili hawa wanaoachwa basi, waweze kuwa na mahali pa kuanzia.

Lakini hamjaangalia suala la fidia ya mazao, fidia ya mazao imebaki kuwa 100,000/= nadhani kwa eka 4 na ndio mwisho. Eka 4 mwisho, zinazobaki kama ukiwa na eka 10, eka 20, hizo haziangaliwi, lakini mwisho eka 4. *(Makofi)*

Sasa hapo inakuwaje? Maana tumeambiwa tembo walikuwa 1,200,000 Afrika, sasa hivi wako tembo 400,000. Sasa sisi tulidhani hawa wanyama wamezidi sana wanakuja katika maeneo yetu, labda wamezaliana. Lakini inavyoonekana kuna ujangili ndani humo kwenye maeneo yao, basi wanakimbilia kwenye maeneo ya watu...

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Lwanji. Sasa namwita Mheshimiwa Said Nkumba, ajiandae Mheshimiwa Injinia Ramo Makani.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kutoa pole

kwa wananchi waliofariki pale Kitunda, kwenye Jimbo langu, kwa ajali ya gari iliyotokea hivi karibuni. Nawaombea kila la heri, wale ambao wamepata matatizo haya na wale ambao wamepata maumivu, basi Mwenyezi Mungu, awape nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, kwa Hotuba yake hii nzuri. Na mimi bila kusita, naomba kabla sijasema jambo lingine niunge mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shughuli za kusaidia kuleta maendeleo kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali zinazofanywa na Wizara, lakini jambo kubwa ambalo kwa kweli, ni la manufaa ni utatuzi wa migogoro ambayo inawagusa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Sasa katika jambo hili, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Wizara, kwa kuumaliza ule mgogoro wa Juhiwahi ya Ipole, ambao sasa umekwisha, makubaliano tayari yamefanyika na kazi sasa za maendeleo zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo amefanya kwa kushirikiana na Wasaidizi wake kutatua mgogoro huu wa Juhiwahi ya Ipole. Nikuombe vilevile usaidie kutatua mgogoro wa muda mrefu sasa ambao umekaa kwa muda mrefu, ule mgogoro wa *sheme* ya Ulula, Mibono, ambayo ilikwishajengwa na zaidi ya shilingi milioni 300 zilikwishatumika pale. Lakini bahati mbaya sana baadaye Wataalam, wakaja kutoa maelekezo kwamba, *scheme* hii iko katika eneo la *reserve,* lakini fedha za Serikali, tayari zilikwishatumika

na Wataalam wa Idara zote wakiwemo wale wa Kanda. Lakini vilevile Wataalam wa Halmashauri, walishirikishwa kutoka sehemu ya kwanza mpaka hatua ile ya mwisho.

Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwa kushirikiana basi na Wataalam, ambao ulishirikiana nao katika kutatua mgogoro ule wa kwanza, ushirikiane nao kutatua huu mgogoro mwingine. Jambo hili lilishafika mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu, akateua Tume. Bahati nzuri sana kazi zote zilikwishakamilika, sasa tunachohitaji ni ufafanuzi ambao utatolewa na Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nizungumze kidogo suala ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wameligusia. Suala la mapato ambayo yanatokana na suala la uwindishaji katika maeneo mbalimbali nchini. Niiombe sana Wizara, basi katika jambo hili, iendelee kuwahimiza sana wale ambao wanapata nafasi ya kuwinda katika maeneo mbalimbali. Vile vijiji ambavyo kwa kweli, vinazunguka Hifadhi hizi, ndivyo vijiji ambavyo vinasaidia kwa namna moja ama nyingine hata suala la Hifadhi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana suala la kuleta maendeleo kusaidia changamoto za maendeleo katika hayo maeneo, liwe suala la wajibu. Sio suala la kwenda tena tunawabembeleza, watu wamekaa pale wanavuna maliasili zetu, jambo hili haliwezi kuwezekana kuendelea kuachiwa bila sababu za msingi. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, utoe maelekezo ambayo yatasaidia katika kuhakikisha kwamba, hawa wanaopata nafasi hizi, basi

wanakwenda kusaidia. Vilevile masuala ya maendeleo katika maeneo ambayo vijiji hivi vinazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba tu nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, nalo hili utusaidie. Sisi tuna eneo kubwa sana la uwindishaji, kwa sehemu kubwa liko maeneo ya Sikonge, lakini baadhi ya maeneo utayakuta yako katika baadhi ya Wilaya nyingine, kwa mfano Mpanda kuna eneo dogo na Manyoni kuna eneo dogo. Sasa nilikuwa naomba sana, suala la Uwindishaji unapokuwa unafanyika, basi Wataalam wa Wilaya zote mbili, wawe wanashirikishwa. Haliwi jambo zuri sana Sikonge tuna eneo kubwa, halafu baada ya kuwa na eneo kubwa mapato tunapata kidogo kwa sababu, wawindishaji wanachukuliwa kutoka katika maeneo ya Wilaya nyingine. Kama kuna uwezekano Mheshimiwa Waziri, basi utoe maelekezo pale ambapo Wilaya zinapakana wakati wa uwindishaji, basi Wataalam wa maeneo yote mawili wachukuliwe, ili ile *quota* iwe inatolewa kwa kuzingatia usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili, naomba tena nirudie kuipongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii, nikupongeze sana Waziri, umeanza vizuri. Umenza vizuri na Wasaidizi wako, wale ambao kwa kweli, wanaitakia mema nchi hii, wataendelea kukuunga mkono wewe na wasaidizi wako, ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya naomba nitumie nafasi hii tena kukushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niwe mmoja wa wachangiaji katika hoja iliyoko mezani siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima lakini pia kwa kuwezesha niweze kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi ni muumini sana wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao kwa kweli na kwa hakika kila nikiona mmoja wetu anasimama na kuzungumza, nikienda kufanya rejea nakuta kazi ilikwishafanyika na kinachobaki sasa ni kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja iliyopo mezani, ukurasa wa 77 wa Mpango wa Maendeleo unaeleza malengo ya utekelezaji katika sekta hii, kwa sababu nimesoma *version* ya Kingereza inasema *operational objectives.* La kwanza, ni kuimarisha menejimenti ya maliasili, malikale na shughuli za utalii. Ya pili, inasema ni kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na maliasili, malikale na shughuli za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo inazungumzwa ili sekta au Wizara hii iweze kufanya vizuri katika malengo yake ni mambo ya fedha. Lakini ukirejea katika Mpango wa Maendeleo umeeleza vizuri kwamba Wizara ifanye nini ili iweze kukusanya mapato. Kwa hiyo, tuondokane na tatizo la kusema kwamba hatuna fedha za kuweza kutekeleza mambo yanayotakiwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatakiwa kuimarisha namna ya kuweza ku-*manage* maliasili zetu tulizonazo yaani malikale pamoja na shughuli za utalii. Sasa katika hili mimi nitazungumzia sana juu ya *Selou Game Reserve* ambayo Kiswahili chake tunasema Pori la Akiba, hapa tuna *reservations* lakini mtaalamu wa Kiswahili Prof. Kulikoyela Kahigi nitaomba wakati ujao aweze kutushauri vizuri zaidi kama kweli tuendelee kutumia neno pori la akiba kwa maana ya *Game Reserve*, mimi kwa upande wangu naona ina ukakasi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa vyovyote vile iwavyo, nataka kusema kwamba kwa kweli sasa hivi imefika wakati Serikali iache kutelekeza linaloitwa Pori la Selou. Huko nyuma tatizo kubwa la Selou limekuwa ni kwamba halifikiki, hakuna miundombinu ya kufika kule lakini kubwa zaidi ni *management,* jinsi ambavyo tuna *manage Selou* kwa kuichanganya na mbuga na mapori mengine yaliyopo ambayo hayafanani na sifa za Selou ambazo mimi nitasema kwa haraka na ninaomba nizitaje hapa. Kwanza *literature* zinatofautiana, wengine wanasema ni ya kwanza kwa ukubwa Afrika nzima lakini wengine wanasema ni ya

pili, haijalishi hata kama ikiwa ni ya pili bado ni kubwa sana *square kilometre* 55 za eneo ni mara nne ya Mbuga ya Serengeti, ni 5% ya eneo lote la nchi. Nisipoteze muda sana kutaja sifa za mbuga hii achilia mbali idadi ya wanyama na aina tofauti za wanyama waliopo lakini tembo ikiwa ni kundi kubwa zaidi lakini tunaacha utajiri ule bila kuufanyia kazi ili tuweze kuongeza pato la taifa, ni makosa makubwa sana. Naomba Serikali sasa ielekeze nguvu katika kuwezesha Selou kuweza kuibuka kuwa mojawapo ya kati ya vyanzo vikubwa sana vya nchi hii vinavyotokana na utalii pamoja na mazao mengine ya mapori na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa pili, mojawapo ya malengo ambayo yanatakiwa kutekelezwa na Wizara ambayo yamenukuliwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya miaka mitano, ni kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na raslimali za wanyamapori na misitu. Sisi ambao tumezunguka Selou, Mikoa imetajwa mara nyingi lakini nitaje Mkoa wa Ruvuma lakini hasa nitaje Kata zangu katika Jimbo la Tunduru Kaskazini. Kata ya Ngapa, Mindu, Namihungo, Muwesi, Sisi kwa Sisi, Masonya, Nandembo, Ligunga, Jakika, Kalulu na Namwinyu. Idadi ya Kata zote hizi maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba eneo kubwa la Jimbo la Tunduru Kaskazini linapakana na Selou.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukizungumza juu ya suala la ujirani mwema, tuna kasoro na upungufu mkubwa sana kuhusisha Selou kama Pori la Akiba lakini uhusiano wake na majirani zake haupo. Wengi

waliotangulia kuzungumza wameshasema kwamba uhusiano ni mbaya. Watu wanaopakana na mbuga na mapori, kuna haja ya Serikali kuboresha uhusiano kwa kipengele ambacho nimeshakisoma kwamba kumbe ni kazi ambayo inatakiwa kutekelezwa chini ya maagizo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini pia Mheshimiwa Waziri ameweza kui-quote vizuri sana katika *speech* yake, sasa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi kuna tatizo la mipaka, wananchi wanakosa maeneo ya kulima kwa sababu wanaambiwa kwamba huku ni mbugani au ni Pori la Akiba, watumishi mbalimbali wanaohusika na pori hili huwanyanyasa wananchi lakini mbaya zaidi ni masuala ya kufikia hatua ya kuwaadhibu kwa kutumia mikono, kwa kuwapiga lakini kubwa zaidi la mwisho ni la mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano wa hivi karibuni ningeomba Wizara ifuatilie suala hili. Mimi niko nyuma yake nalifuatilia lakini ningeomba Wizara tushirikiane wote kwa pamoja kufuatilia mauaji ya hivi karibuni kabisa yaliyofanyika katika Kata ya Ligunga lakini ni kijiji cha Ligunga hasa zaidi kwa kupitia Polisi na kushirikiana na Wizara ya Utalii, itafute chanzo cha mauaji yale na wale wote waliohusika waweze kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushirikishaji hatuwezi kuliepuka, bila kushirikisha wananchi katika maeneo ambayo yako karibu au jirani na mbuga zetu au mapori yetu, maendeleo au mafanikio hayataweza kupatikana kwa sababu watumishi wapo wachache

na uwepo wao katika maeneo husika hauwezi kukidhi haja ya kuweza kulinda maliasili hizi, ya kuweza kuzitunza, wenye dhamana wanakuwa ni wananchi kwa sababu wao ni wengi na wao ndiyo wako jirani kabisa na mali hizi ambazo tunazo. Kwa hiyo, tuweze kuwatendea vema na kuwatendea haki, tusiwaonee na tusiwadhulumu, katika namna hiyo tunaweza kuwafanya wakashiriki vizuri zaidi katika jitihada za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushuru sana na sasa namwita Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye na ndiye mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza na kuchangia machache kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wizara nzima wakisaidiwa na Makatibu Wakuu na watendaji wengine kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya hivi sasa, tunaona nuru ya Wizara na ninaamini kabisa kutakuwa na changamoto nyingi lakini najua wako tayari kuzirekebisha ili pato la Taifa liweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka, naomba nichangie mambo mawili tu. Kwanza, ni utalii wa ndani. Ninaomba kusisitiza sana juu ya utalii wa

ndani. Hivi sasa nchi yetu ni kubwa sana na tunaweza tukafanya mambo mengi sana ndani ya nchi yetu. Kama tutaendelea kutegemea utalii wa nje, siku moja kwa kweli tutakwisha kwa sababu mambo yanaweza kutokea huko nje yakakwamisha utalii wa nje kuweza kufanyika katika nchi yetu, tunaweza tukafika mahali tukakwama kiuchumi. Kwa hiyo, naomba sana tujaribu kuandaa wananchi wetu ili waweze kujiandaa kwa utalii huu ambao tunaweza kuutawala sisi wenyewe kwa mfano *cultural tourism* ambayo sasa hivi inapanda chati kwa nguvu sana tunaweza tukapata mapato makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna milima ambayo sisi wenyewe tunajivunia, tunayo milima mingi sana ambayo inaweza ikahifadhiwa lakini wananchi wakaweza kuitunza ikawa ni milima ya kuvutia. Kwa mfano, Milima ya Uluguru, ni milima inayovutia sana tena sana lakini tumeacha ikiangamia. Ile milima ingeweza kutumika sana kwa utalii. Pia kuna *Livingstone Rangers* ambazo zipo kandokando ya Ziwa Nyasa, milima ile inavutia sana lakini tumeiacha tu wala hakuna mtu anayeifuatilia. Kwa hiyo, naomba sana utalii wa ndani tuukazanie na tuweze kuusisitiza na nchi yetu iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nizungumzie suala la hifadhi ya misitu. Nchi yetu ni kubwa sana na ina misitu mingi. Hivi sasa ninavyozungumza misitu au mapori ambayo yalikuwa katika maeneo ya *public lands* yote imekwisha, miti imekatwa, watu wamechoma moto na hakuna kiongozi ambaye anakemea jambo hili. Naomba tuungane, tuungane

Watanzania na viongozi tukemee jambo hili kwa kufuata sheria za nchi ambazo zinakataza kukata mapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nina mfano mdogo. Mimi nasafiri sana kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya kwa gari. Ukianza safari kutoka Mikumi kuelekea Ruaha, huko nyuma kulikuwa na mapori mazito sana ambayo yalikuwa ni misitu ambayo huwezi kupita ukaona hata mtu akitembea lakini hivi sasa watu wengi wamehamia katika eneo lile si kwa sababu nyingine yoyote na si kwamba wamekosa maeneo ya kuishi lakini wamehamia kule ili kwenda kukata miti tu na zao lao kubwa ni mkaa. Wamesambaa katika maeneo yale, wanakata miti hovyo, hakuna anayewakemea, miti imekatwa na unaona kila mahali ni mwanga mtupu. Sasa tunafanya nini na wale watu, kwa kweli hawalimi kazi yao ni kukata miti tu, hivi Serikali haioni? Hivi sisi viongozi hatuoni? Ninaomba sana wale wananchi na ninafahamu kila mtu ninapozungumza kwa yeyote anayesafiri kwenda Mbeya au Songea na kadhalika analifahamu hilo pori ninalolizungumzia. Wale watu warudishwe kwenye vijiji vyao, wametoka kwenye vijiji vyao kwenda kwenye maeneo yale ya Milima ya Ruaha kwenda kukata miti na kumaliza maeneo ya mapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuungane na ninataka niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba hapa Bungeni sisi Wabunge wachache tumeanzisha Chama cha Marafiki wa Mazingira ambacho tunataka Wabunge tuungane tuzungumzie

suala hili na tubaini ni matatizo gani ambayo nchi yetu inakabiliana nayo kuhusu hifadhi ya mazingira. Tutatoka na tutakwenda katika maeneo mbalimbali hata kama ni mambo ya *capacity building* tukayafanye kama Wabunge watu watashtuka. Ninaomba mtuunge mkono kwani hii ni vita kubwa sana, tuangalie nchi yetu inavyokwisha ili tuweze kuitetea na tuweze kwenda mbele na hifadhi ya mazingira iweze kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, naiomba na kuishauri *TANAPA* kwamba kwa kuwa kiwanja cha ndege cha Mbeya kinakaribia kuisha, ninaomba waanze kuyabaini maeneo ambayo sasa yataanza kuwa ni maeneo ya vivutio ili watalii nao sasa waanze kwenda Kusini Nyanda za Juu. Kule kuna vivutio vingi sana lakini nitataja vichache. Ukienda katika Wilaya inayoitwa Rungwe, kuna vivutio vingi sana, kuna maporomoko, kuna chemchem, maziwa ya asili yaani *Crater Lakes* na kadhalika, watalii wangependa kuona maeneo hayo. Naomba muanze kuyatangaza maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna milima ya Livingstone Makete ambayo kila siku Wabunge wanazungumzia, kuna maua ambayo hayako huko duniani na sehemu nyingine yoyote ile. Tuyabaini yale maeneo ili watalii waelekezwe huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna eneo la Mbuga za Wanyama za Ruaha ambalo na lenyewe sasa limeshakuwa ni eneo kubwa sana la hifadhi na ni eneo ambalo litakuwa ndiyo hifadhi kubwa sana katika

Tanzania. Hebu tujaribu kulitangaza lile eneo. Ile mbuga ni kubwa na wananchi wale ambao wako kandokando ya mbuga zile wengine wanatoka kwa Mheshimiwa Lukuvi, wengine wanatoka Mbarali, wengine wanatoka kati ya Iringa na Mbeya nao watafaidika sana na mbuga ile kwani imeshakuwa ni mbuga kubwa yenye wanyama wengi ambao si rahisi kuwaona katika maeneo mengine. Anzeni kuyabaini hayo maeneo ili yaorodheshwe na kuyaangalia namna yanavyoweza kutangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Hilda na huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho na sasa kuna matangazo ya wageni.

Kuna wageni 52 wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai ambao ni Wanakwaya kutoka Kwaya ya Tumaini ya Mt. James – Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna wageni wanne wa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara ambao ni wataalam wa michezo kutoka Idara ya Mafunzo Chuo Kikuu cha Clemson Marekani, Prof. Kenethy Beckham, Prof. Shella Beckham, Bi. Augustino Makayo na Bwana Lenard Thadey. Walikuwepo lakini naona wameshatoka. *(Makofi)*

Pia, kuna wageni watano wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni familia yake wakiongozwa na mdogo wake Margareth Matiko, hongereni sana kwa kuja Dodoma. *(Makofi)*

Pia kuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo nao ni wanafunzi 80 pamoja na Walimu wao kutoka chuo cha *VETA* Dodoma ambao ni majirani zetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia kuna wageni wa Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kutoka Mbeya-Ipinda nao ni Ndugu Issa Mwaisumo, Ndugu Bernard Mwaijepule na Ndugu Erasto, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa namkaribisha Naibu Waziri, una dakika 20 na Mheshimiwa Waziri atakuwa na dakika 55.

Waheshimiwa Wabunge, tunamaliza saa saba.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la mpaka kati ya Ngorongoro na Karatu, bado kuna mgogoro unaoendelea kati ya mipaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Wilaya ya Karatu Wizara ikae na wadau kwa pamoja kushirikiana ili kumaliza tatizo hilo kwa kuwa mamlaka ya Ngorongoro imekuwa ikiongeza mipaka bila kushirikisha wananchi jambo linalopelekea mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ulipaji wa *gate fee* ulioanzishwa ni mzuri, lakini malipo hayo kwa wageni ni sharti yafanyike *bank* kwani ndipo *electronic system* ilipo na kwa kuwa *bank* zetu nchini mwisho wa *week* hazifanyi kazi, kufungwa huku kunapelekea usumbufu mkubwa kwa wageni. Nashauri mashine hizo na *system* za ulipiaji ufanyike siku zote bila kujali *weekend* na pia huduma itolewe geti la kuingilia, Ngorongoro badala ya sasa huduma mpaka mgeni alipie *bank* zilizo Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Game rangers,* kumekuwa na malalamiko mengi toka kwa wananchi na madereva *tours* wanaopeleka wageni ndani ya hifadhi wakiwalalamikia kuwa-treat vibaya, tofauti na utaratibu wa *game reserve*. Mfano mzuri ni tatizo lililotokea Tarangire *National Park* tarehe 2/7/2012. Tunamshukuru Waziri kwa hatua alizochukua, tunashauri uchunguzi ufanyike zaidi na pafanyike mabadiliko ya mfumo na utendaji wa kazi wa *game rangers* hao ili kuondoa usumbufu kwa wageni, tunatambua kazi yao ya kulinda wanyama na hifadhi kwa ujumla lakini maadili na umakini uzingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyongeza ya mishahara kwenye sekta ya Utalii, wafanyakazi katika sekta ya utalii wanapata mishahara duni bila kuangalia na kujali elimu ya mhusika na au aina ya hoteli kama ni *one star au five star,* lakini pia hakuna hela za likizo jambo ambalo huonesha kuna ukiukwaji wa sheria za kazi. Tunashauri pawepo na mwongozo maalum katika sekta binafsi kuhusu ajira ambao utaendana na sheria za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu katika mahoteli ya kitalii, waliokuwa wafanyakazi katika mahoteli ya kitalii yaliyobinafsishwa wanalalamikia kutopata kiinua mgongo na wamefanya kazi takribani miaka kati ya 25 – 33. Baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wa Lake Manyara hoteli ni miongoni mwa wafanyakazi wanaolalamika. Nashauri Wizara kuwalipa wafanyakazi hao ambao wametumika kulihudumia Taifa hili bila kupata kiinua mgongo kwa miaka yote ya utumishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utozaji wa kodi uwanja wa *KIA* – Moshi, watalii wengi hupanga safari zao kuja Tanzania lakini hawashukii uwanja wa *KIA* kutokana na gharama kubwa, hivyo hushukia Nairobi na kufuatwa na magari huko, Wizara itazame jambo hili kwa kuongea na makampuni ya ndege ili kupunguza gharama jambo ambalo litaongeza mapato ya nchi, lakini kuwahakikishia wageni usalama wa safari yao hivyo tutaendelea ku-*maintain* watalii wanaokuja nchini.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unaliingizia Taifa letu asilimia 25% ya fedha za kigeni na asilimia 17.2% ya pato la Taifa. Kwa mazingira hayo utalii una umuhimu wa kipekee katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina mbalimbali za utalii ikiwemo utalii wa fukwe, uwindaji wa wanyamapori, upigaji picha wa wanyamapori na utalii wa mali kale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ni muda mrefu imeendesha biashara ya utalii wa picha kwa kutoa leseni, yanapatikana mapato kutokana na leseni hizo, imefika wakati Wizara kuangalia upya hawa watalii wanaokuja kupiga picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana wako watalii wengine wanapiga picha kwa lengo la kumbukumbu za ujio wao hapa nchini, lakini wako wengine wanakuja piga picha kwa lengo la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko filamu inayoitwa *Lionking* ambayo imetayarishwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika mandhari ya Nyasirori, filamu inaonesha hali ya wanyama katika mbuga zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa waliotayarisha filamu hii wamelipwa dola za Kimarekani 36 milioni na filamu hii mauzo yake duniani imefikia dola za kimarekani nne billioni, Serikali yetu haikupata na haipati chochote kutoka kwenye mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda wamepata fedha kwa filamu kama hiyo iliyopigwa nchini kwao. Msingi wa kupata fedha kutokana na filamu hiyo ni mambo mawili; kwanza, eneo lao wamelitia thamani na la pili lina hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ziko filamu duniani ambazo mandhari yake ni maporomoko ya Kalambo yaliyoko Rukwa. Wauza filamu hizo wanapata fedha wakati nchi yetu haipati chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili na sisi tupate fedha kutokana na filamu aina hizo itabidi maeneo yetu yathaminike na ipatikane hati miliki.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza na kuwatia moyo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji na watumishi wote kwa utendaji wao wa kutumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo baadhi ya changamoto ambazo ni vema Wizara ikazifanyie kazi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa lengo la saba la milenia la uhifadhi na uendelezaji wa mazingira endelevu katika sekta zote za misitu, Mbuga za Wanyama, (vivutio vyote vya utalii) Mlima Kilimanjaro, Makumbusho ya Taifa na kadhalika, Tanzania je, tumefikia asilimia ngapi ya utekelezaji wa vipengele vya lengo hili katika sekta ya maliasili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma zinazotolewa na wapanda Mlima Kilimanjaro ni hafifu sana hasa vituo vya Mandara, Horombo na Kibo. Huduma kama vile sehemu za kuogea, vyoo, maji baridi, umeme wa *solar* na kadhalika hazitoshelezi. Mfano, mtalii anayepanda mlima kwa siku sita bila kuoga. Ni aibu! Menejimenti ipatiwe mafunzo ya kisasa ya kutoa huduma kwa wateja kulingana na ada wanayoitoa ambapo ni zaidi ya $ 1,026 kwa kila mtalii mpanda mlima. Pia kuweza kuhimili kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma wa Watanzania kuhusu umuhimu wa kuthamini viumbe hai na hasa kulinda hifadhi ya mbuga zetu na umuhimu wake kwa uhai wa binadamu kwa kuwa kila kiumbe hai hutegemeana na mwenzake.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa nchi yetu yenye kila linalowezekana kujitangaza huko nje huwezi kupata faida za vivutio vyote vya utalii tulivyonavyo kama nchi yetu na vivutio hivyo havijulikani huko nje, ukiwa nchi za nje ukasema unatoka Tanzania watu wengi hawajui Tanzania iko wapi na ni nini, wengine wanajua kuwa Serengeti na Kilimanjaro vipo Kenya. Hii ni fedheha! Ni bora tutumie fedha kiasi kujitangaza na kutangaza vivutio vyetu vya utalii ili tuongeze watalii na kwa kufanya hivyo tutaongeza mapato ya Taifa letu kutokana na utalii. Tuna vivutio vingi sana ambavyo havitumiki kikamilifu na havituingizii mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tudhibiti wanyama waharibifu, Bukoba limekuwa eneo ambalo tembo wamekuwa wakivamia mashamba na makazi ya watu mara kwa mara. Lazima tufanye jitihada kuondoa baa hili.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, sina budi kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Kagasheki na Naibu wake Mheshimiwa Nyalandu kwa kazi ambazo wanazifanya katika kipindi kifupi tu ambacho tangu waingie katika Wizara hii tumeona ni namna gani wanavyojituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni moja kati ya taasisi muhimu katika kuchangia pato la Taifa. Wizara hii ndio jicho la nchi kwani ndiyo ambayo inahusika na historia ya nchi, utalii uliomo nchini pamoja na vivutio, kumbukumbu, majengo ya historia, lakini pia Nyara za Serikali pamoja na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya kihistoria ni kumbukumbu yoyote ya majengo, kama vile nyumba, makaburi au ngome yenye umri wa miaka mia moja au zaidi na ambayo yana umuhimu fulani kiutamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara bado haijajikita vizuri katika eneo hili, ambapo eneo hili linaweza kusaidia utalii wetu, uchumi kukua. Vile vile eneo hili lina uwezo wa kusaidia pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 15 kutokana na ukuaji wa utalii, wageni wengi hupendelea kujua historia za mambo ya kale ama kuangalia urithi huu wa utamaduni ambao tunauita unaoshikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atupe maelezo ya kina ni kwa namna gani eneo hili linasuasua pia atupatie maelezo ni maeneo gani ambayo Serikali imeyasajili kama ni urithi wa utamaduni unaoshikika ili na sisi tuelewe.

Mheshimiwa Spika, suala la malikale nalo lina umuhimu mkubwa katika sekta nzima ya utalii na eneo hili pia linasaidia kukuza uchumi wa nchi kutokana na watalii na wageni kutaka kufahamu historia zinahusika na hili. Ni vyema Waziri atueleze ni kwa nini malikale haijapewa kipaumbele katika Wizara yake na atueleze

maeneo ambayo yameainishwa kulingana na kanuni na sheria za Serikali zinazosimamia malikale nchini.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu kwa sababu tumebarikiwa kuwa na maliasili yenye uanuwai wa kipekee duniani, na tukipanga mipango yetu vizuri kama Taifa tunaweza kupata kipato kikubwa kupindukia, si kutokana na utalii tu ( wa utamaduni, mazingira na makumbusho), bali pia kutokana na uwindaji, ufugaji nyuki, mazao ya misitu na kadhalika. Je Serikali imeweza kutumia fursa zilizopo za kupata kipato kikubwa kutokana na maliasili zetu? Ni kweli kuwa katika miaka 50 iliyopita toka tupate Uhuru, kiasi fulani cha juhudi kimeonekana lakini si kama ilivyotarajiwa. Baadhi ya vikwazo ambavyo baadhi vimetajwa na Waziri ni pamoja na bajeti isiyotosheleza, ubinafsi wa baadhi ya watumishi waandamizi na ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya majukumu ambayo Wizara inapaswa kutekeleza ni haya yafuatayo:- kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na rasilimali za wanyamapori na misitu, kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji miti, uvunaji na udhibiti wa moto, kuboresha miundombinu ndani ya hifadhi, kuhifadhi mazingira, kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta, kukuza utalii wa kiutamaduni, mazingira na makumbusho, kudhibiti wanyamapori wasiharibu mazao ya wakulima au wasiwashambulie na kuwaua watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya ni mengi juhudi zinazoelezwa katika hotuba ya Waziri hazitoshi, na ni dhahiri katika maeneo kadhaa tatizo ni ufinyu wa bajeti lakini tatizo kubwa zaidi ni kuwa yaelekea hakuna mpango kabambe ambao ni endelevu wa kuhakikisha kuwa majukumu hayo yanatekelezwa kikamilifu na kwa uwiano katika kila Wilaya. Nitatoa mfano wa Wilaya mpya ya Bukombe, (Jimbo la Bukombe) kuonesha kuwa mengi ya majukumu haya hayajatekelezwa au utekelezaji wake ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na kunufaika na rasilimali za wanyamapori wa misitu; kwa kweli watu wa Bukombe hawajaona manufaa kutokana na wanyamapori. Hifadhi iliyopo ya Kigosi amepewa mwindaji mtalii, lakini kwa mahesabu yaliyo katika hotuba, ukurasa 60 Bukombe (ya zamani, yaani Wilaya ya Bukombe na Mbogwe) mwaka 2010/2011 ilipata sh. 2,204,145.81; mwaka 2011/2012 sh. 1,554,581.95 na makisio kwa mwaka 2012/2013 ni sh. 2,667,016.43, huku ndiko kunufaika? Badala ya kuendelea na hali hii ingefaa kabisa kuanzisha mbuga ya wanyama katika eneo la Hifadhi ya Kigosi kwa sababu mbuga huwa ina faida sana kuliko hali ilivyo. Je, Serikali iko tayari kuanzisha mbuga ya wanyama katika eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majukumu mengine hayajatekelezwa Bukombe. Hakuna utaratibu endelevu ambao ni shirikishi wa upandaji miti, uvunaji miti wala udhibiti wa moto. Miti inakatwa ovyo kwa ajili ya mbao na mkaa au matumizi mengine na wala hakuna udhibiti wa mioto. Mfano mzuri wa uvunaji ovyo ni Hifadhi ya Halmashauri ya Bukombe

ambayo siku hizi miti inaonekana tu pembeni mwa barabara, lakini ukiingia ndani ya hifadhi unakuta ni kweupe kabisa miti ilishavunwa kwa ajili ya mbao na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitajielekeza kwenye mada ya uendelezaji wa ufugaji nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta. Tanzania ina makoloni takribani milioni 9.2 ya nyuki na ina uwezo wa kuzalisha tani 138,000 za asali na tani 9,200 za nta. Lakini sasa hivi inazalisha tani 4,860 za asali na tani 340 za nta. Kwa hiyo, hata hapa juhudi za Wizara hazijaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji nyuki ni shughuli isiyohitaji mtaji mkubwa sana mathalani, huko Bukombe mizinga ya asali (ya miti) bei yake ni sh. 6,000/= kuanzia kutengeneza hadi kuuning'iniza kwenye miti. Kwa mizinga 100 mtu anahitaji sh. 600,000/= tu iwapo msimu wa uvunaji ni mzuri, kila mzinga ulio salama huzalisha asali isiyopungua lita 10, kwa misimu miwili ni lita 20. Kwa hiyo, kwa mwaka mfugaji wa nyuki mwenye mizinga 100 anaweza kupata lita 2000 za asali. Kama atauza asali yake kwa sh. 8,000/= kila lita, pato lake litakuwa shilingi 16,000,000 kwa mwaka, kabla ya kuondoa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu kwa Serikali ni kwamba, ikazanie sekta ndogo ya ufugaji nyuki kwa kupanua Chuo cha Nyuki cha Tabora na kuanzisha shahada za Uzamili *(M.A)* na Uzamivu *(Ph.D.)* za ufugaji nyuki katika Chuo Kikuu cha Sokoine ili kuongeza wataalam wa ufugaji nyuki. Wataalam hawa watasaidia katika kutoa elimu kwa wananchi

kuhusu ufugaji wa nyuki na pia kufanya utafiti katika njia bora za ufugaji na magonjwa ya nyuki. Mathalani kuna kupe wa nyuki aina ya *Varroa destructor* ambao huwaathiri nyuki wakubwa na huua watoto wa nyuki. Hawa lazima watafitiwe ili njia bora ya kuwadhibiti itafutwe. Kadhalika, mbinu za kizamani za ufugaji ziboreshwe na pia za kisasa zianze kutumika kwa watu wanaoweza kumudu gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, maliasili tuliyonayo ina uwezo wa kutupatia kipato kikubwa. Sikuzungumzia utalii kwa kuwa Wabunge wenzangu wamezungumza vya kutosha. Ila kwa kuwa mimi ni Mtaalam wa Isimu (Sayansi ya Lugha) nitatoa pendekezo moja tu katika eneo hili. Serikali iandae mkakati kabambe wa kufundisha vijana lugha mbalimbali (mfano, Kijapani, Kijerumani, Kifaransa, Kihispania, Kireno, Kiarabu, Kichina, Kirusi na kadhalika). Ili waweze kutangaza utalii wetu wa kitamaduni, mazingira na makumbusho na uwindaji wa kitalii. Bila kuwa na kundi la watumishi wenye ujuzi wa lugha mbalimbali itakuwa vigumu kuwavutia watalii wengi hapa nchini. Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika utangazaji wa utalii ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri kwa kuchukua hatua ili kupunguza ufisadi katika sekta hii. Nashauri kuwa wakubali maoni mbalimbali pamoja na yale ya

Kambi Rasmi ya Upinzani, ili kuhakikisha kuwa sekta hii inawanufaisha Watanzania wote.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita sana katika hifadhi ya misitu; katika Wilaya ya Geita tunayo hifadhi ya misitu, lakini kutokana na shughuli za kila siku za kibinadamu kama vile kuchoma mkaa inasababisha misitu hii kuteketea. Ninachoomba Wizara ya maliasili iweke mkakati wa kutoa elimu ya mara kwa mara (program endelevu) kuwaelimisha wananchi kuhusiana na umuhimu wa kutunza misitu. Hii itapunguza uharibifu wa misitu. Vile vile Serikali iandae utaratibu mahususi katika Halmashauri kuwa na Mfuko Maalum wa misitu kwa ajili ya kuandaa miche ya miti itakayouzwa kwa bei nafuu ili wananchi wahamasike kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni ufugaji nyuki; kwa kuwa ufugaji nyuki ni chanzo cha mapato kwa wananchi wetu. Naomba Serikali iwekeze katika kuwaelimisha wananchi hasa Wilaya ya Geita namna bora ya ufugaji nyuki. Wananchi hasa vijijini hawana utaalam wa ufugaji nyuki, tunaomba Serikali iajiri wataalam wa nyuki kwa ngazi ya kati ili kuweza kuwasaidia wananchi katika ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni changamoto kutokana na wanyamapori ambao wamekuwa wakivamia vijijini na kujeruhi wananchi

katika Jimbo la Busanda hasa katika Kata za Nyamalimbe na Kamena hasa katika Kijiji cha Bushishi na Ndelema kumekuwa na matukio ya watoto kuliwa na kuuawa na fisi wala watu. Tatizo hili limekuwa ni changamoto kubwa sana. Naomba Wizara ifanye utaratibu wa kuwasaka na kuwaua hao fisi ili wananchi waishi maisha ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo mambo matatu muhimu, naomba Serikali ifuatilie na kushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme naridhika sana na utendaji wa kazi wa Waziri na Naibu Waziri, mna uwezo mkubwa na kauli zenu ni thabiti na zina heshima ya kulinda au kuwakilisha heshima ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri yafuatayo:-

Wafugaji katika mbuga zetu waondolewe na pawepo utaratibu wa kuweka na kudhibiti kabisa mifugo katika mbuga kwani ni waharibifu sana na misitu mbuga na ardhi yetu, Mito sasa imekauka kabisa, miti haipandwi tunavuna tu. Wekeni utaratibu kila anayefanya biashara ya kuvuna misitu yetu lazima awe na shamba la kuendeleza misitu yetu kwa kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga za wanyama, Wilayani Nkasi ipo mbuga ya Lwanfi ambayo kwa hiyari yao wenyewe kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi walitoa Pori hilo lilikuwa mali ya Halmashauri ya Wilaya na kwamba mipaka yake irekebishwe. Naomba Wizara ione umuhimu huo ili wakati wa kuweka mipaka walizingatie hili. Vipo Vijiji vya Mkole, Paramawe, Kakoma, Mtapenda, Isale, Ntuchi, China, Kate, Kingombe Mlambo Namansi, Masolo Kabwe na vinginevyo, hasa vile vya Jimbo la Nkasi Kusini hawana eneo la kulima kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukatili wa wahifadhi, naomba Wizara itambue kuwa mauaji ya raia katika mbuga zetu za wanyama hasa wale ambao hawana tishio la kiusalama wasiwauwe raia, wasitumie nguvu nyingi na mateso yasiyo ya kibinadamu ni dhambi na sina maana kuwa wale waharibifu wasidhibitiwe la hasha! Naipongeza vile vile Wizara kwa kuwakamata wale majambazi waliotajwa kuwavamia na kuwaua watalii na kuiba vifaa na pesa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi kuna pori la akiba la Liwati, hilo pori ni eneo kubwa sana, tatizo kubwa hakuna wafanyakazi wa kutosha kabisa kudhibiti wawindaji haramu, pia wavuna mbao, pia wafugaji wa ng'ombe, ndiyo balaa zaidi. Pia hata baadhi ya sehemu zinavamiwa na wakulima, sasa hali inatisha

kabisa, maana baada ya muda hali inaweza kuwa mbaya sana kwa sababu hata wachoma mkaa wamehamia hiyo mbuga ya Liwati. Mheshimiwa Waziri hali ni mbaya tafadhali, tuongezee watumishi maana kwa sasa hilo pori liko chini ya *TANAPA,* angalia kama litabaki pori la akiba maana kuna wachoma mkaa, wapasua mbao, wafugaji wa ng'ombe na wawindaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge naona hali mbaya na ni pori zuri sana tena sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuokolee.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kusimamia Wizara hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba Wizara ishughulikie masuala yafuatayo:-

(i) Kujenga uhusiano mwema baina ya wananchi na wahifadhi wa pori la *Grumeti Game Reserve,* wananchi wa eneo hili huonesha mifugo yao Mto Rubana ambao ndio mpaka baina ya vijiji na hifadhi, ng'ombe wao wakivuka na kuingia katika eneo la *reserve* wenye mifugo wakifuatia mifugo hukamatwa kuteswa na kutozwa faini kubwa sana bila risiti, ili tuondokane na tatizo hili lazima tuweke *buffers zone* na kukomesha kabisa unyanyasaji wa wananchi

ambao uharibu mahusiano baina ya Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na unyanyasaji huo, *Grumeti Fund* imekuwa haisaidii sana maendeleo ya wananchi. Licha ya kutopewa leseni za uwindaji kwa ahadi ya kutoa fidia kwa kijiji, fidia ambayo haitolewi kwa wakati wala haiongezeki tangu ilipoanzishwa. Hali hii inakatisha tamaa kiasi cha kuomba eneo linalopatikana Bunda lipewe mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walipwe fidia kwa uharibifu wa mazao unaofanywa na tembo na kusababisha njaa. Madai ya fidia yamewasilishwa Wizarani muda mrefu bila mafanikio, Sheria ya Wanyamapori, inaweka utaratibu wa kulipa fidia ya uharibifu, lakini hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishaiomba *TANAPA* ichangie maendeleo ya Jimbo la Bunda kama wanavyofanya katika maeneo mengine. Kutokana na kupuuzwa kwa wananchi wa Bunda na Shirika la *TANAPA* tulifikia hasa kusema kama hali hii itaendelea ni bora wananchi waruhusiwe kuwinda, kwa vile wananchi hawaoni faida ya kupakana na hifadhi ya Serengeti, Mkurugenzi wa *TANAPA* anayafahamu malalamiko haya na yeye ameahidi kushughulikia suala hili, kupitia kwako Waziri naomba kukumbusha suala hili, miradi ya maendeleo ilikwishawasilishwa *TANAPA*.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri na kasi ya utendaji aliyoanza nayo baada ya kuteuliwa, naomba timu yote ya watendaji nayo iunge mkono ili kurejesha hadhi ya uhifadhi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara kwa mizinga 80 na mavazi ya kuvunia asali yaliyotolewa kwa vikundi vya ufugaji nyuki katika Jimbo la Bunda, msaada huo umeleta hamasa kubwa kwa vikundi, lakini vikundi vingine vinaomba navyo kupata mizinga hiyo ya mfano. Naomba tafadhali tupatiwe mizinga zaidi angalau mia moja ili kuvipatia vikundi zaidi. Pamoja na vifaa, naomba sana vikundi vipatiwe mafunzo, uongozi wa Wilaya mpya ya Busega imedhamiria kuifanya kuwa ni Wilaya ya nyuki. Naomba utupatie ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimesikitishwa na uamuzi wa Serikali wa kudhoofisha uongozi wa Idara ya Nyuki katika ngazi ya Wizara baada ya kubadilisha muundo. Hatua ya kuunda Wakala wa Misitu unaelekea kuimarisha uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Hivi nani atashughulikia ufugaji nyuki kwa wananchi wa kawaida? Katika ngazi ya Wizara, Idara hii imefunikwa kama kijisehemu tu kwenye idara ya Serikali, ni vipi wataalam wataweza kushiriki kwenye maamuzi muhimu ya Kitaifa na kuendeleza na kusimamia mazao ya nyuki Kitaifa na Kimataifa! Nashauri Idara ya Nyuki sasa ipandishwe hadhi katika Wizara ili iendane sambamba na kampeni inayoendeshwa na Waziri Mkuu ya kukuza sekta ya nyuki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha ahadi ya Wizara ya kuchimba mabwawa ya maji katika vijiji vya Mwabayanda, Mwakiloba na Chabutwa kwani wananchi hawana chanzo cha maji baada ya kukata mipaka kutenga pori la Kijilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wimbi kubwa la uwindaji haramu wa wanyamapori. Hata hivyo, inaweza kuwa rahisi kuwalaumu wafanyakazi bila hata kuangalia mazingira yao ya kazi. Hawa watu wamepewa dhamana kubwa, lakini mafao yao na mazingira ya kazi ni duni. *TANAPA* inaonekana kwa nje ina hali nzuri, lakini siyo kweli mishahara ya wafanyakazi iko chini, lakini kazi hii pia ina hatari nyingi wanyama wakali, nyoka, kuanguka kwenye makorongo, kuambukizwa magonjwa ya wanyama, mishale, waya za majangili na hata kupigwa risasi, lakini hakuna mtu anayewasemea. Askari akiuawa hakuna watu wanasema, jangili akiuawa utaona hata taasisi za haki za binadamu. Tatizo lingine kubwa ni kutengwa, wanaishi mahali ambapo hawawezi kukaa na wake na watoto, mfano, Mlele, Katavi ni kilomita 120 kutoka *shopping centre* ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira haya hayawezi kuboreshwa sasa hasa baada ya Serikali kuanza kuitaka *TANAPA* kulipa gawio la Serikali la bilioni 10 kila mwaka. Sasa *TANAPA* inashindwa kuongeza vifaa na kutoa motisha kwa wakazi hata faru wameuawa baada ya motisha iliyokuwa ikitolewa na shirika la uhifadhi la *Frankfuit Zoological Society* kuondolewa. Hivi sasa shirika hilo lina manufaa gani kwa Tanzania

iwapo magari hawasaidii, gereji hawasaidii, wanapeleka misaada zaidi Congo na Zambia wakati ofisi ipo Tanzania, ununuzi wa mahitaji yao ni Nairobi, sasa wana mchango gani kwa *TANAPA,* nadhani mikataba yao iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Kituo cha Wanyamapori, Lukunga lini kitajengwa? Kero ya wanyamapori imekuwa sugu Jimboni Busega. Eneo lipo, naomba utekelezaji pia kituo kitadhibiti uchungaji wa mifugo unaofanyika katika pori la akiba la Kijilishi ambao sasa umefanywa mradi wa maaskari wa kukusanyia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba usumbufu wa mipaka wa hifadhi ya msitu wa Sayaka usiendelee, mipaka inayojulikana siku zote iheshimiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho *TTB* waongezewe fedha ya kutangaza Tanzania sehemu za mambo ya kale zilizopo kwenye Halmashauri zirudishwe Wizarani ili zisimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa ujumla kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu naelekeza katika maliasili yetu aliyotupa Mwenyezi Mungu ambayo ni misitu. Hali ya misitu yetu ni tete

sana, misitu yetu inaangamizwa sana kwa ajili ya kuchomwa mkaa kutokana na umaskini uliokithiri, biashara ya mkaa imekuwa ni dili kubwa sana, watu wameingia msituni kuchoma mkaa, wanakata miti kama hawana akili nzuri. Tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limekuwa kubwa na litazidi kukua kama Serikali haitaamua kuweka mkakati wa makusudi kabisa kumaliza tatizo hili. Tatizo hili limekuwa kubwa sana na lilizidi kukua tangu Serikali ilipoamua kuongeza bei ya mafuta ya taa, bei ya umeme kupanda na kuwafanya Watanzania walio wengi kushindwa kutumia majiko ya umeme na majiko ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutaweza kuangalia upya bei ya mafuta ya taa na gharama za umeme kupunguzwa Taifa letu litaangamia kwa ukame na ukame ukizidi hata biashara ya utalii itapungua sana kama siyo kufa kabisa kwa wanyama wengi kwa kukosa chakula. Wakifa wengi wale wanaokula nyasi na wale wanaokula nyama pia watapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha biashara ya magogo na mbao zinazofanywa kwa njia ya panya nalo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upungufu huo niliouainisha, kwa maoni yangu naona ni vigumu sana kuilinda misitu yetu kama hatutatatua tatizo linalosababisha misitu izidi kuangamia, dawa naiona ni kupunguza bei ya mafuta ya taa na gharama za

umeme. Vinginevyo sitegemei muujiza wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni huo, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu anategemea kufanya nini kutatua tatizo hili ili nijiridhishe, vinginevyo shillingi hana nitazuia, lakini akiniridhisha kwa majibu mazuri sina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia Mheshimiwa Waziri kazi njema.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kwa kuanza kuunga hoja hii mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja tu ambalo napenda kuchangia katika hoja hii. Wilaya ya Masasi na Nachingwea zinaunganishwa na hifadhi ya wanyamapori ambayo inalindwa kuliko hata ofisi ya Rais. Askari wa Wanyamapori waliopo katika mbuga hii hawana tabia ya kibinadamu, wanawatesa wananchi wa Nachingwea ambao wanapita katika mbuga hii. Wananchi wakikutwa na kuni tu wanateswa sana mpaka wanaishia hospitali wakiwa na majeraha makubwa. Kweli tunawapenda wanyama wetu, lakini tusiwapende kuliko binadamu ambao ndiyo wanaowatunza wanyama hao kwa faida ya binadamu wenyewe, wanyama wapo hapa kwa ajili yetu na kinyume chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali Mheshimiwa Waziri awaonye watumishi hawa ili wajue kuwa

binadamu ana thamani kubwa zaidi kuliko wanyama tunaowatunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya kuitangaza Tanzania katika anga za Kimataifa, kuvutia watalii watembelee nchi yetu. Pamoja na pongezi hizo naomba nichangie yafuatayo:-

Sekta ya Utalii, pamoja na jitihada za Wizara tungehitaji zaidi watalii wa daraja la kwanza ambalo wataiingizia nchi mapato makubwa zaidi. Hii inakwenda sambamba na uwepo wa hoteli kubwa za nyota tano. Naomba Wizara kupitia Mabalozi wetu nchi mbalimbali wazitangaze fursa za kitalii zinazopatikana nchini ili tuongeze idadi ya watalii wa daraja la kwanza.

Uchomaji moto misitu, kuna tabia iliyojengeka kwa baadhi ya Mikoa kuchoma moto ovyo wakati wa kiangazi kwa malengo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia hii inaharibu mazingira na kuleta athari kwa viumbe wanaoishi katika misitu hiyo. Naomba Wizara itoe elimu kwa wananchi wanaoishi katika maeneo husika kuachana na tabia ya moto vichaa ili kunusuru mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa kuni na uchomaji mkaa, kama kuna watu wanaopaswa kulalaumiwa ni Jeshi la Magereza kwa kukata kuni kwa wingi kila siku kwa kuwapikia wafungwa na mahabusu wao, lakini iko mikusanyiko mingine inayotumia kuni nyingi kwa kupikia kwa mfano, hospitali zinazolaza wagonjwa na mashule yenye mabweni ya kulaza wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri watumiaji hawa wa kuni washauriwe kutumia gesi badala ya kuni hasa kwa sababu nchi yetu sasa ina rasilimali kubwa ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza matumizi makubwa ya makaa bei ya umeme ni budi ishuke sana, lakini vijiji vipatiwe gesi pia kwa bei nafuu au uwezekano wa kutumia makaa ya mawe.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maliasili inaliingizia Taifa pato kubwa sana ikiwa ya pili, lakini kwa bahati mbaya sana Wizara hii bado haijapewa kipaumbele kibajeti na mbaya zaidi hata kile kidogo kinachopatikana hakitumiki vizuri. Tanzania imebahatika kwa kuwa na rasilimali nyingi sana, lakini kumekuwa na ujangili wa wanyama. Majangili wamekuwa wakitamba kwani wamekuwa na silaha nzito, kibaya zaidi baadhi ya wananchi wamekuwa wakiwahifadhi, ni vema tuwe na uzalendo wa kulinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zetu zina watumishi wachache sana hali inayopelekea

wanyama kuvamiwa, tunaitaka Serikali ione umuhimu wa kuhifadhi mbuga zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima Kilimanjaro ni kivutio kikubwa kwani ndio kilele cha Afrika, lakini mlima huu unaelekea kukosa mvuto kutokana na theluji kupungua theluji hii ndio inayowafanya watalii wengi waingie nchini. Hata hivyo, Wizara bado haijatangaza vyema mlima huu na hata Mabalozi wetu hawajautangaza vizuri. Ni vyema basi, fedha nyingi zitengwe kupitia Bodi ya Utalii ili waweze kutangaza si tu mlima bali pia vivutio vingine. Kumekuwa na malalamiko mengi kuwa Kenya imekuwa ikiutangaza mlima huu kuwa uko kwao. Ni vema na sisi wenye mlima kuwaelezea ulimwengu kuwa mlima uko Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ni mali na kwa kweli imekuwa ikituingizia fedha lakini imekuwa chanzo cha mvua na uhifadhi wa mazingira. Ni jambo la ajabu sana kuona kitengo muhimu hivi, tena ambacho watendaji wake wana weledi wa misitu na nyuki na huku tukitambua umuhimu wa asali, Wizara imekuwa na muundo mpya ambapo kitengo hicho sasa kinakuwa chini ya Mkurugenzi wa Sera na Mipango. Hali hii itafanya eneo la misitu na nyuki kutokupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *tour operation* ni biashara nzuri inayoweza kuletea Taifa fedha, lakini ajira pia. Jambo la kushangaza *operators* wa ndani wanaambiwa wawe na magari mapya matano jambo

ambalo ni gumu sana, matokeo yake wanashindwa na hivyo kuwa na ubia au kuwapa wageani leseni zao. Hii si sawa, ni lazima kama nchi tuwawezeshe wananchi wetu kufanya kazi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze watendaji wakuu wa Wizara hii kwa kuweza kubadili haraka usimamizi wa Wizara hii muhimu. Nianze kuchangia juu ya mbuga ya Hifadhi ya Katavi iliyopo Wilaya ya Mpanda. Hifadhi hii ni kubwa na ina wanyama wengi na msitu mkubwa wenye kuvutia watalii. Lakini kumekuwepo kasoro kubwa ya kutoitangaza hifadhi hii, kwani idadi ya watalii wanaofika katika mbuga hii ni kidogo sana. Naiomba Wizara iweke mpango mkakati wa kuitangaza hifadhi hii ili iweze kupata watalii wa kutosha pamoja na kuiwezesha Serikali kupata mapato makubwa yatakayoiwezesha kutoa huduma kwa wananchi wanaoizunguka hifadhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani, utalii wa ndani ni muhimu sana ambao ukiimarishwa kwa kutoa hamasa kwenye jamii za Watanzania waweze kushiriki utalii wa ndani. Ni jukumu la Serikali kuweka kitengo maalum kwa ajili ya kushughulikia na kuhamasisha utalii wa ndani. Nchi kama Afrika Kusini watalii wengi wanaokwenda kuzuru mlima Meza (*Mount table*) uliopo *Cape Town* wengi wao ni wananchi wazawa hapo *Cape Town,* ni vyema tukaiga wenzetu jinsi wanavyoweza kuwashawishi wananchi waweze kujenga utamaduni wa kupenda kilicho chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka ya vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya *WMA* ni mkubwa sana.

Namwomba Mheshimiwa Waziri tutafakari kwa kina kuhakikisha mipaka ile ipimwe upya kwani kuna vijiji vipatavyo ishirini ambavyo kumekuwepo kelele nyingi sana ambazo zinahatarisha amani katika maeneo hayo. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aje Mpanda atembelee Mpanda ili aone mwenyewe wanavyoishi katika maeneo hayo ambayo akifika naamini kabisa atatoa uamuzi yenye busara itakayowasaidia wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Kabage, Kungwi, Sibwesa, Kasekese, Kasega, Vyama na Kapala, Msenga ambavyo viko katika Jimbo langu vina mgogoro mkubwa sana wa mipaka. Wananchi wamekosa maeneo ya kufanyia kazi za kilimo na kuwafanya wananchi wawe maskini. Niombe sana Serikali ilishughulikie mapema ili tuweze kutoa kero katika eneo hilo ni pamoja na vijiji vilivyoko katika Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu ambalo linamchafua kisiasa, ni vizuri likashughulikiwa mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mwingine upo katika Kijiji cha Vikonge Kitongoji cha Igalukilo. Eneo hili linatambuliwa na Serikali ya Wilaya kama makazi halali ya wanakijiji hao ambao wameishi hapo kwa miaka zaidi ya ishirini na kuwa na uongozi unaotambuliwa na Serikali mwaka huu wamewaambia wananchi wahame katika maeneo hayo ambayo wamekuwa wakiishi na kufanya shughuli za kilimo kwa muda mrefu. Je, Serikali iko tayari kuwafidia wanakijiji hao ambao wanafukuzwa kama wakimbizi katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana busara itumike na iangalie upya ili tuwapimie mipaka hiyo upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo nitapata majibu, nitaunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa kujali kazi zao na kumsaidia Mheshimiwa Waziri kumudu kazi zake kwa wepesi na zenye mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli najali utendaji kazi za Mheshimiwa Waziri, hivyo, najua kwamba Wizara yake haimo katika shughuli za Muungano, lakini kutokana na mipango yake ya kazi, mizuri ningemshauri pia wakati wanapokuwa na vikao vya ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani angewapa utaalam wake ili na wao Zanzibar waweze kufuata nyayo zake kama alivyoelezea katika ukurasa 24 hadi 28 hasa mimi nimevutiwa na kifungu cha 57 na hayo ndio maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara muhimu hii, muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia kwa Wizara hii ihakikishe vipaumbele vitatu muhimu vinatekelezwa:-

Kwanza, raslimali za nchi hii zinalindwa na kuwanufaisha Watanzania wote.

Pili, kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi zinufaike na rasilimali za wanyamapori na misitu.

Tatu, kuboresha mazingira na makazi ya watumishi wa Wizara hii wanaoishi kwenye mazingira magumu kama vile Rungwe na Kizigho *Game Reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *core functions* tatu zikitekelezwa tutafika mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rungwe na Kizigho *Game Reserve* inachangia takriban shilingi billioni mbili, kwa mwezi kwenye pato la Taifa, lakini cha kusikitisha ni fedha kidogo sana inayorudi kuboresha mapori haya ya akiba. Wilaya ya Manyoni mwaka huu imeambulia shilingi 98 milioni tu kutoka Idara ya Wanyamapori. Matokeo yake hakuna *impact* yoyote kwenye maendeleo ya vijiji vinavyozunguka mbuga hizi. Naishauri Wizara hii ifanye makusudi kutoa fedha za kutosha kuchangia kwenye maendeleo ya maeneo haya. Aidha, napendekeza wazo la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori litekelezwe, liliahidiwa, lakini hadi leo hakuna nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa mapori ya akiba ya Rungwe na Kizigho na Mhesi wanakabiliwa na matatizo makubwa ya upungufu wa vitendea kazi na magari ya doria, fedha za kuendesha shughuli za hifadhi za mbuga hizi. Naiomba Serikali ichukue

hatua kurekebisha hali hii. Pia namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake watembelee Rungwe na Kizigho na Mhesi wajionee wenyewe hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliiomba Wizara itoe kibali kwa wananchi wa Kata ya Upande wanyweshe mifugo yao kwenye mabwawa ya Itwaga na Kengelege, hadi leo maombi hayo yapo Wizarani bado hayajashughulikiwa ingawa wataalam ngazi ya Mkoa na Wilaya walipendekeza kuwa inawezekana. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maombi ya Kijiji cha Lulanga kupanua mpaka wa Halmashauri ya Kijiji hadi leo hakuna majibu yoyote. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Rungwe mpaka leo hii bado halijakarabatiwa, baada ya kuharibiwa na mvua za mwaka 2008 na *TWPF* kutenga shilingi milioni 200 kwa kazi hiyo, kulikoni? Naomba majibu.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza Waziri, watendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla kwa jitihada kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu cha CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na kwa umuhimu naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu hatima ya wananchi wa Nzasa Chanika wanaonyanyaswa na watendaji wa Wizara yake licha ya kuwa Wizara ya Ardhi ilishatoa uamuzi kuwa mpaka uliopo kwenye ramani ya awali ndio unaotakiwa kufuatwa. Kwa kuwa Serikali ni hiyo hiyo moja, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na uamuzi wa hatima ya mipaka ya Msitu wa Kazimzumbwi na wananchi wa Chanika ili wananchi wajue na kupata fursa ya kuendelea na shughuli zao za kiuchumi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri Mheshimiwa
Balozi Khamisi S. Kagasheki kwa hotuba yake nzuri, nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Lazaro Nyarandu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania idadi ya watu imezidi kuongezeka kwa kasi zaidi, lakini maeneo bado ni yale yale hayaongezeki. Huko vijijini maeneo yanatumika katika kilimo yamekwisha kutokana na ongezeko hilo kubwa la watu. Hivyo, naomba Serikali ilete Muswada Bungeni, ili Bunge liweze kufanya marekebisho ya sheria kusudi maeneo ya mipaka ya hifadhi yasogezwe kusudi wananchi waweze kupata maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Naamini dhamira yao njema ya kuwakomboa Watanzania kutoka katika ukandamizwaji unaopelekea sekta ya utalii nchini kutokuwa yenye mchango mkubwa katika kuongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimechelewa kuomba kuchangia kwa kuongea, basi naomba nitumie nafasi hii kuiomba Serikali ikaribishe wanamichezo wakubwa duniani. Mfano, David Beckham alitembelea Liberia kuhamasisha kuijenga nchi ile baada ya vita, lakini hali hiyo ilivutia sana watalii kuitembelea Liberia na alipohamia *Real Madrid* nchini Spain watalii wengi hasa Waingereza walimiminika Spain.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yetu ijitahidi kufanya hivyo kusudi tuzidi kukuza utalii nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga hoja mkono.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni sekta muhimu sana kuliko

inavyochukuliwa na Serikali. Ni vyema Serikali ikaipa umuhimu wa pekee sekta hii maana ni mlango unaoweza kutumika na ukaongeza uchumi wa nchi kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wizara na Bodi ya Utalii kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA)* na *TANAPA* wakishirikiana na wadau wengine na kushirikisha Balozi zetu za nchi ambazo zina watu wapenda utalii, tukaweka maofisa wa kushughulikia utalii tu, kwa kuuza nchi yetu (*marketing)* ili iwe kazi na kutafuta soko la kutosha, ikawekwa mikakati ya kuvitangaza vivutio vyetu vya nchi nzima katika sehemu hizo duniani, mpaka sasa tumekuwa tunategemea watalii waje na wakishaondoka watangaze utalii wetu, hiyo siyo njia sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara sasa ivumbue masoko mapya kama vile Korea Kusini, China, Japan na India na hata soko la ndani liangaliwe upya, hata soko la ndani ni kubwa kama elimu ya kutosha itatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa wanyama hai kupelekwa nje ya nchi, suala hili lichukuliwe kama uhaini.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara izingatie utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwani una dira nzuri

sana. Ukurasa 77, malengo ya utekelezaji *coperational objectives* mawili kati ya manne yanasomeka:-

(a) Kuimarisha menejimenti ya maliasili, malikale na shughuli za utalii; na

(b) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato ya Serikali yatokanayo na maliasili, malikale na shughuli za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, hatupaswi kuwa na changamoto ya kibajeti (100%) katika utekelezaji wa hapo juu. Kwa hiyo, tunatakiwa kuboresha tulivyonavyo, lakini wakati huo huo kubuni vipya, wakati wenzetu katika nchi nyinginezo wanakalia kutafuta vivutio Tanzania tunavyo tele je, tunavitumia kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pori la akiba, Selous, sifa za Selous ni kubwa sana:- ni pori kubwa kuliko yote Afrika (*literature* nyingine zinasema ni ya pili), lina wanyama wakubwa zaidi ya milioni moja, lina msitu, mimea na kadhalika ambavyo ni vya pekee vinavyotosha kuvutia utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya pori hili liko katika *remote area,* halifikiki kwa urahisi kutokana na ukosefu wa miundombinu, Serikali imejipanga vipi kuondoa tatizo hili? Serikali itangaze vivutio vya Selous, Selous inahitaji utawala na uongozi wake yenyewe (*autonomy or semi autonomy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya bajeti ya Wizara (ukurasa 2) ikizingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, sehemu ndogo inasema mojawapo ya majukumu ambayo Wizara imepewa ni:-

Kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na rasilimali za wanyamapori wa misitu. Serikali itekeleze kikamilifu jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Tunduru, Jimbo la Tunduru Kaskazini, Kata karibu 12 zinapakana na Selous lakini badala ya kunufaika na ujirani mwema, wananchi katika Kata hizo wanasumbuliwa na yafuatayo:-

- Matatizo ya mipaka kati ya pori na mashamba na maeneo ya kuishi kwa wenyeji;

- Mahusiano mabaya kati ya watumishi wa pori na wadau wengine *against* wananchi; na

- *Reported cases* za mauaji ya wananchi hivi karibuni katika Kata ya Ligunga, huduma za jamii kwa wananchi zinapaswa kuwa matunda ya ujirani mwema, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasababisha kukosekana kwa dhana ya ushirikishaji wananchi, hawaoni kama wao ni sehemu ya mali hii ya Taifa. Hivyo, hawashiriki kwa moyo mmoja katika kuziboresha na kuzilinda mali hizi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Ligunga, Jakika, Kaluhi, Namnyangapa, Mindu, Namingo, Muhuwesi, Sisi kwa Sisi, Masonya na Nandembo, ambazo zinapakana na Selous mipaka ipitiwe upya na kuthibitishwa kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi v/s yale ya wanyama na mauaji yakomeshwe mara moja, tunaomba maeneo hayo yasaidiwe kupatiwa huduma za jamii kama sehemu ya ujirani mwema. Jina " Pori la akiba" kwa maana ya "*Game reserve*" linahitaji kuangaliwa upya, halivutii na halileti mantiki ya utalii na kadhalika, utalii wa ndani uboreshwe kwa kufungua njia za kuingia porini kutokea maeneo ya mipakani. Njia nyingi zaidi (rasmi) zitaongeza uwezekano wa watu kuona haja ya kutembelea mbuga na pori.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri kwa uamuzi wako wa kumtuma Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kuja kujionea migogoro iliyopo kati ya wananchi wa kando kando na wahifadhi katika pori la akiba la Maswa katika Jimbo la Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Nyalandu kwa jinsi ambavyo aliweka msingi mzuri wa kutatua kero hizi ikiwa ni pamoja na kuunda Tume ya kuchunguza chanzo na suluhu ya migogoro hiyo, kulipa ng'ombe waliopigwa risasi (20) jumla ya Sh. 6,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi mahususi, fedha za fidia Sh. 6,000,000/= niende nazo ili kurejesha imani kwa wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Tume ya Uchunguzi haijaanza kazi yake, Wabunge wote Meatu na Kisesa tukubaliane *terms of reference*, tume ianze kazi mapema na kuwasilisha ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na utafiti uliofanywa katika sekta ya utalii na Dkt. Charles Kitima (*Vice Chancellor SAUT*) , biashara ya utalii inanufaisha zaidi wageni kuliko wazawa, *wildlife hunting area ni 95%* inamilikiwa na wageni, *local 5%* tu, *hotels 20%* ndizo zinamilikiwa na wafanyabiashara wa ndani, *hunting blocks 53% (foreigner),* je, kwa kuwa Taifa linawategemea sana mtafanya nini kuhakikisha kuwa Watanzania wanamilki *majority shares?* Pia je, mtakomesha vipi ujangili uliokithiri nchini katika mapori na hifadhi zetu za Taifa.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa uwindaji, bei zetu kwa ajili ya uwindaji ni ndogo sana kwa mfano, Simba mmoja akiwindwa hapa kwetu ni karibu $ 4,000 lakini wenzetu South Africa kuwinda Simba mmoja ni $ 17,000, hapa kwetu ni ndogo sana, ushauri bei hizi kwa uwindaji kwa wanyama wote ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wa Bodi kwa taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara inaonekana wengi wao hawana *idea* yoyote na sekta hizi. Ushauri wangu ni kwamba, wakati wa kuteua wajumbe wa Bodi lazima muangalie au mchague watu wenye uzoefu na uelewa wa shirika husika na tujaribu sana

kuwakwepa wanasiasa, wawekwe wataalam zaidi. Tunaona yanayotolewa kwenye Bodi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafisa wa hifadhi wanakuwa wakikaa sehemu moja kwa muda mrefu, inabidi wabadilishwe ili kupunguza rushwa katika sehemu husika hata kuruhusu nafasi ya kutorosha nyara za Serikali.

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanyika, naomba kutoa ushauri kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kisarewa ina mbuga ya Selous kutoka *Airport* mpaka Selous ni muda mfupi sana kwani kilometa 120 tu. Naiomba Serikali iweke utaratibu wa kitalii katika eneo la Wilaya ya Kisarewa kwa mbuga ya Selous ili kukuza uchumi wa Wilaya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu wa Kazimzumbwi ni muhimu sana kwa kupunguza hewa ya ukaa kwa Mkoa wa Pwani na Jiji la Dar es Salaam. Naiomba Serikali ilinde msitu huu kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi walikuwa wakijihusisha na biashara ya kuuza wadudu nje ya nchi, naiomba Serikali iangalie upya katazo la kutouza wadudu nje ya nchi kwani limenyima ajira vijana wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ianze utalii wa Bahari kwani una tija kubwa sana kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa kitongoji cha Mwambisi waliotolewa bila kulipwa fidia limeleta usumbufu sana kwa wakazi hao, kwani kitongoji kinachotambuliwa na uongozi halali ( GN 250) kufukuzwa wananchi hai kaya 140 bila kulipwa fidia, kimeleta usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Kagasheki pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Nyalandu. Pia nampongeza bibi Tarishi Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *fence* kuzunguka makumbusho ya Majimaji imekamilika, lakini Mkandarasi hajalipwa hela yake. Ni vema deni hilo lilipwe mapema, ni kero kwa kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa umedhaminiwa kufungua utalii wa Kalambo *falls,* kwani Zambia wenzetu kasi yao ni kubwa, tunahitaji kupima maeneo ya hoteli, *air strip* na mambo mengine yanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msaada wa *ticket* ya ndege kwenda na kurudi kwa watu watatu tu kutembelea *Victoria falls/livingstone falls* ili kujifunza kilichofanyika. Hii ni kwa ajili ya Maafisa Mipango wetu pamoja na Maafisa Ardhi. Pia tutaomba ufadhili wa kitaalam pamoja na pesa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Kalambo ni mpya haina vyanzo vya kutosha vya mapato zaidi ya kutegemea kodi ya mazao ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu inayohusu hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Pamoja na kuunga mkono Wizara hii bado ina changamoto nyingi ambazo zinahitaji kuangaliwa na hatimaye kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto hizo ni uharibifu mkubwa wa misitu yetu hasa katika Wilaya ya Rufiji. Wilaya hii kwa kiasi kikubwa ilikuwa na misitu mikubwa ya asili ambayo kwa sasa imepotea kabisa pamoja na jitihada kubwa zinazofanyika za kuzuia ukataji magogo na miti unaofanywa kwa kushirikiana baina ya Wizara na Halmashauri ya Wilaya Rufiji, bado ukataji unaendelea. Ni vizuri kwa Serikali ikaendelea kuweka doria ili kuhakikisha kuwa miti iliyobaki inaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali Wilaya hii ina miti mingi, lakini siku hadi siku miti inakwisha. Pamoja na ukataji magogo kwa ajili ya mbao, kumezuka ukataji mbaya zaidi wa miti unaotokana na kundi la wakataji na wachomaji mkaa maarufu kama *Wamalila*. Kundi hili ni kubwa na hawachagui mti wa kukata, wanakata miti yote iliyo mbele yao hasa Kata ya Dimani ambayo kwa sasa imeanza kuwa jangwa. Halmashauri ikishirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji inajitahidi kuzuia kundi hili, lakini bado hawana nguvu ya kutosha. Utashangaa ukiliona tanuru la mkaa linatoa gunia mpaka 1000! Je, ni kiasi gani cha miti imekatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni nyeti sana kwa hifadhi ya misitu yetu, naomba Serikali iweke doria maalum katika Kata hii ili jangwa lisiweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu hifadhi ya *Selous* (*Selous Game Reserve*). Hifadhi hii kubwa kuliko yote hadi sasa haina manufaa makubwa sana kwa nchi yetu pamoja na utajiri mkubwa iliyonayo. Hii inatokana na hifadhi kutokuwa na Mamlaka yake. Naiomba Serikali iangalie upya hifadhi hii kwa kuipatia Mamlaka ili iwe na Bodi maalum itakayoratibu namna ya kuiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa siku ya kupanda miti kwa kiasi kikubwa hauna tija. Kila mwaka Serikali na Halmashauri zote nchini hutumia fedha nyingi katika upandaji miti (siku ya kupanda miti tarehe moja Aprili). Kila Wilaya imeelezea namna walivyopanda miti hiyo na kujisifu kuwa tumepanda

miti elfu kadhaa, lakini miti hiyo haionekani. Naishauri Serikali siku ya kupanda miti itumike kwa kupanda msitu, kwa maana kuwa kama Wilaya inataka kupanda miti 10,000 basi litengwe eneo maalum la kupanda miti hiyo na hatimaye kuwe na watu maalum watakaofuatilia siku hadi siku utunzaji wa miti hiyo kwa kufanya hivyo fedha nyingi zinazotumika zitaonekana. Hivi sasa miti hiyo inapandwa *randomly* na wala haijulikani kama imepandwa au imeota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono bajeti ingawaje iliyopo ni tegemezi zaidi kutoka nje. Naishauri Serikali kwa kuwa Wizara hii inaiingizia mapato mengi Serikali ni vema ikapewa kipaumbele. Vile vile ili iweze kuboresha zaidi shughuli zinazoweza kuliongezea mapato Taifa na kukamilisha mipango ya maendeleo iliopo. Kwa kufanya hivyo tutaongeza mapato na uwezo wa kusimamia Wizara hii utakuwa mkubwa zaidi. Aidha, lipo tatizo la uharibifu wa mazingira kwa kukatwa misitu hovyo kwa ajili ya mkaa na uchomaji wa matofali, kukaushia tumbaku, chai na kadhalika. Nashauri Serikali Maafisa Maliasili na Misitu waliopo hawatoshi kufuatilia uharibifu unaojitokeza, ufanyike utaratibu wa kuongeza watumishi hao ili kazi ya kutoa elimu kwenye vijiji vilivyokithiri uharibifu iendelee kwa kuwashauri wapande miti na kuachana na ukataji miti hovyo.

Aidha wapo baadhi ya watumishi miongoni mwa hao wachache waliopo, hawatendi kazi yao kwa

uadilifu hushirikiana na Wilaya na Vijiji kukata miti na kutengeneza mkaa hii ipo zaidi kwa watumishi ambao wamekaa muda mrefu katika maeneo wanayofanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuwepo utaratibu wa kutowaacha watendaji kukaa muda wa miaka 10-20 bila ya kuhamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mungu kwa jinsi anavyonipigania na kunishindia katika maisha yangu.

Pia nampongeza Waziri kwa hotuba yake mzuri, vilevile kwa Naibu Waziri na jopo lake zima linalomwezesha kufanya kazi yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa machache ikiwa ni pamoja na kuiomba Serikali iongeze watumishi katika Wizara hii, kwani mwaka jana nilitembelea ofisi ya Maliasili ya Nachingwea, kwanza lile jengo ni chakavu sana na wala halina hadhi ya ofisi. Pia lipo pembeni mwa Mji kiasi kutokana na uchache wa watumishi, nilimkuta mhudumu msaidizi wa ofisi ambaye alinipa taarifa za uchache wao. Vile vile kwa vile ofisi ipo kando na nyumba zingine watu huona ukiwa. Hivyo, kutokana na hali hiyo ni vema Serikali ikarabati jengo hilo na kuongeza idadi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazungumzo yangu pale nilimhoji juu ya upatikanaji wa vibali vya kupata nyama. Aliniambia utaratibu ni kwamba, unapata kibali na bei ya mnyama umtakaye lakini risasi ni juu yako. Pia gharama za posho ya mwindaji ni juu yako. Nikaona kama ni hivyo hali kama hiyo haitakuwa rahisi kutoa mpenyo wa rushwa? Maana kutokana na gharama hizo kuwa kubwa kupita thamani na bei ya mnyama. Hivyo ni vema Serikali iliangalie suala hilo na utaratibu huo.

Vile vile napenda kuzungumzia juu ya hifadhi iliyopo katika Kata ya Namatutwe, Masasi. Hifadhi hii ipo karibu na vijiji. Kutokana na ukaribu huo, ndovu hushambulia mashambani kwa kuharibu mazao. Fidia Serikalini hupatikana kwa shida kwa wale ambao wanabahatika kupata. Hata hivyo, ni ndogo ambazo hazikidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde la Mto Lukuledi katika maeneo ya Nanganga kuna ardhi mzuri yenye rutuba nzuri kwa mazao ya chakula na hata kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini kuna adha kubwa ya boko. Boko hawa hushambulia sana mazao na kusababisha njaa kwa wakulima, Serikali ya Wilaya imekuwa ikilalamikiwa lakini hakuna msaada wowote. Hali hiyo imefikia hatua ya wakulima kukosa mashamba kwa kuwakimbia boko hao. Vile vile Mto huu una mamba wengi ambao karibu kila mwaka zaidi ya watu wawili huuliwa na mamba hao. Hivyo, naiomba Serikali itafute suluhisho la boko hawa ili wakulima waweze kulima mashamba yao ili waondokane na baa la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uharibifu mkubwa wa miti ufanywao na sisi viongozi. Imebainikka mahali pengi viongozi tunapasulisha mbao bila vibali. Ninao shahidi juu ya hilo. Nimewahi kudokeza kwa vyombo vya dola yaani Polisi, lakini bila utekelezaji niliwaaambia hata eneo nyumba walimokuwa wanazihifadhi tayari kwa kuzisafirisha. Siku ya usombaji nilipata taarifa kwa dereva na tajiri mwenye gari itakayotumika. Hata hivyo, Polisi hawakuchukua hatua yoyote, wahujumu hao ilidaiwa walisema kwamba, mbao hizo ni kwa ajili ya Halmashauri kwa ajili ya madawati, lakini mbao zikasombwa usiku na kuelekezwa njia ya Dar es Salaam. Viongozi hao ni wa Kata wakiwemo na Halmashauri pia. Naiomba Serikali ifuatilie hili.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Momba kulipwa fidia iliyoahidiwa kutokana na wananchi wa maeneo hayo kuliwa na mamba. Hii ni ahadi ya muda mrefu kwa takribani miaka 27 sasa. Mamba hao wakali wanapatikana katika Mto Mombo uliopita katika Kata za Kamsamba, Mkulwa, Chilulumo, Msangano, Chitete na Myunga. Hivyo basi, tunaomba kwa mwaka huu wa fedha suala hilo lichukuliwe hatua za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri hawa wapya katika Wizara hii, lakini pia niwaambie kwamba kuteuliwa kwao na kupewa Wizara hii kwao wao hii ni changamoto kwani waliopita kabla yao

walioonekana na udhaifu katika maeneo mengi na ndio maana Mheshimiwa Rais alilazimika kufanya mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe kipaumbele kwa wanavijiji ambao katika maeneo yao ya vijiji wana maeneo ya kitalii, *Game Reserve*, mabwawa ya uvuvi na hata misitu ya kuvuna mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba wananchi ambao Mungu amewajalia kuwepo katika eneo lao ambalo lina rasilimali lakini pakatokea watu ambao wanamkono wa Serikali na wakazuia kwa nguvu zote watu hawa wasifaidike na rasilimali waliyo nayo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanauawa kwa risasi na Maafisa wa Wanyamapori na baadhi kutoswa katika mabwawa yenye mamba. Inasikitisha kwamba kila eneo Mungu amejaalia na uchumi wake wa watu wa eneo hilo kwamba waishi kwa kutegemea rasilimali hizo zilizopo katika eneo hilo, lakini kama vile sio Watanzania askari hao wanawafanya kuwa "chakula cha mamba" wananchi bila kujali kwamba watu hao ndio wenye eneo hilo jambo ambalo pia linaleta kutoelewana baina ya wanakijiji na watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri aendelee na utaratibu wake huo wa kutembelea vijiji kwa lengo la kuzungumza na wananchi ili kujua matatizo yao, lakini pia jambo hili litawezesha

wananchi pia kusaidia Serikali katika kulinda rasilimali hizi lakini pia kupunguza wadau baina ya wanakijiji na watendaji, lakini pia rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linapoteza mapato mengi kutokana na utalii kutokana na kwamba watu tuliowapa jukumu la kusimamia na kukusanya mapato kwamba sio waaminifu, lakini pia wanyama wanauawa ovyo bila utaratibu kufuatwa ule wa uwindaji ulio halali, lakini watu wanajifurahisha tu kwa kuwapiga risasi wanyama na wao huona raha vile mnyama anapouawa baada ya kumpiga risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji na uvunaji wa mbao, jambo hili linaonekana kama vile hakuna mwenye dhamana katika kutoa vibali hivi, kwani vibali hutolewa kutoka kila eneo na kila ambaye ana uwezo (ni kiongozi) hujiona kwamba ana nafasi hiyo ya kutoa kibali hicho. Jambo hili linaleta utata na mizozo mingi kwa wanaohusika lakini pia wanakijiji husika kwani wao wenyewe hawapati fursa hii na bila kujali kwamba kwao misitu hii ndio rasilimali na uchumi ambao Mungu amewajalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio mambo ya kuzingatiwa na yanayohitaji kufanyiwa kazi kwa faida ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru

Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwenye wingi wa rehema kwa kuweza kutufikisha hapa tukiwa na hali ya uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni katika Bandari ya Zanzibar kumekamatwa pembe za ndovu katika makontena, ambayo yametokea Tanzania Bara, kwa udanganyifu wa kusafirisha madagaa makavu na kupeleka nchi za nje. Je, ni hatua gani wamechukuliwa wafanyabiashara wale. Nakuomba Mheshimiwa Waziri utakapofanya majumuisho, nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Kagasheki na Naibu wake Nyalandu kwa kuanza kazi kwa kasi inayoridhisha. Nawaunga mkono sana, nawaomba wafanyakazi wawape ushirikiano kama walivyonisaidia mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri yafuatayo ambayo tuliyaanza yaendelezwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Utalii, ili kutatua tatizo la uhaba wa fedha *TTB*, naomba wazo la kuanzisha Mamlaka inayojitegemea kifedha ianzishwe haraka kwa kurekebisha Sheria ya *TTB* na Sheria ya Utalii ya 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ulinzi wa maliasili kwa kuanzisha kanuni za *KDU* kama *Paramilitary Force*, kukamilisha mchakato wa kuanzisha

*TAWA*, kununua vitendea kazi vya kisasa na hasa vifaa vya doria za anga - Helikopta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* & *NCAA* kuwa na kampuni ya *hospitality*, "Bandes" za TANAPA ziboreshwe kwa kuanzishia kampuni ya kutoa huduma za *lodges* ili kuongeza mapato TANAPA na pia kuweka changamoto kwa mabepari waliopendekeza hifadhi wamekataa kuongezewa *"concession fees*" ili kufikia azma hiyo, *TANAPA* na *NCAA* isitoe ardhi, hifadhini bure kwa wawekezaji badala yake watumie ardhi hiyo kama mtaji na hivyo kuwa na hisa (*free carried stocks*) kwenye *lodges.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia heri na fanaka nyingi Waziri Kagasheki na Naibu wake na timu yote ya watendaji katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima na fursa ya kuchangia hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa ya kuchangia Wizara hii muhimu na nyeti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwateua Mheshimiwa Kagasheki kuwa Waziri na Mheshimiwa Nyalandu kuwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu mama Tarishi na *team* yote ya Wizara. Tunawaombea kazi njema katika kusimamia rasilimali yetu kupitia Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwashauri viongozi wote wa Serikali waangalie upya suala la misitu na hifadhi ya misitu. Leo hii imebaki kuwa siasa tu suala la kuhifadhi misitu yetu na upandaji miti, ukame uliopo tunasingizia tabianchi (*global warming),* si kweli (*global warming*) tabianchi, huchangia sehemu ndogo tu. Sheria za kulinda misitu na maeneo ya hifadhi ipo, haifuatwi kabisa. Kama kuna uharibifu jirani na Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya ambapo viongozi wa Serikali wanapaona kila siku na hakuna hatua wanazochukua. Waziri, Naibu Waziri hawataweza kusimamia kila sehemu ya Tanzania. Ni vyema Serikali ikaweka msimamo wa pamoja na viongozi wote wafanye juhudi kuboresha misitu yetu na wachukue hatua za kupanda miti. Tunashukuru Serikali kuanzisha na kuhamasisha suala la ufugaji nyuki, itaweza kuwapa wananchi kipato mbadala na kuacha kuvuna misitu na miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya kitaalam inayotolewa na watafiti wetu inaonesha kuwa baada ya miaka mitatu, nishati ya kuni na mkaa itakuwa adimu na ghali, kasi ya uvunaji miti na misitu ni kubwa mara tatu kuliko kazi ya upandaji miti. Itafika muda vijijini hawatakuwa na nishati na uwezo wa kununua nishati mbadala ya mafuta ya taa, umeme na gesi hawatakuwa nayo sababu ya mapato duni na kutokuwa na kipato cha kila siku. Mfano, ni kule Sao hii katika misitu iliyovunwa kuna hekta efu 40,000 bado hadi leo hii haijapandwa miti. Je, katika maeneo mengine nchini ambayo hakuna usimamizi mzuri, hakuna kabisa miti inayopandwa tunaongeza jangwa?

Maeneo ya vyanzo vya maji pia yameharibiwa sana, maji katika Mito yetu yanapungua sana na hatuoni jitihada ya kuboresha. Tunaomba hizi tafiti mzichukulie kwa umuhimu wake na zifanyiwe kazi. Naomba nichukue fursa hii kwa uongozi mzima wa Wizara na hasa *TANAPA* kwa kutukubalia Babati .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungua geti la Iyambi katika Hifadhi ya Manyara na juhudi ya kufungua geti ya Sangaiwe katika hifadhi ya Tarangire na tunaomba mwaka huu wa fedha pia mfungue geti ya Mwinkantsi (Mamire) ili kuongeza utalii Babati. Itafungua eneo jipya *(New circuit)* ya utalii, leo hii hifadhi ya Tarangire na Manyara zipo Wilaya ya Babati lakini yenyewe haifaidi kabisa utalii na mapato yote yanabaki Mkoa wa Arusha. Tunashukuru hifadhi hizi mbili pamoja na uongozi wake kwa kufanya jitihada ya ujirani mwema na kusaidia miradi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iangalie namna ya kuitatua kero ya mipaka katika hifadhi hizi mbili, Manyara na Tangarire, ni tatizo na kero ya miaka mingi. Tunaamini kuwa kwa uongozi wa sasa tatizo hilo la mipaka kati ya Lake Manyara *National Park* na vijiji vya Mayoka na Moya utamalizika na suala la wachimbaji wadogo huko Mayoka litapatiwa ufumbuzi. Pia tatizo la mgogoro wa ardhi ni baina ya Tarangire na vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gidejabong upatiwe ufumbuzi mapema, migogoro hii ikipatiwa ufumbuzi wananchi wataona umuhimu wa kuwa na hifadhi jirani na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Wizara ikubali mapendekezo ya kusaidia wananchi wanaopakana nazo kwa miradi ya kiuchumi ambayo italinda hifadhi hizo na kuondoa kero ya mahusiano mabaya hasa katika miradi ya upandaji miti ya matunda na ufugaji nyuki. Pia geti hizo zikifunguliwa na wananchi wa Babati watapata fursa ya kufanya biashara kuhudumia watalii kwa kuuza matunda na mbogamboga, vitu vya utamaduni na kuwa na *campsites.*

Pia tunashauri *TANAPA* wawape Afisa Vijana wanaotokana na maeneo hayo na si lazima wabaki hapo katika hifadhi hizo, wapelekwe kwingine pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha mfumo wa kulipa kifuta jasho na mkono wa pole pale wanyama wanapoharibu mazao ya wananchi au kumwua mwanadamu, fidia ni ndogo sana na hata mkono wa pole ni kidogo, lakini pia na malipo hayo yanacheleweshwa, inaongeza kero na hasira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri na nilishawahi kuchangia hifadhi hizi katika maeneo wanapopakana na wananchi waweke *electric fence*, wanyama wasije kwa wananchi na pia mifugo ya wananchi isiende katika hifadhi, pia Tarangire na Manyara ni hifadhi ya tatu na nne kwa mapato kwa wingi katika hifadhi zote za *TANAPA,* tunaona mchango kwa jamii iliyozunguka bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamkaribisha Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, watutembelee Wilaya ya Babati na wajionee fursa kubwa ya utalii iliyopo, yenye vivutio vikubwa kama Mlima Kwasaa, Ziwa Babati, Burunge na Manyara pamoja na maporomoko ya Mto Magara na Mto Erri na kivutio cha bonde la ufa na misitu ya Bugher na Nou inaweza kuwa eneo jipya (*new circuit*) katika maendeleo ya utalii nchini. Pia kutoka hapo kwenda Hanang kupanda Mlima Hanang na Mbulu kuitembelea yaenda chini kwa Watindiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia *TANAPA* na Hifadhi ya Ngorongoro iangalie namna ya kujenga Hosteli katika kila hifadhi mahali ambako hakuna ili tuweze kukuza utalii wa ndani kwa kuwapunguzia gharama ya malazi wananchi wa kawaida hasa wanafunzi.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka, malisho na uvamizi wa wanyama; ni vizuri Serikali itazame upya suala hili na kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wasio waaminifu wafuatiliwe; kutokana na baadhi ya watumishi wachache wasio waaminifu wanalitia hasara Taifa, ni vyema wafuatiliwe na pia hatua kali za kisheria zichukuliwe. Mfano, mwezi Agosti, 2011 mtumishi aliye katika Hifadhi ya Serengeti, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, Herman Msaki alitoa bastola ofisini kumtishia mwanachi. Hadi leo hii hakuna hatua zilizochukuliwa mbali na *TANAPA* kulifahamu suala hili na ufuatiliaji uliofanyika na hatua gani zilichukuliwa?

Watumishi wa aina hiyo wanaweza kuwa ndio wanashirikiana na kuwa na mtandao wa majangili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani, uhamasishaji ufanyike ili wananchi wote washiriki katika kuimarisha hasa utalii wa ndani ambao uko chini sana, nchi nyingine kama Japan, Botswana, Malysia, Kenya na kadhalika wana *programme* maalum za utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majimoto iboreshwe ili pawe kivutio cha utalii, eneo hili lina chemchem ya maji ya moto na pia kuna gesi aina ya *Helium,* ni vyema suala hili la kusaidia kuinua uchumi lifanyiwe kazi kikamilifu kwa kusaidiana na Wizara ya nishati na madini ili chanzo hiki kizuri kisaidie kuinua uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa kiutamaduni (Tanzania utalii *cultural Festival*), utalii wa aina hii ni vyema eneo la Serengeti lipewe kipaumbele kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Waziri (sehemu ya 105), Serengeti imetengwa ni vizuri ijumuishwe.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uharibifu wa misitu yetu kwa kukata misitu hiyo na kuichoma moto, jambo ambalo linapelekea mvua kupungua na hivyo uzalishaji wa chakula nao unapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi fulani Serikali imetoa elimu juu ya kukabiliana na uharibifu wa

mazingira hasa uchomaji moto misitu na uchomaji wa mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tatizo la kukabiliana na uchomaji wa mkaa Serikali bado iangalie mkakati wa nishati mbadala ili kuweza kuokoa misitu yetu isimalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la wananchi wasiowaaminifu wanathubutu kuvuna mbao kinyume na taratibu na kuharibu misitu hiyo. Nashauri Serikali kutoa elimu zaidi kwa wananchi walio karibu na mazingira ya misitu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neema ya kupatikana kwa madini ya urani *(uranium)* itaangamiza kwa kiwango kikubwa msitu wa Selous, hivyo, Serikali imejiandaa vipi na tatizo hili na je, tathmini ya uharibifu wa mazingira imeshafanywa? Kama bado ni lini Serikali itafanya tathmini hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani bado haujapewa nafasi kubwa ya wananchi wenyewe watumie kutokana na mwamko mdogo uliopo Serikalini ni vyema ikaandaa mpango maalum wa kutoa elimu juu ya utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vyema vivutio vyetu vya watalii vinaonekana na wageni tu, lakini sisi wenyewe hatuvioni, hivyo Serikali ijiandae na mikakati ya uhakika ya utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Wanyamapori, baadhi yao waangaliwe kwani sio waaminifu na wanashirikiana na majangili kuharibu wanyama na misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuelewa ni Askari Wanyamapori wangapi wamekamatwa kwa kubainika na raia wasio waaminifu kuharibu maliasili zetu kwa kipindi cha Julai, 2011 hadi Juni, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusiana na makadirio na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa kwa wingi wa vivutio vya utalii ulimwenguni na hivyo kuwa na fursa kubwa ya kiushindani katika sekta ya utalii. Taarifa mbalimbali zimekuwa zikiisifu Tanzania kwa uwepo wa vivutio hivi, ikizidiwa tu na nchi kama Brazil. Endapo vivutio hivi vingetumika vizuri, sekta ya utalii ingeweza kusaidia katika kutoa ajira kwa makundi mbalimbali wakiwemo vijana na hatimaye kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, pamoja na kuwa na fursa hii ya kimkakati katika kukuza sekta ya utalii nchini, ni jambo la kusikitisha kuwa kama Taifa tumeshindwa kuitumia fursa hii hata kwa kufikia lengo dogo tulilojiwekea la kuwa na watalii milioni moja wanaoitembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa wadau muhimu katika sekta ya utalii nchini wamehusisha huduma huku kwa ongezeko la idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu na mfumo mbovu wa utoaji leseni kwa kampuni za wazawa na hata zile za kigeni. Lazima tuondokane na urasimu usio wa lazima ili kuwezesha watu wengi zaidi kuwekeza katika sekta ya utalii. Ieleweke kuwa urasimu katika utoaji wa leseni si tu unazuia uanzishwaji wa Makampuni ya Utalii, bali pia unadumaza ukuaji wa huduma zinazotolewa na sekta nyingine za uchumi kama uzalishaji wa chakula, usafiri, hoteli, wapagazi na watu wengine wanaotegemewa kutoa huduma kwa watalii wawe wa ndani au wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa mbalimbali zinaifananisha Tanzania na nchi kama Australia kwa kuwa na mfumo mbovu wa utoaji leseni, mfumo ambao hautoi mwanya kwa ukuaji kwa sekta ya utalii. Aidha, utafiti wa *IFC* unabainisha kuwepo kwa urasimu mkubwa katika udhibiti wa leseni za utalii na upatikanaji wa mtaji, hali ambayo inasababisha ugumu kwa wanaotaka kuingia katika sekta ya utalii hususan wazawa. Kwa kuwa kama Taifa tunakubaliana kimsingi kuwa sekta binafsi ni injini ya kukuza uchumi wa nchi yetu, lazima tuhakikishe tunatoa fursa pana kwa wazawa hususan wale wenye mitaji midogo ili nao waweze kushiriki katika haki ya kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ina nafasi kubwa ya kuendelea kuwa mhimili muhimu wa kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, kufanikiwa kwa hili

kunategemea sana kufanyika mambo kadhaa muhimu kama vile kuongeza jitihada katika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika kila kona ya nchi yetu, kuboresha miundombinu muhimu, kuboresha taaluma ya utalii ili kuwa na watu wenye elimu na taaluma stahiki na halikadhalika kuondoa urasimu katika maeneo mbalimbali yahusuyo sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada hizo ni muhimu vile vile kuelekeza nguvu zetu katika kukuza utalii wa ndani. Hii inatokana na ukweli kuwa utalii wa ndani ni uti wa mgongo katika ukuzaji wa sekta ya utalii katika nchi yoyote ile. Ni kutokana na ukweli huu, hatuna budi kama Taifa kuelekeza nguvu zetu katika kujenga utamaduni wa wananchi kutembelea vivutio vilivyopo nchini, kuwa na mikakati ya kuhamasisha wanafunzi na vijana kwa ujumla kutembelea mbuga zetu na maeneo ya vivutio katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe na mkakati kabambe wa kuongeza jitihada zetu katika kutangaza vivutio tulivyonavyo. Ikibidi suala la utalii wa ndani liwe sehemu ya mitaala yetu ya kufundishia katika shule zetu. Aidha, wakati umefika wa kuanzisha wiki maalum ya uzinduzi wa utalii wa ndani kila msimu wa utalii unapoanza nchini. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa jitihada zetu za kukuza na kutangaza utalii zinalenga makundi mbalimbali ya watu nchini kwa kuzingatia umri, jinsia na uwezo wa kipato ili kumwezesha kila Mtanzania kuweza kushiriki.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Alhaji Khamis Kagasheki na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ambayo inafufua matumaini kwa Watanzania wanyonge ambao wamekosa haki zao kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa wakazi wa Rufiji wanaoishi kandokando ya Pori la Akiba Selous katika Vijiji vya Mloka, Nyaminywili, Mwaseni, Mtanza Msoma na kadhalika wamekuwa wakipoteza baadhi ya wanafamilia kutokana na vifo vinavyotokana na kuuawa kwa kupigwa risasi na Askari Wanyamapori katika pori hili la akiba Selous kwa kujaribu kwenda kuvua katika mabwawa ya asili takriban nane yaliyopo ndani ya pori hili la akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2010 – 2012, ni takribani vijana nane (8) wameuawa hii nguvu kazi inayopotea ambayo inaacha pengo kubwa sana kwa familia walizozihudumia. Lakini miaka ya nyuma Serikali kupitia Wizara iliweka utaratibu wa kuwaruhusu wananchi hawa wanaoishi kandokando ama pembezoni mwa *Selous* kwenda kuvua katika mabwawa haya kwa kukata leseni na kusindikizwa na askari na baadaye utaratibu huu ulifutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kupitia Wizara kurudisha utaratibu huu wa kuruhusiwa kuvua kwa leseni, vinginevyo vijana wetu wataendelea kuuawa na tukishuhudia Wazungu wakiingia katika pori hili na kutoka na rasilimali zetu ambazo Mungu

ametupatia na sisi wenyewe tunashindwa kunufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tangu mwaka 1978 imekuwa ikitoa ahadi ya kujenga mabwawa mbadala, lakini hadi leo ni 2012 hakuna hata bwawa moja lililojengwa na mabwawa ya asili yote yameingizwa katika pori la Selous. Je, wananchi hawa waliokuwa wanategemea uvuvi kuwa ndio shughuli yao ya kuwaingizia kipato kidogo cha kujikimu wataishi vipi? Tunaomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wako mtuangalie kwa jicho la huruma, mabwawa yaliyopo ndani ya hifadhi ni haya:-

(1) Mzizimia.

(2) Suwando.

(3) Nzelekela.

(4) Maze.

(5) Tagalala.

(6) Mwantonga.

(7) Songasonga.

(8) Kandoi, Utunge.

Mabwawa yaliyo karibu na vijiji ni: Mzizimia, Suwando na Maze, tunaomba utaratibu wa leseni urudi vinginevyo mtatuua Wanarufiji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujangili unazidi kwa sababu kuna wazawa wachache ambao wanaomba kibali cha kuwinda na hatimaye wanaondoka na magari kinyemela kuingia ndani ya mbuga zetu kwenda kuua wanyama wetu muhimu kama tembo. Wageni hawa ni kutoka nchi za Qatar, Bahrain, Oman, Kuwait, Afrika Kusini na kadhalika na wanakosesha Taifa malipo ya zaidi ya dola 1,000 kwa kila 400-500 za Kimarekani. Je, Serikali kupitia Wizara wamejipanga vipi kukabiliana na ujangili huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwenye mfungo huu Mtukufu wa Ramadhani na nawapa pole wale wote waliopata ajali jana kwenye magari yaliyotokea huko barabara ya Morogoro na kwingineko na wawe pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na malikale, sera na sheria katika kutekeleza Sera ya Sheria hii ya Utalii, Wizara imekamilisha maboresho ya kanuni za tozo ya maendeleo ya utalii na matumizi yake kwa mwaka 2012/2013 na kwa kuwa elimu imetolewa kwa wadau kutekeleza Sheria ya Utalii mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada, Serikali hii inatambua kabisa Wilaya ya Kondoa ingekuwa mojawapo ya kupata mafunzo hayo na kujengewa hoteli na wana Kondoa wangepata ajira kutokana na watalii kuja wengi na wana maeneo ya kufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara hii pamoja na kusema imefanikiwa kuandikisha magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na michoro ya miamba ya Kondoa Irangi kwenye orodha ya urithi wa utamaduni wa dunia, chini ya mpango wa Shirika la Elimu, Kisayansi na Kiutamaduni la Umoja wa Mataifa *UNESCO* imeanzisha vituo kule Oldupai, Ujiji na Kalenga, kumbukumbu imeanzishwa sehemu kama Isimila, Bagamoyo na Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwomba Mheshimwa Waziri atueleze yafuatayo:-

Hivi katika nchi yetu yenye rasilimali, watu, ardhi, Bandari, Misitu yetu ya utalii zikiwemo mbuga kuu tano za kujivunia na madini pia. Je, tumepata mapato kiasi gani tokea tuanze kuingiza watalii na wawekezaji wametunufaisha nini Watanzania na bado uchumi wetu haukidhi mahitaji ya wananchi kwa nini mapato yanapatikana kidogo na yanawanufaisha wachache?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuiona Kondoa ni moja ya Wilaya yenye sifa kwa Tanzania yetu, lakini Wilaya hii imetengwa kila kitu, kuanzia maendeleo, hivi lini basi Serikali itaiona Wilaya ya Kondoa ina muhimu wa kuleta maendeleo kwa nchi hii na wanakondoa wajione kama wenzao kwani maeneo mengi yana haja ya kuboreshwa hasa nikianza na mpango yametelekezwa wakati zamani yalikuwa yanaingiza fedha kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapango yale yakaendelezwe na kupakwa rangi kuimarisha michoro ile isipotee. Tunayo maeneo ya Mialo, Mlima Kisau ni wa kihistoria, lakini umeachiwa watu wameuharibu kwa kuvunja nyumba iliyojengwa pale na Waarabu wakati wa vita na kuna mbuga za wanyama, uvunaji wa miti umekuwa wa kiholela mno. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwashirikisha wananchi kulinda na kujua umuhimu wa kutunza mali za misitu? Kama Kondoa kujenga Taraja iliyokuwa ni kivutio iimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini Kondoa ni muhimu kuikumbuka.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru *Allah* muweza wa mambo yote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu kwa kuzungumzia utalii. Utalii una umuhimu mkubwa katika nchi yetu, unachangia wastani wa asilimia 17% katika pato la Taifa wakati fedha za kigeni unachangia wastani wa asilimia 25%. Hivyo, ni jambo la kuendelezwa na si jambo la kubezwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wetu hapa ni ule wa fukwe, uwindaji upigaji picha na ule wa malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingiaji wa watalii mwaka 2010; Kenya iliingiza watalii 1.6 millioni; Uganda 945,899 na Tanzania tulipokea wageni 782,699, inaonesha wazi kuwa tuko nyuma sana wakati sisi ndio

ambao tuko mbele sana kwa vivutio vya utalii. Hii inaashiria kwamba hatujajipanga vizuri katika kuutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kutilia mkazo kwa kuisaidia Wizara hii kwani ni miongoni mwa Wizara zinazoipatia Serikali pato kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa picha watalii mara kwa mara wanakuja nchini mwetu na kupiga picha sehemu mbalimbali na kuzisafisha nje. Je tunajua thamani ya picha hizo? Naishauri Serikali kufuatilia na kupata thamani halisi ya picha au filamu hizo. Hii ni kwa sababu kuna picha inaitwa *lionking*, hii ilichukuliwa au ilipigwa katika Hifadhi ya Serengeti katika mandhari ya eneo la Nyasirori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliopiga picha hiyo walilipwa dola za Kimarekani milioni 36, wakati huo huo mauzo ya picha hiyo (filamu) mpaka sasa yamefikia dola bilioni nne za Kimarekani wakati malipo ya kulipia leseni za kupiga picha ni kati ya dola 300 – 500 za Kimarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhahiri kwamba utalii wetu hautufaidishi ipasavyo. Naishauri Serikali ijitahidi juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawezekana sababu yake ni kwamba maeneo yetu hayajathaminiwa wala kuwa na hati miliki. Kwa hiyo, yathaminiwe na yawe na hati miliki kisheria ili Serikali iweze kutiliana mikataba ya ubia kwa mauzo ya picha ambazo zinapigwa katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa vitalu upya, dosari ya ukataji upya wa vitalu vya uwindaji haikupaswa idadi ya vitalu kuongezeka kwa sababu wanyama wamepungua. Utafiti mwaka 1980 -2000 umebainisha wanyama wamepungua, Kijarida 2007 *Stoner et al* 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa vitalu vya uwindaji, pia haukuzingatia ikolojia ya eneo husika. Mfano, Ugala *Game Reserve*. Kitalu hiki kimegawiwa sehemu mbili wakati kina mto mmoja. Wanyama wanaoishi hapo ni viboko na mamba. Vitalu viwili hivyo vinamilikiwa na watu wawili tofauti. Mto huu ni mmoja tu bali hugawika sehemu wakati wa Mvua na wakati wa kiangazi mto hurudi katika hali yake ya kawaida. Hivyo kuigawa sehemu hii kwa watu wawili haikupaswa kwa Mto mmoja tu na uko katika kitalu kimoja.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSFU MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana tumeelekeza nguvu zetu nyingi katika utalii wa wanyamapori zaidi tukiacha maeneo mengine ya utalii. Kuna haja sasa kujikita pia katika utalii wa aina ya *culture tourism, eco-tourism, beach* au *mArine based tourism*. Hili linaweza kufanikiwa ikiwa tutaweka mkakati kabambe wa kutumia vizuri ukanda wa Bahari ya Hindi kuanzia Kilwa, Bagamoyo na hasa Visiwa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini niseme hasa Visiwa vya Zanzibar? Kwa sababu Zanzibar ina vivutio vingi na vya kila aina ambavyo kama tutavitumia vizuri

tunaweza kuona mafanikio makubwa kwenye maeneo mengine ya utalii niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar tuna tamaduni za aina yote hasa kutokana na mchanganyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali, Zanzibar kuna historia yenye kuvutia ikiwemo majengo ya kale ya kila aina. Zanzibar tuna wanyama na wadudu wa ajabu ambao ni nadra kuwakuta sehemu nyingine duniani, mfano, *red collubus monkeys* waliopo Jozeni, ndege wa kurubia makobe wenye umri mkubwa waliopo katika Kisiwa cha Changuu. Zanzibar tuna fukwe na Bahari zenye kuvutia, tunaweza tukaimarisha *deep sea* fishing, kwa mfano au *scuba driving* kuna samaki wa kila aina ya *coral reets* ambazo ni kivutio kikubwa kwa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar tuna viungo vyote tunavyovijua, Zanzibar tuna mapango wa ajabu na kihistoria kule kwenye Pwani na soko la watumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaona kwamba, tukiwekeza vya kutosha katika sekta ya utalii Zanzibar, tukitangaza vivutio hivi vya Zanzibar, Tanzania kwa ujumla itafaidika sana na kama kuna mtalii ambaye angetaka kwenda South Africa kwa mfano kufuata mbuga za wanyama ataone bora aje Tanzania kwa kuwa atafika mpaka Zanzibar, lakini pia atatumia muda zaidi wa kukaa nchini, atatumia zaidi na nchi yetu itapata pato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi nyingi zenye uasili wa visiwa zilizotumia vema fursa ya ukisiwa wake zinanufaika sana kupitia sekta ya utalii, ukiachilia mbali Phillipines ambao utalii ni chanzo chake cha pili cha mapato, Singapore ambao wanakitumia vizuri kisiwa chao kidogo cha Sentosa kinachoingiza watalii zaidi ya milioni tano kwa mwaka Mauritius ambao ni jirani yetu hapa wamekitumia vizuri kisiwa chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mauritius kwa mfano, wanaingiza zaidi ya *USD* 400m kwa mwaka, sisi Tanzania visiwa vyetu vizuri tulivyo navyo hatuzidi *USD* 1.5m kwa mwaka. Hii ni aibu, lakini kwa nini Mauritius wameweza kukitumia Kisiwa cha Mauritius wakati Tanzania imeshindwa kukitumia Kisiwa cha Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mmoja mdogo sana, visiwa vya *nature* yake vinavutia sana wapenzi wapya kwa ajili ya *honeymoon* ambao watalii wengi wanaotoka Ulaya na ambao sisi ndio wateja wetu wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mauritius mbali ya kuwa na huduma hizo nzuri kwa wanandoa, lakini pia wanajitengezea vema. Tena wanapamba kweli matengenezo yao. Mfano unakuwa matangazo wanasema Mauritius *is a top romantic destination in Africa* au sisi huduma hizo hafifu na bajeti yetu ya matangazo inasikitisha ambayo ni *USD* 2.78m, *against USD* 16.30m za Kenya na *USD* 70.10m za Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la kwanza, kuanzisha Mamlaka ya Utalii Tanzania ili iweze

kujitengea fedha za kutosha kwa matangazo. Serikali kwa upande wake iongeze nguvu kwenye kuimarisha utalii wa ndani, kurekebisha sheria ili Watanzania waweze kushiriki katika uwekezaji ili kupunguza *package tour arrangements* kutoka 65% ya sasa, kuimarisha sekta ya Anga, ndege zaidi ziweze kuja moja kwa moja nchini na kuimarisha usafiri wa ndani, kuimarisha Chuo cha Utalii ili kitoe wahitimu waliobobea, kuteua masoko ya Middle East, Asia, Marekani na Ulaya Mashariki ili ikitokea *crisis* Italy, UK na Ulaya kama iliyotokea Greece isituathiri. *Payment method* hasa kwenye mahoteli ziimarike matumizi ya *credit cards ATM* na kadhalika.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize Mheshimiwa Waziri atusaidie sana Wilaya ya Kaliua kwa kuutengeneza utaratibu wa kudumu wa kuwaondoa wavamizi wa misitu yetu ya hifadhi. Akishamaliza kuwaondoa ahakikishe *patrol* za misitu hii ziwe za kudumu wavamizi hawa ni hatari sana kwetu, wanatunyanyasa na kutuua sana wanazuia wananchi kwenda kufanya shughuli halali za kiuchumi kama vile kuvuna asali katika misitu hii. Hii imeanza kutishia amani kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza kuwa zoezi la kuwaondoa wavamizi hawa isiwe ndio sababu ya kuwaadhibu na wananchi walio katika vijiji halali vilivyoanzishwa kwa kufuata taratibu halali za Kiserikali,

Vijiji vya Luyembe, Usimba, Nzugimlole, Uyumbu, Kangeme, Ukumbi, Siganga, Lumbe, Usinga na Kakoko katika Tarafa mpya ya Ukumbi Siganga ni vijiji halali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri suala la kutoa kifuta machozi kwa wale waliouawa wakati wanafanya kazi iliyopaswa kufanywa na Wizara yake alipe umuhimu sana. Nimejitahidi kuomba kifuta machozi kupitia Halmashauri bado hatujafanikiwa na waliouawa ni Yasini Nyembe, *VEO*; Makenzi Magida, Mwenyekiti wa Kitongoji; Emanuel Gabriel, Mgambo na M. Ramadhani, Mgambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu Utalii wa kiikolojia ambao una faida zifuatazo:-

- Matumizi endelevu ya rasilimali.

- Kupanda miti badala ya kutegemea misitu asili.

- Kwa kuwashirikisha jamii katika shughuli za kuandaa shughuli za Utalii na kunufaika kibiashara,

- Serikali itanufaika endapo wananchi wa maeneo husika yatakayofanya Utalii wa Kiikolojia watasaidia kutangaza utaliii bila hofu ya kutokunufaika na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia faida nyingi zitokanazo na utalii wa kiikolojia ni vema Serikali ikawahamasisha wakazi wanaoishi maeneo ya hifadhi kushiriki kwenye shughuli za Utaliii wa kiikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa nafasi wananchi waishio karibu na maeneo ya hifadhi kununua hisa kwenye Makampuni ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia hii itawawezesha wananchi wakiwemo wafugaji wa maeneo ya hifadhi kujisikia kuwa nao ni baadhi ya wanaonufaika na Utalii. Hivyo, watakuwa ni walinzi wakubwa wa mbuga zetu na vile vile watatangaza Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara hii bado haijasimama imara kwa kulinda majangili wanaowateketeza tembo ndani ya hifadhi zetu. Ikiwa kwa siku takribani wanapotea ndovu 30, ni kwa nini mkakati mkali na endelevu usiwekwe kuhakikisha walinzi wa kutosha pia wanaopata maslahi yao vizuri pia kupewa motisha ili wapende kazi yao na kulinda mali za Taifa lao. Namwomba Waziri aongeze wafanyakazi walio wengi pia wenye imani ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mbali ya kutangaza utalii pia wapange au waandae mandalizi yaliyo rasmi ya kuweza kuwahakikishia safari za kusafiri toka Dar es Salaam kwenda Zanzibar kwani ukizingatia Zanzibar nako kuna mambo mengi yanayowavutia watalii. Pia watalii wanaokwenda Bagamoyo washawishiwe ili wafike Zanzibar ili kujua sehemu waliyokuwa wakifikia watumwa baada ya kutoka Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri mpya wa Wizara hii Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa juhudi za dhati wanazoonesha kuisimamia Wizara. Nasisitiza waongeze juhudi zaidi ili sekta hii iweze kuukwamua uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la utalii wa ndani; ni ukweli usiopingika na ulo dhahiri kuwa Watanznia wengi hawajui dhana hii ya utalii hasa utalii wa ndani. Hali hii inapelekea wengi wao kupuuza vivutio vya utalii tulivyonavyo hapa nchini na hivyo kuwaona wageni kuwa ndio wenye haki pekee ya kuvifaidi vivutio hivyo. Naishauri Wizara hii ikishirikiana na Halmashauri za Wilaya zetu kuhamasisha Watanzania wengi kutembelea vivutio vya utalii tulivyo navyo kama vile wanyama, ndege, milima, mabonde, mambo ya kale na kadhalika. Hali hii itachochea

uzalendo kwa Watanzania kuipenda na kuithamini nchi yao na pia itaongeza kipato cha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kuhusu utalii wa kihistoria na utamaduni *(Cultural Tourism),* ifahamike wazi kuwa nchi yetu ya Tanzania imebahatika kujaliwa vivutio vingi vya kihistoria hasa mambo ya kale kama vile mapango, nyimbo za makabila, mbalimbali, mila na desturi za makabila mbalimbali, ushujaa na ujasiri wa mababu zetu kama vile *Chief* Mkwawa na kadhalika. Vitu hivi vyote ni vivutio vya Utalii ambavyo vikitumiwa vizuri vitasaidia sana kukuza utamaduni wetu kwa upande wa Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama vile South Afrika inatumia vivutio hivi kukuza utalii wa kihistoria na kiutamaduni. Si ajabu kusikia kuwa wanamtumia Mzee Nelson Mandela kama kivutio cha Utalii nchini mwao. Je, ni kwa nini sisi Watanzania hatuwatumii waasisi wa Taifa hili kuendeleza utalii wa kiutamaduni na kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni lugha ya Kiswahili kama bidhaa ya Kitalii; nchini Kenya lugha ya Kiswahili hutumika kama bidhaa ya utalii kwani wageni wengi waingiapo nchini humo hupenda kujifunza lugha hii ya Kiswahili. Ndio maana katika nchi ya Kenya kuna vipeperushi vijarida vitabu vingi ambavyo huonesha tafsiri ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kigeni kama vile Kingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na kadhalika.

Hivyo, naishauri Wizara hii iweze kushirikiana na Wizara ya Elimu Baraza la Kiswahili na hata Taasisi ya

uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuangalia ni namna gani ya kuweza kuifanya lugha ya Kiswahili ili iwe bidhaa kwa watalii wote wanaoingia hapa nchini. Jambo hili linaweza kufanikiwa ikiwa kwa kila *Information Centre* ya Watalii tutaweka kituo cha kujifunzia na kufundishia lugha ya Kiswahili au kituo cha tafsiri yaani *(translation centre)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la migogoro ya mipaka, suala la migogoro ya mipaka kati ya hifadhi zetu, mbuga zetu, mapori ya akiba, misitu yetu baina ya wananchi (vijiji) wanaozunguka maeneo hayo inatakiwa kuangaliwa kwa makini sana ili kuleta uhusiano mwema. Hali hii itaweza kutatuliwa ikiwa Wizara mbalimbali kama vile Tamisemi Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii zitakaa pamoja na kupitia kwa makini suala la mipaka halali inayotenganisha maeneo hayo na makazi ya wanakijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Waziri aweze kutekeleza suala hili haraka iwezekanavyo ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima baina ya wanavijiji wetu na Serikali yao hasa Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Katika kutekeleza hili naiomba Wizara iangalie tatizo la *TANAPA v/s* Vijiji vya Bonchugu na Bisarara, Wilayani Serengeti, *Grumeti Game Reserve v/s* Kijiji cha Bonchugu, Wilayani Serengeti; *TANAPA v/s* Vijiji vya Mrito, Gong'ora, Gibaso ,Ketawasi, Masanga, Mangucha na Kegonga Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la Watanzania kuhamasishwa kuwekeza katika sekta ya Utalii, ni vizuri ifahamike wazi kuwa Watanzania walio

wengi hawajawekeza vya kutosha katika sekta hii ya Utalii. Hali hii imepelekea sekta hii kushikwa na wageni hasa wale wenye asili ya Asia. Hii ni kwa sababu Watanzania wengi hawajaelimishwa vya kutosha juu ya uwekezaji katika Sekta ya Utalii. Hivyo, elimu ya uhamasishaji inahitajika kwa kiasi kikubwa ili kuweza kuwaelimisha Watanzania umuhimu wa kuwekeza katika Sekta hii ya Utalii. Ni matumaini yangu kuwa Watanzania hasa wafanyabiashara wakubwa wanaomiliki hoteli mbalimbali katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na kadhalika wakielimishwa vizuri umuhimu wa kuwekeza katika Sekta ya Utalii watajenga hoteli nyingi katika hifadhi zetu na hivyo kuweza kuleta ushindani mzuri katika sekta hii na hivyo kuifanya Serikali ipate fedha za kutosha kutokana na biashara ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la misitu; misitu yetu ni muhimu ihifadhiwe vizuri, lakini wakati huo huo iliingizie Taifa pato la kutosha. Kwa bahati mbaya katika nchi yetu ya Tanzania bado misitu haijatumika kama bidhaa adhimu ya kuinua uchumi wa nchi. Wajanja wachache ndio kwa kipindi kirefu wamenufaika na misitu hii kwa kusafirisha magogo nje ya nchi kwa muda mrefu! Naishauri Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kuwa inalinda misitu yetu kwa kuzuia isivamiwe na wananchi na kuwahamasisha wananchi kulinda vyanzo vya maji na kupanda miti, kupiga marufuku biashara yoyote isiyo halali inayohusisha ukataji miti na magogo. Swali la kujiuliza je, sekta ya misitu inachangia asilimia ngapi katika pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ugawaji wa vitalu vya uwindaji; kumekuwa na maalamiko mengi na ya muda mrefu juu ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji. Malalamiko hayo yanahusisha suala la rushwa pamoja na upendeleo. Aidha, kuna tetesi kuwa baadhi ya wazawa walinyimwa vitalu hivyo kwa kuwa wanashirikiana na wageni. Swali, je, Wizara imejipanga vipi ili kutatua tatizo hili? Je, Wazawa wa Tanzania wanapewa upendeleo gani ili kuvipata hivyo vitalu?

Mheshimiwa Spika, suala la ujangili katika hifadhi zetu ni kero na linaleta picha mbaya hata kwa wageni wanaotembelea hifadhi hizo. Kwa kuwa suala hili linahusisha watu hatari sana katika biashara ya wanyama na nyara nyinginezo, naishauri Serikali kupitia Wizara hii ifanye *operation* maalum na endelevu itakayohusisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili kutokomeza kabisa hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *concession fee*; kupitia Wizara hii naishauri Serikali isimamie malipo ya *fixed rate* badala ya *variable rate* kwani wamiliki wa hoteli hizi si waaminifu. Hali kadhalika ifahamike wazi kuwa, katika nchi yoyote ile inayotaka maendeleo ni lazima isimamie maamuzi magumu yasiyoyumbishwa na vibaraka wenye nia mbaya, roho mbaya na hata wanaojali maslahi binafsi kuliko kuweka maslahi ya Taifa mbele. Hivyo, suala la baadhi ya wamiliki wa hoteli kukimbilia Mahakamani kupinga suala la *fixed rate* ni la kuchukua uamuzi mgumu na Serikali isiyumbishwe. Wazawa wanaokimbilia Mahakamani kupinga uamuzi huu ni sawa na wahujumu uchumi. Namshauri Waziri asimamie *fixed*

*rate* ili kuweza kuliletea Taifa letu pato la kutosha kupitia rasilimali za asili alizotujali Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, suala la wanyama waharibifu katika vijiji vinavyozunguka hifadhi au mapori ya wanyama katika nchi yetu limewatia umasikini watu wengi sana. Pia hali hii hupelekea mahusiano mabaya baina ya hifadhi zetu na wanavijiji wanaoharibiwa mazao yao. Hali kadhalika wanyama hao kama vile ndovu, simba, fisi chui na kadhalika huhatarisha maisha ya wanavijiji. Hali hii imejitokeza sana katika Wilaya ya Serengeti na Tarime ambapo katika Vijiji vya Bonchugu na Bisarara Serengeti na Vijiji vya Gibaso, Mrito, Gong'ora, Ketawasi, Masanga, Mangucha na Kegonga, Tarime tumeshuhudia uharibifu mkubwa wa mazao na watu kupoteza maisha kutokana na uharibifu wa wanyama wanaoishi katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii ibuni mbinu mbadala ya ulinzi wa raia na mazao yao kutokana na uharibifu wa wanyama hao. Pia iangalie utaratibu mpya wa kulipa kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utangazaji wa utalii, ni ukweli usiopingika kuwa bado hatujaweza kuvitangaza ipasavyo vivutio vya utalii tulivyo navyo. Bodi ya Utalii ya Tanzania *(TTB)* imepewa jukumu la kutangaza vivutio vyote vya Utaliii hapa nchini, lakini imeshindwa ku-*perform* ipasavyo. Napenda kuishauri Serikali kupitia Waziri wa Wizara hii kuwa kazi ya kutangaza vivutio vya utalii iachwe kwa Mamlaka husika yenyewe mathalani *TANAPA* itangaze vivutio vya utalii ilivyo navyo. *NCAA* nayo ijitangaze kwa kutangaza vivutio vyake vya utalii. Halikadhalika

Idara ya Wanyamapori, Idara ya Misitu nayo ijishughulishe kwa kutangaza vivutio vya utalii ilivyo navyo. Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* ibaki kutoa ushauri na kutangaza vivutio vingine vilivyo nje ya mamlaka hizo kama vile vivutio vya kihistoria, vivutio vya kiutamaduni na kadhalika. Hali hii ikifanikiwa ni dhahiri kuwa nchi yetu itapata watalii wengi sana kwani itaruhusu hali ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya ujirani mwema; masuala ya ujirani baina ya *TANAPA (Tanzania National Park)* na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo ya hifadhi yameimarika kwa kiasi kikubwa baada ya *TANAPA* kutoa huduma za kijamii. Katika maeneo hayo huduma za kijamii zinazotolewa katika maeneo hayo ni kama vile ujenzi wa zahanati, ujenzi wa vyumba vya madarasa, uchimbaji wa malambo ya kuhifadhia maji, uchimbaji wa visima, ujenzi na ukarabati wa mabwawa, ukarabati wa barabara na zinginezo nyingi. Ingawa miradi imekuwa ikihujumiwa na wanasiasa katika baadhi ya maeneo, lakini imekuwa ni chachu ya kuimarisha uhusiano katika vijiji vinavyozunguka hifadhi zetu na hifadhi zenyewe. Ushauri wangu kwa Serikali kupitia Wizara hii ni kuangalia ni namna gani ya kuwaelimisha wananchi watambue umuhimu wa kuhifadhi ili kutokomeza kabisa suala la uhujumu, ujangili na vitendo vyingine viovu katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza, ni imani yangu kuwa sisi Watanzania tukijitambua tukathamini rasilimali tulizonazo, tukijiamini, tukiacha kulalamika na

tukashikamana wote kuwa kitu kimoja Tanzania yenye neema tele itawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kushirikisha jamii katika uhifadhi ziendelee ili kuleta ufanisi katika uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi katika mbuga waongeze kuwa na mahusiano mazuri na ya karibu na jamii zinazozunguka mbuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* iwe makini kuangalia inapoajiri ili isisahau jamii zinazozunguka mbuga angalau kwa kazi wanazoziweza hasa jamii za wenzetu wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B.BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyoileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige aliniandikia barua akinieleza kuwa ardhi ya eneo la Kitongoji cha Mishenyi, Kata ya Bweranyange, Wilayani Karagwe na hifadhi ya pori la Kimisi imerudishwa kwa wananchi wa Kijiji cha Chamuchuzi. Barua hiyo ninayo na Mwanasheria wa Wizara ndugu Rweyemamu alinithibitishia jambo hilo kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iniopatie ratiba kamili na mwaliko rasmi ili twende pamoja katika Kitongoji hiki cha Mishenyi tuwakabidhi wananchi wa kitongoji hiki ardhi yao ili wananchi waweze kufanya shughuli zao za maendeleo bila ya bughuudha yoyote. Naomba ratiba hii ifanyike baada ya kikao cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa maombi ya wananchi wa Kata ya Nyakasimbi na Nyakakika kuwa ardhi yao imemegwa na pori la akiba Kimisi naomba Serikali iwaonee huruma kwa kuwarudishia maeneo yao yaliyomegwa na mipaka ya pori hilo. Hakuna sababu yoyote ya msingi kuendelea kukalia ardhi ya wananchi maskini kwani wananchi wanaihitaji kwa ajili ya matumizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvamizi wa Pori la Kimisi; pori hili limevamiwa na wafugaji wengi wao toka nchi jirani na wanalisha mifugo yao ndani ya Pori la akiba Kimisi kwa kuwa wanyama wengi hukimbia harufu ya dawa ya kuoshea ng’ombe, hivyo wamezagaa katika vijiji jirani na kuleta usumbufu mkubwa. Maafisa wanyamapori inasemekana wanashirikiana na wavamizi wa pori kwa kuwatoza fedha ambazo

haziingii kwenye mfuko wa Serikali. Pia Tembo wengi sana wameuawa na wanaendelea kuuawa na majangili toka nje na ndani, Serikali ichukue hatua haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara haijatangaza utalii wa nchi hii inavyotakiwa, watalii wengi toka nje wanaishia Kenya kwa sababu Kenya imejitangaza vizuri, Serikali iwe serious, *TANAPA* na Bodi ya Utalii ishirikiane na Balozi zetu moja kwa moja kutangaza utalii wetu na iziwezeshe kifedha badala ya kutumia makampuni binafsi. Mfano, Ubalozi wetu Canada unalalamikia suala hili. Watalii toka Amerika hasa Canada wanashindwa kuja East Africa hasa Tanzania kwa sababu hakuna ndege ya moja kwa moja. Nashauri Serikali iingie mkataba na Shirika la Ndege la Ethiopia na kadhalika. Ili watalii toka Canada, Marekeani na Cuba na kadhalika wapate ndege za moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani uboreshwe zaidi kwa kutoa mabasi mazuri ya kisasa na *centres* zitangazwe, mfano, wakazi wa Dar es Salaam wengi wanapenda kufanya utalii wa ndani, lakini hakuna matangazo ya kutosha, usafiri wa uhakika, malazi na kadhalika. Ziwepo ofisi maalum kwa ajili ya wananchi kufanya *booking* zao za muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii kwa Vyuo, Sekondari na Shule za Msingi ni muhimu uboreshwe ili vijana wetu wapende utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya japo ni kipindi kifupi tangu wateuliwe na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iboreshe ulinzi katika hifadhi zetu ili kuendelea kutunza sifa nzuri ya nchi yetu ambazo ni amani na utulivu ili watalii wanapokuja kutembelea nchi yetu waondoke na sifa nzuri ili watusaidie kutangaza nchi yetu na vivutio vyake ili wengi wazidi kuja kutembelea vivutio vya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweke mikakati mizuri ya kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu katika Mataifa mbalimbali ili waielewe Tanzania vizuri na maliasili tulizonazo iwapo Serikali itatangaza vizuri utalii wetu hali ya uchumi katika nchi yetu itakuwa kwa kasi ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuweka mkakati mpana wa utunzaji misitu, misitu imekuwa ikiharibiwa hovyo katika nchi yetu. Wamekuwa wakikata miti kiholela, hali hii italiingiza Taifa letu katika ukame isiposhughulikiwa haraka. Siku za usoni mvua itakua haipatikani sababu ya uharibifu wa misitu. Naomba Serikali iliangalie hili kiundani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha. Naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na wakati huo

huo kumpongeza Mheshimiwa Balozi Khamisi Kagasheki, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Kwa hotuba hii iliyojaa uchambuzi wa hali ya juu na inayo *vision* ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Lazaro Nyarandu Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu. Hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kukumbushia ombi la wananchi wa Wilaya ya Siha kufungua *route* mpya ambayo inapitia Kijiji cha Ngaronyi. Aidha, naomba kukumbushia ombi la Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro la kupata sehemu fulani ya ushuru utokanao na huduma *services levy* ambayo wananchi wanaozunguka Mlima huu maarufu hawaupati kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvamizi haramu kwenye mbuga zetu za wanyama; leo kwenye taarifa ya habari ya saa moja asubuhi tumesikia Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii akiitaka *TANAPA* kutoa taarifa ya ujangili unaofanywa kwenye mbuga za wanyama na wavamizi wanaoshirikiana na watumishi wa *TANAPA*. Ni kwa nini Serikali imekaa muda mrefu kiasi hiki wakati

kilio cha uvamizi katika mbuga zetu na kutoroshwa kwa wanyama wetu wakiwemo twiga kimekuwa cha muda mrefu? Kama tulivyosikia kwamba kuna idadi kubwa ya tembo waliouawa na meno yao kwa idadi kubwa kusafirishwa nje ya nchi. Je, ni kweli kwamba, Serikali kwa muda wote huu haikuwa na habari au ni uzembe na makusudi? Si kweli kwamba watendaji katika Wizara hii wanahusika moja kwa moja na kashfa ya kusafirisha twiga wetu ambao ni ishara thabiti ya Utanzania wetu? Nani mpaka sasa ameshafikishwa mbele ya sheria kwa kitendo cha kusafirisha twiga wakiwa wazima? Naomba maelezo ya kina katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchimbaji wa madini katika mbuga zetu; kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wawekezaji wa kigeni kutumia makampuni yao kuchimba madini katika mbuga zetu za wanyama hasa Serengeti. Je, Serikali mpaka sasa imechukua hatua gani kwa wawekezaji hawa ambao wanakiuka masharti ya uwekezaji kwa kuingilia uhuru wa wanyama mbugani? Mpaka sasa ni makampuni mangapi yameshakamatwa maana Naibu Waziri amekiri kulijua jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na migogoro ya ardhi kati ya wananchi na hifadhi; kumekuwa na migogoro mikubwa sana kati ya wananchi wanaoishi karibu na hifadhi na Serikali kwamba ni nani ana haki ya kumiliki ardhi iliyopo. Wanyama wamekuwa wakiharibu mazao ya wakulima kila mara na wananchi wanapojihami kwa kuwaua wanyama hao

wanachukuliwa hatua za kisheria za kufanya ujangilim lakini wananchi wanapouawa na wanyama hupewa kifuta jasho ambacho ni sawa na kichekesho. Je, Serikali inajali mnyama zaidi kuliko mwananchi wake mlipa kodi? Ni lini Serikali itatatua migogoro hii kati ya wananchi wanaoishi jirani na hifadhi? Serikali inatoa ulinzi gani wa makusudi kwa wananchi wake dhidi ya wanyama hawa?

Mheshimiwa Spika, upotevu wa silaha *TAWIRI*, katika ripoti ya *CAG* ya mwaka 2010/2011 imeonesha kwamba kuna silaha ambayo ilipotea chini ya *TAWIRI* tangu mwaka 1984 na mpaka sasa hakuna jitihada zozote zinazofanyika kuipata silaha hiyo. Mimi kama mjumbe wa *POAC, TAWIRI* walipokuja walionesha uzembe wa hali ya juu kwani suala hili hawakuliripoti Polisi wala popote mpaka leo hii! Je, Serikali imechukua hatua gani mpaka sasa kuhakikisha silaha hii inapatikana? Kuna silaha nyingine ambayo pia iliibiwa Serengeti na baadaye ikakamatwa kwenye ujambazi huko Mara na suala hilo bado lipo Mahakamani. Je na hii silaha iliyopotea si kweli kwamba inatumika kwenye matukio ya ujambazi? Je, ni amani ya namna gani wananchi wataendelea kuwa nayo kama suala nyeti kama hilo la kufuatilia silaha linaachwa hivi hivi? Je, si kweli kwamba watumishi wasio waaminifu wanaiba silaha hizo na ndiyo wanaohusika na ujangili wa wanyamapori na uporaji wa watalii katika mbuga zetu? Naomba maelezo na ufuatiliaji wa kina katika suala hili nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ni nyeti sana kwa uchumi wa Taifa, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Wizara. Yapo matatizo mengi katika Wizara hii na hasa hujuma mbalimbali zinazofanywa na baadhi ya Watendaji wasio waadilifu ambao wamekuwa wakishirikiana na wawindaji haramu? Je, Wizara imejipanga vipi katika kukabiliana na tatizo hili? Ni watendaji wangapi wanaohujumu Wizara hii wamechukuliwa hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kushirikiana vyema na wananchi wanaozunguka hifadhi katika kulinda na kuhifadhi maliasili zetu hasa ukizingatia kuwa majangili wengi hujificha kwenye makazi ya wananchi. Wananchi kwa ujumla baadhi ya majangili huwa wanawafahmu. Kwa vile Shirika la *TANAPA* limekuwa na migogoro ya mipaka na wananchi wanaozunguka hifadhi na hivyo kutokuwa na mahusiano mazuri. Je, Serikali ipo tayari kwa sasa kutatua migogoro yote katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbarali tumeunganishwa na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa maana ya Usangu *Game Reserve* na Ruaha *National Park*. Wananchi wa Mbarali walipokea kwa furaha kubwa kuunganishwa huko, tuliomba baadhi ya maeneo wananchi wahamishwe kupisha upanuzi wa hifadhi. Zoezi hilo lilifanyika ambapo Kata ya Msangaji yote ilihamishwa, Vijiji na Vitongoji vyote

vinavyozunguka Ihefu viliondolewa. Baada ya zoezi hilo ramani iliandaliwa wananchi wa Mbarali hatuna tatizo nayo. Tatizo lipo kwenye ongezeko la mpaka ambalo lilipendekezwa na Mkoa bila kufanyika utafiti wa kutosha wala kuwashirikisha wananchi wa Mbarali. Hata hivyo, mgogoro huu ulitatuliwa tulipoketi pamoja na Kamati ya Maliasili na Utalii na Wizara pamoja na viongozi wa *TANAPA* Taifa katika kumbi za Bunge. Agenda kubwa ilikuwa ni kutatua migogoro mbalimbali. Kwa upande wa Mbarali tulikubaliana kuwa itumike ramani iliyochorwa mwanzo na siyo iliyopendekezwa na kikao cha Mkoa *(RCC)* tatizo likawa limekwisha. Naomba uwekaji mpaka huo ufanyike haraka ili kuondoa utata na pia migogoro kati ya wananchi na walinzi wa hifadhi.

Aidha, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kipindi cha kampeni aliwaambia wananchi wa Mbarali kuwa hapatakuwa na ongezeko tena la kupanua mpaka hivyo hapatakuwa na zoezi la kuhamisha watu tena. Alisema hapatakuwa na uhamisho wa kijiji wala kitongoji. Lakini kumekuwa na visingizio mbalimbali vya kutaka kuwahamisha wananchi na kuchukua maeneo yao ya mashamba na ya malisho. Hali hii imefanya Mbarali kuwa ngumu kuiongoza kutokana na wananchi kukosa imani na Serikali yao. Naomba jambo hili lizingatiwe kwa manufaa ya wana Mbarali na Chama cha Mapinduzi vinginevyo watu wasiokitakia mema Chama cha Mapinduzi na Mbarali hutumia mwanya huu na kutupaka matope viongozi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na minong'ono kwamba huenda wananchi wa Mbarali ni

chanzo kimojawapo cha kuzuia maji yasiende Mtera kuzalisha umeme. Kwa kifupi ni kwamba, Mbarali hatuna chanzo cha maji, Mbarali tumezungukwa na milima na hivyo mvua zikinyesha mito yote huleta maji bondeni maji yanapokuwa mengi kwa maana ya mvua za kutosha hujaza Ihefu na hutiririka kuelekea Mtera. Kilimo cha Mpunga Wilayani Mbarali huyatumia maji haya yanapopita lakini hawana uwezo wa kuyazuia kabisa kwani yanapotumika kuna mikondo inayoruhusu maji kuendelea. Mvua zikiwa chache wananchi wa Mbarali nao huathirika kwa kukausha mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ushirikiano wa Wizara katika kuweka mpaka kama tulivyokubaliana na vile ambavyo Mheshimiwa Rais aliwaambia wananchi wa Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya ni kubwa sana kieneo. Asilimia 46 ya Mkoa wa beya ni Chunya. Maliasili zilizopo Chunya ni hifadhi za wanyamapori za Rungwa, Katavi na Piti, Misitu na Nyaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maliasili zote hizi na ukubwa wa eneo, Wilaya ya Chunya haina gari la Idara ya Maliasili ili kusimamia maliasili hizi. Mwaka jana mwezi wa Nne Waziri wa Maliasili aliahidi Bungeni kuwa Wizara itatoa gari jipya kwa Idara ya Maliasili Chunya ikifika mwisho wa mwaka. Mwaka huo

umekwisha na mwaka mpya huu nao karibu unakwisha, kuna uvunaji haramu wa misitu hasa kwa mbao kwenye Misitu ya Rungwa na pia kuna uwindaji haramu kwenye hifadhi zote tatu nilizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara itoe magari ya kusaidia usimamizi wa maliasili Wilayani Chunya.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuanza kazi vizuri, pia nawapongeza Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanaoifanya wakiongozwa na Katibu Mkuu Mama Tarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni nyeti sana na ina wadau wengi na wenye maslahi binafsi, watu wengi watajitokeza kuwapatia ushauri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, naomba watafakari na kuchuja ushauri wa aina yoyote kutoka kwa mtu yoyote kamwe wasikurupuke kufanya maamuzi yanayohusu tasnia hii muhimu ambayo ina *potential* kubwa sana ya kuipatia nchi fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu pia kuutafakari ushauri watakaokuwa wanapewa na wataalam wao. Mara zote wawaulize kama ushauri wanaowapatia unazingatia sheria na kanuni zinazohusika. Hata michango ya Wabunge waichuje baadhi ya Wabunge wanachangia kwa jaziba na kwa kutoka jasho, lakini wakiwa na ajenda zao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uteuzi wa Watendaji na Wakurugenzi wa Bodi, siku zote wateue wataalam kwa kuzingatia sifa na uadilifu na uzalendo na uwezo na *track record* siyo kwa urafiki na udini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imebahatika kuwa na maliasili nyingi na vivutio vya watalii. Tunazo mbuga nzuri za wanyama 15. Tunazo *Game Reserve* na tunayo Hifadhi ya Ngorongoro kivutio kikubwa duniani. Mpaka sasa hatuja- *manage* vizuri Sekta ya Utalii. Hoteli zetu bado siyo nzuri sana, bado tuna changamoto ya kuendelea kujitangaza kama *the best tourist destination*, bado kuna changamoto ya kuendelea kuboresha mbuga za wanyama, *tour operators* wanahitaji kufundishwa somo la *customer care* namna ya kuwahudumia vizuri watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto ya ujangili katika mbuga zetu za wanyama. Naomba jambo hili Mheshimiwa Waziri alivalie njuga, baadhi ya watumishi katika mbuga zetu za wanyama siyo waaminifu wana uhusiano na majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Domestic Tourism*; mtikisiko wa uchumi wa mwaka 2008/2009 huko Marekani na Ulaya uliathiri sana idadi ya watalii waliotembelea vivutio vyetu vya utalii, mapato yalipungua sana. Katika hali kama hii ni muhimu ku-*promote domestic tourism*. Wizara na Mashirika yake wawe na mikakati ya kuwahamasisha Watanzania kupenda kutembelea mbuga za wanyama. Hii itasaidia wakati idadi ya watalii kutoka nje ikipungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji wa kitalii *(Tourist hunting),* bado Serikali haifaidiki sana na tasnia hii ya *hunting industry*. Kuna wajanja wengi katika sekta hii, kuna ujanja mkubwa upande wa *foreign hunters*. *Foreign hunters* hawataki kuwatumia *professional hunters* wazalendo au kuingia ubia nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Tume na Kamati ya wataalam chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Ntukamazina iliyoundwa na Waziri Diallo mwaka 2006. Wajumbe wa Tume hiyo walikuwa 10, wakiwemo Mheshimiwa Ndugai na Mheshimiwa Mzindakaya. Tume hiyo ilizungukia nchi nne, Botswana, South Africa, Zimbabwe na Msumbiji kuona jinsi nchi hizo zilivyokuwa zikisimamia Uwindaji wa Kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hiyo iliandika ripoti na kutoa mapendekezo sina hakika kama ripoti hiyo imewahi kufanyiwa kazi. Pamoja na mambo mengi mazuri tuliyoyaona katika nchi hizo tulifurahishwa na sera za usimamizi wa uwindaji wa kitalii, katika nchi za Zimbabwe na Msumbiji katika Mwindaji wa Kigeni haruhusiwi kuwinda bila kwanza kuingia ubia na *professional hunter* mzalendo kwa nini na sisi tusiwe na sera hiyo.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hongera Waziri kwa mipango mizuri ya Wizara pia kwa kusoma vizuri, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko na suala la Mjusi (*Dainaso*) aliyepo Ujerumani Berlin katika Museum ya Nature Kunde na mifupa mingine kuwepo Uingereza ambayo ilichukuliwa wakati wa ukoloni tarehe 10/1/1910. Mjusi huyo alichukuliwa mifupa yake tu mifupa kama hiyo hapa Duniani imeoneka Afrika ya Kusini na Marekani ya Kusini Los Angeles. Agenda yangu hapa ni kufuatilia mali zetu zilizochukuliwa Tanzania wakati wa ukoloni kwa faida yao, mjusi, vito mafuvu ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjusi huyo alichukuliwa Jimboni kwangu Lindi Vijijini, kwa hiyo ni mali zetu, urithi wetu, ni utamaduni wetu, ni elimu kwa vizazi vyetu na ni rasilimali yetu watu wa Lindi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kuwa Wajerumani hao wanazalisha pesa nyingi kutokana na mjusi huyo, kwa mwaka tu huzalisha bilioni tatu mia mbili na zaidi kwa kuingiza watalii laki tano (500,000). Sisi Watanzania au watu wa Lindi tunapata nini, Serikali leo itoe kauli, sisi tunapata nini kwa utalii wa mjusi yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 katika kikao cha Bunge la Africa *(Pan African Parliament)* ilipitisha azimio la kuunga mkono huo. Nchi zote za Afrika ambazo wanataka kurejeshewa mali zao basi ruhusa baadhi ya nchi zimechukua mali zao kama Ethiopia na Misri. *UNESCO* wapo tayari kusaidia harakati za urejeshaji na uhifadhi wa mali hizo Tanzania. Kwa nini hatufuatilii mali zetu. Hapa Tanzania tulituma ujumbe tarehe 7/5/2010 kwenda kuona suala la mjusi na kufanya mizunguko ya awali. Mazungumzo yalikuwa mazuri na waliwekeana *MoU* kati ya Wizara, Kitengo

cha Malikale na Makumbusho ya Tanzania pamoja na *Museum* ya Ujerumani Naturkunde (Berlin) wakiwemo *Director General* Profesa Dkt. Reinhold Leinfelder na *Head of Department of Exhibitions* Dkt. Ferdinand Damaschun.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walikuwa saba ambao ni Costancia Rugemamu, Mwenyekiti wa Makumbusho Tanzania; Donatus Kamamba, Mkurugenzi Mambo ya kale Tanzania; Mr Kayombo, Mkurugenzi Mkuu Tanzania Makumbusho;, Mr. Kihiyo Kaimu Mkurugenzi wa Makumbusho; Caroline Mchome, Mwanasheria wa Wizara Maliasili; Ndugu Thomas Ngawaia, Mjumbe wa Bodi ya Makumbusho na Fatuma Abdallah Mikidadi Mstaafu Bodi ya Makumbusho. Hawa wote walifanya mazungumzo. Serikali ituambie ile *MoU* imefikia wapi kuhusu Mjusi huyo. Makubalianao yetu kati ya Ujerumani na Tanzania tangu 7/5/2010 sasa yameishia wapi? Lindi wanataka kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme kuwa, Lindi nako kuna utalii, tunaiomba Serikali itupie macho. Lindi kuna *Culture Tourism*, utamaduni wa watu, vitu na kama Lindi kuna vivutio zaidi ya 23 kuna maboko wanaosema na watu wapo Kilwa, kuna *Dainaso* mwingine milimani Lindi Vijijini. Kuna Miji Mikongwe tangu *A.D* 900- 1700 hapo Kilwa kuna kumbukumbu ya vita vya Majimaji (Kinjeketile), kuna pango kubwa katika Afrika lipo Kilwa, kuna mbuga za Selous za uwindaji wa kitalii, kuna maeneo ya Pwani *KL* 449 kuelekea Dar es Salaam safi kwa utalii. Kuna *gas, gypsum,* dhahabu, *uranium,* yapo mambo mengi.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kusema kuwa nitakuwa tayari kuunga mkono hoja baada ya Mheshimiwa Waziri mara atakapotoa majumuisho anipe maelezo ya kina kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri anijulishe Wizara yake kwa kushirikiana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imefikia wapi katika harakati za kuyarejesha mabaki ya Mjusi kutoka Ujerumani na kwa sasa ni kwa kiasi gani Tanzania imeshanufaika kutokana na pato la mjusi huyo huko aliko? Je, Lindi eneo ambalo mjusi (mabaki) ametolewa wamenufaikaje na pato hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulinzi na hifadhi zetu; ni mara nyingi kwenye sekta ya utalii ndani ya hifadhi hutokea matukio ya ujambazi na mimi nikiwa ni mwakilishi wa wananchi nikiwa hapa Dodoma nimepokea vijana 62 waliomaliza JKT kwa lengo la kuniomba niwatilie mkazo kwa barua yao waliyoituma kwenye Ofisi yako wakiomba kupewa nafasi ya ulinzi kwa njia ya kujitolea. Kwa kufahamu umuhimu wa ulinzi kwenye hifadhi zetu na kwa kuwa wanaomba wanataka kufanya kazi hiyo kwa kujitolea, nilichukua jukumu la kumwandikia barua nikiambatanisha na majina ya vijana hao. Je, Wizara inalipokeaje ombi hilo la vijana hao walioonesha moyo wa uzalendo? Je, mchakato wa kuwapata walinzi unachukua muda gani wa wale wanaohitajika wanatakiwa na wawe na sifa zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa maswali yangu yote yatapata majibu na kushughulikiwa bila urasimu, nikiridhika nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, maliasili Tanzania inachangia kiasi gani kwenye bajeti ya Serikali? Je, Waziri anaridhika na kiwango hicho? Waziri ana mkakati gani wa kuongeza mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ruaha *National Park,* Mikumi *National Park, Kitulo National Tourist Areas,* Serikali ina mpango gani wa kuboresha. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri ya mwaka 2012/2013. Nawatakia utekelezaji wenye mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa Wizara hii, naomba kutoa rai zifuatazo kwa niaba ya wananchi wa Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvamizi wa tembo katika mashamba ya wananchi wa Tarafa ya Ngerengere, Bwakira na Kisaki. Tatizo la tembo kuvamia na kuharibu

mashamba ya wananchi kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, mwaka huu katika Kata za Mkulasi Mabuli Ngerengere na Kidugalo. Wananchi hawa hawana chakula hata kidogo, hivyo naomba Wizara hii iwalipe fidia mapema iwezekanavyo. Aidha, naomba Wizara itafute suluhisho la kudumu la kuzuia hawa wanyama wasitishie usalama wa chakula na wa raia. Hawa wanyama wanatoka pori tengevu la Selou. Hivyo, hata njia wanayopita inajulikana na hata majira wanayoanza uharibifu wa mazao yanajulikana, ni kwa nini wahusika wasijipange kuwazuia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio la mamba kwa wananchi katika Kata ya Tununguo na Mkulasi. Naomba Wizara ichukue hatua ya kupunguza hawa mamba katika eneo husika ili wananchi waweze kuondokana na hofu kubwa walio nayo. Aidha, kuna wanyama wengi waharibifu wa mazao, kwa mfano, nyani, ngedere, panya na nguruwe pori. Naomba wawaagize Maafisa Maliasili kutoa ushirikiano kwa wananchi katika kupambana na wanyama hawa waharibifu kwani wanachangia sana umaskini katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, naomba kukumbusha Wizara kuhusu ahadi yake ya mwaka 2010 ya kuchangia *cement* mifuko 150 na nondo 20 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mto Mbezi (Ruvu) katkika eneo la kijiji cha Lung'ala Kata ya Kinole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi hii haijatekelezwa mpaka leo na imewafanya wananchi wafikirie na

wahisi kwamba Serikali imewadanganya. Ahadi hii ilikuwa itekelezwe na mhifadhi wa *Selous Game Reserve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuiarifu Wizara kwamba bado Misitu ya Milima ya Uluguru inaendelea kuharibiwa kwa moto na ukataji wa miti. Tatizo kubwa ni umaskini, hivyo wananchi wanawinda ndezi kwa ajili ya kitoweo kwa kutumia moto. Wengine wanakata miti kwa ajili ya mbao ili wajipatie kipato. Hivyo napenda kushauri Wizara itoe ushirikiano katika miradi ambayo viongozi wa maeneo hayo wamekuwa wanaomba ufadhili kutoka Mradi wa Tao la Mashariki. Miradi hiyo ni pamoja na kilimo cha tangawizi, ufugaji wa kuku na sungura pamoja na nyuki. Miradi hii itapunguza vitendo vya uharibifu wa misitu ya Milima ya Uluguru.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Utalii ni moja ya sekta kubwa sana duniani inayokuza pato la Mataifa mbalimbali. Kwa upande wa Tanzania, Sekta ya Utalii imeonekana kuleta tija kwani imeendelea kuongeza ajira kwa Watanzania wanaotoa huduma kwa watalii, inachochea maendeleo, imeongeza miundombinu, majengo mbalimbali ya kisasa kama vile hoteli na kumbi za mikutano, imekuza biashara kama vile maduka yenye bidhaa za utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile sekta hii imevutia matukio mbalimbali kama maonyesho ya biashara na michezo. Sekta hii kwa ujumla wake imeweza kutambulisha kwa haraka uzuri wa nchi yetu kama namna ya kuwavutia watu wa Mataifa mbalimbali kufika na kujionea wenyewe uzuri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha *TTB* (Bodi ya Utalii) ambayo imeendelea na kazi kubwa ya kuitangaza nchi yetu kwenye Mataifa mbalimbali kuweza kuvutia watalii. Hata hivyo lipo eneo la muhimu sana ambalo bado halijatangazwa vya kutosha. Tanzania ina kumbi za mikutano zenye hadhi ya Kimataifa ikiwemo Arusha *International Conference Centre* ambayo ni mali ya Serikali. *AICC* imekuwa ikifanya mikutano mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo ule wa *ADB* uliofanyika mwaka huu. Hata hivyo, mikutano mingi imekuwa ikifanyika kutokana na juhudi za *AICC* wenyewe kujitangaza ambapo imekuwa ikipata mikutano michache ikilinganishwa na gharama zinazotumika kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali ili *convention centres* zote ziweze kufanya kazi ya msingi ambayo ni kutoa huduma ya kumbi za mikutano, ni vema ianzishwe *visitors convention Bureau* kwa ajili ya kutangaza sekta hii muhimu ya mikutano ya Kimataifa. Wageni wanaofanya mikutano pia watapata fursa ya kufanya utalii na hivyo tutakuwa tumeongeza pato katika nchi yetu kwa upande wa utalii na kwa kazi za Mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Serikali kuweka msisitizo wa *convention Bureau* kama ambavyo imeweza kuweka msisitizo kwenye *TTB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimtakie mfungo mwema wa mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pia nimpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumpatia Mheshimiwa Waziri Wizara hii na tumeanza kuona cheche zake. Uzuri wake Mheshimiwa Waziri anashaurika na ndio maana mchango wangu unajikita katika kumpatia ushauri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua uhusiano uko vipi kati ya Wizara na Wizara ya Mambo ya Nje katika masuala ya kuendeleza Utalii. Nasema hivyo kwa sababu ni muda mrefu watalii nchini mwetu sio wengi kama nchi zingine ambazo hazina mandhari nzuri ya kuvutia kama Serengeti, Ngorongoro *Crater,* Selous, mwambao mwanana wa Zanzibar. Nchi kama Cuba imewekewa vikwazo zaidi ya miaka 50 tangu 1961, lakini ina watalii zaidi ya 2,500,000 kila mwaka na Misiri zaidi ya milioni 10 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora Manispaa, Tembe la Livingstone, liko Kwihara, Kata ya Itetemia (Kipalapala) limesahaulika sana. Hali yake kwa sasa sio nzuri japokuwa mwaka jana Wizara iliahidi kuweka kisima cha maji ili iweze kusaidia kuvutia watalii wa nje na nyumbani ambao wangependa kuona mahali Dkt. Livingstone alipokutana na Stanley. Iko haja Tembe hili

likaangaliwa kwa makini kwani kuna kumbukumbu nyingi za kihistoria, lakini naomba kwa Mheshimiwa Waziri atilie mkazo; barabara itokayo kwenye barabara kuu itiwe lami mpaka kwenye Tembe la Livingstone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Wizara ya Maliasili na Utalii uliopitishwa tarehe 3 Juni, 2011 umeishusha hadhi Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki kutoka kwenye idara na kuwa kijisehemu, nadhani hasa kwa upungufu mkubwa sana. Hivyo nashauri suala hili liangaliwe vizuri ili sekta hii ikiwezekana iwe na idara kama ilivyopendekezwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asali kwa sasa ina bei nzuri sana na inaweza ikawa miongoni ya bidhaa ambayo inatupatia fedha nyingi za kigeni. Ningependa kumpa mfano Mheshimiwa Waziri wa mazao:

Mahindi magunia 20 x 30,000 = 600,000; Mpunga magunia 25 x 30,000 = 750,000 na asali mizinga 10 x lita 15 x 6 = 900,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la *nicotine* kwenye asali; kwenye utafiti wa kisayansi uliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine umebainika *nicotine* iliyopatikana katika maeneo ya Urambo Sikonge ambako kuna kilimo cha tumbaku ni 0.0042 na asali ya Dodoma, Same ambako hakuna kilimo cha tumbaku ilipatikana kati ya 0.00.33/0.0039 mg/kg.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *European Food Safety Authority Parma Italy Regulation no*

396/2005 *nicotine* ambayo haitakiwi ni lazima iwe 0.1 mg/kg. Hata hivyo, *nicotine* iko pia kwenye mimea kama vile nyanya, pilipili na hata viazi. Kwa maana hiyo basi iko haja ya Serikali kusimamia kwa nguvu zote asali ya Tabora ili iweze kupata bei nzuri.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika bajeti ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kimondo cha Mbozi ambacho nimekuwa nakisemea mara kwa mara hapa Bungeni bado hakijapewa uangalizi wa kutosha. Kimondo cha Mbozi ni moja ya vimondo vichache sana duniani ambavyo mbali ya kuwa kivutio cha utalii lakini pia kinatoa nafasi ya wanasayansi wakiwepo wanafunzi kujifunza mambo mbalimbali hasa mambo ya vimondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba kimondo cha Mbozi kinajengewa mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na kutangazwa sana nchini kote na duniani ili kupata watalii wengi zaidi. Aidha, kimondo cha Mbozi hakina machapisho au vitinyi vya kuwawezesha wanaofika pale basi waweze kujua historia ya kimondo cha Mbozi. Naomba pia Wizara ijenge jengo zuri ambalo litawafanya wageni wanaofika pale kupata mahali pa kupumzika. Naomba pia awekwe Afisa wa Wizara Mtaalam wa Vimondo ambaye anaweza kutoa maelezo mazuri na ya kisayansi kwa wale wote watakaotembelea eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina rasilimali za kusaza kuanzia misitu, wanyama, mapango na mengine mengi. Ni aibu kubwa sana kwa nchi yetu hii kushindwa kutumia rasilimali hii kujiletea maendeleo. Nafikiria tukiri kuwa hizi rasilimali tulizonazo zinageuka kuwa laana. Wizara na Serikali kwa ujumla ni lazima isimame kidete kurudisha imani ya watu juu ya rasilimali hizi. Ni fedheha kununua samani toka nje wakati mazao ya misitu yamejaa tele na Vyuo vya *VETA* vinaweza kutengeneza samani hizo. Serikali iwawezeshe wazawa kufungua na kufanya biashara karibu na maeneo ya utalii ili ajira nyingi zitengenezwe badala ya kuisha kuuza vinyago tu. Wazawa wakifungua hoteli kwa mfano ajira za ndani zitakuwa nyingi badala ya kuwapa wageni ambao watakuja na watu wao toka nje pia.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali ituondolee hii kadhia ya wanyama na nyara nyingine kuibiwa. Naamini nia ikiwepo watu hawa wanaofanya haramu hii watakamatwa na kuchukuliwa hatua stahili. Hali hii isipodhibitiwa tutaendelea kuwapoteza wanyama na nyara zetu na mwishowe tutawakosa hata hao watalii kwani watakuwa wamejikusanyia wanyama wetu huko kwao. Serikali ionekane ipo, katika hili wako watu wengi wanajitokeza na ushahidi nafikiri watafutwe wasaidie Serikali kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi ya namna Utalii unavyotangazwa kwamba inalenga

kuwanufaisha watu binafsi. Mfano mzuri ni ziara za nje kwa ajili ya mafunzo ambapo msafara wa watu wengi wanatumia pesa za walipa kodi, lakini mwisho wa siku hakuna faida inayopatikana. Mara zote watu wengi nikiwemo wamekuwa wakiiona nchi jirani ya Kenya ikifanya vizuri sana katika nyanja mbalimbali pamoja na kutangaza utalii nje. Tujiangalie tumejikwaa wapi na turekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi Serikali ilisikika ikitaka kuvunjwa na kubinafsishwa eneo la Mahakama Kuu ya Tanzania. Tukumbuke kuwa hii ni mojawapo ya mali kale ambayo ni fahari ya nchi yetu. Tusikubali kila kitu toka nje, maana mwisho wa siku tutachekwa na hao hao wanaotushawishi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuleta kilio cha watu wa Jimbo langu wanaoishi karibu na Mto Ruvu ambao baadhi yao wameshapoteza maisha yao kwa kuliwa na mamba. Wizara ieleze kinagaubaga namna itakavyowanusuru watu hawa ili nao waishi kwa usalama na pia wailinde rasilimali iliyo karibu na Mto huu.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kagasheki; Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu pamoja na maafisa na wafanyakazi wote wa Wizara yake kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa hotuba nzuri Wizara imefanya mambo mengi na ya tija katika kuinua na kuboresha shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa kutoa maoni yangu kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuwianisha maliasili na kuondoa umaskini moja moja.  Zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanaoishi vijijini wengi wanategemea kilimo na maliasili za misitu na mazao yake pamoja na wanyamapori kule ambako wanaruhusiwa kutumia.  Kwa hali hiyo, kuna uwiano wa karibu kati ya usimamizi wa maliasili na mikakati ya kuondoa umasikini ingawa sera na mikakati mingi ya Kitaifa inatambua uhusiano huu bado suala hili halijashirikishwa vizuri katika makabrasha ya mkakati wa kuondoa umaskini. Kwa sasa hali ilivyo ardhi na maliasili usimamizi na uratibu wake ulio kwenye Serikali kuu na maeneo ya vijijini na vitongoji vimekuwa nje ya utaratibu wa kupanga matumizi nje ya mipango ya Serikali kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii hata fursa zinazoweza kujitosheleza zinakuwa nje ya ngazi hizi. Ni maoni yangu kuwa kuimarisha kimkakati shughuli za usimamizi wa maliasili na kuondoa umaskini pamoja na kuweka uwazi na ushirikishwaji zaidi wa jamii katika kusimamia maliasili kutahamasisha zaidi kuondoa umaskini na kuimarisha utunzaji wa maliasili na kuboresha maisha ya Watanzania wengi wanaoishi vijijni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili la mchango wangu ni lile linalohusu kuwianisha maliasili wanyamapori katika usimamizi wa maliasili kwa ajili ya utalii na uboreshaji wa maisha ya jamii zinazozunguka maeneo ya maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri makazi ya watu yanavyoongezeka na kukaribia maeneo yanayolindwa (*protected areas*) yanajitokeza maswali juu ya haja ya kuendelea kulinda na kuzuia matumizi ya maeneo haya kwa wanadamu, kuna haja ya kuweka mipango ya usimamizi wa wanayamapori na maliasili nyingine zilizopo kuhakikisha kuwa zinaboresha utalii na hali ya maisha ya wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana nayo. Hii itaboresha maisha ya wananchi, kukuza utalii kwa kuhakiksha kuwa wananchi hawa wanatunza maeneo haya kwani wanafaidika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo napendekeza kuwa pale kwenye mwingiliano wa aina hii, juhudi zifanywe kuhakikisha kuwa watu na wanyama wote wananufaika kwa kushiriki kiutendaji kusimamia na kuendesha shughuli za kiutalii na jamii hizi. Kwa hivyo, wafundishwe na kuwezeshwa kuendesha miradi ya utalii. Jamii hizi wapewe hati miliki za maeneo wanayoendeshea miradi hii ili waweze na kupata mikopo na au kuingia ubia na wawekezaji wa ndani katika kuendesha miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inashauriwa kuhamasisha na kukabidhi usimamizi wa wanyamapori na maliasili nyingine katika jamii. Kuwapa umiliki wa ardhi jamii hizi, kuwapa elimu wananchi waishio kwenye maeneo haya juu ya utunzaji wa maliasili hizi, sayansi za wanyamapori, pamoja na magonjwa, utibabu, uratibu wa magonjwa na kutengeneza mipango kwa ujumla. Serikali na Wizara ijiunge na

Taasisi za Kimataifa zinazosimamia masuala ya afya na usimamizi wa rasilimali wanyamapori kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na maarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kampeni ya kutangaza vivutio vya utalii dunia nzima; napenda sasa nimalize kwa kuhimiza Wizara ya Maliasili na Utalii ipange jitihada za ziada kuutangaza utalii na vivutio vyote vya nchi nzima kwa sababu kwa kutofanya hivyo Tanzania inakosa watalii na kipato kikubwa kinachotokana na utalii. Tuone Tanzania ikitangazwa kwenye mitandao ya *Internet, blogs,* Runinga na *DSTV,* Ofisi za Ubalozi, *Video, DVD, CDs,* na Watanzania walioko nje ya nchi watumiwe kuuza ama kugawa vifaa hivyo kwa *Tour Agents.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mkuu wa Mkoa asaidiwe kutengeneza *DVD, CD* na *Video* ama filamu za *documentary* kuainisha vivutio vilivyopo, halafu Wizara iboreshe filamu hizi na kutengeneza machapisho yatakayoainisha vivutio Tanzania nzima na ibaki sasa Wizara kuratibu uendelezwaji wa vivutio hivi katika maeneo husika huku ikiwashirikisha kwa kiasi kikubwa wakazi wa jamii katika maeneo hayo kwa maendeleo yao na utunzaji wa vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuipongeza Wizara kwa mwelekeo mzuri mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. VINCET J.NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu kwa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi na pindi nipatapo nafasi pia nitachangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kukushukuru wewe na pia kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuionesha tangu waliposhika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi ambazo naziona katika Sekta ya Utalii ni uhamasishaji kwanza wa Utalii wa Ndani, *charity begins at home*, bado uhamasishaji wa utalii wa ndani ni mdogo sana na leo hata Mtanzania wa kawaida akienda nje ya nchi hawezi kusemea kwa kuutangaza utalii na utajiri wa nchi kwa kuwa kukosekana kwa uhamasishaji wa utalii wa ndani ambao ni tofauti na zamani. Hapa ni muhimu sana kwa Wizara kufikiria upya namna ya kuutangaza utaliii wa ndani kama ilivyo nchi ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Uchina leo utaona watalii wa ndani ni wengi kuliko watalii wa nje na pia ni watu(Wachina) wanaoweza kuutangaza sana utaliii wan chi yao kwa wageni kwa kuwa wanazo taarifa nyingi na sahihi za utalii wao na pia maeneo yaliyopo maeneo hayo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutahamasisha kwanza utalii wa ndani basi hapo baadaye tutaiona faida yake na uhamasishaji huu ni vizuri ukianzia katika shule za msingi, sekondari na vyuo kupitia *study tour* na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ingetenga kupitia nafasi za hifadhi na mashirika yake kuwapa Wabunge muda na safari za kutembelea kwenye vivutio vya kitalii ili nao waweze kuitangaza Tanzania kwa kuwa Wabunge wanapata sana sana Safari za nje ambazo zinawakutanisha na watu wengi tofauti na wenye uwezo wa kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu sana kuletewa watalii na nchi nyingine wakati wao pia wana vivutio, nalisema hili kwa kuwa hatuna Shirika la Ndege ambalo linaweza kuutangaza utalii wa moja kwa moja wa nchi yetu. Mashirika mengi ya Ndege yanazitangaza nchi zao mbali na juhudi za Serikali katika kuutangaza utaliii ila itafanya vizuri zaidi pale tutakapoimarisha Shirika letu la Ndege ambalo litaweza kuutangaza vizuri utalii na vivutio vilivyopo ndani na hapo tutaweza kusogea hatua moja mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa Wizara hii ikakaa na Wizara ya Uchukuzi kwa ajili ya kubuni mbinu ya kutumia mabasi ya ndani na yavukayo mipaka kwa kuutangaza utalii na pia kutumia Mashirika ya Nje ya Ndege kama vile *Emirates, Qatar, Ethiopian, Etihad* na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii na pia nitashukuru kama maoni haya yatazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba haya hayakuwepo toka mwanzo ila tu nakumbushia kwa

kuwa eneo hilo la hamasa za ndani zimekuwa hafifu kulingana na siku za hapo awali.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maliasili na Utalii ni fursa ambayo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu kuweza kukuza uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Hata hivyo kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za kiuchumi za misitu na uwindajji kwa mwaka 2011 kimepungua mpaka asilimia 3.5 kutoka asilimia 4.1 ya mwaka 2010. Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki ilikusanya shilingi bilioni 18.9 ikiwa ni kushuka kwa asilimia 59.3 kutoka bilioni 46.5 za mwaka 2010. Wizara itoe maelezo ya sababu za kupungua na kushuka huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hali hii imefanya pia shughuli ndogo za mahoteli na migahawa zinazojumuisha utalii kukua kwa asilimia 4.6 mwaka 2011 ukilinganisha na asilimia 6.1 mwaka 2010. Aidha, changamoto kuu imeendelea kuwa Sekta Ndogo za Wanyamapori na Utalii kuwa na mchango mdogo kwenye kuongeza ajira ukilinganisha na mchango wake kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, mkazo maalum uwekwe katika kuwezesha muunganiko wa mbele na nyuma (*forward and backward link ages*) kati ya Maliasili na Utalii na sekta zingine katika uchumi wa nchi ili kupanua wigo wa ajira kwa wananchi. Pia kuhakikisha ushiriki na manufaa ya ndani (*local content and participation)* kwenye uwekezaji mkubwa kwenye maliasili na utalii ambao

umetawaliwa na wawekezaji kutoka nje wakati mwingine kwa kutumia mawakala wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 102, ukurasa wa 48 kuhusu Sekta Ndogo ya Utalii, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, mamlaka zingine na wadau wengine ina mpango wa kuendeleza Jiji la Dar es Salaam kuwa kivutio cha utalii. Hata hivyo, nieleze masikitiko yangu kuwa kwenye mwaka wa fedha 2011/2012, niliomba Wabunge tushirikishwe kutoa mchango mkakati wa miaka mitano (2012/2017) kwa ajili ya kufanikisha azma husika, lakini sikupata mrejesho wowote. Naomba sasa kupewa nakala ya mpango mkakati huo kwa ajili ya kutimiza wajibu wa Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 63 wa kuishauri na kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa mpango mkakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Skta Ndogo ya Wanyamapori, aya ya 17 ukurasa na tisa (9) juu ya utekelezaji wa ahadi zilizotolewa mwaka 2011/2012 juu ya mipango ya uendelezaji wa mapori ya akiba, naomba majibu ya Wizara kuhusu uendelezaji wa Pori la Akiba la Pande katika Jimbo la Ubungo na Manispaa ya Kinondoni. Aidha, Wizara irejee ahadi iliyotoa Bungeni kufuatia maswali niliyouliza kuhusu pori husika ikiwemo kuhusu pendekezo nililotoa la kufanya pori husika kuwa hifadhi ya wanyamna mjini *(Urban Animal Park)* kama ilivyo katika miji mingine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi za chini ya Wizara hususan Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Tanzania, Shirika la

Hifadhi za Taifa, Wakala wa Huduma za Misitu, Mfuko wa Misitu, Taasisi ya Utafiti wa Misitu na Bodi ya Utalii ziingize Pori la Akiba la Pande kati ya maeneo ya kazi. Badala ya msitu huo kuwa na sifa mbaya ya eneo la mauaji ugeuzwe kuwa kivutio cha maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale, kwenye aya ya 66 ukurasa wa 31 na 32, Wizara imetoa mrejesho kuhusu uchimbaji wa urani katika pori la Akiba la Selous ambalo ni eneo la urithi wa dunia. Ni muhimu Kamati husika za kisekta za Bunge kupewa nakala ya nyaraka ya idhini ya kipekee na isiyokuwa ya kawaida (*exceptional and unique approval)* ya tarehe 2 Julai, 2012 iliyoruhusu kufanyika marekebisho ya mpaka wa eneo la urithi wa dunia kwenye Pori la Akiba la Selous. Hii itawezesha Wabunge na Bunge kutimiza vizuri wajibu wa Kikatiba wa kuishauri Serikali kuhusu shughuli za uchimbaji wa madini hayo unaokusudiwa kufanyika katika eneo la kilometa 215 za mraba ambalo ni sawa na asilimia 0.8 ya Pori la Akiba la Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Serikali irejee masula niliyohoji tarehe 15 Julai 2011 na tarehe 24 Julai 2012 wakati nikitoa maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani juuya Wizara ya Nishati na Madini ili kuwezesha mapato ya kodi ya ongezeko la mitaji (capital gain tax) kufuatila mauziano baina ya kampuni ya Australia na Umsi kuhusu eneo hilo na mkuju. Wizara ya Maliasili na Utalii ifuatilie ili sehemu ya mapito hayo ielekezwe katika uhifadhi wa mambo ya kale katika maeneo ya urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mapato kutokana na kifungu cha 87(A)(i) na kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010, ni muhimu kuwe na mgao kuelekezwa kwenye Mfuko Maalum wa Uhifadhi ya Maliasili kama fidia ya eneo la asilimia 0.8 lililotengwa kutoka katika urithi wa dunia kwa kuwa litaendelea kubaki kuwa Pori la Akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na idhini iliyotolewa na Kamati ya Urithi wa Dunia, *UNESCO* bado kuna hatua ya utafiti kuendelea na athari za uchimbaji kwa maeneo ya jirani na hifadhi katika aya ya 79 Wizara ya Maliasili na Utalii imeeleza changamoto katika utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2011/2012. Kati ya changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa watumishi katika Sekta za Wanyamapori, Misitu na Malikale hususan walinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza uwezo wa Vyuo vya Wizara wa kudahili, napendekeza kwamba Shirika la Hifadhi ya Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mfuko wa Misitu, Bodi ya Utalii na vyombo vingine vya Wizara vipanue wigo wa kudhamini wanafunzi kwa kutoa *scholarships* kupitia mapato yatokanayo na Maliasili na Utalii. Aidha, pamoja na uhaba wa walinzi lipo tatizo kubwa la uadilifu wa baadhi ya maaskari na watendaji wa vyombo vinavyohusika na ulinzi na maafisa wanaosimamia utawala. Serikali ieleze mikakati ya Tanzania iliyowekwa katika kushughulikia mitandao ya kifisadi inayohusisha hata baadhi ya watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza hotuba ya bajeti ya Waziri iliyosomwa leo. Pamoja na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa jitihada waliyoanza kuimarisha idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia maeneo machache tu, kwanza Wizara itafute mikakati ya kupambana na ujangili ambao unaongezeka siku hadi siku. Pili ugawaji wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii katika maeneo ya Jumuiya *(WMAs)* unafanywa na Serikali (WMU na Hazina) kama kifungu cha 66(1) cha kanuni za *WMA* kinavyoelekeza ugawaji unaofanyika unagandamiza *WMA* na hazitaweza kujiendesha kwani wanapunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *Block Fee TWPF 25% WMA 75%DC 0"%* Hazina 0%; *Game Fee TWPF 25% WMA 45% DC* 15% Hazina 15%; *Conservation Fee, TWP 25% WMA 45% DC* 0% Hazina 30%; *Observation Fee TWP25% WMA 45% DC* 0% Hazina 30% na *Permit Fee TWP 25% WMA 15% DC* % Hazina 60%. Kwa kawaida jumla ya fedha zinazopaswa kurudi kwenye WMA baada ya kutoka Hazina zinakuwa pungufu ya kiwango halisi kutokana na kukatwa kwa fedha nyingi na maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ina dhamira kuziimarisha *WMAs* haina budi kuzipatia asilimia 90% ili ziweze kukamilisha shughuli za uendeshaji wa *WMAs*. Makato ya fedha za makusanyo ni makubwa mno. Mfano:-

(i) Jumuiya ya Mungata iliyopo katika Wilaya ya Rufiji; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 44,124,807.50; mgao kwa *WMA* 16,043,780; Vijiji viwili, kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa 4,010,945.00;

(ii) Jumuiya ya Ikona iliyopo katika Wilaya ya Serengeti; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 46,103,850.00; mgao kwa *WMA* 16,763,359.00; Vijiji vitano , kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa1,676,335.99;

(iii) Jumuiya ya Nalika iliyopo katika Wilaya ya Tunduru; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 11,410,522.00; mgao kwa *WMA*4,148,865.98; Vijiji tisa, kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa 230,492.55;

(iv) Jumuiya ya Magingo iliyopo katika Wilaya ya Liwale; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 20,786,415.00; mgao kwa *WMA* 7,557,940.00; Vijiji tisa, kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa419,885.00;

(v) Jumuiya ya Ipole iliyopo katika Wilaya ya Sikonge; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 57,781,327.50; mgao kwa *WMA* 21,009,290.68; Vijiji vinne, kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa 2,626,161.34;

(vi) Jumuiya ya Mbomipa iliyopo katika Wilaya ya Iringa; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 10,701,288.00; mgao kwa *WMA* 3,890,988.00; Vijiji ishirini

na moja, kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa 92,642.58; na

(vii) Jumuiya ya Enduimet iliyopo katika Wilaya ya Longido; makusanyo kwenye *WMA* yalikuwa 25,086.55; mgao kwa *WMA* 9,121,471.00; Vijiji tisa, kiasi cha gawiwo kwa kila Kijiji kilikuwa 506,748.41.

Mheshimiwa Spika, jedwali linaonesha hapo juu baadhi ya vijiji mgawo wanaopata ni chini ya sh. 1,000,000.00. Kwa mtindo huu *WMA* watakata tamaa na kuua WMA. Ombi langu ni katika maeneo mawili kwanza, *WMAs* wamekwishapewa *use right* kwa WMAs 14 nchini. Kwa hiyo basi, wapewe kuwatafuta wawekezaji na kuwaruhusu wachaguwe watakaowataka wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapewe makusanyo asilimia 90% ili waweze kujiendesha na kulinda majangili kwenye *WMAs* pamoja na kuwalipa askari na waajiri wengine ambao wataajiriwa na *AA* kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini kwa nini Hazina au Halmashauri wachukue kwenye *WMAs,* kinachotakiwa ni kutoa kodi tu. Serikali ikiendelea kuchukua kiasi kikubwa cha mapato basi *WMAs* zote nchini watashindwa kujiendeleza. Pili, ujangili utaendelea kukua kwenye maeneo yote ya *WMAs* zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, makusanyo yatokanayo n uwindaji wa kitalii kutoka *WMA* yasipelekwe Hazina bali yabakizwe kwenye Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori *(TWPF)* na kutumwa kwenye *WMA* kwa wakati badala ya kuingizwa kwenye bajeti ya Wizara na kuombwa Hazina, hurudishwa kiasi pungufu na wakati mwingine kucheleweshwa kwani Jumuiya inategemea fedha hizo kuendeleza ulinzi wa wanyamapori kwa askari wanaolinda maeneo ya *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea Waziri atajibu masuala ya mgao huu.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii yenye dhamana ya kusimamia rasilimali za Maliasili na Malikale na kuendeleza utalii. Ni matumaini yangu na matumaini ya Watanzania wengi kuwa Mheshimiwa Waziri ataifanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinalindwa na kuwanufaisha Watanzania wote hasa wanaozunguka maeneo ya hifadhi, misitu na fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapango ya Amboni Tanga, ni moja ya maajabu Duniani chini ya ardhi ya asili. Mapango haya ni makubwa zaidi katika Afrika ya Mashariki na yanavutia sana. Mapango ya Amboni ni eneo zuri la kupumzika, kwa tafiti za kihistoria, kijiografia

na kijiolojia. Hata hivyo, inasikitisha kuona kuwa mapango haya hayapewi umuhimu mkubwa na Wizara hasa katika kuyatunza na kuyatangaza ili kuvutia watalii wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimefarijika kusikia na kusoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara itaanza ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa katika kituo cha Mapango ya Amboni. Hatua hii ni ya kupongezwa sana. Hivyo nitoe rai kwa Wizara kuhakikisha ujenzi wa kituo hiki unafanyika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ujenzi wa Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu umepangwa, nitoe rai kwa Wizara pia kuwa na mkakati mahsusi wa kutangaza na kuendeleza Mapango ya Amboni ili kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi. Hatua hii itaboresha maisha ya wakazi wa Wilaya ya Tanga na pia kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya Watanzania wa leo na vizazi vijavyo yanategemea maliasiili ya nchi. Tanzania imebahatika kuwa na rasilimali nyingi ikiwemo misitu, wanyamapori, mito, maziwa na maeneo kinamasi. Rasilimali hii ni muhimu kwa utoaji wa huduma kiuchumi na kijamii. Kufifisha rasilimali hii ni kuharibu mazingira endelevu ya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi, taasisi za kijamii na washikadau wengine, wana wajibu mkubwa katika kufanikisha maendeleo endelevu ya sekta hii. Hii inatokana na ujuzi na utaalam walionao, mchango wao ni muhimu na utaongeza uwekezaji, utaboresha biashara na uendeshaji kwa ujumla, pia utatoa nafasi kubwa ya ajira kwa vijana. Ni wajibu wa Wizara kutilia mkazo sekta hii ili kujikwamua katika dimbwi la umasikini wa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina misitu na mwitu. Kuna misitu iiyopandwa na kulindwa kama vianzio vya maji. Misitu hutoa hifadhi kwa wanyama, ufugaji wa nyuki, misitu pia huchangia pato la Taifa. Thamani ya misitu Tanzania ni ya juu kwa sababu huongeza mapato ya nchi kutokana na mazao ya kuuza nje pamoja na mapato ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kuwa na umuhimu wake lakini sekta ya misitu ina matatizo yake mojawapo ni ukataji miti hovyo, viwanda vya mazao ya mbao visivyo na ufanisi na miundombinu duni, ushirikishwaji wa washikadau katika kusimamia rasilimali hiyo, ukosefu wa vituo vya takwimu na kutokuwepo mipango ya kutumia rasilimali ya misitu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa sekta hii umegubikwa na matumizi madogo japo rasilimali iliyopo ni kubwa vilevile rasilimali hii ina uwezo mkubwa wa kutoa bidhaa zisizo za mbao. Huduma mbalimbali kama utalii, wanyama, mazao ya nyuki, vinahitaji kuendelezwa vizuri. Matumizi na usimamizi wa rasilimali

hii unahitaji usimamizi wa misitu wenye kuzingatia wingi wa matumizi na uboreshaji wa soka na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii Tanzania ni sekta yenye uwezo wa kukua sana kiuchumi. Tanzania imebahatika kuwa na vivutio vingi vya utalii. Tanzania inashinda nchi nyingi kwa kuwa na wanyamapori wengi, mandhari ya kuvutia, fukwe za bahari na vivutio vingi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukubwa wa nchi unatoa nafasi ya kuendeleza shughuli za utalii. Tanzania ni mahali pa pekee katika Afrika ambapo kuna maajabu ya mimea na viumbe visivyopatikana kwingine. Kilimanjaro ni Mlima Mrefu kuliko yote Afrika wenye theluji ingawa sasa inapungua lakini ni kivutio kikubwa ambacho kinaipa haiba nchi na kutambulika lakini tumelala, tumewaachia Wakenya wautangaze na kuupigia debe na mwisho kuwafanya watalii waingize fedha za kigeni huko Kenya badala ya kuja moja kwa moja Tanzania kwa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii bado haijafanya shughuli zake. *TANAPA* na Ngorongoro wote kwa pamoja wanajukumu la kutangaza vivutio hivi kwa kuvipiga picha na kuvisambaza nje na ndani ya nchi kwa kutumia njia mbalimbali kama vile matangazo yanayotangazwa Malyasia. Matangazo yake ni ya kuvutia kama tangazo lake la *'Malyasia True Asia'.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio yanayojitokeza ya kuuliwa kwa watalii, kuporwa au kupigwa na kuibiwa, hii itaiweka Tanzania katika ramani mbaya. Ni

wakati sasa wa Serikali kutoa kauli ya kuwataka wale wote wataokamatwa kuwachukulia hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atapokuja kufanya majumuisho, atueleze lile tukio lililojitokeza Arusha kwa kuuliwa watalii limefikia wapi? Kuna hatua gani zilizochukuliwa mbali na ile ya yeye kwenda katika sehemu ya tukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wimbi la wizi wa nyara unaendelea pamoja na upungufu wa wanyama. Kuna sensa yoyote ile iliyofanywa kwa wanyama kama Tembo, Simba, Twiga, Faru na kadhalika kwani wimbi la kuuliwa kwa baadhi ya wanyama linasababisha kuwa na upungufu mkubwa wa wanyama hawa mbali na wanyama hawa kuhama wenyewe. Napenda kumuuliza Waziri sensa hii ilifanyika mwaka gani? Je, kuna ongezeko au upungufu wa wanyama hao? Kama Wizara kuna mpango au mkakati gani wa kuzuia wimbi hili la wizi wa nyara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kunahitajika elimu ya kutosha kuwahimiza Watanzania kufanya utalii katika mbuga hizi hata ikiwa itawezekana kuwe hakuna malipo ili waweze kujua nchi yao ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu pamoja na mashirika ya utalii, wawe na programme ya kuwataka wanafunzi kutembelea mbuga hizi na sio kwa zile shule zenye uwezo tu. Hii itasaidia wanafunzi kujua jiografia ya nchi yao na vilivyo ndani ili wakipata nafasi hiyo kuwafunza

wazazi wao na wengine walio nje ya nchi. wanafunzi hawa watakuwa kama ni mabalozi wa nchi.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa. Upanuzi wa wigo wa utalii *(widening of tourism base)*. Kama vile tunavyozungumzia katika fedha juu ya upanuzi wa *tax base* yaani kodi, ni muhimu upande wa utalii, Wizara ikapanua shughuli za utalii ili kuongeza siku anazokaa mtalii nchini lakini pia watalii wanapokuja Tanzania waweze kurudi Tanzania wakijua kuwa kuna vivutio vingine ambavyo wanaweza kuvipata. Msisitizo uwekwe kwenye *cruise tourism* katika Ziwa Victoria na Maziwa mengine, utalii wa utamanduni, Tanzania kuna makabila zaidi ya 120 na hivyo kuna mambo mengi ambayo watalii wataweza kuona. Hii pia itaongeza kipato kwa wananchi mbalimbali nchini. Watalii pia wataweza kutembelea majengo ya zamani na kujifunza na kufurahia historia ya maeneo haya. Hii itapanua utalii nchi nzima na Halmashauri zitaweza kushirikishwa kupanga mipango hii lakini pia wafanyabiashara katika ngazi za Wilaya na Mkoa wataweza kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utangazaji wa utalii ni muhimu sana. Fedha ambazo zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya kutangaza utalii zimekuwa kidogo ukifananisha na fedha za nchi jirani. Kwa mfano Tanzania inatumia asilimia $^{1}/_{8}$ ya fedha zinazotumika Kenya na asilimia $^{1}/_{35}$ ya fedha zinazotumika Afrika

Kusini. Ni muhimu kama tunataka kuwa *serious* katika sekta hii muhimu fedha zaidi zitengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii na usafiri. Wakati watalii wanakuja Tanzania kununua tiketi kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni karibu asilimia 60 ya fedha zote ambazo mtalii hutumia ni kwa ajili ya tiketi. Kama nchi ina ndege yake au ndege ambayo kuna '*shares'* nyingi za nchi yake basi angalau sehemu ile ya asilimia 60 inakwenda katika nchi ile. Hivi sasa Tanzania ina ndege kama moja tu au Tanzania ina hii ndege lakini haifanyi safari za nje. Hapa Tanzania kuna ndege ya *Precision* ambayo hivi karibuni iliuza *share* kwa Watanzania na mashirika mbalimbali ijapokuwa *Precisian* ilishawishi Serikali kununua *share* lakini Serikali haikufanya hivyo, kama ingefanya hivyo basi angalau Tanzania ingekuwa na '*voice'* katika Bodi ya Ndege ya *Precision*. Hivi karibuni *Precision* inaandaa safari kwenda nje ya nchi katika masoko ambayo watalii wetu wanatoka. Hivi sasa Watanzania wanamiliki asilimia 59% ya shares zote za Precisian. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais alifungua karakana ya kutengeneza ndege za *Precision* na inasemekana alisema bila ya ndege za *Precision* sijui Tanzania ingekuwa wapi katika usafiri wa anga. Nafikiri hatukuchelewa, ni vizuri Wizara ikawasiliana na Wizara ya Uchukuzi ili kuona kama tunaweza kurekebisha jambo hili ili mapato zaidi kutokana na watalii yaweze kubaki hapahapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. Wizara hii ya Maliasili na Utalii ni sekta ambayo mchango wake katika Taifa hili hauna mfano kwani vivutio vilivyomo nchini mwetu ni vingi na vinaongoza kwa kuwavutia watalii kutoka nchi za nje pamoja na utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Wilaya mpya ya Mbogwe, Bukombe na Kahama, tunalo Pori la Akiba la Kigosi ambalo linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ujangili unaosababisha upungufu mkubwa wa wanyama katika maeneo ya pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa sekta hii katika kuchangia mapato kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ambayo ni Wilaya mpya ya Mbogwe, inaonyesha dhahiri kuwa mchango ni hafifu sana ikilinganishwa na mapato ya fedha zilizotumwa kwenye Halmashauri za Wilaya (asilimia 25%) kutokana na uwindaji wa kitalii mwaka 2010/2011 na 2011/2012 na makisio kwa mwaka 2012/2013. Bukombe mwaka 2010/2011 shilingi 2,204,145.81, mwaka 2011/2012 shilingi 1,554,581.95, mwaka 2012/2013 makisio shilingi 2,667,016.43 ukiangalia utaona ni kwa jinsi gani mchangao wa asilimia 25% ya mapato ya uwindaji wa kitalii uko kwa kiwango cha chini sana hasa kutokana na udhaifu mkubwa wa utangazaji wa Pori la Akiba la Kigosi, pia kutokuwepo kwa mwekezaji mwenye nia njema ya kuliendeleza pori hili. Naishauri Wizara na Serikali kwa ujumla iweke kipaumbele katika kuongeza fedha za maendeleo kwenye bajeti ili hatimaye

miundombinu hasa katika Mapori ya Akiba ikiwemo Kigosi yaweze kujengewa miundombinu ya uhakika ili kuboresha huduma za kitalii ili ziweze kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la shughuli za utafiti wa madini ya dhahabu katika kitalu cha *Kigosi North*, kimetengwa katika uwekezaji kwa kisingizio kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe imetoa kibali cha kufanyika kwa utafiti katika Pori la Akiba la Kigosi. Kwa hakika, ukweli ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe haijawahi kutoa kibali cha kufanyika kwa utafiti huo katika eneo la kwa Rwahika. Naishauri Wizara ichukue hatua kwa ukiukwaji wa Sheria ya Wanyamapori Na.5 ya mwaka 2009 inayoruhusu uchimbaji wa madini ya urani, mafuta na gesi ndani ya Mapori ya Akiba. Utafiti wa madini ya dhahabu katika Pori la Akiba Kigosi ni kinyume cha Sheria Na.5 ya mwaka 2009. Naomba Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iweke kipaumbele katika kuongeza fedha katika eneo la miradi ya maendeleo, kuongeza watumishi hasa walinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Naibu Waziri, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Nampongeza sana Mheshimiwa Balozi

Kagasheki kwa kazi nzuri aliyokwishaifanya tokea ashike wadhifa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Bibi Maimuna Tarishi, Katibu Mkuu, Bibi Nuru Milao, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara pamoja na Wenyeviti wa Bodi ya Watendaji na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza ufugaji wa nyuki. Ufugaji nyuki ni moja ya miradi yenye gharama ndogo sana. Ufugaji nyuki unaweza kuwa mkombozi wa vijana wengi wasio na ajira wala kipato hivyo kuendelea kuwa ombaomba. Tatizo kubwa katika kuendeleza tasnia hii ni upungufu wa Maafisa Ugani na mtaji kwa vijana walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri idadi ya wakufunzi wanaodahiliwa Chuo cha Nyuki Tabora iongezwe ili wanapohitimu waajiriwe na kupelekwa kwenye ngazi ya Kata ili watoe mafunzo na ushauri kwa vijana, waanzishe ushirika wa ufugaji nyuki. Aidha, Serikali iruhusu wahitimu wa Chuo cha Nyuki waajiriwe moja kwa moja mara wanapohitimu. Wizara ianzishe Mfuko wa Ufugaji Nyuki kwa lengo la kutoa mikopo kwa ushirika wa vijana wafugaji nyuki nchini. Tukumbuke kuwa asali ni chakula, dawa na zao muhimu sana la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji miti. Kiasi cha mvua inayopatikana maeneo mbalimbali ya nchi yetu imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Hii imeathiri sana uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na

ustawi wa wananchi wetu. Moja ya sababu za kupunguza mvua ni kukosekana kwa baioanuai muhimu kutokana na vitendo vya uharibifu wa wanadamu. Kwa kuzingatia Maazimio mbalimbali ya Jumuiya ya Kimataifa juu ya mbinu za kulinda miti na baioanuai katika nchi zetu ikiwemo motisha ya '*carbon credit'* nashauri yafuatayo:-

(i) Ipitishwe Sheria ya Upandaji Miti itakayoweka masharti ya kila raia mijini na vijijini kushiriki kupanda na kutunza miti.

(ii) Sheria iweke sikukuu ya kupanda miti ambayo itasherehekewa kikanda kutegemea msimu wa masika. Nchi ya Israel imefanikiwa kugeuza ardhi yake kuwa ya misitu kwa kutumia utaratibu huu. Nilipokuwa mwanafunzi huko, nilishiriki sherehe hizo kwa kupanda miti badala ya kusoma au kufanya shughuli nyingine kwa siku hiyo.

(iii) Wananchi wasaidiwe kupata malipo chini ya mpango wa Umoja wa Mataifa wa '*Carbon Credit'*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wananchi na jamii kutunza miti. Ili kulinda misitu yetu, uhusianao mwema na ushirikiano baina ya uongozi na watumishi wa miradi ya misitu na jamii inayozunguka ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali hiyo. Katika Wilaya ya Arumeru, uhusiano wa jamii na mradi wa Meru, si mzuri sana. Hii imeathiri kwa kiasi fulani maendeleo ya mradi huo. Kwa mfano mwaka 2010/2011, upandaji miti ulichelewa kwa sababu ya uvamizi uliofanywa na

wananchi hususani Kata ya Bangata na kadhalika. Chanzo cha malalamiko hayo ni wananchi kudai kuwa kuna ubaguzi katika ugawaji wa maeneo yaliyovunwa ambapo watu hugawiwa walime na kuotesha mazao ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini kuwa kufuatia mabadiliko ya Meneja wa mradi huo, uhusiano wa mradi huo utaboreshwa kwa menejimenti kuwa karibu na kushirikisha wananchi kwenye shughuli za utunzaji na ulinzi wa misitu. Vilevile nashauri kuwa mradi utumie sehemu ya mapato yake kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi maalum, wananchi wa Kata ya Olmotonyi waliwasilisha ombi la eneo dogo lililoingia kwenye kijiji cha Ngaramtoni ili wajenge shule ya sekondari kwa kutumia fedha walizopewa na mfadhili mmoja. Naomba ombi hili lipokelewe kwani eneo hilo halitaathiri msitu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nathibitisha kuwa naunga mkono hoja hii. Nawasilisha.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumpongeza kwa dhati Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti ya kisayansi na inayotekelezeka. Ni imani yetu kuwa iwapo bajeti itatekelezwa jinsi ilivyopangwa, ni dhahiri kuwa

maendeleo makubwa yatafikiwa kwa Taifa letu na kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine kuendesha mafunzo ya kupanga hoteli katika daraja na wanatambulika na wanaweza kufanya zoezi la kupanga hoteli katika daraja kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni hatua kubwa iliyofikiwa katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hoteli nyingi zilikuwa zikijipangia madaraja kwa jinsi walivyopenda kwa kuwa sasa wataalam wamekwishapatikana, je, Serikali itatoa kauli gani kuhusu hoteli zilizojipangia madaraja? Je, zoezi la kupanga madaraja kwa hoteli kwa kutumia wataalam waliofuzu litaanza lini? Je, wataalam hao watahusika pia kupanga madaraja kwa *Lodgings* pia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wataalam wa kupanga madaraja kwa hoteli waje Kondoa kwa zoezi hilo. Ili kufanya zoezi hilo, kuna utaratibu gani unaofuatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Akiba ya Mpanga imeleta hofu na mgogoro mkubwa kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hii baada ya

*TANAPA* kutaka kubadilisha mpaka wa awali na ambao wananchi walifidiwa ijapo si kikamilifu na kutaka kuongeza maeneo mapya. Jambo hili halikubaliki na wananchi hao kwani hakuna kwa kuwapeleka na sasa hivi idadi ya wananchi imeongezeka sana na kuitaka Serikali ione haja ya kuwafidia wananchi hawa kuwa huru ndani ya nchi yao. Nashauri Wizara ikae na wananchi hawa kufikia muafaka. Ni vyema na kwa maslahi ya Taifa kupata muafaka haraka ili wananchi waendelee na kujenga huduma za kijamii na kiuchumi zikiwemo shule, zahanati na kadhalika. Vijiji hivyo ni Malangali, Mpanga, Mambegu, Mtapa, Ludiga, Hanjanam na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kuona ziara hiyo mimi kama Mbunge wa Jimbo hilo la Njombe Magharibi nitashirikishwa.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Balozi Khamisi S. Kagasheki na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwa kazi nzuri wanayofanya. Naomba kutumia fursa hii kuishauri Wizara katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi jirani na mashamba ya miti ya Serikali wapewe kipaumbele ili nao waone manufaa ya uwepo w mashamba haya maeneo yao. Kila mara wakiomba mgao wa kuvuna hawapati na hivyo kuwafanya waamini kwamba Serikali haioni umuhimu wao na

mashamba yale ni kwa ajili ya matajiri wachache wenye mitaji mikubwa ya kuvumilia vyenzo za upasuaji tu. Kwa hali hii ili ku-*balance interests* ni vema kukawa na migao ya aina mbili; ule wa wenyeji na ule wa wenye mitaji. Hili ni jambo kubwa sana kama kweli dhana ya uhifadhi shirikishi tunataka ipokelewe vyema na kuyafanya mashamba na misitu hii kuwa endelevu. Mashamba haya yawe chachu ya maendeleo kwa wananchi wanaoishi jirani nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishauri Wizara juu ya taratibu za uwindaji wa kienyeji na ule wa kitalii. Uwindaji wa kienyeji umegubikwa na urasimu wa Maafisa Wanyamapori wa Wilaya na wale wa Kanda (*Antipoaching*) kwa kuzuia kwa makusudi wananchi kuwinda kulingana na *Quota* zilizotolewa. Hili nalo linaleta hisia mbaya kwa wananchi wenye uwezo mdogo wa kununua wanyama kama baadhi ya matajiri wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji wa kitalii unafanywa bila usimamizi madhubuti wa Wizara. *PH* hawapati usimamizi mzuri wa Maafisa Wanyamapori wakati wa uwindaji mfano ni kule Sikonge ambako kuna Afisa Wanyamapori mmoja ili hali kuna vitalu takribani 11 vya uwindaji. Huyu mtu peke yake hawezi kusimamia ipasavyo hawa *PH* wote walioko katika vitalu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi ni namna wenye vitalu hivi wanavyodharau mamlaka za Wilaya, Mikoa na Vijiji ambavyo vinastahil kunufaika na uwepo wa vitalu hivi katika maeneo ya vijiji. Taratibu za kupata

migao ya kuwinda kila mwaka hazifuatwi na wawekezaji wenye vitalu na pia watendaji katika Wizara. Taratibu hizi zikifuatwa, Vijiji, Wilaya na Mikoa itaheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ina nafasi kubwa katika kuongeza pato la Taifa letu. Tanzania imebahatika kuwa na vivutio vingi Duniani zaidi ya vivutio vya utalii 15 yakiwepo Maporomoko ya Maji, Mbuga za Wanyama, Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Sekta hii ambayo ni ya pili katika kulipatia Taifa letu pato bado inakabiliwa na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inakabiliwa na uchache mkubwa wa hoteli, huduma zinazotolewa ziko chini ya viwango vya kimataifa, kipato kinachopatikana hakitumiwi vizuri. Aidha, miundombinu iko chini ya viwango vinavyotakiwa kimataifa. Uhaba wa vitendea kazi na rasilimali watu, Serikali iangalie jinsi ya kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana kwamba vivutio vya utalii ni kwa ajili ya watalii na wazungu kutoka nje tu. Bado hakuna msisitizo wa kutangaza utalii wa ndani. Somo la utalii litolewe shuleni ili kujenga utamaduni wa jamii wa kupenda kutalii ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii hapa nchini haiko makini, inafanya kazi zake kwa kubahatisha. Si jambo zuri kusikia kwamba watalii wanaoingia hapa nchini hawafikii milioni moja, suala la utalii halijapewa kipaumbele. Napendekeza Bodi hii ivunjwe na *TANAPA* itangaze vivutio vya utalii bila kutegemea Bodi. Bodi ibakie kutoa ushauri tu au vinginevyo ivunjwe. Ngorongoro pia ijitangaze yenyewe bila kutegemea Bodi hii. Wale waliopewa dhamana katika sekta hii wanatakiwa kuwajibika na wale wote ambao watabainika kushindwa basi wawajibishwe kwa kushtakiwa Mahakamani na kuondolewa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwamba kuanzia mwaka 1989 hadi 2010 karibu ¼ ya meno ya Tembo yaliyokamatwa Duniani, *DNA* inaonyesha kwamba Tembo hao wanatoka Tanzania. Ujangili wa kisanyansi unafanyika lakini kutokana na ukosefu wa Askari wa kutosha, Tembo wengi waendelea kuuwawa kila mwezi. Ni kwa nini Jeshi letu lisishirikishwe katika kufanya operesheni maalum ili kukabiliana na changamoto hii? Hivi tamko la Serikali kuhusu wale wote waliopewa dhamana katika sekta hii ya utalii na hasa Idara ya Wanyamapori na hawakuwajibika ipasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga na hifadhi ya *Selous* haitangazwi ipasavyo. Ndani ya *Selous* kuna madini ya aina nyingi, *uranium*, dhahabu lakini mbuga hiyo imeachwa kama kichaka cha ujagili. Tembo katika hifadhi hii wanauawa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yanayohitaji kutangazwa vizuri ni Kilwa, Mapango ya Amboni na kadhalika. Bodi ya Utalii imeshindwa kutangaza utalii itawezaje kutekeleza mikakati mipya ya miaka mitano ya utangazaji utalii kimataifa? Huenda waliopo katika Bodi hawana *interest* na utalii, wapo tu kujaza nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE.ANNA MARYSTELLA J. MALLACK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina umuhimu wa kipekee katika kuliingizia pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania. Serikali isimamie kuimarisha miundombinu imara ili kuleta ufanisi mzuri na rahisi kufikiwa maeneo ambayo ni magumu kufikika mfano hifadhi ya Katavi. Hifadhi hii ina uwezo mkubwa wa kuliingizia pato Taifa sababu ina sifa zinazoonekana, ina wanyama wakubwa wanaopendeza kuangalia kama Simba, Tembo, Twiga, Nyati na kadhalika. Kuna madini ya dhahabu sehemu ya Kapapa ndani na pembezoni mwa hifadhi hiyo. Hivyo Serikali ikiwa na mikakati mizuri ya dhati na ubunifu, Tanzania ni nchi tajiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watalii wengi wanashindwa kufika sababu ya ubovu wa miundombinu kama barabara zisizopitika hasa kipindi cha masika, nyumba za watumishi na ukosefu wa magari ya kukagulia hifadhi. Naiomba Serikali izingatie haya. Nyumba za watumishi wa hifadhi mfano Katavi zimechakaa kiasi cha kuchusha. Ziboreshwe nazo ziwe

chachu ya kuangalia maliasili na utalii. Pia familia za Askari hao wa Wanyamapori wawe katika usalama kwani wanaishi porini na wanyama wanazunguka mpaka maeneo ya makazi ya Askari hao. Wakati mwingine wanyama hao huleta madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara, Serikali ihakikishe barabara kuu ziendazo hifadhi zinatengenezwe kwa kiwango cha lami ili watalii washawishike kufika mara kwa mara bila kuogopa usumbufu. Serikali ijenge madaraja yaliyo mafinyu ili yapitike mfano kutoka kijiji cha Stalike (Mpanda) kuelekea hifadhi ya Katavi kuna Mto unaohifadhi viboko wengi lakini daraja hilo ni finyu sana na kona yake ni mbaya. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua daraja lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sumbawanga tuna kivutio cha maporomoko ya Karambo, ni kivutio kizuri ambacho watalii wamekuwa wakifika pale kutoka Zambia wakati Watanzania hatujitokezi sana na kuona kama hakuna umuhimu. Hii yote ni kukosa ubunifu. Serikali ikilisimamia hili, aidha, kukaribisha wawekezaji waboreshe maporomoko hayo kwa kujenga hoteli ya kitalii na kukoleza vivutio, italeta maana nzuri na kuvutia zaidi watalii. Kwani Tanzania sisi ni nchi tajiri lakini tunakosa ubunifu. Naiomba Wizara kuvaa taswira ya ubunifu kwani wageni wanapofika na kufaidika na rasimali zetu huku sisi tumetulia na hatuoni kama kuna umuhimu, ni aibu kwetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma na uhamasishaji. Pamoja na kushirikisha jamii katika

uhifadhi na uendeshaji wa malikale na Shirika la Utangazaji la Taifa kuandaa, kurusha vipindi 10 kuhusu malikale kupitia *television* katika kipindi cha Zamadamu. Naiomba Serikali kupitia Wizara ilenge kutoa elimu kwa umma ili watambue faida ya kulinda maliasili yetu na utalii pia watambue hasara athari ya kuharibu maliasili na utalii wetu ili wananchi ambao ndiyo umma waepuke kuua wanyama hovyo kama uwindaji haramu wa kuua Tembo na kuchukua meno yake na ngozi za Chui na wanyama wengine kwa kuuza nyama bila kibali na hii ipo mpaka sasa tena kwa wingi Mkoa wa Katavi. Umma wa vijijini wanahitaji elimu sana kwani wengi hawaangalii *television* bali *radio*. Hivyo elimu ni muhimu kwa *radio* pia *television* kuhusu athari za uwindaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasli na Utalii kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara yake kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Balozi Khamis Sued Kagasheki kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika utendaji wake wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwasilishaji wa hotuba, tumeona kuwa wananchi wanasisitizwa

kuwatunza wanyamapori lakini pia uhifadhi wa mazingira, hapa pana tatizo kwa maana wananchi bado hawajanufaika na rasilimali husika kwa maana hata gawio la mapato inachukua muda mrefu sana kupatikana. Kwa mfano, Wilaya ya Kilwa haijapokea gawio toka mwaka 2008, kwa nini tusibadilishe mfumo kwa kuweka tozo husika zikalipwa na kubaki Wilayani au ngazi za vijiji ili kuondoa usumbufu kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fidia kwa wanyama waharibifu yawiane pia na uhalisia huku ikizingatiwa kuwa wananchi wanaumia sana na matatizo haya ya wanyama licha ya kupoteza mazao yao pia wamekuwa wanakufa au kupata ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa nyuki. Nakubali ni njia bora sana katika kuimarisha uchumi ila tatizo kubwa ni elimu kwa wakulima lakini tatizo lingine kwa maeneo yetu ni migogoro isiyoisha baina ya wananchi na viongozi kuhusu matumizi ya misitu ukizingatia kuwa eneo letu limezungukwa na *Selou Game Reserve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maeneo ya hifadhi na mipaka ya vijiji, ni mgogoro usiokwisha na unastahili sasa uchukuliwe hatua za makusudi kumalizwa lakini pia mazingira yaliyo karibu na mbuga yaboreshwe kwa kuweka miundombinu na huduma ili wananchi wanufaike na rasilimali hizi na kuondoa dhana ya kutoona manufaa ya wanyamapori na pia misitu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo katika uhifadhi wa mikoko na wazalishaji wa chumvi ambao kila mwaka wanalipa laki tatu lakini Serikali inashindwa kuwalinda wazalishaji hawa katika soko kwa kuweka mfumo huria kwa chumvi kuagizwa nje ya nchi huku iliyopo hapa nchini haina soko. Kwa kuwa imeonekana mikoko ina soko kubwa, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kupanda mikoko kibiashara au kuwapa wananchi utalaam na vyenzo za upandaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba pia imezungumzia uhifadhi wa malikale lakini kuhusu mapango sijasikia wakizungumzia Mapango ya Nang'oma, Kipatimu wala mpango wa uhifadhi wake hali ya kuwa wamezungumzia Mapango ya Amboni. Jitihada ifanyike ili kubaini maeneo mapya ya utalii na kuyaboresha, ikumbukwe Waziri wa Maliasili wa zamani, Mheshimiwa Zakia Meghji alitoa ahadi kwa wananchi wa Kilwa kuimarisha miundombinu na kuyaweka mapango haya katika ramani ya vivutio vya utalii nchini. Tuna Makanisa na Misikiti ambayo ina uhai wa zadi ya miaka mia moja. Pia baada ya Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete kuzindua Mnara wa Kumbukumbu ya Majimaji, tunaiomba Serikali itangaze mnara wa Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji Nandete kuwa ni miongoni mwa vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru na kuipongeza Serikali kwa kutangaza vivutio vya nchi vikafahamika katika maeneo mengi zaidi duniani na hatimaye kuliongezea Taifa mapato, pesa za kigeni. Naishauri Wizara iongeze jitihada katika kuongeza na

kupanua wigo wa aina za utalii kuhusisha utamaduni, mazingira, historia, makumbusho na michezo. Naishauri Serikali iangalie upya namna ya kutangaza vivutio vya utalii nchini haswa kwa kuitisha mkutano wa wadau ili tuishauri Serikali namna bora ya kutangaza haswa katika nchi za mataifa ya Ulaya, Asia na Amerika. Serikali iweke mpango maalum wa kushirikisha Balozi zetu nje ya nchi, Watanzania waishio nje na wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kutumia teknolojia zilizopo sasa kama *youtube, facebook* na *twitter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote mazuri, nadhani lipo tatizo katika sekta ya utalii nchini kwa maana ingeweza kufanya zaidi ya hayo. Tukiangalia kwa jicho la tatu na kwa undani, tutaona changamoto nyingi sana na kubwa. Changamoto hii iko katika mgawanyo wa kile kinachokusanywa baina ya mawakala wa utalii na Serikali, sina uhakika kama Wizara au Idara inazo takwimu sahihi za wageni wanaoingia Tanzania na viingilio vyao. Kama kweli, tunaweza kuzidisha idadi ya wageni na viingilio tukapata mapato yanayotolewa Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna tatizo kubwa kwa maana watalii wanaingia wakiwa tayari wamelipia kila kitu (*visa,* viingilio, hoteli, usafiri na kadhalika) baadaye wakala analipa kwa kuieleza Serikali na kutaja tarehe ambazo walileta wageni. Sijui kama kunakuwa na uangalifu *(cross checking)* kwa idadi ya wageni na taarifa zao ni sahihi kiasi gani? Hata kodi anayotakiwa kulipwa inakuwa hivyohivyo. Hivi kwa nini wasije kulipia tozo hizi zote hapa nchini na

kuongeza mzunguko wa fedha za kigeni hapa nchini? Ukweli ni kwamba mzunguko wote wa ada, *visa*, *hotel* na usafiri zinabaki watokako na sisi tunaambulia vumbi tu na makombo tu ya watokako huku ajira kwa vijana wetu ikiwa mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa watalii ambao wanapenda kuja Tanzania kuhusu upatikanaji wa *visa*. Tatizo hili ni la kweli kwa kuwa hatuna ofisi nyingi za balozi ulimwenguni. Kwa nini Serikali isishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuweka utaratibu wa *visa* za *electronic* haswa kwa nchi ambazo zinaaminika kama Marekani na nchi nyingine za Ulaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma katika magazeti na majarida mbalimbali kuwa Tanzania, Kenya na Uganda zinafikia uamuzi wa kuwa na *visa* ya pamoja ili kuimarisha utalii. Hili ni jambo zuri lakini linahitaji tahadhari kubwa sana kwa kuangalia ushindani na hujuma ambazo zimekuwa zikifanywa na wenzetu hawa. Sioni sababu kuharakisha hili maana hatujakuwa na utayari wa kutosha kukabiliana na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera na sheria za maliasili zilenge kumnufaisha mwanachi wa kawaida ikizingatiwa kuwa wao ndio washiriki wakubwa katika kulinda na kuhifadhi rasilimali hizi hivyo wanastahili kunufaika nazo. Wawindaji wanalipa mirahaba sawa na 30% ya faida zitokanazo na pato (biashara na

uwindaji) kwa ajili ya maendeleo kupitia Halmashauri zao kwa mujinu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasiilsha, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba nchi yetu inazidi kuchakaa na kuwa jangwa bila kuwa na mkakati madhubuti wa kuzuia janga hili. Hii imetokana na ukataji mkubwa wa misitu wa takribani hecta 450,000 kwa mwaka kwa ajili ya kuni na mkaa. Asilimia 90 ya wananchi waishio vijijini hutumia kuni kama nishati yao, wakati asilimia 75% ya wananchi waishio mijini hutumia mkaa kama nishati yao. Mathalani, Jiji la Dar es Salaam peke yake hutumia gunia 40,000 za mkaa kwa siku licha ya miji mingine hapa nchini. Serikali ieleze mkakati wa kuzuia janga hili lisiendelee kutokea kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhamasisha wananchi kupanda miti, hakujakuwa na mwamko mkubwa wa upandaji wa miti hiyo. Aidha, miti mingi inayopandwa ni ile ya aina ya kigeni lakini siyo ile ya kiasili ya nchi hii jambo ambalo tunaweza kupoteza mbegu na miti ya kiasili. Ni vema Wizara ikaanzisha *Gene Bank* ya mbegu asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia utoroshwaji wa wanyamapori hai kupitia *KIA,* Novemba 2010, Serikali haijawahi kutoa kauli kuhusu hatma ya wahusika? Ni vema Serikali ikatoa kauli juu ya tukio hili kubwa na Serikali ililipwa nini kufuatia tukio hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilolo, sehemu ya Lugalo kuna Kaburi la 'Nyundo" la Kamanda wa Kijerumani aliyezikwa hapo kutokana na vita vya Wahehe. Sehemu hii imekuwa ni kivutio kwa watalii na Wajerumani wengi hutembelea eneo hili kwa ajili ya kumbukumbu. Hata hivyo, eneo hili halitunzwi hata kidogo. Je, Serikali ina mpango gani kutunza eneo hili ambalo linaweza kuingizia mapato Taifa letu?

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu wake, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwa hotuba nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza viongozi hawa kwa kuanza kazi yao vizuri kwa kuchukua hatua kali dhidi ya wale wote wanaohujumu maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kwa taarifa kwamba Bodi ya Utalii ya Tanzania itaaanza kuonyesha matangazo ya utalii katika ligi kuu ya mpira wa miguu ya Uingereza na ligi ya mpira wa miguu Marekani. Hatua hii hakika itaiuza Tanzania maradufu

katika nchi hizo mbili kubwa Duniani kwani zama za ‘chema chajiuza kibaya chajitangaza’ imepitwa na wakati. Sasa hivi chema na kibaya vyote havina budi kujitangaza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuwatia moyo kuwa chini ya uongozi wenu mpya wa Wizara, nina uhakika sekta ya maliasili na utalii itachukua nafasi yake halali nchini ya kuwa mchangiaji mkuu katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko sana kuwepo kwa ongezeko la kasi la raia wa kigeni kuja kufanya kazi katika hoteli za kitalii nchini na hivyo kufanya vijana wengi kutonufaika na kuwepo kwa hoteli hizo. Pia Watanzania wengi hawafanyi kazi za staa na badala yake kazi nyingi za staa hufanywa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaowaongoza watalii hasa wanaopanda Mlima Kilimanjaro, wamekuwa wakilalamika kulipwa fedha kidogo huku wakipata manyanyaso kutoka kwa wenye makampuni yanayoongoza wageni na hata wakipewa tipu na watalii hunyang’anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Serengeti wamekuwa wakilalamika suala zima la kulipishwa fedha kila abiria katika gari ambalo linapita katika mbuga ya wanyama Serengeti kwa kigezo cha

kuwaona wanyama lakini kuna magari ambayo yanapita kwenye mbuga ya wanyama Mikumi ambao wanapita karibu na wanyama lakini hawalipi chochote. Kwa nini upande wa Serengeti walipishwe?

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba ya Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Waziri wa Maliasili na Utalii, ya bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga za Loya na Nyahua katika Wilaya za Igalula, Sikonge, Igunga na Singida Vijijini, wanyama wanatoweka. Wizara ina mkakati gani kuokoa rasilimalli hii ili wanyama waweze kuzaliana na kuwa kivutio kwa utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Waheshimiwa Wabunge tarehe 2/11/2012 huko Thailanda na China, tulitembelea Ukuta Mkuu wa China *(Great wall of China).* Kutoka kituo cha utalii mpaka kwenye ukuta huu mkubwa usafiri ni kupitia gari za nyaya *(cable cars)* kusafirisha watalii takribani *2km*. Mradi kama huu unaweza kubuniwa kwa eneo la Kitonga, Kilolo, Iringa  na kuwa kivutio cha utalii pamoja na Kaburi la Nyundo alikozikwa Kanali wa Kijerumani aliyeuwawa na wapiganaji wa Chifu Mutwa Mkwawa karne ya 19, hii ni sehemu nzuri. Pia kujengwe sehemu ya wasafiri kupata vinywaji na vyakula *(rest area)* na kuchimba dawa. Wizara hii wanaweza kushirikiana na Wizara za Ujenzi, Uchukuzi, wawekezaji wa ndani na nje

(Uchina) kujenga kwa utaratibu wa *PPP* na kupata watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu asili na miti migumu kama Mninga Mkola, Mtundu, Mvule inatoweka Jimboni Igalula. Wizara iweke utaratibu wa kuanzisha vitalu vya miche na kuiotesha na kugawa kwa wananchi kwa kuweka sera ya kila kaya ipewe miche 100 kuipanda na kuitunza. Uvunaji ni asilimia 100 upandaji hakuna. Tujizatiti kwa hili ili pia mazingira yaboreshwe, mbao zitapatikana, tupande miti 10 tunapovuna mti mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tembe la Livingstone Kwihala -Tabora litunzwe kwa historia ya Mkoa na nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urinaji asali ni muhimu kwa Igalula na Tabora na kwingineko Tanzania. Tupate mizinga ya kisasa Loya, Tura, Malongwe ili ajira iongezeke Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii ya kutuwezesha kuchangia hata kwa njia ya maandishi pale mtu anapokosa nafasi ya kuchangia kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa hotuba yenye

mwelekeo wenye matumaini kwa Watanzania lakini pia niwapongeze kwa utekelezaji mzuri wa mpango wao wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa ni moja kati ya Mikoa iliyo na historia nyeti kama Mikoa ya Tabora, Ruvuma, Iringa na kadhalika. Mkoa huu wa Rukwa umeendelea polepole kupoteza historia yake ya kale kwa kuwa hakuna uhifadhi maalum wa mali za kale. Historia za akina Mwene Milanzi na Wene wengine ikiwa ni makazi yao na vifaa vingine vilivyotumika wakati huo zinapotea. Hivyo, natoa rai, Serikali ifanye kila linalowezekana historia ya Wafipa na makazi na mali nyingine zifuatiliwe na zianzishiwe uhifadhi. Makumbusho ya mambo ya kale si Dar es Salaam bali Rukwa hukohuko ikiwa ni Sumbawanga au Nkasi ili vizazi vijavyo vya Wafipa visipoteze *identity* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii, Mkoa wa Rukwa kuna rasilimali nyingi sana ambazo zingetayarishwa kwa ajili ya utalii basi Taifa hili lingeweza kujiingizia kipato kikubwa cha fedha za ndani na nje na kuinua uchumi kwa Mkoa wa Rukwa na Tanzania kwa ujumla. Rasilimali hizi ni maporomoko ya Mto Kalambo ambapo Mto huu unaendelea kuingizia fedha nchi jirani ya Zambia kwa vile maporomoko kwa upande wa Zambia yameandaliwa vizuri na kuwawezesha watalii kuyafikia maporomoko hayo kwa urahisi kuliko upande wa Tanzania, matayarisho hayo ni pamoja na barabara na kutangazwa. Mamba walioko Ziwa Rukwa ambao ni wa aina yake, wangetangazwa, watalii wa ndani na nje wangetembelea Ziwa Rukwa na kujionea mamba hao hivyo kutuingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya Taifa ya Katavi, hifadhi hii ni ya aina yake, wapo Twiga weupe ambao hawajapata kuonekana dunia nzima. Hivyo Serikali ingefanya jitihada ya kuwatangaza Twiga hawa mpaka nchi za nje, basi watalii wengi wa nje lakini pia wa ndani wangekuja kuwaona Twiga hao pamoja na wanyama wengine hata hifadhi nyingine za hapa nchini hazina Twiga weupe kama walio Katavi (Rukwa). Hivyo, natoa rai yangu kwa Serikali na Wizara yenye dhamana kutangaza rasilimali zote zilizo na vivutio Mkoa wa Rukwa ili vifahamike ili tupate watalii kwa wingi toka Rukwa yenyewe, Tanzania na nchi za nje waje kutembelea na kuchangia mfuko wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri. Naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga ya Selou. Wilaya ya Ulanga ni kati ya Wilaya ambayo sehemu kubwa ni pori la *Selou*. Katika pori hili, kuna wawindaji ambao wamepewa leseni za uwindaji lakini watu hao hawasaidii hata kidogo upande wa huduma za jamii, ni jeuri, hawana ushirikiano na wenyeji wa Ulanga. Naomba Wizara iliyowapa leseni iwaambie wasaidie kutoa huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa maliasili hasa misitu. Wilaya ya Ulanga ni kati ya Wilaya zinazotunza mazingira hasa misitu ya asili. Kwa kuwa tumejitahidi

kutunza miti, je, Wizara ina mpango gani wa kuzipa motisha Wilaya zinazotunza mazingira ili tuendelee kutunza mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ulanga ni mojawapo iliyopigana vita vya majimaji na makaburi ya wapiganaji hao yapo na mapango waliyojificha wakati wa vita yapo. Naomba watu wanaoshughulikia malikale waje Ulanga kufanya utafiti kuhusu maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kazi nzuri ambayo ameanza nayo pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu uvunaji wa misitu. Naomba suala hili lisimamiwe sana hasa ukataji miti ovyo. Tusiposimamia, huko mbeleni kutakuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuchangia kuhusu vitalu vya miti. Naomba sana wananchi waangaliwe kwa sababu ndio wanaozunguka msitu wa Mufindi hata kwa kuwapa kidogo kidogo ili waendelee kuulinda vizuri.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake waungwe mkono kwa hatua kubwa wanazofanya za kupambana na majangili yanayohujumu uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *KINAPA* Mkoani Kilimanjaro kwa kuhudumia wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro mfano mzuri ni kwa *KINAPA* kuchangia shilingi 20,000,000 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa tanki la maji katika kijiji cha Ashira-Marangu. Baada ya tanki hili kukamilika, *KINAPA* inakusudia kutoa karibu shilingi 43,000,000 kwa ajili ya kununua mabomba ya kusambaza maji Marangu Mtoni iliyoko katika Kata ya Marangu Mashariki. Napongeza *KINAPA* kwa kazi nzuri wanayofanya katika Jimbo la Vunjo na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *KINAPA* ifungue barabara ya Marangu hadi Kilema Kaskazini kama njia nyingine ya kupanda Mlima Kilimanjaro. Kwa bahati nzuri Serikali inaweka lami barabara ya Marangu Mtoni kwenda Kilema Kati na katika awamu ya pili itajengwa kupitia Kilema Kaskazini. Ninaomba sana *KINAPA* iweke kwenye programu yake barabara ya kutoka Kilema Kaskazini kwenda kwenye mbuga za Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Maliasili na Utalii unaingiza zaidi ya shilingi 80,000,000 kutoka kwa watalii wanaotembelea Mlima Kilimanjaro, nashauri *TANAPA* itoe 10% ya fedha hizo kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika Halmashauri za Moshi, Manispaa ya Moshi, Hai, Same, Pare, Mwanga na Rombo.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu hoja ambayo iko mbele yetu, napenda kupata maelezo toka Wizarani juu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga na kuimarisha uwezo wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori Tanzania *(WMA'S)* na uhifadhi kwa ujumla, kuna mambo ambayo ofisi ya Muungano wa Jumuiya zilizoidhinishwa na maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania (*Authorized Association AAS Consortium*) ilipenda kujua au kuleta hoja 4 ambazo ni:-

(i) Mgawanyo wa mapato *(benefit sharing scheme*) yatokanayo na matumizi ya wanyamapori kwenye *WMAs* haulengi kuziwezesha *WMAs* kujiimarisha na kujiendesha zenyewe;

(ii) Wizara ya Maliasili na Utalii kuidhinisha mikataba ya uwekezaji kwenye vitalu vya uwindaji wa kitalii ambayo haikufuata taratibu halali za kimchakato (Jumuiya za Ukutu, Jukumu na Mbarang'andu) mkataba wa *Green Miles*;

(iii) Jumuiya *(AA)* kuingiliwa majukumu yake na Halmashauri za Wilaya au wakuu wa Wilaya. Mfano Jumuiya ya Wamimbila Wilaya ya Mvomero. Mkuu wa Wilaya kuingilia mchakato wa kumpata mwekezaji kwa dai la kutotambua kanuni za *WMA* ambazo zimetolewa na Wizara husika na kumwagiza Mwanasheria wa Halmashauri kuandaa mikataba

mipya kinyume na muundo wa mkataba kama kanuni za Wizara zinavyoelekeza.

(iv) Kutolewa vitambulisho kwa Maaskari wa Wanyamapori wa Vijiji *(VGS)* ili kuweza kushiriki kikamilifu kusimamia maeneo ya *WMAs* kwa kuzingatia kuwa ujangili ni mwingi katika maeneo hayo. Je, Wizara katika bajeti imetenga bajeti ya kuandaa vitambulisho kwa Maaskari wa Wanyamapori wa Vijiji? Mapendekezo kwa Wizara yametumwa Wizarani na Muungano wa Jumuiya Zilizoainishwa *(AAs)* tarehe 23/07/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, nataka kujua toka kwa Mheshimiwa Waziri, Sheria Na.5, kifungu namba 31(7) cha Sheria Kuu za Wanyamapori kinaipa uwezo *Authorised Association (AA)* kutangaza kupata na kuingia mkataba na mwekezaji kwa kushirikiana au kushirikisha Halmashauri za Wilaya husika na wawakilishi wa Mkurugenzi katika majadiliano na uwekaji saini. Ili sheria hiyo iweze kutekelezwa, ni lazima iende sambamba na kanuni ambazo zinaandaliwa na Wilaya kwa kushirikiana na wadau husika zikiwemo *AAs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya kupitia Muungano wao (*AA)* tarehe 7 na 9/05/2012, zilizotoa tangazo magazetini la kutafuta wawekezaji wa uwindaji wa kitalii, picha na mengineyo kwa mujibu wa Sheria Kuu ya Wanyamapori, Namba 5 ya mwaka 2009, kifungu namba 31(7). Tangazo hilo lilisitishwa na Wizara kwa hoja ya msingi ya kanuni kutokamilika

kutolewa au kukamilika ili kukidhi matakwa ya Sheria hiyo Namba 5 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia gazeti la Serikali Na.206 la tarehe 15/6/2012, kanuni hizo zimetoka kupitia muungano wa *WMA (AAs).* Wizara ilijulishwa kuhusu dhamira ya tangazo jipya la kukaribisha wawekezaji katika *WMA* kwa mujibu wa makubaliano ya kikao kati ya Wizara na wawakilishi wa *WMAs* cha tarehe 23/5/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea tarehe 15/06/2012 hadi leo hii, Wizara inasema haijapokea rasmi kanuni hizo toka Mpigachapa Mkuu wa Serikali na haijui watazipokea lini na hivyo kufanya mchakato usubiri hadi zipatikane hata kama ni mwakani. Kwa mujibu wa Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2010, kifungu namba 8(1) zilizochapishwa na gazeli la Serikali tarehe 2/7/2012 zinazungumzia kipindi cha mpito cha uwekezaji wa kitalii hakitazidi Julai 2013 kwa wawekezaji wote. Kwa mantiki hiyo, Serikali imeshatangaza vitalu vyake kwa msimu mpya wa Julai mwaka 2013-2018, kwa utaratibu huo Wizara kutomhusu au kufuatilia upatikanaji wa kanuni kwa wakati na *AAs* kutangaza na kutafuta wawekezaji kutafanya *AAs* kushindwa kupata wawekezaji makini na watakaofaa ili kuleta maendeleo katika jumuiya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Muungano wa Jumuiya (AA) unapata mashaka na Wizara kuwa na dhamira ya kuendelea kupachika wawekezaji wenye maslahi nao watendaji wa Wizara badala ya Jumuiya husika. Lingine kuchelewa kutangaza na kupata

wawekezaji katika vitalu hivi hasa ambavyo havina wawekezaji (Magingo WMA) kunasababisha kutokuwa na ulinzi wa kutosha, kuongezeka wimbi la ujangili na uharibifu kwa wanyama wetu. Mheshimiwa Waziri alikuwa huko juzi na ameona hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kukwamisha mchakato wa awali uliotangazwa na Muungano wa *WMA (AAs)* katika magazeti tarehe 7 na 9/5/2012 kumeleta usumbufu mkubwa na wakati mgumu kwa *WMA* kujibu hoja za wawekezaji ambao walijitokeza na walitoa ada za maombi kutofautiana na daraja za vitalu. Wizara inasemaje kuhusu upatikanaji wa kanuni na hivyo kufanya mchakato huu uendelee kwa muda na wakati muafaka na WMA ziweze kupata wawekezaji wanaowataka na watakaokuwa na manufaa au maslahi kwa jumuiya husika na si kwa watendaji wabadhirifu wa Serikali Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja za Wabunge wakati wa majumuisho nipate majibu ya hoja zangu kwa maslahi ya wanajumuiya wote.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misitu, naipongeza Wizara kwa kuanzisha Wakala wa Huduma za Misitu. Ushauri wangu ni kusisitiza uadilifu na weledi wa utendaji. Wakala apambane kwa dhati na uwajibikaji usioridhisha, rushwa na umangimeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maombi kwa Wakala na Wizara kwa ujumla:-

(a) Usimamizi wa misitu ya hifadhi. Wilaya ya Lushoto imeathirika sana kwa usimamizi mbovu wa misitu ya hifadhi katika Wilaya hiyo. Umekuwepo wizi wa mbao ukihusisha watumishi wa hifadhi. Nashauri Wakala ichukue hatua ya kuhamisha watumishi waliofanya kazi kwa muda mrefu katika maeneo waliyokaa kwa muda mrefu na kujenga mazoea. Nashauri Mamlaka au Wakala pia wapewe mamlaka ya kusimamia misitu ya hifadhi zinazosimamiwa na Halmashauri za Wilaya kwa kuwa Halmashauri hazina uwezo.

(b) Mfuko wa Misitu Tanzania. Naamini Mfuko huo ungeelekeza nguvu zake kwenye maeneo yaliyoathirika na uharibifu wa misitu kama Lushoto. Naomba Mfuko upeleke huduma Lushoto ambako kuna kasi kubwa ya kutoweka na kuharibika kwa misitu ambayo ndiyo chanzo cha ongezeko la gesi ukaa. Madhara ya uharibifu wa misitu katika Wilaya ya Lushoto hayahitaji utafiti, vyanzo vingi vya maji vimekauka, uoto wa asili umepotea kabisa, mvuto wa mazingira mazuri ya Lushoto umepotea. Naomba Mfuko utoe hela za kwenda Lushoto kurekebisha hali hiyo kwa kutoa fedha za upandaji miti kwa vikundi na Serikali kuzidisha juhudi za kulinda misitu ya hifadhi iliyopo.

(c) Malalamiko ya watumishi. Wako watumishi walioajiriwa na TAFORI –Lushoto zaidi ya miaka kumi na

hawajapata haki zao za ajira kama barua za ajira, kuchangia kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Nimefuatilia matatizo yao mpaka Wizarani lakini urasimu umekuwa mkubwa sana hadi leo hakuna ufumbuzi. Mkurugenzi wa Misitu, ndugu Kilahama anaelewa tatizo la watumishi hao, kwa kweli wameanza kukata tamaa, naomba watendewe haki.

(d) Ukusanyaji wa gawio kutoka *TANAPA*/Ngorongoro. Ni kweli kwamba ukusanyaji maduhuli ni jambo jema. Kwa upande wa Serikali kuchukua gawio kutoka *TANAPA* na Ngorongoro, mimi nakubaliana na ushauri wa Kamati kwamba Serikali au Hazina wasichukue gawio kutoka Mashirika haya kwa kuwa suala la uhifadhi ni ghali na ni uhai wa Taifa letu. Kwa kuchukua gawio ni kudhoofisha Mashirika haya na kutishia uhai endelevu wa hifadhi zetu. Akiba inayochukuliwa na Serikali ni wazi kwamba inapaswa kutumika katika mambo ya uhifadhi wa dharura.

(e) Kuhusu mauzo ya wanyama nje ya nchi. Nakubaliana na jitihada za Serikali kulinda maliasili zetu hasa wanyama wakubwa na wanaotishiwa kutoweka. Naomba Serikali itafakari kuruhusu uuzwaji nje ya nchi wanyama waliotamkwa katika daraja la 12, 13, 15 na 16 ya sheria. Uamuzi huo wa kuruhusu uuzwaji wa wanyama hao utasaidia kujenga ajira kwa vijana na kulipatia Taifa mapato.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za fidia/kifuta machozi za tarehe 22/4/2011 *(The Wildlife Conservation (Dangerous Animals Damage Consolation) Regulations 2011.* Kanuni hizi mpya kabisa ambazo zina mwaka mmoja tangu zitungwe

zimeonesha kushindwa kwake kabisa kwani haziko *fair* kwa pande wa wananchi. Ukurasa wa 105 wa Kanuni hizo umeonesha jinsi gani ambavyo Kanuni hizi hazifai. Mfano hakuna jina la chui kwenye orodha ya wanyama hatari wakati chui hawa wamekuwa wakikamata mbuzi na kondoo wengi wa Watanzania na hata kwenye hotuba ya Waziri hajaonesha ni fidia ngapi zimelipwa na Serikali kwa wanyama waliokamatwa na hajaonesha idadi ya ng'ombe, mbuzi na kondoo ambao wameuwawa na wanyama hatarishi. Naomba tuambiwe, hivi hakuna wanyama wowote waliokamatwa mwaka uliopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *rates of consolation payments. Crops per acre (maximum 5 acres) up to 0.5km from protected area = rate to be paid =Tshs. 0.00.* Mheshimiwa Waziri anafahamu kuna vijiji vingi vilikuwepo tangu mwaka 1974 na hifadhi nyingi zilikuta vijiji hivi na hifadhi zingine hivi karibuni zimeongeza maeneo ya mipaka yao na kuingia maeneo ya vijiji, hivi ni kwa nini Kanuni hii imewaadhibu wananchi wengi ambao wanapakana moja kwa moja na mipaka ya hifadhi mbalimbali, kwani wale ambao wamewekwa mpakani mwa hifadhi na wamewekewa Sheria za Vijiji wao ndio waathirika wa kwanza, hao wawalipwi kabisa wanalipwa 0 mita 500 toka mpaka wa hifadhi wakati mashamba yao ndio ya kwanza kabisa kuvamiwa na wanyamapori. Waziri naomba Ofisi yenu ipitie upya Kanuni hii na kuiondoa kwani sio wanakijiji/vijiji vyote au wote wanaopakana na hifadhi ni wavamizi wa maeneo ya hifadhi wengine wamekutwa na hizo hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *loss of human life*. Naipongeza Serikali kuongeza kiasi cha kifuta machozi pale ambapo mtu anakuwa ameuwawa na wanyamapori *to* 50,000 hadi 1,000,000/=, lakini hadi sasa kifuta machozi kinachotumika ni kile cha zamani cha elfu 50,000/=. Naomba Waziri atoe kauli juu ya hili na vifuta machozi hivi bado vinachelewa sana, vinatumia mpaka mwaka mmoja hadi miwili kumfikia mhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya wanyama. Haiingii akilini kondoo, punda, nguruwe anapokuwa ameuwawa alipwe kifuta machozi Tshs. 25,000/= ni wapi leo ukienda mnadani utapata ng'ombe wa Tshs. 50,000/= kondoo 25,000/=? Naishauri Serikali itumie bei ya soko kuliko kuwadanganya wananchi kuwa hichi sio fidia bali ni kifuta machozi, hata kama ni kifuta machozi kizingatie bei ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya hifadhi na vijiji. Waziri hajaongelea kabisa migogoro ya Hifadhi ya Tarangire na vijiji vya Gijedabuu Ayamango, Gedamar na Moyamayoka vyote viko Babati Wilayani. Mbona wananchi hawa wameteseka sana ni kwa nini Wizara/hotuba imewapuuza wakati mgogoro wao ni wa tangu mwaka 2008 hadi leo hakuna uvumbuzi? Nimelisema hili mara nyingi hapa Bungeni kwa michango yangu yote katika Wizara zote nilizowahi kuchangia hata kwa njia ya maswali lakini hotuba ya mwaka jana Waziri aliliongelea vizuri mwaka huu yupo kimya. Naomba kufahamu kama huu ndio usikivu wa Serikali na mgogoro huu utapatiwa uvumbuzi lini?

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Wizara hii kwa kuwasilisha malalamiko yangu kuhusiana na tatizo la unyanyasaji wananchi wasio na hatia na uingiliaji mipaka unaofanywa na Askari wa *TANAPA* katika Hifadhi ya Mikumi katika vijiji vya Maharaka, Doma na Mkata. Kumekuwa na tabia ya Askari wa *TANAPA* kuingia vijiji hivi kuwapiga na kuwabambikizia kesi wananchi kwa kisingizio cha wananchi kuingia kwenye hifadhi. Mwaka huu nimefanya ziara kijiji cha Maharaka na Doma, wananchi walinieleza tatizo hili na nilimwandikia barua Waziri wakati ule Mheshimiwa Ezekiel Maige kuomba aingilie kati tatizo hili lakini mpaka sasa sijapata jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipaka, *TANAPA* wameongeza na kumega eneo Kijiji cha Doma na wananchi wanaogoma kuhama wanabambikiwa kesi. Naomba sana Waziri afike maeneo haya ili kuepusha umwagaji damu maana wananchi wangu wameshavumilia vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala la wanyama waharibifu wa mazao, naomba *TANAPA* wadhibiti suala hili na zaidi fidia kwa ajili ya uharibifu wa mazao na vifo ni ndogo sana. Naomba sana Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nilimpa Waziri ujumbe juu ya

tukio la mifugo ya wananchi iliyoliwa na simba kijiji cha Kwabada Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijafanya tathmini juu ya gharama halisi kama zilivyotolewa na wahusika. Naomba kauli ya Mheshimwa Waziri juu ya hasara waliyopata wananchi hao na hisani juu ya uwezekano wa fidia kwa walioathirika. Simba wanadaiwa kutoka hifadhi ya jirani Saadani (Mkwaja Ranchi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao kuongoza Wizara hii nyeti. Kwa jinsi Mheshimwa Rais alivyoonyesha imani kubwa kwa Waheshimiwa hawa Mawaziri nasi tunaimani kubwa sana juu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Mufindi wanayo masikitiko makubwa sana katika utaratibu unaotumika kutoa vibali. Walikuwa na mategemeo makubwa ya kupata ajira ya uhakika katika maeneo haya kwani wao ndio waliotoa ardhi na pia wao ndio wanaolinda misitu. Ni vyema Serikali ikaangalia upya utaratibu wa kutoa vibali hata ikitoa kwa vikundi ingekuwa bora zaidi hasa vilivyosajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya nchi kuwa Watanzania wote wana haki sawa. Ni sahihi kabisa, lakini ukiangalia wanaofaidika zaidi na msitu ule ni watu wanaotoka maeneo ya mbali na Mufindi na

yanapotokea matatizo ya moto, wananchi wa Mufindi inabidi waache kazi zao za kuzalishaji mali waende kuzima moto hata kama utachukua miezi mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1970 wakati wa Operesheni Vijijini, wananchi wengi wa Wilaya ya Mufindi waliacha maeneo yao na kusogea katika vijiji na Serikali iliyachukua maeneo haya bila kuvishirikisha vijiji wala wananchi wahusika na leo hii idadi ya wananchi katika maeneo hayo imeongezeka, hawana ardhi ya kutosha na hivyo Serikali imeshindwa kuyaendeleza maeneo hayo yote. Umezuka mgogoro mkubwa sana kati ya Serikali, Vijiji pamoja na wananchi. Ni vyema Serikali ikayaacha maeneo yote ambayo hayajaendelezwa yabaki kwa wanavijiji na wananchi wayaendeleze. Jukumu la Serikali kwa sasa si kuingia mgogoro na wananchi, cha msingi ni kuwaachia maeneo haya na kuwapatia utaalamu wa kuendeleza misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapato makubwa yanayotokana na misitu bado Wilaya ya Mufindi haioni tija ya mradi huu kwani Msitu wa *Sao Hill* unashindwa kutengeneza barabara zote zinazopita katika vijiji vinavyozunguka msitu. Ni vyema vijiji hivi vingefaidika kwa matengenezo ya barabara zinazozunguka msitu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uvunaji mbao hali ya barabara hizi huwa zinakutwa zikiwa nzuri lakini baada ya mavuno tunakuwa hatuna barabara, tunabakiwa na makorongo. Ni vyema kama kweli

wanataka kuendelea na uvunaji huu, wawe wanazitengeneza mara baada ya mavuno kama wanavyofanya Kampuni ya MPM *(Mufindi Paper Mills).* Safari hii hatutakuwa tayari kuruhusu uvunaji wa misitu mpaka tutakapokubaliana juu ya matengenezo ya barabara baada ya mradi huu kwani Halmashauri yetu haina uwezo kabisa wa kutengeneza barabara hizi baada ya mavuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikaangalia eneo la utalii kwa upana wake kwa kuingiza msitu wa Uhafiwa kwenye Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vyema tukatangaza mambo adimu tuliyokuwa nayo kama vyura ambayo havipatikani sehemu yoyote zaidi duniani zaidi ya Bwawa la Kihansi, Wilaya ya Mufindi, Jimbo la Mufindi Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Serikali kuja kujionea Bwawa la Mpanga Tazara ambapo kuna visiwa vinavyohama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pia Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri lakini pia kwa namna ambavyo

wanasimamia utekelezaji wa majukumu waliyopewa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maliasili na Utalii inayo dhamana kubwa ya kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia sekta ya utalii. *Multiplier effect* ya sekta ya utalii ni kubwa sana. Watalii wanatoa fursa kwa wawekezaji wa mahoteli, mahoteli yanatoa fursa kwa wakulima kuuza mazao yao, wavuvi, ajira kwa vijana na kadhalika. Utalii hutoa nafasi kwa wasafirishaji hivyo sekta hiii inayo nafasi kubwa kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba *mulitiplier effect* ya utalii kuwa ni pana na ya uhakika, sekta hii bado haijaendelezwa vya kutosha. Naishauri Serikali ihakikishe kwamba sekta hii inaendelezwa kwa kuwekewa miundombinu ya uhakika. Pawepo usalama wa uhakika dhidi ya watu wachache wasioitakia mema nchi yetu ambao wamekuwa wakiwavamia watalii, kuwaibia na hata kudhuru maisha yao. Mambo haya lazima yadhibitiwe kwa nguvu zote. Aidha, naomba Serikali itumie vyombo vya magharibi kutangaza vivutio mbalimbali ambavyo vipo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ilidhibiti Kundi la Uamsho ambalo linahamasisha chuki dhidi ya watalii wanaotembelea Zanzibar na hivyo linaweza kuathiri mapato yatokanayo na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie upya sera ya kuruhusu wanyama hai kusafirishwa kwenda nchi za nje. Utaratibu huu utaua utalii wetu kwani wageni hawatakuja tena Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mikataba ya vitalu vya uwindaji iangaliwe upya kwani baadhi ya mikataba hiyo haina manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali yetu ijitahidi kuhamasisha utalii wa ndani, nchi ya Japan na baadhi ya nchi za Asia zimewekeza katika uhamasishaji watu wao kuthamini maliasili za nchi zao na kutembelea vivutio vilivyomo katika nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi wanaokaa karibu au jirani na Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba kote nchini waweze kushiriki kulinda rasilimali hizo asili kwa Taifa letu. Naomba paweko mpango kabambe wa kuwashirikisha wananchi hao na kuwagawia mojawapo ya mapato yatokanayo na Hifadhi hizo na Mapori ya Akiba. Wananchi wakishirikishwa ipasavyo, wao ndio watakuwa walinzi nambari moja wa rasilimali zetu vinginevyo hawatakuwa na uchungu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mheshimwa Waziri Kagasheki na Naibu wake wasaidie kutatua tatizo sugu la athari za wanyama waharibifu

linalowakabili wananchi wa Jimbo la Masasi waishio kandokando mwa mto Ruvuma kwa kuliwa na Mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu niingie kwenye Bunge hili mwaka 2010 nimekuwa nikifuatilia suala hili na kupelekea aliyekuwa Waziri Mheshimwa Maige kufanya ziara na alipata fursa ya kuongea na wananchi katika Kata ya Mnavira, alielezwa na wananchi jinsi wananchi wanavyopoteza maisha na kujeruhiwa na Mamba, watu zaidi 30 wamepoteza maisha kati ya mwaka 2003-20012 na wengi kujeruhiwa. Kutopatikana na kwa vyanzo vingine vya maji zaidi ya maji ya Mto Ruvuma, kumepelekea wananchi wengi kutegemea maji ya mto huo kwa shughuli zote za kibinadamu ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuchangia fedha kwa ajili ya kuchimba visima kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Mheshimiwa Maige aliahidi kuchangia shilingi milioni ishirini kusaidia ujenzi wa vituo vya afya viwili (2) cha Mnavira na Chikolopola vilivyopp kandokando ya Mto Ruvuma, pia aliahidi kusaidia kuchangia uchimbaji wa visima shilingi milioni kumi na tano. Tunashukuru ahadi hizo zimetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namfahamisha Mheshimiwa Waziri tatizo kubwa ni watendaji wa Wizara kutokubali kutoa kibali cha kuvuna Mamba wengi kwa madai kuwa tutawapunguza, sawa lakini swali tunathamini zaidi Mamba kuliko maisha ya Watanzania wenzetu? Ninaomba atakapohitimisha

hotuba yake awatoe mashaka wananchi wa Jimbo langu kwa kutoa tamko la Serikali litakaloeleza lini vibali hivyo vitatoka na angalu Mamba 100 wavunwe hasa kipindi hiki cha kiangazi ambapo uvunaji wake unakuwa rahisi kuliko wakati wa masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii mara tu nitakapopata maelezo ya Serikali. Maisha ya watu yapewe umuhimu wa kwanza na siyo uwepo wa Mamba wengi.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawapongeza viongozi wakuu wa Wizara, Mheshimiwa Balozi Khamisi Kagasheki na Mheshimwa Lazaro Nyalandu kwa kuaminiwa na Mheshimwa Rais na kupewa jukumu la kuongoza Wizara hii muhimu. Nawaombea Mwenyezi Mungu wafanye kazi kwa umoja na upendo. Nawapongeza pia Katibu Mkuu, Bibi Mainuna Tarishi, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya mbuga za wanyama ni (zaidi ya) au 13. Hifadhi ya Kilimanjaro (*KINAPA*) ikiwa mojawapo, lakini *KINAPA* ndiyo inaliingizia *TANAPA* fedha nyingi kuliko mbuga nyingine yoyote. Ziko hata taarifa kuwa *KINAPA* imechangia kuliko mbuga nyingine zote kwa pamoja katika baadhi ya miaka. Kilio cha Halmashauri za Rombo, Moshi, Manispaa ya Moshi, Hai, Siha na Longido kimekuwa siku zote kuiomba Wizara itenge fedha asilimia fulani kwa Halmashauri hizi zinazoitunza hifadhi hii na ambazo pia zinajinyima huduma za mbao, kuni, asali na dawa

kutoka *KINAPA*, ili hifadhi hii iendelee kutumika kwa shughuli iliyokusudiwa. Sasa hivi wimbi kila mahali nchini ni kwamba rasilimali zitumike pia kuwanufaisha wananchi wanaozizunguka na kuzitunza. Tumeona *Ngorongoro Conservation Area* na maeneo mengine yenye hifadhi ya wanyamapori na tunaona maeneo karibu yote yenye madini yakitengewa fedha. Naiomba Wizara itoe kauli juu ya maombi haya ya Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro wakati wa kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Moshi Vijijini naleta ombi kwa Waziri, Mheshimiwa Balozi Kagasheki na Mheshimiwa Nyarandu kuwa njia ya kwenda Mlima Kilimanjaro inayoanzia Kiboriloni kupitia Kikarara, Tsuduni na Kidia (njia ya *Old Moshi*) ifunguliwe sasa. Njia hii ilifungwa kwa sababu za kisiasa, naomba tuweke siasa kando, tuifungue barabara (njia) hii ya utalii kwani kwa kufanya hivyo, siyo tu idadi ya watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro itaongezeka, ila pia ajira zitaongezeka na mapato yataongezeka zaidi. Namwomba Mheshimwa Waziri atakapohitimisha hoja yake atoe kauli ya matumaini kwa wananchi wa *Old Moshi* kule Moshi Vijijini.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa jinsi ambavyo wameanza kazi vizuri, nasi tupo nyuma yao na tunawaunga mkono kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia tatizo la wingi wa Mamba katika Ziwa Rukwa. Ziwa Rukwa Mamba wamezaliana kwa wingi sana jambo ambalo linatishia usalama wa wananchi kwa ujumla wakiwemo wavuvi, akina mama na watoto wanaokwenda kuoga ziwani pamoja na kuchota maji. Hivyo naomba Serikali iwaondoe Mamba hawa, pamoja na binadamu vile vile wanamaliza samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ipande wanyamapori katika Mbuga ya Uwanda *Game Reserve*. Eneo hili limekuwa likifahamika kama ni hifadhi lakini halina mnyama hata mmoja. Hivyo ili kuendelea kulitunza na wananchi waamini basi pelekeni wanyama, bila kufanya hivyo wananchi wafugaji kwa wakulima wataendelea kuyaharibu, maana hadi sasa ni mapori matupu. Kwa maana hiyo watumishi wa maliasili ndiyo wanaofaidika kwa kukodisha wafugaji na wakulima na wasio na fedha za kukodi hunyanyaswa na kunyang'anywa mali zao.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuchangia katika suala la ulinzi wa wanyamapori. Ni vyema Serikali kupitia Wizara hii kuendelea na *programme* ya kuwapatia mafunzo ya kiaskari kutoka Jeshi la Polisi kama walivyoanza kwani mafunzo hayo yataweza kusaidia ulinzi wa wanyamapori na kadhalika. Aidha, Walinzi hao wapatiwe vifaa vya ulinzi vya uhakika hata bunduki za moto na za kileo, vilevile walinzi wapatiwe maslahi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka mkakati au utaratibu mzuri wa kuwawezesha wananchi wa Tanzania kutembelea mbuga za wanyama na sehemu za utalii. Kama inavyoelekea kwamba nchi yetu imejaaliwa na vivutio vingi vya utalii. Hata hivyo imekuwa ni vigumu kwa wananchi wetu kutembelea kutokana na umbali au hata kukosa gharama za kuwafikisha huko kutokana na usumbufu wanaopata wananchi wetu. Ni vyema Wizara ikaweka utaratibu wa usafiri wa mabasi au daladala na ziandikwe majina ya hifadhi ili wananchi wapate usafiri wa uhakika. Pia katika hifadhi hizo zijengwa nyumba ndogondogo za kulala wageni na za bei nafuu. Aidha, wananchi wapunguziwe gharama za viingilio na kadhalika.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika kubaini changamoto za Wizara hii muhimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kuomba Wizara itusaidie kutatua kero ya wafugaji *vs* Askari wa vitalu vya uwindaji. Wafugaji wanafanya makubaliano ya kulisha kwenye vitalu hivi kwa malipo. Fedha ikipungua, wafugaji wanakamatwa na kutozwa fedha nyingi ambazo zinaishia mikononi wa Askari tu na siyo Hazina. Utatuzi wa kero hii ni kwa Wizara hii kuachana na biashara hii ya kuwinda na maeneo haya yawe malisho kwa utaratibu wa Ngorongoro ambapo mifugo na wanyamapori wanalishwa pamoja lakini bila shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwa na maelezo kwamba wanyamapori hawawezi kuchanganyika na ng'ombe, tatizo la maelezo haya katika *Maswa Game Reserve* vijiji vya N'wamutani, Ng'wampwali, Lounga-lo-mhopo, miaka yote mifugo na wanyamapori wanalisha pamoja isipokuwa kwa njia ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni mtindo wa Ngorongoro utumike katika kuhalalisha kinachotokea sasa kiharamu. Naomba Wizara ifikirie hili kama njia ya kupata malisho ya mifugo kwani mifugo ina mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa labda hata kupita mchango wa vitalu vya kuwinda. Aidha, kwangu hakuna mantiki ya kuwinda kama tumetenga ardhi kwa ajili ya kuhifadhi wanyamapori, *why kill*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ziara ya Meatu. Namwomba pia aje Bariadi Mashariki kwani kero kwa wafugaji wa Meatu na Bariadi au Itilima zinafanana. Naamini mtazamo mpya wa uongozi wa Wizara hii utapunguza kero za wafugaji na misitu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nautakia uongozi huu kila mafanikio.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niupongeze uongozi wa Wizara na Mawaziri wapya kwa kuchaguliwa kuongoza Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa letu linalotunza maliasili yetu na vilevile kutumia maliasili yetu hii kulipatia Taifa letu fedha za ndani na kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika kabisa na mikakati mbalimbali inayotumika kutangaza vivutio viivyopo ndani ya mali yetu ya asili. Mauzo na masoko ya siku hizi yanahitaji kutangazwa kisasa kwa kutumia teknolojia ya kisasa na hasa *ITS*. Bodi za mamlaka mbalimbali kama *TANAPA, KINAPA* na kadhalika bado hazijajipanga kimkakati ni namna gani zitumie teknolojia ya kisasa kutangaza maliasili zetu kwa kuleta tija zaidi kimapato. Natoa ushauri kuwa, kwa makusudi Wizara ielekeze Bodi hizi kujikita kutangaza vivutio vya utalii kimkakakati. Hii ni pamoja na kuchagua makundi maalumu ya kufikiwa kwa kutumia wasanii, watu mashuhuri, wawakilishi mbalimbali kama warembo na kadhalika, muda umefika sasa tuamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga zetu za wanyama zinakabiiwa na uwindaji haramu mkubwa, unaoongezeka siku hadi siku. Wakati Serikali inasema kiasi cha Tembo wanaouwawa kwa ujangili ni wastani wa tembo 200 kwa mwaka, habari toka kwa Taasisi zinazojitegemea *(independent report)* zinasema ni wastani wa Tembo 1000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ujangili kwa sasa umekuwa mkubwa na unaongezeka mfano mwaka 2008 ilikuwa 104, mwaka 2009 ilikuwa 127, mwaka 2010 ilikuwa 259, mwaka 2011 ilikuwa 276 kila mwaka uwindaji haramu unaongezeka. Sababu kubwa ni pamoja na upungufu wa fedha, watumishi wa kutosha ikiwa ni pamoja na Askari wa Wanyamapori, vitendea kazi na pia hata kupotea kwa uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa la kusononesha pamoja na changamoto hizo bado Idara ya Jeshi la Polisi na Mahakama zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kupiga vita ujangili wa wanyamapori. Ukiangalia takwimu, kuanzia mwaka 2007 hadi 2012, zaidi ya kesi zipatazo 20, ambazo zina ushahidi bayana zimeharibiwa aidha na Polisi au na Mahakimu mbalimbali wasiokuwa watiifu na waaminifu katika kazi zao. (Taarifa hii inapatikana Idara ya Wanyamapori Wizarani kwa kumbukumbu zaidi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Askari wa Wanyamapori kwa uchache wao na vitendea kazi vichache wanakamata wahalifu/majangili kwa kutumia fedha za Serikali na wanaachiliwa huru Mahakamani bila hata kesi kusikilzwa, ni wapi moyo wa kazi utapatikana na wapi majangili wataogopa na kuacha ujangili? Naomba sana Serikali sasa iweke mkakati maalumu na ikiwezekana basi hata Mahakama Maalumu ya uhujumu uchumi iundwe kwa kazi hiyo pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu yetu sasa ni muhimu iendelee kutunzwa na kuhakikisha ukame hauzidi kuathiri mazingira yetu. Lakini ni vyema tukaelewa kuwa maeneo kama Moshi (Kilimanjaro), Iringa, Mbeya na kadhalika wananchi wameotesha miti wenyewe na ni haki yao kiutumia kujipatia kipato. Jambo la msingi hapa sio kuwanyima kuvuna miti hii bali ninaomba sana Serikali isaidie mafunzo ya programu ya namna gani wananchi watafundishwa kupanda miti kwa ajili ya kuchukua nafasi ya ile anayokatwa. Hapa sasa sera iwe ni panda mti, tunza

miaka kadhaa angalau robo au nusu ya umri wa mti, *then* kata mti. Kwa maeneo wazi panda miti miwili (2) kata mmoja (1). Siamini kama kuwanyima wananchi kukata miti yao waliyopanda wenyewe, wasitumie hata kwa ujenzi kama ilivyo kule Kilimanjaro, haitaweza kuleta tija bali ni mgongano kati ya wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ifanyie kazi mawazo hayo. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja, pili naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri, nawatakia kila la kheri katika kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utangazaji wa utalii, tusiendelee kwa utaratibu wa kuhudhuria maonyesho tu, ni lazima sasa kuanza kufufua *road shows* kwa nchi mbalimbali kama ilivyokuwa zamani. Twende kwenye *traditional markets* na masoko mapya ya Urusi, China, India na Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *General Management Plans* za hifadhi zetu na *Game Reserves. GMP* za hifadhi za Taifa ni za muda mrefu, nyingine *over 10 years, they need to be reviewed to accommodate more up market,* zina *low impact- lodge* zenye vyumba 10 hadi 20 tu lakini zenye bei kubwa kwa *special market*, hili lifanyike haraka kama tunataka kuvutia watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupambana na ujangili, *I need not say more on this scourge. Honorable Ministers, please determine to wipe out these pouchers. They are a danger to survival of our tourism industry-particularly so when our tourism is entirely wildlife based. If you succed, your name will go down in History books of our beloved nation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya upandaji miti ni ndogo mno. Kwa mfano pale *Sao Hill* wana ekari 100,000 (laki moja) ambazo hazijapandwa misitu. Kwa vile tuna sheria ya *PPP* ni vyema sasa mkaanza kupanda misitu kwa ubia na makampuni yenye uwezo mkubwa wa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa *Old Boma Pangani*. Wilaya yetu imepata Ofisi mpya ya Wilaya na hivi karibuni Ofisi hiyo ya Mkuu wa Wilaya itahama. Jengo la *Old Boma* baada ya kuhama litaachwa kama gofu tu, tunaiomba Wizara *seriously* ipange fedha za ukarabati maana *within a shortime will collapse*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya *Ubende WMA*, ni kero ya muda mrefu katika eneo letu na kuhodhiwa bila ridhaa ya wananchi na kufuata taratibu na Serikali kushindwa kufanya maamuzi kwa zaidi ya miaka sita (6) tangu nilipoanza kulisemea jambo hili, ilfike wakati tupate ufumbuzi wa kumaliza kero hii. Tayari kumekuwepo wananchi kupoteza maisha kwa ajli ya mgogoro wa ardhi katika eneo hilo,

nataka na wananchi wanataka kufahamu uamuzi wa Serikali juu ya *Ubende Wildlife Management Area.*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Balozi Khamisi Kagasheki, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Katibu Mkuu, Mama Maimuna Tarishi, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri na iliyowasilishwa kwa ufasaha wa juu. Ni matumaini yangu makubwa kuwa endapo Wabunge tutawaunga mkono, tutawapa nguvu sana, utendaji wao utakuwa na maslahi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya makaa majumbani. Bado kuna tatizo kubwa sana la wananchi hususani akina mama kuendelea kutumia mkaa kwa matumizi ya nyumbani. Hii inatokana na kukosekana kwa nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Ili kuondokana na adha hii, ni Serikali kuharakisha kupeleka umeme vijijini ili Watanzania wapate nishati mbadala. Kuna aina nyingi za kupata umeme bali tumekuwa wazito wa kuamua na kutekeleza. Mfano nchi za wenzetu kama Thailand na China umeme wa *solar*, umeme wa pumba za mpunga, umeme wa maganda ya miwa, gesi, umeme wa upepo na vinginevyo, vyanzo vyote hivi na vinginevyo tunavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya umeme, kuna nishati zingine mbadala za msingi, hapa ni elimu kutolewa kwa watumiaji. Naomba maelezo ya Serikali

ili tuweze kunusuru misitu yetu ya asili ambayo ina kazi nyingi kwa maslahi ya nchi yetu, sina haja ya kutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ya hifadhi. Ni kweli Serikali imejitahidi sana kutenga maeneo ya hifadhi kwa ajili ya kuepukana na ukame. Tatizo hapa bado maeneo haya hayana ulinzi wa kutosha, hivyo wananchi wanachungia mifugo huku wanakata miti na kufanyia shughuli zingine mbalimbali na za kijamii. Napenda kusikia kauli ya Serikali ambayo itakomesha tabia hii mbaya ya kuvamia maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vivutio vingi vya watalii Mkoa wa Singida lakini havijulikani rasmi kwani Serikali haijaweza kufika ili kuvihakiki ili viweze kujulikana rasmi na kutangazwa ili watalii waweze kufika Singida. Baadhi ya vivutio ni mapango ya kale yenye kumbukumbu nyingi, mapango ya Wajerumani ambayo inasemekana walizika vitu vingi vya thamani, katikati ya nchi yetu ya Singida, Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Kilimatinde, Kata ya Sorya, kijiji cha Sukamahela, kuna maji ya moto yasiyopoa yenye uwezo wa kupika chakula na kadhalika. Napenda kujua lini timu ya wataalam itakuja Singida kuangalia vivutio hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti ya mikaratusi kuvunwa yote. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa bado kuna miti hii mingi ambayo inafyonza maji sana ardhini, matokeo yake ardhi inakuwa kame na kusababisha mimea kutokustawi kila inapopandwa. Miti hii ya mikaratusi ipo sana Manispaa ya Singida, vijiji vya Kititimo, Unyamikumbi, Mandewa na vinginevyo.

Wakati mwingine sio lazima kufuata mlolongo mrefu wa utekelezaji, ni Serikali kutoa kauli ya utawala ili Taasisi husika zitekeleze. Ninakuomba Mheshimiwa Balozi Kagasheki, Waziri Mwenye dhamana kutoa kauli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti ya mbao. Napenda kutoa tahadhari kwa Serikali katika suala zima la kutoa vibali vya kuvuna miti ya mbao. Kulikuwa na tatizo la watu kuchukua vibali vya uvunaji wa miti ya mbao kisha wanaviuza kwa watu wengine. Naomba sana Serikali kuwa makini ili tabia hii ikome kabisa. Naamini kwa uwezo wa Mheshimiwa Balozi Kagasheki, Waziri mwenye dhamana na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Naibu Waziri, tabia hii itakuwa imetoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majangili/wawindaji haramu. Napenda kuitaka Serikali kuendelea kuongeza ulinzi katika eneo hili ili kukomesha kabisa majangili na wawindaji haramu hususani misitu ya hifadhi iliyoko Wilaya ya Manyoni mfano Ruangwa na kadhalika. Bado ujangili upo na wawindaji haramu pia wapo. Ushauri wangu Serikali iongeze idadi ya Askari pamoja na kutoa gari la *patrol*. Nasubiri majibu yenye huruma ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Nawaombea Mungu awape nguvu, afya na mshikamano ili waweze kutekeleza azma yao kama ambavyo wameonyesha uwezo wao wa juu.

**MHE. DKT. TEREZYA P.L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia,

ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya maliasili ni jambo muhimu sana katika kuendeleza uchumi wa nchi hasa ukizingatia matatizo ya mabadiliko ya tabia ya nchi yaliyoko. Ninaomba Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane kwa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuhifadhi mazingira ya Maliasili hasa maeneo oevu na vyanzo vya maji. Sasa hivi kuna hatari ya kukauka vyanzo vyote vya maji kama hatutachukua tahadhari ya utekelezaji wa mkakati kabambe wa kuzuia shughuli za wananchi kwenye hifadhi zinazohusu vyanzo vya maji na misitu. Shughuli za kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini kwenye hifadhi ni lazima zikatazwe kwa nguvu zote. Msisitizo ukizingatiwa kwenye hifadhi ya mazingira ya maliasili, sehemu kubwa ya nchi yetu itakuwa imehifadhiwa na vyanzo vingi vya maji na misitu vitabaki katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kati ya Wizara zinazoweza kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Serikali, kwa maana hiyo ni vyema kuweka kipato mbele kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kutangaza utalii. Pamoja na juhudi za Wizara hii ya kutangaza utalii

bado hailingani hata kidogo na baadhi ya nchi jirani kama vile Kenya, South Afrika wanatumia *budget* kubwa kutangaza utalii. Hivyo niishauri Wizara kutenga fedha zaidi kutangaza kwa mashindano ili Tanzania iweze kuongeza watalii zaidi na hivyo kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kutunza vyanzo vya utalii na hifadhi. Tunaelewa kwamba Wizara kupitia uongozi wake wanajitahidi kutunza na kuhifadhi wanyamapori lakini kila siku zikiendelea hujuma za wanyamapori zinaendelea na majangili wanapora nyara mbalimbali za wanyamapori. Juhudi hizi zinahitajika kulinda nyara za wanyamapori kwa sababu bila ya kulinda uhifadhi basi utalii unaweza kushuka mwaka hadi mwaka. Nitoe wito kwa Wizara lazima ifanye juhudi kubwa kuweka ulinzi mkali kwa nyara za Tanzania na hifadhi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhifadhi historia. Wizara ya Utalii ijitazame zaidi katika kutafuta historia ya vijiji mbalimbali vya Tanzania. Hii itasaidia watalii kuwa na hamu kuweza kutafuta historia na kuitangaza ili kuvutia watalii na hivyo kuongeza pato la Taifa. Tanzania ina historia pana sana, tunaweza kuibua mambo mbalimbali yanayovutia watalii mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kufanya utafiti. Pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu tafiti, mimi nina mawazo tofauti kidogo juu ya utafiti. Hadi sasa wapo wanyama ambao Tanzania hawajawatambua, ni vyema kufanya utafiti wa kina ili

kujua ikolojia yote ya wanyama tulionao hapa Tanzana. Hivyo, naomba Wizara hii kujikita na kuelewa *variety* ya wanyama tulionao Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utalii uliopo nchini mimi na wananchi wangu wa Rukwa tungependa kujua kama Mkoa wa Rukwa katika miaka yote ya kuwa na Katavi Mbuga za wanyama ni kitu gani tunachoweza kujivunia kwa miaka yote iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mgawanyo wa kufanya *Lwaji Game Reserve* kuwa mbuga za wanyama, je, tutaamini vipi kama wanyama waliopo Katavi wataelekea Lwanji na kufanya maskani yao huko? Kama wanyama hao hawataweza kuweka maskani yao Lwaji, Serikali itawajibika vipi kuhakikisha ile Mbuga ya Lwaji nayo inakuwa kama Mbuga zingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mgawanyo huo wa Katavi Mbuga za Wanyama na *Lwaji Game Reserve* kuwa mbuga za wanyama, ni kweli mgawanyo huo utatutendeaje haki sisi tunaobaki na *Lwaji Game Reserve* kama mbuga za wanyama ikiwa mamba na viboko vingi vimebakia Katavi? Je, mgawanyo wa mamba na viboko utakuwaje? Au viboko na mamba wa mto Sitalike ni wa Katavi na mamba walioko ziwani ndio wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kuna watu wanaofugia nyuki katika eneo la Mtimka Lwaji, ni vipi Serikali imeruhusu kuipandisha hadhi mbuga hiyo na kisha kuachia watu kuendelea kufanya uharibifu eti wanafugia nyuki mle na kuchungia ng'ombe wa Kisukuma mle?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni sana wahusika kuhakikisha watalii wanaoingia *Lwaji Reserve* wanachunguzwa sana kwani inasemekana wamechimba mashimo ya madini sehemu za Ninde Milimani na si hivyo tu Wazungu wanaoishi kule ziwani wawachunguze sana mzunguko wao na kama ninavyosikia huwa wana mizunguko ya usiku. Wengine wako Mbeya huw wanakuja usiku toka Mbeya na kurudi usiku kwa usiku Kilaugala Hospitali, kufuatana na tetesi za wananchi inasemekana wanapora mali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute njia ya pekee ya kuboresha maporomoko ya Kalambo kwa kupunguza lile gema la kilima ili maporomoko yale yaweze kuvutia watalii kupitia Tanzania ili sehemu za Kalambo nazo zichangamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri aliyoianza, kaza buti, la sivyo Makatibu Wakuu wa Wizara huwa ndio waharibifu namba moja kwa kutenda hiana ya uhujumu uchumi. Nakutakia afya njema pamoja na Naibu Waziri wako, Mshoneni Katibu Mkuu na wala msiwaonee haya Watendaji wabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa umakini mzuri wanaoufanya katika uendeshaji wa Wizara hii. Pia nampongeza Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu kwa nini vikao vya mashirikiano baina ya Wizara hii na Wizara inayoshughulikia mambo ya utalii Zanzibar yamesitishwa kwa muda mrefu sasa, kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa nini bahari ya Hindi *(Indian Ocean)* haitumiki kwa utalii kwani hiki ni kimoja sehemu ya utalii kwa Bara la Hindi na utalii huu unaweza kuongeza mapato ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua njia ya utalii kwa kutumia njia ya watumwa (*slave rout*e), kwa nini haishirikishwi Zanzibar wakati historia inatueleza soko la Afrika Mashariki la utumwa limeanzia Zanzibar katika Kanisa la Mkunazini na kwenda Bara kupitia Bagamoyo. Kwa hiyo, kwa nini katika utalii huu Zanzibar haishirikishwi? Nashauri Zanzibar nayo ishirikishwe ili tutunze historia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango gani au juhudi gani za kurudisha miti ya kienyeji/kiasili iliyomalizika kwa kukatwa na kuchomwa mkaa na kuni (*gene bank*)? Wizara ina mkakati gani wa kunusuru Tanzania kugeuka jangwa kwani tumeshuhudia miti mingi imeshaondoka kwa uharibifu wa mazingira na

mabadiliko ya tabia ya nchi na kupotea kwa uoto wa asili kwa sehemu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Naibu Waziri, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuleta hotuba ya bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ya hifadhi. Tanzania tumejaaliwa kuwa na misitu yenye rasilimali nyingi sana lakini bado Serikali haijakuwa na utaratibu mzuri wa utunzaji, uhifadhi na hata kusababisha kuwapo na migogoro ya umiliki, mipaka haieleweki, hifadhi nyingine zimevamiwa, ni vizuri uwepo utaratibu mzuri wa ushirikishwaji wa wanavijiji na hizi hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu wa Kihesa, Kilolo Iringa. Hifadhi hii muda mrefu sana Halmashauri ya Iringa imeshaleta barua kuomba hifadhi ya msitu huu sasa uhamishwe ili kupima viwanja, lakini hatuelewi tatizo ni nini? Msitu huu kwa sasa upo katikati ya majengo ya wakazi ya watu kiasi kwamba hifadhi hiyo imekuwa vichaka vya majambazi na hakuna kitu chochote katika hifadhi hiyo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja zetu atueleze ni lini sasa msitu huo utahamishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu wa Mufindi. Msitu huu tulitegemea Wizara iweke utaratibu wa wananchi

wanaoishi katika Wilaya na Mkoa wa Iringa wapatiwe kipaumbele na kupatiwa vibali vya kukata miti, ajabu yake vibali vingi vinatolewa kwa watu wa kutoka nje ya msitu na Mkoa wa Iringa. Aidha, katika mapato ya hifadhi uwepo utaratibu wa kutenga fungu kuisaidia Halmashauri ili kusaidia uboreshaji wa barabara zinazozunguka hifadhi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii. Napenda Waziri anieleze ni jitihada gani Serikali inafanya kuinua utalii Kanda ya Kusini ili kukabiliana na changamoto za utalii za Ngorongoro na Serengeti ambazo kwa sasa magari ya utalii yamekuwa mengi na kusababisha msongamano. Je, Serikali haioni umuhimu kuanzisha Bodi Maalum ya Ukanda wa mbuga hizo ili ziweze kuji-*market* zenyewe? Bodi hiyo itengewe pesa maalumu kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo maeneo ya Kusini kama vile Kitulo, Ruaha, Udzungwa ambapo kuna nyani wa kipekee kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia neleze masikitiko yangu kuhusu mbuga ya *Ruaha National Park* iliyopo Mkoa wa Iringa. *Ruaha National Park* ina wanyama wengi sana lakini bado hakuna mkakati wa kuhakikisha kwamba inatangazwa na kuifanyia *marketing* ili Serikali iweze kuongeza idadi ya watalii wanaokuja kutembelea katika mbuga ile. Ni imani yangu kuwa Iringa yetu ni mji wa utalii na wananchi wanaweza kujiongezea kipato kutokana na utalii uliopo katika Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamba waliopo Mto Ruaha- Mbuyuni Iringa. Naomba Serikali itueleze inawasaidia vipi wananchi waliopo kandokando ya Mto Ruaha (Mbuyuni), Jimbo la Kilolo, Mkoa wa Iringa, kina mama wamepata ulemavu, wamepoteza maisha kutokana na mamba waliopo katika mto ule. Ni kwanini Wizara isitoe fungu la pesa ili maji yavutwe, yawepo mabomba ili wananchi wasiendelee kupata madhara ya mamba hao? Naomba tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalamu na Taasisi za Wizara kwa kuandaa hotuba na bajeti ya mwaka 2012/2013 vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti katika hifadhi zetu si mzuri sana, hivyo kuna haja ya kuboresha ulinzi na usalama wa watu, wanyama na wadau wengine katika hifadhi zote. Jitihada zifanyike zaidi ili watu jirani na hifadhi za Taifa wapate manufaa zaidi kutokana na hifadhi na pia wawe wahifadhi pamoja na *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itoe maelezo na Hifadhi zote na Mapori ya Akiba yasitanue tu mipaka yao bila kujali wananchi na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Mipaka ya Pori la Akiba na Mkungunero zirekebishwe zisiingie Wilayani Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ianzishe mfuko wa programu ya kuwezesha na kuendeleza *WMA* zote nchini ili zisaidie hifadhi ya wanyama katika maeneo haya. *Paradigm* ya hifadhi iwe *re-visited* na *focus* kwa sasa iwe ni "*wise use*" badala ya kukataza matumizi ya kila kitu ndani ya hifadhi.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa hili kwa sababu Idara zake zinatengeneza sehemu kubwa ya pato la Taifa. Naipongeza Serikali na kipekee kwa kufanya maamuzi mazuri ya kusimamisha watendaji wabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya *TANAPA* inafanya vizuri kukabiliana na ujangili wa nyara za Serikali. Nashauri Serikali iongeze Askari wa Wanyapori ili hifadhi zetu za Taifa zilindwe na nyara za Serikali ambazo ndio kivutio cha utalii zisipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia iangalie na idhibiti fedha za utalii zinazolipwa nje ya nchi, kwa nini fedha hizi Serikali isitoe amri zilipwe katika akaunti za wafanyabiashara wa utalii za hapa nchini za Tshs na za USD? Kulipa gharama zote nje ya nchi inawezekana kukawa na udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Serikali iweke *Tours Parks* katika Mji wa Arusha na Moshi. Hii itawavutia watalii hasa wale ambao wangekwenda Nairobi kupumzika, wanaweza kupumzika katika eneo hili. Inawezekana kabisa kutumia sheria ya *PPP*, *private sector* ikajenga kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni za utalii ni ghali kiasi kwamba wafanyabiashara wengi ni *foreigners.* Nashauri Serikali iangalie jinsi ya kusaidia kampuni za wazawa ili nao waweze kupata kipato cha kutosha kwa familia zao hata kama ni kwa njia ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kubwa ya kuwa na ndege zetu ambazo zitaondoka kwenda bara nyingine na mtalii afahamu kuwa akipanda ndege hiyo anakuja *direct* Tanzania, kutokuwa na *Airline* yetu na ndege kunaathiri sana utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali (Wizara) ishirikiane na Balozi zetu za nje kupeleka Maafisa Utalii hasa katika Balozi zile zilizoko nchi zenye watalii wengi. Balozi nyingi hazitangazi utalii ipasavyo. Nashauri Afisa huyu awe ni mfanyakazi wa Wizara hii na alipwe mshahara na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Utalii *(Travel Agents)* wamekuwa wakiwapunja *porters* mafao yao. *Porters* hawa wanaenda kwenye eneo la mlimani (katika kilele) cha mlima Kilimanjaro na hawana Bima ya aina yoyote. Nashauri Serikali iwasaidie Wakala hawa wawalipe *porters* fedha ya kutosha na Serikali iwabane Wakala hawa ili *porters* hawa wawekewe Bima ya Maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuweka viwango vinavyotakiwa kwa aina ya *Tour guides* wanaotakiwa, viwango vya hoteli na lugha inayotakiwa wafanyakazi wawe nayo wanapokuwa wanafanya kazi katika mahoteli. Iko haja wafanyakazi

hawa wawe na lugha zaidi ya moja ili kuwa na uhakika wa kupokea wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani usiwe tu Watanzania kwenda Manyara na *Ngorongoro crater*, Watanzania wahamasishwe watembelee katika maeneo ya kumbukumbu za kale na kadhalika. Serikali ifanye *advocacy* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupata fedha ya utalii kutoka Ukanda wa Kaskazini, kuna haja hifadhi ya mlima Kilimanjaro na Mkomazi katika Wilaya ya Same kutunzwa. Ziko Halmashauri za Wilaya zimezunguka maeneo haya ambayo ni wadau wakubwa. Je, Serikali kupitia *KINAPA* kwa nini hawalipi *serve levy* kwa Halmashauri hizi (Moshi, Siha, Hai, Rombo na Same). Ninaomba kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuweka fursa sawa, sijaona nguvu ya Serikali kuhamasisha *Tour Guides* wanawake. Naomba kauli ya Serikali ni namna gani itawapa fursa wanawake katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuruhusu kuchimba Urani katika mbuga ya *selous* ni cha kusikitisha, nashauri Serikali isiendelee kumega hifadhi kwa *pretext* ya kupata fedha, itafute maeneo mengine. Itakuwa vigumu kuzuia wachimbaji wadogowadogo mfano maeneo ya Mahene - Nzega, Lushoto, wanaovamia hifadhi kutafuta dhahabu au madini mengine, kama Serikali itajiingiza katika kuchimba madini katika hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa vitalu vya uwindaji ulitolewa kwa njia isiyokuwa na uwazi na walioomba wengi ambao sio matajiri walikosa, hii inaondoa dhana ya kumpa uwezo Mtanzania. Nashukuru Mheshimiwa Rais amempa Mheshimiwa Balozi Kagasheki Wizara hii, naamini kabisa yeye kama mchapa kazi na mzoefu wa *foreign service* anaelewa utalii ni nini na ni vitu gani vitamvutia mtalii, naamini ugawaji vitalu *next time* utakuwa wa uwazi na haki zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali ianze mapema kuwatangazia Watanzania kuhusu shindano la kutafuta "*wonders of the world",* redio, meseji za simu, *facebook, twitter*, *jamii forum* na kadhalika zitumike kikamilifu kuanzia sasa. Vikundi vya sanaa, waimbaji wa muziki wa kawaida, miziki ya injili wote kwa pamoja tufanye kazi hiyo. Lakini Madiwani, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya waelezwe waelewe pia Wenyeviti/Watendaji katika vijiji na kata ili sote tufanye kazi ya kunadi vivutio vyetu vilivyoteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii, kwa kipindi kifupi imeonyesha matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi nzuri yenye maliasili lukuki na za kupendeza. Ni vema Serikali ikawekeza kwa kiwango kikubwa ili badala tu ya kuwa na kilimo kama uti wa mgongo, tunaweza tukaingiza

fedha nyingi za kigeni na kufanya maliasili na utalii kuwa eneo linaloiingizia Taifa fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujangili linarudisha nyuma sana kukuwa kiuchumi kupitia sekta ya maliasili hususan katika Pori la Akiba la *Selous.* Katika pori hili ujangili umekithiri, unafanyika bila woga, nyara mbalimbali zinaibiwa/zinaporwa, tembo wanauwawa hovyo na inaonyesha kana kwamba pori hili halina mwenyewe, ni shamba la bibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Pori la Akiba la *Selous* lifanyiwe utaratibu wa kuundiwa Mamlaka yake au iwe hifadhi ya Taifa na hatua hiyo itaimarisha ulinzi wa pori hilo na kuongeza mapato yatokanayo na pori hilo kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujangili na uporaji wa maliasili unachangiwa sana na ufinyu wa bajeti, wakati mwingine katika maeneo yanayozunguka *selous* hususan Wilaya ya Liwale inapotokea ujangili au uporaji wa mazao maliasili kama vile mbao na kadhalika, wahusika wanapopewa taarifa huwa wanakosa vitendea kazi, kama vile mafuta ya gari na kulazimika kuomba katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hivyo kukwamisha zoezi zima la kuokoa uporaji na ujangili huo. Aidha, kutokuwa na wafanyakazi/askari wa kutosha katika Pori la Akiba inakwamisha pia suala zima la ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji nyuki, ni dhahiri kuwa asali ni zao lenye kuongeza thamani ambalo likiwekewa mkakati mzuri wa kuendelezwa na

kuenezwa kwa nguvu zaidi katika Mikoa mingine hususan Mtwara na Lindi ambapo kuna misitu na uoto wa asili wa kutosha na kumekuwepo na makundi mengi ya nyuki ambapo warina asali wa kienyeji wamekuwa wakivuna na endapo wataalam wa ufugaji wa nyuki wakisambazwa katika Halmashauri zetu wakafanya kazi ipasavyo bila mashaka asali inaweza kuwa zao bora la kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Nashauri programme ya nyuki ya Taifa ipanue wigo wake na kuongeza maeneo ya kuyashughulikia badala ya kujielekeza kwenye Mikoa michache nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba pia Wizara iangalie na kutoa mwongozo wa athari za kuvuna misitu yetu (mbao) kwa kutumia mashine mbalimbali za kisasa za kichina ambazo zinaharibu kabisa uoto wa asili na kutoruhusu miti kuota tena katika maeneo husika.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, pia napongeza kazi nzuri yenye mwonekano wa wazi na makusudi wa kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake pamoja na changamoto zinazoikabili Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na mikakati ya wazi yenye kutoa au kubeba *programs* endelevu zenye *activities* zinazolenga vijana na zionekane kama zipo, ziainishwe katika majumuisho. Fursa mbalimbali za vijana katika sekta ya Utalii na Maliasili ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Wizara ishirikiane kwa karibu na vijana katika vijiji vinavyozunguka au vilivyo karibu na mbuga za wanyama kwa ku-*support* ulinzi shirikishi wa vijana katika sehemu zao hasa sehemu zilizopo mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa ndege ni muhimu sana kwa uhakika wa kukua kwa utalii wetu, *one direct stop* kuja Tanzania bila kutua nchi nyingine ya Afrika Mashariki ni muhimu. Ushirikiano kuhakikisha sekta hii ya usafiri wa ndege inakuwa ni muhimu itatoa ajira, *exposure* kwa watu wetu na watalii watatumia miundombinu yetu mbalimbali nchini sio kuwa *transported* kutokea nchi za jirani. Napongeza sana "Qatar" kutua moja kwa moja Kilimanjaro. Inawezekana China, Korea, Rusia pia watue na waende pia kiwanja cha ndege cha Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza ukulima/ufugaji wa nyuki ni njia moja rahisi kwa kuwapa vijana nafasi rahisi ya kazi na kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa dhati juhudi na bidii za kukuza utalii wa utamaduni na michezo na ushirikiano wa karibu na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napongeza pia vyuo na hasa Chuo cha Utalii na hoteli Dar es salaam. Nashauri suala la lugha za kigeni pamoja na *hospitality* itilie umuhimu na ikiwezekana kuwe na kozi fupifupi za lazima kwa watakaoajiriwa katika *hotels*. Lakini pia

Wizara iangalie vyuo vingine *(mushrooming)* kila mahali vya utalii/*private* viwe vya *standard* au vifungwe. Wenye hoteli waajiri vijana waliopitia kozi mlizozipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha Idara ya Habari, Elimu na Mawasiliano ya Wizara inapewa nafasi inayostahili. Msemaji wa Wizara hiyo basi apewe rasimali stahili ikiwa ni pamoja na watu, fedha na *equipments*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri na ngumu na inazimudu, Katibu Mkuu kila la kheri. Naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu na Wataalam wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maliasili kutokana na rasilimali ya maliasili tulizojaliwa ina utajiri mkubwa sana ambao ungeweza kuondoa kabisa umaskini kwa Watanzania uliokithiri kama ingesimamiwa vizuri. Kukosekana kwa uzalendo miongoni mwa watendaji wa Serikali, ubinafsi, ulafi na kutokuwepo na mipango makini ya matumizi ya rasiliamli zetu, kumetupelekea sisi kuwa ni watazamaji tu huku wachache wakinufaika na rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 pamoja na mambo mengine ilikuwa na lengo la kuwapa fursa Watanzania kushiriki kwenye

tasnia ya uwindaji wa kitalii ambao kwa miaka yote biashara hii ilihodhiwa na wageni/wazungu. Cha kusikitisha pamoja na sheria kuanisha wazi kuwa asilimia 75% ya vitalu vya uwindaji vimilikiwe na wawindaji wa Kitanzania, bado vitalu vingi tena vizuri, vinono vinamilikiwa na wageni. Kila leo wazee, vijana wa kigeni wanaingia nchini na kupewa leseni za uwindaji wakati Watanzania wataalam wa uwindaji *(professional hunters)* wakinyimwa leseni. Tunaitaka Serikali ilete orodha/idadi ya Watanzania *(professional hunters)* waliopewa leseni kwa miaka mitatu 2009-2012 na wageni waliopewa leseni kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya hifadhi za jamii *(WMAs)* mengi yameanzishwa kwa nguvu za wananchi na kusaidiwa na wafadhili, pale wafadhili wanapoondoka kabla ya hifadhi hizi kusimama na kujiendesha zinabaki kama yatima na rasilimali/maliasili iliyotunzwa kwa miaka mingi inakuwa kwenye hatari ya kupotea/kutoweka. Ni utaratibu gani umeandaliwa na Serikali kwenye hifadhi hizi kujenga uwezo kwa wananchi na wadau wa maeneo haya ili waweze kusimamia maeneo haya pale wafadhili wanapoondoka? Kanuni za uanzishwaji *WMAs* zinaainisha wazi kwamba wananchi watajengewa uwezo, wasimamie wenyewe matumizi ya maliasili zao na Serikali itatoa ushauri wa kitaalamu pale unapohitajika. Je, ni kwa nini kwenye maeneo ambayo yameanza kuvuna rasilimali zao Wakala wa Serikali wanachukua asilimia 55%?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani unadorora kwa sababu ya kukosekana kwa makazi ya

bei nafuu ndani ya hifadhi zetu ambayo wanaweza kumudu. Watanzania wanapenda kutembea na familia zao wakae *park* angalu siku 3-7 wafurahie vivutio vilivyoko. Hoteli kubwa zilizoko *park* zimejengwa/zinamilikiwa na wawekezaji kutoka nje. Safari zote zinauzwa nje, pesa zinalipwa nje kinacholetwa nchini ni *(just a peanut)* kidogo sana. Hoteli wana-*charge* USD 500-1500, Watanzania tunajua vipato vyao hawawezi kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itenge maeneo maalum kwenye vivutio vya utalii kwa ajili ya kuwapa Wazawa/Watanzania wajenge hoteli za gharama nafuu kwa ajili ya utalii wa ndani (asilimia 100 zimilikwe na wazawa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe majibu nini hatma ya hoteli ya Mikumi Lodge iliyopo *Mikumi National Park* ambayo ilikuwa na kesi na Serikali. Serikali ilishalipa mamilioni ya pesa? Watanzania wamekuwa wanaomba wawekeze pale bila mafanikio, tunasubiri wageni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha hoteli zilizoko hifadhi kukaidi agizo la kulipa *concession fee* mpya zilizowekwa na *TANAPA*, ni kitendo cha uhujumu wa uchumi. Haiwezekani tozo za miaka ya 1990 wakati kitanda kimoja wakilipa USD 100-200 walipe *concession fee* US 5-15, leo hii wana-*charge* kitanda kimoja USD 300-1500 hawataki kulipa viwango vipya. Hii jeuri ya kuamua wao walipe kiasi gani wanaipata kwa nani? Nani yuko nyuma yao? Ananufaika na nini? Kuna kigugumizi gani cha Serikali kuchukua hatua au wapo

vingunge wa Serikali wana hisa Sopa na Serena hoteli hivyo wanakula wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Misitu *(TFS)* imeanzishwa kwa lengo la kuboresha sekta na misitu na huduma zake ili kuwezesha sekta hii muhimu kuchangia zaidi pato la Taifa na kuinua kipato cha wananchi. Zipo taarifa kwamba Mamlaka hii imepelekwa kwenye Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Serikali ihakikishe sekta hii/Mamlaka hii inabaki chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii ya Taifa *(TTB)* haiwezi kutangaza vivutio vya Tanzania na kuwezesha tasnia ya utalii kukua kama haitengewi fedha za kuweza kufanya kazi. Hatuwezi kuvuna bila kuwekeza! Bodi haina watumishi wa kutosha, rasilimali watu, fedha na kadhalika. Miaka miwii hawajapewa kibali cha kuajiri hata mtumishi mmoja japo wana upungufu mkubwa wa watumishi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa waliyofanya ya maandalizi ya bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa katika maeneo ya misitu inayozunguka (iliyoko Mkoa wa Pwani) na maeneo mengine ya mjini, uendelezwaji wa malikale na utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu mingi iliyopo mijini kama vile Vikindu na Mwandege Mkuranga, misitu ile inamalizwa na wananchi kwa kulima na kujenga nyumba za kuishi, lakini pia misitu hiyo haitunzwi matokeo yake yanakuwa makao ya majambazi. Nashauri Serikali iangalie jinsi ya kuitunza na kuhifadhi misitu ile na kuwa kivutio cha watalii na hata kubadili matumizi kwa baadhi ya maeneo na kujenga hoteli za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezwaji wa malikale, tunayo maeneo mengi ya urithi wa utamaduni lakini maeneo haya hayaendelezwi na fungu la fedha wanazopewa ni ndogo wakati maeneo hayo hi muhimu sana kwa utalii wa wetu wa ndani. Serikali ifanye juhudi za makusudi kuboresha utalii wa ndani ambao ni chanzo kizuri cha uchumi, tusitegemee sana watalii kutoka nje. Lakini *cultural heritage* zetu hazina maelezo na hazijatangazwa kwa wananchi wazitambue. Naomba Serikali itoe fedha za elimu kwa wananchi watambue urithi wao na wazitembelee sehemu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Mkurugenzi na Bodi ya Makumbusho ya Taifa kwa kujitangaza na kufahamika na wanafunzi wengi na hasa shule za msingi na inatumika vizuri, hongereni sana na jitahada ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara hii kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa kwanza kwa Serikali ni kwetu kama Taifa kutambua kuwa kama tutaendeleza na kusimamia sekta hii, tunaweza kuendeleza Taifa letu kwa kutumia sekta hii kwa kasi ya hali ya juu. Jambo linalohitajika pamoja na mipango na mikakati mwingine ni ushirikiano wa Watanzania wote chini ya usimamizi wa Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasii inapaswa kuwa Wizara kiongozi katika kuendeleza sekta hii pamoja na Wizara ya Ardhi, Mambo ya Ndani, TAMISEMI, Vijana na Utamaduni kwa kutaja baadhi zinapashwa kutoa kipaumbele kwa suala la maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uoto wa asili na maumbile ya nchi tunayojivunia na kutumia kama vivutio vimekuwepo au kujengeka kwa miaka mingi. Kitendo cha kuharibu vivutio kinachofanyika sasa kitatunyima faida ya kiushindani tuliyonayo lakini tutakuwa na hali ngumu ya kurudisha asili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu katika misitu ya hifadhi katika Mikoa ya Magharibi imekuwa ikifanyika mbele yetu, Mikoa ya Kagera, Kigoma na Geita nimeshuhudia uharibifu wa misitu ya hifadhi kwa shughuli zisizokuwa na manufaa kwa Taifa. Ushauri ni kuwa Seriiali iamke na kukomesha uharibifu huu kwa kuanza kuwawajibisha watendaji waliopewa dhamana

ya kulinda misitu hiyo, kutambua Idara za Serikali na mamlaka nyingine ambazo kwa kuzembea tumefika hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uharibifu wa hifadhi, shughuli za ufugaji/uchungaji wa ng'ombe limechangia, tusimamie imara na kuamua uchungaji wa ng'ombe katika hifadhi ukomeshwe. Hapa ushirikiano wa Wizara mbalimbali unahitajika kulenga kutatua tatizo hili. Idara ya Uhamiaji kwa ng'ombe watokao nje ya nchi, Jeshi la Polisi na Wizara ya Mifugo wanapashwa kutoa ushirikiano. Kwa kuwa waendeshaji wa uchungaji huu wana nguvu zikiwemo za kijeshi, Jeshi la Wananchi lihusishwe. Yote hayo ni kulenga kuondoa shughuli za kibinadamu katika hifadhi na kuacha eneo la asili listawi lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uwepo na utendaji wa maliasili ngazi ya Wilaya. Wataalamu hawa wamemezwa, utaalamu wao hautumiki, wamebaki watu wa kukamata mbao tu na mkaa wakiacha misitu inateketea, lakini mchango wao katika kuelimisha na kusimamia jamii katika kulinda maliasili ikiwemo ufugaji wa nyuki katika baadhi ya Wilaya ni mdogo sana. Wataalamu hawa wanahitajika wakiwa na majukumu yaliyo wazi ili tuje tuwawajibishe inapobidi. Ili kuhifadhi na hatimaye kupata faida ya maliasili yetu, wataalamu wetu hawa wanapashwa kujengewa uwezo kwa kila hali, tuwe nao kwa kadri ya mahitaji, tuwawezeshe na wawajibike. Maelezo ya ufugaji wa nyuki kwa mfano yametolewa vya kutosha, wataalamu wasimamie kwa kuonyesha mfano na kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri juu ya suala la kujenga taswira ya Wizara. Kwa nje taswira ya Wizara si nzuri na kwa hili dawa yake ni kuongeza uwazi katika utendaji na uwajibikaji. Chini ya utaratibu huu wale wanaokiuka taratibu na sheria zinazoendesha shughuli waenguliwe mara moja na sheria ichukue mkondo wake. Kama nchi tusione aibu kujifunza kutoka kwa wenzetu ambao wanafanya vizuri katika sekta ya maliasili na utalii. Tunapaswa kuwakaribisha wageni kama wawekezaji lakini tuwe macho na mbinu zao za kuendesha shughuli hizi. Utalii usifanyike hapa malipo yenye maana yakabaki ughaibuni. Hii ni pamoja na kuepuka kuingia mikataba ambayo itatufanya sisi tuendelee kuwa watazamaji katika nchi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali kuanza kuhamasisha utalii watu na utamaduni wao. Wapo watalii ambao wanapendelea kwenda kwenye jamii mpya kuishi nao kwa muda, kuangalia wanavyoishi na kuendeleza maisha yao. Kutokana na hali nzuri ya hewa katika nchi yetu, ni imani yangu kuwa sekta ndogo ya utalii watu ikihamasishwa italeta kipato kizuri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuanza vizuri na hotuba nzuri ya bajet.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba Wizara ikishirikiana na Wizara ya Uchukuzi zifanye juhudi za ziada kuhakikisha uwanja wa ndege wa Mwanza unatengenezwa kwa kiwango cha Kimataifa ili kuwezesha watalii kutua kwa kiwango cha Kimataifa na kuelekeza Serengeti, Kigoma, Visiwa vya Rubondo na fukwe za Ukerewe. Vilevile maeneo ya makumbusho ya Wasukuma Bujora na mapango ya Wajerumani Mbarika. Vilevile Kisiwa cha Saa Nane kiangaliwe kama mojawapo ya vivutio katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ihamasishe ujenzi wa mahoteli na kumbi za mikutano kwa ajili ya wakuu wa nchi za Maziwa Makuu kwani jiji hili liko karibu na Makao Makuu ya nchi zote za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia 101.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri inazungumzia juu ya uchimbaji wa Urani katika Pori la Akiba la *Selous* ambalo ni eneo la urithi wa dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nilihoji juu ya uhalali wa Kampuni ya Uwindaji ya *Game Fronters of Tanzania Limited* ambayo imepewa leseni ya uwindaji katika eneo la kijiji cha Mbarang'andu. Kuingia makubaliano na kampuni za utafiti wa Urani za *Uranium Resources PLC* na *Western Metals T. Ltd,* mkataba huo, pamoja na mambo mengine unatoa ruksa kwa kampuni hiyo ya

uwindaji kulipwa malipo mbalimbali ya $6,000,000, $250,000 na $55,000 kwa nyakati tofauti kwa kadri vipengele vya mkataba husika unavyoainisha na wakati huohuo Serikali ya kijiji ambacho mbuga hiyo ipo imegawiwa mgao wa $10,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia sheria mbalimbali za nchi yetu iwe Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 (Mijini na Vijijini), *the Wildlife Conservation Act 1974* na 2009 na *The Mining Act* ya mwaka 2010, sijaona mahali popote ambapo mtu au kampuni ya uwindaji ambayo ina leseni ya uwindaji tu kuingia makubaliano na kampuni ya utafiti wa madini na kulipwa mabilioni ya fedha, wakati huohuo kijiji ambacho ndio wamiliki halali wa ardhi, kuambulia fedha kiduchu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 10 cha mkataba husika ambao naamini Wizara na Mheshimiwa Waziri anajua, umeainisha wazi kwamba kampuni ya uwindaji itatoa tarifa ya maandishi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii juu ya makubaliano hayo ya matumizi ya kitalu husika kwa shughuli ya utafiti wa urani. Naomba Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge hili Tukufu ni kwa kiasi gani ina ufahamu wa makubaliano husika na yana uhalali kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu wa Kazimzumbwi. Niungane na taaria ya Kamati ya Bunge ya Ardhi na Maliasili juu ya mateso na kero kubwa wanayokumbana nayo wananchi wa kijiji cha Kazimzumbwi kutokana na kero na adha wanayokutana nayo kutoka kwa Askari wa hifadhi hii. Wizara ya Ardhi ambayo ndiyo pekee yenye mamlaka

ya kupima na kutambua mipaka ilitekeleza wajibu wake, lakini cha kushangaza baada ya Wizara ya Ardhi kutekeleza wajibu wake na kuainisha eneo la kijiji na eneo la Maliasili (misitu), wananchi bado wameendelea kusumbuliwa sana. Mheshimiwa Waziri nilimletea taarifa pamoja na ramani ya eneo husika, naomba kauli ya Serikali kuhusiana na mgogoro huu ili hili suala lifike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya Tarangire. Katika hotuba ya Ardhi tuliainisha ni kwa namna gani wanakijiji wanaozunguka hifadhi hii wameathirika kutokana na hifadhi kubadilisha mpaka uliokuwa ukiwatenganisha wanakijiji na hifadhi tokea mwaka 1953. Mpaka wa awali ulikuwa ni barabara ambayo iliheshimiwa sana na wanakijiji, lakini tatizo lilianza pale ambapo hifadhi ilitumia vifaa vya kisasa kupima upya hifadhi, hali iliyopelekea maeneo ya vijiji yaliyokuwapo tokea awali kuingizwa kama sehemu ya hifadhi.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maofisa wote wa Wizara hii, naiunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa nyuki. Kwanza niipongeze Wizara kwa kazi nzuri katika eneo hili lakini ufugaji wa nyuki katika visiwa vya Unguja na Pemba bado haujakuwa wa kitaalamu kama ilivyo Tanzania Bara. Misitu mikubwa ya Kitaifa kama msitu wa Ngezi uliopo Pemba na Jozani uliopo Unguja haujatumika

kikamilifu katika ufugaji wa nyuki. Kadhalika kuna maeneo mengine yenye misitu ambayo pia yanaweza kutumika katika ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Idara ya Misitu, Kitengo cha Ufugaji nyuki kishirikiane na Idara ya Misitu ya Zanzibar kwa azma ya kuendeleza ufugaji wa nyuki Zanzibar. Hii itaiwezesha Zanzibar kujitosheleza kwa asali na kuweza kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji wa miti. Faida za miti ni muhimu sana kwa binadamu na viumbevyote ulimwenguni hasa kupunguza hewa mkaa na upatikanaji wa mvua. Hivyo inabidi kufanya juhudi kubwa ya kupanda miti ingawa jumla ya miche 8,730,550 imepandwa nchini lakini zaidi ya nusu ya miti hufa kutokana na kutokuangaliwa. Miti inapokuwa michanga inahitaji kupaliliwa na kutiliwa maji wakati wa kiangazi, mambo haya hayafanywi na matokeo yake miti mingi hufa yaani zaidi ya asilimia hamsini. Hivyo namtaka Mheshimiwa Waziri ahakikishe walau asilimia 70 ya miti haifi na kuwa miti mikubwa.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata fursa hii adhimu kwangu na kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa kila kitu, kwa kunijaalia uhai na uzima. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ndani ya Wizara yao, Mungu awabariki kumudu kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza mchango wangu kuhusu ujangili. Ujangili ni vita mbaya dhidi ya wanyama muhimu Tanzania ambao wanatoweka kwa

kasi sana. Wanyama kama Tembo, Furu, Twiga ambao ni vivutio vikubwa vya utalii wanatoweka kwa kasi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni budi Serikali kuimarisha Askari wa Wanyamapori kwa maslahi mazuri pamoja na mbinu na silaha bora za kisasa. Mimi naomba Askari hawa waangaliwe vizuri kwa sababu majukumu yao ya kazi za kila siku ni kama wako vitani mstari wa mbele, kwa hiyo wawezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na watu ambao hawalitakii mema Taifa letu na kufanya vitendo vya uhalifu kwa watalii kwa kupora mali zao wakiwa wazima ama kuwauwa. Vitendo hivi ya kinyama ni aibu kwa Taifa letu. Vitendo hivi vinasababisha watalii kuogopa kuja Tanzani kwa hofu ya usalama. Mimi nataka kujua Serikali ina mikakati gani ya kupambana na tabia hii ambayo inadhoofisha juhudi ya Serikali kutangazi utalii kwa nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia wanyama hatari kwa maisha ya watu, wanyama kama simba wamekuwa wakitoka katika maeneo ya hifadhi na kuingia katika maeneo ya makazi ya watu. Hivyo husababisha usumbufu na madhara makubwa na wakati mwingine watu wanauwawa na wanyama. Namwomba Waziri aangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia uharibifu wa mazao ya wakulima. Wanyama wanatoka ndani ya hifadhi na kuvamia mazao ya wakulima na kufanya uharibifu mkubwa. Mazao ya mkulima aliyoandaa mwaka mzima tembo wanavamia usiku

mmoja tu na kumaliza kila kitu. Mimi naiomba Serikali iangalie vizuri tatizo hili kwa maslahi ya pande zote na kwa maslahi ya Taifa.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kagasheki pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimwa Nyarandu, kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya katika Wizara hii nyeti. Namwomba Mwenyezi Mungu awalinde na kuwaepusha na balaa kwa wasiyowatakia mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea utalii, kama Serikali ingeweza kutoa fedha kwa wakati na kuiongezea bajeti Wizara hii iweze kujitangaza mfano kule katika Wilaya ya Ukerewe kuna jiwe ambalo likiamrishwa linacheza, uchezaji huo ni kukatika kwa amri ya kiongozi wa Wakerewe wa eneo husika. Hivyo ni muhimu sana kwa utalii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna eneo la Bujora kule Mwanza, pia kuna uwezekano mkubwa kama likitangazwa pia ni utalii wa kuingiza fedha. Huko Bujora kuna Wazungu ambao wanacheza ngoma za Kisukuma, hii ni raha iliyoje sasa tukatangaza maeneo haya, hata kidogo kidogo ili watalii waanze kuyazoea hata kuwahimiza Watanzania kufanya utalii wa ndani kwani utalii wa ndani huingiza fedha. Pia ni wajibu wa Wizara kuutangaza na kutangaza vivutio kwa utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata Wabunge kuna umuhimu wa kuhamasishwa wakafanya utalii wa

ndani. Kuna baadhi ya Wabunge humu ndani hata hawajawahi kufanya utalii huo na hata vivutio vya ndani hawavihamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kule Kigoma kuna jumba la makumbusho, lakini hali yake na hali ya Mwelezi wa watalii katika jumba hilo la makumbusho vimechoka kwa pamoja. Hivi sasa watalii ni wachache kutokana na uchakavu wa picha zilizomo ndani na hata Mwelezi aliyepo hana utaalam kama yule ambaye aliyekuwepo (marehemu). Hivyo ni vizuri kumfuatilia na kumwezesha kwa masomo ya kuweza kuwa Mwelezi hodari na aweze kujali kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na rehema zake nyingi kwangu. Ni wajibu wangu kusema *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu na nyeti sana kwa uhai wa Taifa letu, nasema kwa uhai wa Taifa letu kwa sababu maliasili inaenda sambamba na maisha ya wanadamu. Takribani maliasili zetu kama misitu, mito, maziwa, wanyamapori, milima na kadhalika huwa pia tunahatarisha maisha yetu sisi binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo Serikali iongeze juhudi ya kutoa elimu ya kutunza mazingira, kusema tu misitu ni mali haitoshi kwani watu wanaelewa kuwa misitu ni mali hivyo waikate ili wauze

mbao, kuni na mkaa ili wapate fedha. Inabidi waelimishwe misitu ni mali na ni sababu ya sisi binadamu kupata au kuweza kuishi. Misitu inatoa *oxygen*, hewa ambayo binadamu ndio aivuta ili aishi, kuikata misitu ni kusababisha *oxygen* itoweke na maisha ya binadamu hayatakuwepo pia. Kwa elimu hiyo watu ndio wataelewa maana na umuhimu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iwe macho na makini kwa wahujumu wa wanyamapori. Mimi inanipa wasiwasi tembo watatu (3) kuuwawa kila siku, si jambo rahisi bila ya kuwepo vigogo katika hujuma hizo. Watu wa kawaida hawawezi kufanya biashara hii, Serikali iseme neno na iwachukulie hatua wahujumu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuokoa misitu isikatwe lazima kuwe na nishati mbadala kwani wananchi wengi ni maskini. Serikali iboreshe sekta ya gesi na ipunguze kodi na kuondoa *VAT* kwa majiko ya gesi ili kuwawezesha wananchi walio wengi kumudu gharama. Kwa kufanya hivyo, kutapunguza sana uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni moja ya sekta muhimu sana ya kuliingizia Taifa mapato. Utalii wa ndani pia una umuhimu wake lakini tatizo ni gharama. Sehemu zenye vivutio vya utalii bado mazingira ya kufanya utalii wa ndani ni mgumu. Hoteli zilizoko ni za bei ya juu sana, kipato cha watu wetu ni duni sana, hivyo kuwe na uwekezaji wa wazawa kwa hoteli mahsusi za utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utalii wa nje, ni wakati sasa Serikali kuelekeza macho yake upande wa pili wa dunia. Tutangaze utalii katika nchi za Asia ya mbali na Mashariki ya Kati badala ya kuelekeza nguvu zetu Ulaya na Marekani tu. Takwimu zinaonyesha watalii kutoka Japan wamepungua kwa kasi ya kushangaza kwa miaka kumi mfululizo iliyopita. Serikali ina majibu ya sababu za kupungua sana watalii kutoka Japan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asali ni chakula na ni dawa na ni mali. Serikali ikae mbele kuitangaza asali yetu na ubora wake ili masoko ya asali yaimarike. Nchi nyingi wanahitaji asali yetu lakini wanaiogopa, wana hofu na asali yetu kwa sababu eti ina *nicotin* na bacteria wengine. Serikali itoe majibu ya kisayansi ili asali yetu iuzike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuwasilisha.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja ya nchi ambayo ina vivutio vingi vya utalii, vivutio ambavyo vingalichangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa, cha kusikitisha sekta hii haijapewa haki stahili, jambo ambalo linatumiwa na wenzetu wa nchi jirani kama Kenya juu ya namna wanavyoutangaza mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii Tanzania tumebarikiwa kuwa na sehemu za kumbukumbu (makumbusho), mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama mfano Serengeti, Ngorongoro, Manyara na Mikumi sehemu ambazo ni vivutio vikubwa vya utalii,

tutumie fursa hii kuitangaza Tanzania kwa lengo na madhumuni ya kuipatia Tanzania na Watanzania maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna mito, maziwa, bahari na fukwe ambavyo vyote ni vivutio vya utalii. Katika hili kumekuwa na wizi unaofanyika wa uibaji rasilimali za bahari yetu yakiwemo matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki lakini pia ni mambo ambayo yanatumiwa kwa mapambo katika maeneo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha mbuga za wanyama, Tanzania ina misitu ya kutosha ambayo inazalisha mbao za aina mbalimbali na mbao nyingine au miti mingine ya misitu inatumiwa katika uundani wa vinyago tofauti ambavyo vinatoa historia halisi ya nchi kwa ustawi na ufahamu wa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijani kibichi kinachopamba Tanzania ambacho kinaondoa ukame ambao unatawala nchi nyingine lakini vilevile ni vyema Serikali ikatilia maanani utunzaji na uhifadhi wa maeneo ya historia mfano majengo ya historia ya Bagamoyo na maeneo mengine. Ni ukweli usiopingika kwamba leo Historia ya Mkwawa, Kinjekitile Ngwale na marehemu Sewa Haji, leo hawatajwi tena kwamba wametoa mchango mkubwa katika Taifa hili.

**MHE. ABDULASALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Awali ya yote nawapongeza sana kwa kuteuliwa kwenye Wizara hiyo na nakumbuka kauli Waziri aliyotoa wakati alipopewa

ofisi, alisema, nanukuu, “kabla mimi sijanyongwa, nahakikisha kwanza nawanyonga nyie”. Mwiso wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio changu mimi ni katika maeneo matatu. Kwanza ni mpaka wa hifadhi ya Mikumi na vijiji vya Mikumi, Luwange, Ruhembe, Kihelelo na Kitele. Mwaka 1975 tarehe 13 Juni Bunge ililipitisha na kuidhinisha mipaka kwa kupitia GN. Na.121. Baada ya kutoa hiyo GN.Na.121 na ramani ikachorwa kuonyesha kwamba mipaka hiyo kwa ridhaa ya wanakijiji husika na hifadhi ya Mikumi kupitia Wizara hii. Ramani hiyo yenye namba 16778 imeaninisha sehemu yote kwa kuweka alama nyekundu kuonyesha huo mpaka, kuna mawe (*beacons*), makorongo, milima, misitu na mito na inaelekeza waanze kupima kuanzia jiwe la alama ya barabarani njia ya Morogoro kuelekea Mashariki Km 115.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miaka 35 ndio wamekuja kuainisha mipaka hiyo tarehe 10/6/2010 wakiongozana na wapimaji toka Wizarani bila ya kuwashirikisha wanavijiji husika. Baada ya malumbano na wanakijiji ndio walikubali kushirikiana nao, Viongozi wa vijiji walihoji ramani namba 16778 ipo wapi ili waweze kufuata hiyo ramani kwa bahati mbaya hawakuja nayo hiyo ramani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea viongozi wa *TANAPA* waliweka alama ya mipaka kama walivyotaka wao bila ya kufuata hivyo ramani ambayo Serikali na wanavijiji waliridhia na kama *GN* inavyoagiza. Hiyo

mipaka waliojiwekea *TANAPA* ndio chanzo cha mzozo wa mipaka katika vijiji hivyo. Mheshimwa Waziri ni matumaini yangu kuwa utafuatilia na kuweza kuweka mambo sawa ili kuondoa adhaa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya tembo kuvamia mashamba ya wananchi waliopakana na hifadhi. Juzi katika kijiji cha Ihombwe kundi la tembo lilivamia kijiji na kumaliza mazao na kuwaweka wanakijiji katika hofu. Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Maliasili Wilaya ya Kilosa hawana silaha kwani ziliibiwa. Afisa Tarafa hakuna na wa Kata pia, naomba Wizara iweze kuwaajiri Afisa Maliasili kwa kila Kata iliyo karibia na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wameathiri mazao ya chakula na biashara, mazao ya biashara kama miwa ndio zao la biashara kuu katika bonde la Ruhembe, kila msimu wa mvua ni lazima tembo wale mazao yao. Kwa bahati mbaya wanang'oa kabisa miwa na kuacha mashamba bila hata chembe ya miwa. Mheshimwa Waziri nakuomba sana utuokoe wana Mikumi na balaa hilo la uvamizi wa tembo na kutuacha tukiwa maskini.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ili kurekebisha matatizo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani, napenda kuishauri Wizara hii kujielekeza katika maeneo mapya

kwa utalii wa aina mbalimbali kwa mfano hapa nchini tuna milima yenye mvuto kama milima ya Uluguru, safu za milima ya Livingstone inayoanzia Wilayani Makete kuelekea Rungwe, Kyela, Ludewa, Mbinga hadi Nyasa kandokando mwa Ziwa Nyasa. Nashauri Wizara kupitia sera yake ya utangazaji na itangaze milima hii. Mpango huu uende sambamba na uhifadhi wa milima hiyo kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika. Vilevile sambamba na safu hizi, maua mazuri yanayopatikana katika hifadhi ya Kitulo yanafaa sana kutangazwa kwa nguvu kubwa. Kusini pia (Rungwe) kuna vivutio vingine kama maporomoko ya maji na maajabu mengine ambayo yana mvuto mkubwa kwa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vivutio hivyo, pia mbuga ya wanyama ya Ruaha inastahili sasa kupewa nafasi kubwa, ni kwa njia ya kuwa na usafiri wa uhakika kama usafiri wa ndege. Mbuga hii itachangia uchumi wetu kwa nguvu kubwa. Hivyo nashauri kwamba Wizara hii ifanye kazi kwa karibu sana na Wizara ya uchukuzi kuhakikisha kuwa uwanja wa ndege wa Songwe Mbeya unakamilika haraka ili utalii uanze kuchukua nafasi nzuri hasa kwa watalii kutoka nchi za kusini mwa Afrika kama South Afrika, Zambia, Namibia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa misitu, karibu misitu yote kwenye *Public Land* imeteketea kwa sababu ya uvunaji ovyo wa misitu hiyo. Uvunaji huo hauna usimamizi wowote na hakuna usimamizi wa sheria zilizowekwa. Misitu iliyobaki ni misitu iliyo chini ya hifadhi tu. Huko nako watu wameanza kuingia kukata

mbao na magogo. Ili kurekebisha hali hiyo, nashauri yafuatayo:-

(i) Maafisa Misitu walio chini ya Halmashauri za Wilaya wawajibike chini ya Wizara husika ili kuleta uwajibikaji kwa karibu.

(ii) Suala la upandaji miti na kuitunza liwe chini ya dhana ya ushirikishwaji wa wananchi na kuisimamia.

(iii) Suala la elimu ya mazingira liendelezwe kwa nguvu kwa kuhusisha pia Taasisi zisizo za Kiserikali.

(iv) *Forest Ranger* ni watu muhimu sana katika ulinzi wa misitu ambayo imebaki katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro katika hifadhi zetu na wananchi wa vijiji vinavyopakana na hifadhi hizo. Naomba Serikali ichukue hatua za makusudi katika kuhakikisha kunakuwa na mahusiano mazuri kati ya hifadhi zetu na wananchi wanaopakana na hifadhi hizi. Ni ukweli usiopingika kuwa wananchi wanapaswa kulinda hifadhi hizo maana ni mali yao (rasilimali yao), ni vyema mamlaka husika kukaa pamoja na wananchi wanaopakana nao ili kwa pamoja kukubaliana katika mambo ya msingi kwa mustakabali wa nchi yetu na

rasilimali zake kwa mfano *TANAPA*, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na vijiji vinavyopakana navyo vya Lositeti, Kitete, Kambi ya Simba, Rhotia, Ayalake, Endamaghang na kadhalika. Hali ya kutoelewana kati ya Askari wa Mamlaka *TANAPA* na wananchi inapaswa kuangaliwa kwa upya. Maridhiano yafanyike pasipo kutumia nguvu tu, ni imani yangu kuwa kwa pamoja tutalinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kufikiria tena kuhusu Sheria ya Fidia kwa uharibifu wa wanyama kwa mali za wananchi. Hainiingii akilini kwamba wanyama waharibifu wa mazao ya mtu, shamba zima halafu apewa fidia ya shilingi laki tano tu (500,000) au hata mtu kufa halafu kifuta machozi shilingi millioni moja tu (1,000,000). Sheria iangalie uhalisia wa uharibifu na hata kuhusu maisha ya mtu. Si sawa kabisa kwa mtu kuuwawa na kufidiwa shilingi millioni moja au laki tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uuzaji wa wanyama nje ya nchi, naishauri Serikali iangalie kwa upya juu ya usafirishaji wa wanyama nje ya nchi. Hivi baada ya kuuza/kusafirisha wanyama nje ya nchi tutegemee nini kuhusu utalii? Hii ni nchi ya ajabu duniani kwamba wanyama wake husafirishwa kinyemela huku tukidai kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMA* kote nchini zilindwe na kuimarishwa mfano Serikali iangalie kwa upya sera ya *WMA,* iwape mamlaka tosha na waachiwe mapato yote yatokanayo na *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie maziwa yetu mfano Ziwa Manyara linakauka na ndege aina ya Flamingo wanahama au kufa. Ziwa hilo linapaswa kuondolewa udongo na kufanyiwa kazi, hifadhi ya mipaka yake na kingo zake zitunzwe.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo matatu makuu. Kwanza kabisa ni kusikitishwa na shughuli za uchimbaji wa madini katika mbuga zetu. Nashukuru kwa kauli ya Naibu Waziri kukema kabisa uchimbaji huu wa madini. Lakini leo katika hili la uchimbaji wa madini napenda kongelea wale Maafisa wa Jeshi la Polisi waliokamatwa na wananchi wengine watano wakichimba dhahabu kinyume cha sheria ili hali wao wanatakiwa kulinda rasilimali zetu tena ndio wanakuwa mstari wa mbele kuhujumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza na kusikitisha na hili nililizungumzia kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, siku hiyo *OCD* wa Mgumu, Paulo Mung'ong'o, Afisa Usalama wa Taifa Mussa na dereva wa Polisi walikamatwa na raia wengine watano na Askari wa *TANAPA,* cha ajabu saa nane usiku Maafisa hawa waliachiwa. Cha kushangaza, hivi Serikali inafanya kazi hadi usiku kutoa dhamana? Au kuna makosa ya jinai ambapo wanyonge wanashtakiwa kwa kufuata sheria halali na Maafisa au wenye fedha zao wanakuwa *treated* tofauti? Naomba kupewa majibu kwenye haya kwamba kwa nini hawa Maafisa wao hamkuwashtaki kama wale wenzao ambao ni raia wa kawaida? Badala yake wanapewa

tuzo za kuhamishiwa Musoma mjini, Ofisi ya *RCO* -Mara na dereva kunyang'anywa gari, *that is all*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kujua juu ya wale raia watano wa kijiji cha Gibaso ambao tarehe 30/10/2012 walipotea wakiwa wanachunga mifugo yao kandokando ya hifadhi ya Serengeti ambapo walikuwa kumi, wenzao walikimbia lakini kulisikika milio ya risasi ambapo ilipigwa na Askari wa *TANAPA* na wale manusura walikuwa tayari kuwatambua wale Maaskari. Hili swali nilishawahi kuliuliza humu ndani na Mheshimiwa Maige akaahidi kushirikisha mamlaka husika ambayo ni Jeshi la Polisi (Mambo ya Ndani ya Nchi) ambayo kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Kagasheki ndiye alikuwa Naibu Waziri na hili suala analijua. Hivyo wazazi ndugu wa jamaa wale wanataka kujua hatua ya hawa ndugu zao kwani magereza yote hawapo. Kama walikufa waseme ili maziko ya kimila yafanyike kuliko hivi sasa kuwa kwenye *dilemma*. Huu umekuwa ni mlolongo wa mauaji ya raia wetu ambao ni nguvu kazi huku wakinyang'anywa mifugo huku wauaji wanaopiga raia risasi wanabaki wakitamba, hii si haki kabisa. Naomba haya yachunguzwe na kukemea, inabidi wakae kifamilia na jamii zile husika, wasifanya tujutie kuwa na mbuga kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* nyingine ni ambayo imekuwa ni ugonjwa mkubwa sana yaani ni kuhusiana na ujangili unaofanywa na watu wazito wenye fedha zao huku wakishirikiana na Maafisa wasio waaminifu lakini cha ajabu watu hawa wanaachiwa wakitamba

licha ya kubainishwa na *TANAPA*. Naungana kabisa na maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Bryson na wenzake na cha ajabu wanaishia kuwabambika kesi wananchi maskini tena ambao hawamiliki hata hizo bunduki za *riffle*, wanawapiga, wanawauwa, wanatiwa vilema na Polisi. Tunaomba uzalendo ndani ya Wizara ili wananchi hawa wazawa waishi kama wananchi wenzao ndani ya nchi yao, hii si haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *concession fee*, hili suala linaitia nchi hasara kwani mara baada ya kuamua kutenguliwa kwa ulipaji wa hii ada uliokuwepo kwa mapendekezo ya Kamati ya Mashirika ya Umma. Hawa watu wakafungua kesi Mahakamani na hii kesi imekuwa ikicheleweshwa bila kujali upotevu na mapato kwani *TANAPA* wanakosa mapato mengi sana juu ya hili. Mwaka huu tulitembelea Afrika ya Kusini, wenzetu yaani SANPARKS wanapata takribani asilimia 80 ya mapato yao kutokana na malazi (*accommodation facilities*) kwenye hifadhi zao lakini sisi Tanzania *TANAPA* inapata asilimia 20 tu. Hii ni fedheha, hivyo Serikali lazima izingatie hili suala la c*oncession fee* ni muhimu sana.

**MHE. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupongeza uwasilishaji mzuri sana wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikumbushe Wizara ya Maliasili kukaa meza moja na Wanarufiji katika kuondoa matatizo na changamoto ya mipaka ya *Selous* ambayo imekuwa ikipigwa tarehe kila mara na matokeo ya hatua zisizosahihi na kinyume cha Katiba kwa baadhi ya Askari wa Maliasili kwa

wavuvi wanaoingia *Selous* kama wezi wa samaki katika mabwawa ambayo mengine yapo ndani ya eneo la vijiji kwa mujibu wa ramani za miaka ya 1950s au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maelewano kati ya Hifadhi hii ya *Selous* na Wanarufiji ni kutoa kipaumbele kwa Wanarufiji wanaozunguka eneo hilo, kutoa nafasi za kazi kwa Warufiji hao ambao ni lazima wawe wanufaika wa kwanza wa hifadhi hii ya Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuondoa vizuizi vya kutakiwa kulipa ada ya kuingia kwenye hifadhi kwa kusudio la kufanya kazi kwenye mahoteli yaliyomo humo. Kama ada hizo wanatozwa hao vibarua na wafanyakazi wa hoteli hizo basi ni lazima wafanyakazi wa maliasili waliomo humo wawe wanalipa hizo kodi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhakikisha kazi zote za msingi na za awali zinafanywa na Watanzania wanaoishi katika maeneo hayo na kuharakisha na kukamilisha *WMA* ya Kata ya Ngorongo, Kipugira, Mwaseni na Utete ambayo toka nimeingia kwenye Bunge hili maelezo ninayopata ni kwamba mchakato unaendelea, hadi lini? Naomba maeleo ya hadi lini Jumuiya hii ya uhifadhi itaanza huko Rufiji hasa hasa Kata hizo za Mwaseni – Ngorongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri kuwapo utaratibu wa kutembelea maeneo mengine ya kivutio cha utalii kama kilichopo Kata ya Mbwara, kijiji cha Tawi ambako kuna majengo ya asili mithili ya mihimili iliyosimamishwa kwa madhumuni fulani.

Naomba timu ya wataalamu wafuatilie eneo hilo na ushauri stahili utolewe kabla ya kuruhusu mtu binafsi kuchukua eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naamini Serikali itafuatilia utekeleji wa *WMAs* za Rufiji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Naibu Waziri aweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, karibu!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema pamoja na kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu muhimu wa Bunge unaojadili bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya M. Kikwete kwa kuniamini na kuniteua tena safari hii kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kufanya kazi kwa bidii na kwa kushirikiana chini ya uongozi wa Waziri wangu, Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kaghasheki na vilevile tutashirikiana kwa karibu na wenzetu katika Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu na watumishi wenzetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile natoa shukrani za dhati na niseme tena kipekee kwa uongozi thabiti na

maelekezo thabiti anayoyatoa Mheshimiwa Waziri wangu Khamis Sued Kaghasheki. Ninaomba nimuahidi kuwa nitaendelea kumpa ushirikiano katika kuhakikisha kuwa Wizara hii inaendeshwa kwa ufanisi hususani kuwezesha uhifadhi na matumizi endelevu ya raslimali za maliasili na malikale pamoja uendeshaji wa utalii nchini unakuwa na manufaa na tija kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba kwa unyenyekevu mkubwa niwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Singida Kaskazini. Hawa wamekuwa pamoja nami kuanzia mwaka 2000, mwaka 2005, mwaka 2010 na ninaomba tena niwaahidi kuendelea kuwa mtumishi mwaminifu katika Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa, naungana na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa wananchi kutokana na ajali ya basi la Sabena. Aidha, natoa pole kwa Serikali na wananchi wa Kenya kwa ajali hiyo iliyotokea Wami, Mkoani Pwani ambako wenzetu 11 kutoka Kenya walipoteza maisha yao na wengine kujeruhiwa vibaya. Nawatakia ahueni wale wote waliojeruhiwa na wale waliopoteza maisha namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita katika hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na masuala ya utalii, mambo ya kale na mambo mtambuka wakati Mheshimiwa Waziri ataendelea moja kwa moja na Idara yote ya Wanyamapori na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hoja za Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwamba hali ya ukuaji wa biashara ya utalii nchini hairidhishi na Wizara yangu imeazimia kufanya mageuzi makubwa ili tuweze kuongeza kasi ya mafanikio yaliyopatikana hadi sasa na kuhakikisha fursa hizo zinawanufaisha wananchi na wadau katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyochangia Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa Abuu Hamoud Juma pamoja na Waheshimiwa wengine wengi sana ambao Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kuwataja, nchi yetu inapata watalii wachache ikilinganishwa na fursa tulizonazo. Mwaka jana kama tulivyosema awali, watalii 757,000 walitembelea nchi ya Tanzania Bara, watalii 110,000 walitembelea Tanzania Zanzibar na inafanya jumla ya watalii waliotembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia 867,000. Kati ya watalii hao 642,000 walitembelea Bara pekee na watalii 52,000 walitembelea Zanzibar pekee. Kwa maneno mengine hawakwenda upande wa Bara. Watalii 104,000 walitembelea pande zote Bara na Zanzibar. Hii inaonesha jinsi utalii wa Bara na Zanzibari unavyotegemeana kwa kiasi kikubwa na hivyo juhudi za pamoja kati ya Wizara yangu na Wizara ya Utalii Zanzibar zitapaswa kuongezeka zaidi ili tuhakikishe kwamba ongezeko la watalii wanaotembelea sehemu zote mbili za Muungano linaongezeka na litachangia sana suala zima la ongezeko la watalii katika pande zetu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ndogo ya uwekezaji katika hoteli na *lodge* za kitalii nchini, inachangia kupunguza kasi ya ongezeko la watalii nchini na kupunguza kabisa ushindani utokanao na kuwa na hoteli za kitalii katika maeneo ya miji, fukwe na hifadhi zetu za taifa. Takwimu za kufikia mwaka juzi 2010 zinaonesha kuwa Tanzania ilikuwa na jumla ya vyumba vya kulala wageni hotelini vyenye daraja la A, B na C kufikia vyumba 11,568 kwa nchi nzima. Wakati mji wa Mombasa na Pwani ile ya upande wa Kenya pekee ina vitanda *(bed capacity)* 28,743.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wetu wa Dar es Salaam hadi kufikia sasa hivi unakadiriwa kuwa na hoteli 174 zenye vyumba 3,609 kwa hayo madaraja niliyoyasema ya A,B,C na D. Hauwezi kabisa ukalinganisha na mji wa Nairobi ambao una hoteli za *standard* hiyo 433 zenye jumla ya vitanda 15,684 idadi ambayo bado ni kubwa kuliko uwezo wa vitanda vyote vya hadhi hiyo hiyo katika Tanzania Bara. Inakadiriwa kuwa Masai Mara upande wa Kenya ambayo ni theluthi moja ($^1/_3$) ya hifadhi yetu ya Taifa ya Serengeti, wana vitanda zaidi ya 11,000 wakati hifadhi yetu ya Serengeti ina vitanda vinavyokadiriwa kuwa 1,500. Tofauti hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uwezo wetu wa kupokea wageni wengi bado pia ni ndogo katika miji na maeneo mengine nchini. Nitoe mfano tu wa Mkoa wa Arusha ambao hadi sasa una hoteli 91 na una vyumba 2,800. Mkoa wetu wa Kilimanjaro una hoteli za

kiwango hicho 38 na vyumba 914. Mkoa wetu wa Mwanza hoteli za kiwango hicho ziko tisa (9) lakini zina vyumba 914. Mkoa wetu wa Mbeya umefikia hoteli 64 na umefikisha vyumba vya hadhi hiyo 180. Nimalizie kwa Mkoa wa Mara ambao sasa una hoteli za kiwango hicho 23 na vyumba 477.

Mheshimiwa Mwenyekiti, WIzara yangu inatarajia idadi ya watalii wanaoingia nchini kufikia milioni moja (1,000,000) muda siyo mrefu kuanzia sasa hivi na tunaamini kuanzia mwaka 2015 nchi yetu itakuwa imeanza safari ya kuelekea kupata watalii milioni mbili (2,000,000) ambalo ndiyo lengo kubwa la Serikali kwa mwaka. Ili kutimiza azma hii na kwa kuzingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii, Wizara itasisitiza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuanzia sasa taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zinazohusika na usimamizi wa hifadhi za taifa, hifadhi za Ngorongoro na Hifadhi za Mapori ya Akiba, zitapaswa kuondoa ukiritimba, ucheleweshaji wa makusudi na vitendo vinavyofanywa na watumishi ama Bodi zinazosimamia maeneo haya vya kutotoa leseni za uwekezaji wa hoteli, *lodge* ama *tented camps* katika maeneo ambayo tayari tuna *general management plan.* Hii ni *plan* ambayo inaruhusu kitaalam maeneo yapi ni endelevu na yanaweza yakawekewa uwekezaji wa aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itatusaidia kuongeza idadi ya vitanda na hivyo kusaidia juhudi za

Bodi ya Utalii nchini kuweza kuendelea kutangaza utalii wetu. Sasa hivi tuna tatizo ambapo kuanzia mwezi wa tano, sita, saba, nane na tisa, miezi yote ambayo ni *high season* ukitaka kwenda ghafla Serengeti haupati vyumba. Wenye *tour operators* hapa nchini wengine wamelalamika kwamba wanapotaka kupeleka wageni wao kunakuwa na *block bookings*, hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itahakikisha kwamba wawekezaji wa ndani wenye uwezo wanapewa vipaumbele vya kuwekeza katika hifadhi zetu ili kuwajengea wananchi uwezo zaidi wa kiuchumi, kulinda ajira za ndani na kusaidia fedha za kigeni kubaki ndani ya nchi yetu. Hii itahusu pia mkakati wa makusudi wa kuwajengea uwezo na kuweka mazingira mazuri kwa *tour operators* wa ndani ya Tanzania ili waweze kumudu ushindani na waweze kuwa tayari kwenda katika masoko ya Afrika Mashariki hususan nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge wengi sana ambao baadaye Mheshimiwa Waziri atawataja, Wizara itahakikisha kuwa Bodi ya Utalii Tanzania inaongezewa uwezo wa kibajeti na kimuundo ili iweze kuhimili majukumu yake na kumudu ushindani mkali unaotoka hasa kwa jirani zetu Kenya kwa sababu kama alivyosema mchangiaji mmoja kitu ambacho Tanzania inakiuza, *products* za Tanzania na Kenya zinafanana sana, ushindani ni mkubwa sana. Ikumbukwe kwamba mwaka jana 2011 Bodi ya Utalii ya Kenya kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge ilikuwa na bajeti ya dola za

Kimarekani milioni 16 tukilinganisha na za kwetu milioni mbili (2). Uwiano huu hauwezi kuvumiliwa kama tunataka tushindane na ndugu zetu wa Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba nchi ndogo inayojulikana kama visiwa vya Shelisheli yenye ukumbwa wa kilomita za mraba 445 tu na ukilinganisha na mbuga yetu kama ya Selous ambayo ina ukubwa wa karibu mara mbili ya nchi ya Switzerland na ina ukubwa wa zaidi ya baadhi ya nchi nyingi hapa duniani, ndugu zetu wa Shelisheli walitumia bajeti karibu sawa na ya Tanzania kutangaza utalii wao. Ni lazima sisi kama nchi tubadilike, tuwe tayari kushiriki katika mabadiliko haya na tutasisitiza kuwa sekta binafsi wabadilike, sekta ya umma wabadilike na hii itatusaidia sana kuunganisha wadau wote ili tuweze kuendeleza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendeleza juhudi za kutangaza utalii wa ndani kote nchini. Kama walivyochangia Wabunge wengi kuhusiana na umuhimu huu wa utalii wa ndani, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi na tunasisitiza wananchi kote nchini watumie muda wao na vipato vyao vya ziada kujenga utamaduni wa kutembelea hifadhi zetu na maeneo mbalimbali ya kitalii kama sehemu ya kuimarisha utalii wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendeleza utalii wa mijini hususan katika jiji letu la Dar es Salaam. Fursa zilizopo katika jiji letu la Dar es Salaam ni nyingi sana kwa utalii wa mijini na hii itakuwa ni kuimarisha sehemu

zote zenye mambo ya kale, makumbusho ya taifa, maeneo ambayo tungependa watalii wa kutoka nje na wenyeji waweze kuyatembelea. Katika kuimarisha huu utalii wa ndani na mikakati hii, tunaanza upya kuiweka ikiwa ni pamoja na kuweka sera zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasisitiza vilevile utalii katika mji wa Mwanza. Hoja ya uwanja wa ndege wa Mwanza kuitwa *Serengeti International Airport* kama alivyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe ilitolewa kwanza na Kamati ya Uongozi inayojulikana kama *Mwanza Tourism Association* katika kikao chao cha pamoja na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na walileta taarifa yao hiyo wakati wa ziara yangu ya Mwanza wiki mbili zilizopita. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Zitto na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote tufungue mjadala huu, tuipe nafasi Mwanza iweze kunyanyua utalii katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Wizara tunaamini mji wa Mwanza una fursa kubwa kwa idadi ya watu, una fursa kubwa ya kushindana na miji kama Kigali, Bujumbura na ni mji pekee ambao ni mkubwa kuliko miji mingine yote katika eneo la Maziwa Makuu katika Afrika Mashariki. Tunaamini mji wa Mwanza kama juhudi ambazo zimeanzwa na Wizara zikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Kagasheki za kuhakikisha kwamba tunavutia mashirika ya ndege makubwa duniani kuendelea kuja Tanzania, tutasisitiza kwamba mchakato wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwanza utakapokamilika basi ndege zitoke zinakotoka zije moja kwa moja katika jiji letu la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itashirikiana na wadau kuimarisha Maonesho ya Utalii ya Karibu kama walivyozungumzia baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. *Karibu Fair* ni maonesho ambayo yana uwezo wa kuweza kushikilia hadhi ya utalii wa Tanzania. Ni matumaini yetu kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Arusha itashirikiana kutenga ardhi ya maonesho haya na taasisi zetu zingine chini ya Wizara zitapaswa kushiriki kuimarisha maonesho haya na kuhakikisha kwamba hili jambo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda wangu haujaisha, naomba nirejee tena kusema kwamba tunaazimia kuendelea kuwavutia, kuendelea kuzungumza na mashirika yote makubwa ya ndege duniani, kama mnavyokumbuka Mheshimiwa Waziri alishirikiana na Waziri wa Uchukuzi walipoenda kuzindua hivi karibuni *arrival* ya ndege ya Qatar katika uwanja wetu wa kimataifa wa Kilimanjaro. Ni matumaini yetu kwamba tutaendeleza mazungumzo na mashirika makubwa yote duniani likiwemo la *United Airlines* la Marekani, Virgin Atlantic na mashirika mengine ili waweze kuongeza *frequencies* wanazokuja katika uwanja wetu wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie. Sitaweza kumalizia kama sitataja mjusi maarufu sana *Dinosaur* aliyechukuliwa na wakoloni wa Ujerumani miaka ya 1900 akapelekwa katika iliyokuwa Berlin ya Mashariki. Mjusi huyu kwa taarifa tulizonazo anaingiza dola za Marekani bilioni tatu (3) katika Ujerumani kwa mwaka. Mazungumzo yanaendelea na ninaomba

nilihakikishie Bunge hili kwamba Wizara yangu itaendelea kufanya mazungumzo ili tujue sera na mtazamo wetu kama Taifa tutakavyoamua kuzungumza na Wajerumani. Kuna *options* kadhaa ziko mezani, tunamwomba Mjusi wetu arudi tumweke Lindi, tunaomba mjusi huyu tugawane mapato kwa asilimia fulani na abaki pale pale Berlin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukuhakikishia wewe na Bunge lako ni kwamba Wizara yangu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Kagasheki, tutafanya mazungumzo ya ndani, tutawashirikisha wadau, tukubaliane sisi tunataka ombi letu liwe nini na tutaliweka wazi katika Bunge hili tuhakikishe kwamba jambo hilo linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijagongewa kengele ya mwisho, naomba tena nirejee kukushukuru wewe, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Kagasheki, kumhakikishia tu kwamba mimi kama mdogo wake, mimi kama Naibu wake, tutafanya kazi vizuri. Nitafanya kazi asubuhi, atanituma usiku wa manane, tutafanya kazi kwa ushirikiano na nina imani kubwa na timu iliyoko katika Wizara yetu kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote ambao tunafanya nao kazi. Ninaomba Mungu atupe wepesi, atubariki tuweze kushiriki katika kuongeza utalii wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, waliosema hamuelewani leo wameaibika. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kutupongeza, yaani kunipongeza mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, lakini pia kumpongeza Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Nyarandu, lakini pia hapohapo mkampongeza Katibu Mkuu wa Wizara na watumishi wote katika kutekeleza majukumu yetu ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli kwa kuchangia hoja na kutoa maoni ambayo wameitaka Wizara iyafanyie kazi. Lakini pia naomba niseme kwamba tumeisikiliza kwa makini hotuba iliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani na tumeyasikia maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuingia katika shughuli za mjadala huu tuliokuwa nao ambao unahusu Wizara yangu na makadirio ambayo tumeyaweka katika Bunge lako Tukufu, kwa taarifa nilizozipata kutoka jimboni kwangu, kumetokea misiba miwili ya watu ambao wamekuwa ni mashuhuri katika Chama cha Mapinduzi, wa kwanza akiwa ni Bi. Zulfa ambaye mchango wake umekuwa ni mkubwa. Maziko yake yalikuwa jana, kwa hiyo, nawapa pole Wanajimbo wote kwa msiba huu ambao

watakubaliana na mimi ni mkubwa sana. Lakini pia yuko mama ambaye alikuwa Mwenyekiti wa UWT katika Wilaya yetu ya Bukoba Mjini, Mama Anastazia. Yeye pia amezikwa jana, kwa hiyo, niko nao katika msiba huo mkubwa na mara Bunge litakapokwisha tutakuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue Wabunge ambao wamechangia katika mjadala huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliochangia kwa kuongea humu ndani ya Bunge ni Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa, Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Esther L. Midimu, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, Mheshimiwa Beatrice M. Shelukindo, Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu, Mheshimiwa Maryam S. Msabaha, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa na Mheshimiwa Felix F. Mkosamali. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ally, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa John Paul

Lwanji, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Cythia Hilda Ngoye na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni kama hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Lucy Nkya, Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mheshimiwa Ismail Aden Rage na Mheshimiwa Godfrey Zambi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Hamoud Abuu Juma, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Rebecca

Mngodo, Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Amos Makalla. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Terezya Huvisa, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Waride Jabu, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga, Mheshimiwa Haroub Shamis, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Abdulsalaam Amer, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Seif Rashid. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Charles

Mwijage, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Ally Khamis Seif, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Rajab Mohammed, Mheshimiwa Prof. Kahigi, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Stephen Wassira, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Assumpter Mshama na Mheshimiwa Clara Mwatuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii sasa kuanza kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na hotuba ambayo imetolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwa kweli niseme tu kwamba tumeyasikia lakini baadaye tumeyasoma yaliyoandikwa katika hotuba hii, niseme kwamba hatutoingia sana katika mjadala wa hotuba hii kwa sababu za msingi. Yapo maeneo ambayo mmetaja, lakini ukizingatia kwamba kuna maeneo mengi ambayo naweza kusema kwamba hayana usahihi wowote. Mathalani naweza kuanza na mimi mwenyewe katika kitabu cha hotuba ya Waheshimiwa Kambi Rasmi ya Upinzani wananitaja

kwa jina kwamba faru walipopokelewa nilikuwepo katika Uwanja wa Kilimanjaro *International Airport*. Jambo ambalo sio sahihi maana yake mimi sikuwepo kabisa na hata wangetazama katika rekodi zote. Sasa wanaposema kwamba nilikuwepo wakati faru wanafika na kwamba nilishiriki katika mapokezi mimi nasema huu kwa kweli ni upotoshi ambao kwa kweli hauna sababu. Ni vizuri wakati tunaandika mambo tuyafanyie kazi na tuwe na hakika ni kitu gani tunachoandika. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kusema kwamba faru walipofika mimi mwenyewe sikuwepo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, inasemekana kwamba nilitamka kwamba majangili katika eneo la ujangili kwamba majangili hawa wana mtandao mkubwa na kwamba wana fedha nyingi. Hilo halina shaka ni ukweli, lakini haina maana ya kusema kwamba Serikali imeelemewa au imeshindwa *hasha wakala*, jitihada zinafanyika, wale ambao wana macho wanaona na jitihada ni kubwa sana na matokeo yapo bayana. Sasa kuna watu nafikiri kuna watu ukweli hataki kuutazama ama kuu-*face* basi huna utakachoweza kufanya. Lakini kwamba mitandao ni mikubwa, Waheshimiwa Wabunge ninyi wenyewe ni watu mmesoma, mnasafiri, ni watu waelewa. Niwape mfano, Colombia kumekuwa na matatizo ya *drives cater*. Wale watu wana mitandao yao mikubwa na mpaka Serikali ya Colombia ikakubali kabisa kwamba ndani ya ile *cattery* zile za ma-*drug balloons* ilikuwa ni Serikali ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusiende mbali, Mexico hapa yako maeneo ambayo wanakiri kabisa kwamba mitandao ni mikubwa. Kitu ambacho tunafanya hapa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ni kukiri kwamba tatizo lipo. Ubaya ni kukataa ukasema kwamba tatizo halipo. Tatizo lipo na ni ukweli kwamba mtandao wao ni mkubwa na ndiyo maana unaona kwamba wanayafanya wanayoyafanya, lakini pia ni mitandao kutoka huko nje inakuja mpaka ndani. Lakini haina maana kama inavyoelezwa hapa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kutuhumu kusema kwamba Serikali ya CCM pia inajishirikisha katika habari hii ya ujangili, sasa hii hotuba imetolewa na mtu ambaye kwa kweli nilitegemea mbali na kwamba ni mwanasiasa kwa nafasi yake kama Mbunge, lakini hapa tunazungumzia Mchungaji. Waheshimiwa Wabunge, Mchungaji ni mtu ambaye kwa nafasi yake, kwa shughuli zake ndani ya jamii, ni mtu wa kusema ukweli, lakini mtu wa kukemea, lakini sasa Mchungaji mwenyewe kama ndio anayekuwa anaendeleza habari ambazo hazina usahihi na wala hazina uhakika basi hii ni hatari kubwa. Lakini niseme kwamba kwa kuwa Mchungaji amepotosha na hii nimezungumzia katika habari hii bila hata kwenda katika habari nyingine ambayo nitaisoma katika kitabu chake haina maana kusema kwa kuwa Mchungaji mmoja amepotosha basi Wachungaji wote watakuwa ni watu wa kupotosha, sio sahihi. Hii ndiyo dhana ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi, jana alikuwa anaizungumzia. Unaweza

ukamzungumzia mtu binafsi na ukamchukulia mtu kwa makosa yake kama yeye, lakini unapomchukulia yule mtu kama yeye amefanya makosa ukasema basi ni chama kizima, ni Serikali nzima, nafikiri huo ni upotoshaji ambao kwa kweli hauna sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutuhumu Serikali na Chama na akamtaja mtu ambaye akasema ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwamba yeye ndiye mhimili mkubwa wa ujangili kwa kweli na habari ikawa ni ya uhakika kwamba hii ni huzushi na si ukweli na labda unazungumzia mtu mwingine. Lakini pia unapomtaja mtu kisheria basi taja jina lake kamili kwa sababu unapotaja tu ukasema fulani, sasa ile la Lazaro hatuwezi kujua ni jina lake la kwanza, ni jina lake la katikati au la mwisho, maana yake mtu anakuwa na majina ambayo yanaeleweka. Kwa hiyo, niseme huu upotoshaji wa namna hii na jinsi hii hotuba sisi tulivyoipokea kwa kweli ni hotuba ambayo imeonyesha kwamba kuna chuki ambapo hapa si pahali pa kujenga chuki, hapa ni pahali ambapo Watanzania wanatutegemea kwamba tufanye mambo ambayo yatawasaidia, yatawaweka mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini humu kuna *quotations* nyingi. Kabla sijatoka katika suala hili, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, Mchungaji ameweka *quotations* nyingi lakini nasema kwamba *quotations* zote alizoweka za akina Mahatma Ghandhi, Winston Churchill na kadhalika, mimi nasema ni *quotations* ambazo ziko *misplaced*. Kwa sababu ziwe *quoted*

katika *context* yake isipokuwa kama ni suala la Kiingereza nitamwambia yafuatayo. Yuko mwanafunzi alikuwa akijifunza lakini katika kuandika ili aonyeshe kwamba utaalamu wake ni mkubwa alikuwa anatumia ma-*vocabulary* na maneno ambayo yalikuwa ni mazito kwa ma-*quotations* yaliyokuwa ni mazito ili kuonyesha kwamba ana utaalamu. Lakini yuko Profesa mmoja alikuwa anamjibu mwanafunzi wake na ndio nikimalizia hii nitaondoka katika suala hili, nitakwenda katika mada nyingine za Wabunge, alimjibu akasema: "*arsijoursly and avidly*. *Avoid the Olympian physiology for it's calumniates in calumny and ignominy for you as well as your pedagogue"*. Hapo natoka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuwepo hoja nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa. Niseme kwamba tumezizingatia na tutaendelea kuzifanyia kazi na kwa kweli niseme michango yote ambayo imetolewa ndani ya jengo hili Tukufu nasema kwa ukweli na uwazi kabisa imekuwa ni michango ya kujenga na ni michango ambayo tunaichukua kwa moyo mkunjufu na michango ambayo mingine tumeshaanza kuifanyia kazi, mingine tutaanza kuifanyia kazi na mingine tutaendelea kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupambana na ujangili, kusema kweli Serikali inafanya jitihada, niseme kwamba jitihada ni kubwa na mwamko ni mkubwa na yapo mambo ambayo kidogo yanatupeleka nyuma katika utekelezaji wetu na haya ni mambo ambayo Waheshimiwa wameyataja kwa mfano kuna uchache

wa vitendeakazi, kuna uchache wa upande wa bajeti, lakini niseme na niwatoe hofu na wasiwasi tupo katika majadiliano na wenzetu wa Hazina kuona katika yale makusanyo ambayo tunayapata kutokana na rasilimali hizi ambazo tunazitunza kwa niaba ya Tanzania, ni jinsi gani tunaweza tukafika pahali ambapo Wizara inaweza ikapata katika makusanyo yake kiasi cha kutosha. Lakini sisi tuna kazi kubwa ambayo lazima tusimame kidete, ambayo itakuwa ni kupata makusanyo na hilo ni jambo kubwa ambalo tumelizungumzia ndani ya Wizara, tunataka watu ambao wanashughulikia eneo hili wawe ni watu ambao ni waadilifu, ni watu ambao wanafuata maadili na nina uhakika tutaweza kwenda vizuri katika hilo na nishukuru kwamba tunapata miongozo mizuri kutoka katika Kamati ya Mheshimiwa Lembeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna suala la migogoro ya mipaka, suala hili Wabunge wengi wamelizungumzia. Leo asubuhi waliozungumza wamezungumza, lakini hata jana wale waliozungumza na wengine wameleta katika maandishi. Hili suala la migogoro ya mipaka nikiri ni suala ambalo kwa kweli ni kero. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge haitowezekana wala si msimamo na wala si mwenendo wa Serikali kuwaudhi wananchi. Nalirudia hili si azma ya Serikali, si msimamo wa Serikali na si mwenendo wa Serikali kuwaudhi wananchi. Suala la migogoro ya mipaka nikiri kwamba limekuwepo lakini jitihada sasa zinafanyika na Wabunge wengi mtakubaliana nami kwamba sasa hivi Tume ambayo tumeiunda, ambayo iko Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya

Waziri Mkuu (TAMISEMI), iko Serikali za Mikoa na Wilaya mbalimbali. Kuhusu maeneo husika na hizi kwa kweli ziko katika Menejimenti, zimekwishakwenda maeneo mbalimbali na hata hivi sasa tunavyozungumza wako katika shughuli hii ya kutazama matatizo ni yepi kuhusu mipaka. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika suala la mipaka sisi tuna uchungu kama ninyi mlivyo na uchungu. Hii ni nchi yetu sote na hakuna pahali ambapo tutasema kwamba Serikali itakuwa ama Wizara ya Maliasili na Utalii itakuwa ni kuwaonea wananchi ama kuwakandamiza wananchi ama kuwapora wananchi ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba hii Tume inafanya kazi, itakwenda Tanzania nzima na imekwishapita katika maeneo mbalimbali. Kuna baadhi ya Wilaya ambazo imekwishapita na tunafanya kitu ambacho lazima kwanza tushirikishe watu wote husika, wala hatutaki kufanya uamuzi kama Wizara kusema kwamba tutafanya maamuzi, lakini tunataka yawe ni maamuzi shirikishi ili makubaliano kuhusu haya masuala ya mipaka yatakuwa ni makubaliano ambayo yatakuwa kila upande utaridhika. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwa sababu Wabunge mmelisema kwa hisia nyingi na wengine kwa uchungu mkubwa sana ambao nimeupokea na Naibu Waziri wangu pia ameupokea hivyohivyo hata yeye wiki iliyopita hata ile wiki nyingine kuna baadhi ya maeneo ya mapori na mipaka ambayo alikuwa amekwenda, yote ni katika ile jitihada ya kuona kwamba tunapata muafaka ambao utakuwa ni mzuri kuhusu suala hili. Kwa hiyo, napenda hili suala la mipaka kwa kweli mlielewe kwamba ni

suala muhimu na ni suala ambalo tumelipa kipaumbele na ni suala ambalo tunalifanyia kazi. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutakapokuja huku mbele ya safari na wengine nitakuja mimi mwenyewe katika maeneo hayo, tutakuwa pamoja kuwaelimisha wananchi, kujaribu kufahamu haki zao na kuona kwamba tunakwenda vipi katika hilo suala la mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vitalu vya uwindaji. Suala la vitalu vya uwindaji kwa kweli limekuwa ni suala ambalo limeleta changamoto nyingi sana. Niseme kwamba Wizarani sasa hivi kwa kuwa ule mgao ambao utaanza mwaka kesho zoezi limefanyika na Mheshimiwa Maige wakati akiwa Waziri pale amefanya lile zoezi wamemaliza na niliweke wazi hapa katika Bunge, si dhamira yangu kusema kwamba nilifungue upya suala zima la vitalu vya uwindaji. Kwa sababu kisheria, kwa kuwa tamko lilikwishafanyika na ugawaji ulikwishafanyika na baada ya kutamka na ugawaji kufanyika watu walianza, wengine walikwenda kuchukua mikopo, wengine walianza maandalizi na kadhalika. Kwa hiyo, inakuwa ni vigumu kusema kwamba Waziri kwa kuwa ana dhamana ya jambo anaweza akalifanyia maamuzi aweze kulifungua upya jambo zima isipokuwa kitu ambacho tumefanya, tumesema tunatoa fursa kwa wale ambao hawakuridhika, wanaweza wakaleta malalamiko yao na wakaeleza uzito wa malalamiko yao na kwa nini wanasema kwamba hawakuridhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hilo pia ipo Kamati ambayo inamshauri Waziri na hata kuna baadhi ya Wabunge ambao wamo katika Kamati hiyo ya kumshauri Waziri. Kitu ambacho nimefanya na nitaendelea kufanya, ushauri wote ambao umetoka katika Kamati hii hakuna ushauri ambao mimi kama Waziri nimekuwa pale nimebadilisha. Ushauri unaokuja kutoka katika Kamati hii kwa sababu wao wanautazama katika upana wake na wanatazama katika maelezo na katika ushahidi ambao unajitokeza wakati wanafanya shughuli zao. Kwa hiyo, msimamo ambao tumechukua watakavyokuwa wanatuletea ile Kamati kwa sababu ni Kamati ya Ushauri lakini tumejitahidi kadri tuwezavyo na kwa kweli tumekwishafanya maamuzi kutokana na vikao vya Kamati hii ya Ushauri kwa maana nyingine tunataka tuwe *open,* tunataka tuwe *transparent* na tunataka tufanye mambo ambayo hayana usiri ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapohapo katika suala hilo la vitalu vya uwindaji, kuna suala ambalo Wabunge wengi wameliuliza akiwemo Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Halima Mdee na wengine na hilo linahusu mkataba baina ya kampuni ya *Uranium Resources* na nyingine ni *Western Metals Limited* pamoja na *Game Frontires of Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitamke hapa katika kuwajibu wao lakini pia kuwajibu Wabunge wote na kuwajibu Watanzania, niseme kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imechunguza mkataba tajwa na huu

ni mkataba baina ya *Uranium Resources, Western Metals* pamoja na *Game Fronties* na kubaini kuwa kampuni ya *Game Frontires of Tanzania Limited* ambayo ilipewa haki ya matumizi ya wanyama pori kwa ajili ya kuendesha shughuli za uwindaji wa kitalu katika eneo la Mbarang'andu *open area,* wao walichopewa ilikuwa ni leseni ya kufanya uwindaji katika kitalu na si vinginevyo. Kwa hiyo, hawakupaswa kuingia mkataba na kampuni nyingine kwa kuzingatia kuwa ile kampuni nyingine kazi iliyokuwa inafanya katika eneo lile ni kazi tofauti kabisa ambayo ilikuwa ni kazi ya ku- *explore* madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na mambo ambayo wamefanya hawa *Game Frontire,* imekuwa ni kinyume na utaratibu, imekuwa ni kinyume na msimamo wa Wizara kwa kuwa hawakupaswa kuingia mkataba na kampuni yoyote na hata kama nia ingekuwepo ya kuingia mkataba na kampuni yoyote kitu ambacho wangefanya walikuwa wanalazimika kuleta taarifa Wizarani na kutuambia kwamba mlitupa kibali cha kufanya shughuli (a) lakini kuna watu wamekuja wanataka kufanya shughuli (b) na Wizara ingeweza kufanya maamuzi kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa Sheria zilizopo. Kwa sababu hivi viwili havitoweza kwenda sambamba kwa kuzingatia hayo na kwa mujibu wa kifungu cha 38(12)(e) cha Sheria ambacho kinazuia kampuni za uwindaji wa kitalii kukodisha vitalu vilivyogawiwa kwa sababu yeye atakuwa ni kama amekodisha kitalu ambacho kimegawiwa na kikisomwa kifungu 38(13) vyote ni vya Sheria ya Hifadhi ya Wanyama pori, Namba 5 ya

mwaka 2009, kampuni ya *Game Frontires Tanzania Limited* kwa sababu hii na kwa sababu tumelifahamu wanapewa *notice* ili waweze kujieleza kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupewa *notice* hii Wizara kwa maana ya kusema kuwa Waziri itabidi kufanya maamuzi lakini ningependa kusema bila ku- *prejudice,* kuweza kujitetea au maelezo gani atakuja nayo kwa kuwa tumekwishabaini kuwa ameingia katika mikataba kinyume na taratibu na sheria, tunasema tayari amekwishakiuka kwa maana nyingine itabidi ajieleze kwa nini hilo limetendeka na pia jambo ambalo litafuatia ikionekana kuwa ni wazi katika kujieleza au kujitetea katika *defence* yake itabidi hiyo leseni tuliyompa ya kufanya uwindaji tumnyang'anye. Katika suala hili, Wizara ya Nishati na Madini walitoa maelezo na ninahisi kuna wenzetu sikumbuki ni Wizara gani walitoa maelezo katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa tumebaini kwa kuwa ni jambo ambalo tulikuwa hatuna taarifa nalo lakini baada ya kupata taarifa kuwa jambo hili limetokea tumelitizama kwa undani wake na tumebaini kuwa kuna ukiukwaji wa sheria na taratibu na kwa maana hiyo tutakwenda kwa mujibu wa sheria ambazo tumeziweka kwa sababu tunazungumzia juu ya utawala bora. Kwa maana hiyo, kwa kuwa tunataka ubora katika utawala wetu na isije

kuonekana kuwa kuna mtu anaonewa ingawa yeye tayari kwa mujibu wa ushahidi tulionao kaishavunja sheria tutampa nafasi aweze kujieleza kwa kuwa ndivyo sheria inavyotaka  na baada ya hapo Wizara itafanya maamuzi ambayo inaona inastahili kufuatana na uvunjaji wa sheria na utaratibu mzima katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu hivi vya uwindaji, kumekuwa na kelele nyingi na ningeomba nizungumze hapa ili tuweze kuwekana sawa lakini pia mnisaidie kwa kuwa nyie mnawafahamu labda rafiki zenu au wapigakura wenu ambao waliomba. Sheria tuliyonayo sasa hivi inasema kuwa kila kampuni ambayo itaomba kitalu chochote 25% ya hisa lazima ziwe za Watanzania*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo 75% itakuwa ni hao wawekezaji wa nje lakini Sheria haikuachia hapo wala kukomea hapo kifungu cha Sheria hiyohiyo, kifungu cha 39(3) kinasema katika ugawaji wa vitalu 85% ya vitalu ni lazima yapewe makampuni ya kitanzania na 15% tu ndiyo wapewe makampuni ya nje. Hiki ndicho kilichotokea kwa maana ya kusema kwamba baada ya ule mgao wakapewa Watanzania na wale watu wa nje wakapewa 15%. Sheria hii kumekuwa na mazungumzo kuna wale ambao wanaamini kuwa iko haja ya kujaribu kuzungumza na kutazama kama imekaa sawa na labda huko mbele ya safari inaweza kupunguza matatizo yaliyojitokeza na kuna wengine wana maoni

tofauti, tutakachokifanya hapa itakuwa ni kuleta mjadala kwa sababu sheria tunaweka lakini walengwa ni wadau katika eneo hili na wadau wamekuwa na mawazo tofauti ingekuwa ni vizuri kupata mawazo yao ili kutazama sheria hii kama itakuwa sawasawa ama kama kuna haja ya kuitazama upya kwa maana ya kusema kuwa marekebisho yafanyike itakuwa ni jambo sahihi. Hata Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na wenyewe hili suala wanalifahamu na limekuwa katika upande wa mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala la wanyamapori kuingia katika mashamba ya watu, uharibifu ambao unafanyika na watu kupata hasara kubwa, mimi niseme kuwa upo utaratibu na ipo sheria, nimezingatia maoni ambayo yametolewa hapa ndani ya Bunge. Niseme kwa kifupi kwamba hili suala litataka ushirikino ambao ni mpana zaidi. Ipo haja kubwa kwamba tuwe na ushirikiano mkubwa sana na Halmashauri, tuwe na ushirikiano mkubwa na viongozi wa Serikali za Vijiji lakini pia mimi niseme na Waheshimiwa Wabunge ipo haja tushirikiane kwa ukaribu sana maana yake ninyi mnazielewa sheria hizi zaidi kuliko wenzetu kule chini. Lakini pia niseme hili suala la kutoa kifuta jasho na kifuta machozi nimesikia na sheria iliyowekwa na Serikali imefanya jitihada ukitazama tulikotoka kiasi kilichokuwa kinatolewa na ukitazama wapi tumefika sasa hivi kiasi kinachotolewa ninafikiri mtu anaweza kusema kuwa siyo kwamba Serikali imelifumbia macho jambo hili, jitihada zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo nimelisikia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ni ushirikishwaji wa wananchi. Hao wawekezaji ambao wana vitalu katika maeneo mbalimbali nchini iko haja kubwa sana na sisi tulisimamie kutoka Wizarani kuwa pawepo na ushirikishwaji ulio mkubwa wa jamii, wananchi na Serikali za vijiji. Vinginevyo kama ushirikiano hautokuwa mzuri ina maana maelewano hayatakuwepo, ina maana migogoro haitoweza kutoweka na ina maana ya kusema kuwa ile hali ya kukaa kwa usalama itakuwa haipo. Waheshimiwa Wabunge waliotoa ushauri huu niwaambie kuwa ushauri wao umezingatiwa na ushauri huo tumeupokea. Niseme pia kuwa Serikali itaendelea kufanya kila jitihada kuja kukutana na ninyi Wabunge kupitia kwenu tutaenda zaidi kukutana na Serikali za vijiji na tutakutana na wananchi moja kwa moja na kuwa na vikao na mikutano na wananchi ili kuhakikisha kuwa haya mambo yanatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala la migao ambayo inatokana na *WMA's.* Hizi *WMA's* upo utaratibu ambao umewekwa katika Kanuni lakini kitu ambacho tumekibaini kuzungumza na baadhi ya wadau lakini limegusiwa kidogo hapa ni ule utaratibu wa ukusanyaji na hasa uwindaji wa picha. Pale yapo malipo, kuna asilimia ambayo inabaki katika kijiji, kuna asilimia ambayo inakwenda Wizarani na kuna asilimia ambayo inakwenda katika mfuko mkuu wa Serikali. Hapo kumekuwa na suala la jinsi ya kukusanya mapato haya lakini pia kumekuwa na suala la jinsi ya mgao wenyewe na mapato yanavyowarudia wanakijiji au

wana vijiji. Hili niseme kuwa ushauri mzuri ambao umetolewa hapa tumeupokea na niseme tu kuwa tutaweza kuuzingatia na ninadhani kadri tunavyokwenda tutaendelea kupunguza matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja nyingine inayohusu utafiti na uchimbaji ndani ya hifadhi. Wanasema kuwa kuna vitendo vya uchimbaji wa madini hasa katika hifadhi ya Serengeti. Waheshimiwa Wabunge ambao wamelizungumzia hili niwaambie kuwa sisi hili tulikuwa tayari tumelipata na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Nyalandu amekwisha kwenda kule na kuna ripoti ambayo ametengenezwa, ninayo mimi, ninasema mvute subira, tutachukua hatua kwa sababu bado tunapata ushahidi wa kutosha lakini ripoti ya kwanza tunayo. Kitu kikubwa ambacho ninataka kukiri katika ripoti hii ambayo Naibu Waziri amekwenda Serengeti na amekwenda katika maeneo hayo ambayo machimbo yalikuwepo na tumebaini kuwa kuna watu ambao wanafanya mambo haya kinyume na utaratibu na kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuwa isingekuwa jambo jema niende katika undani wake lakini naomba Bunge litukubalie, Bunge lituamini kwamba ripoti tunayo na bado tunafanya kazi nyingine kidogo lakini hapo mbele ya safari na siyo muda mrefu sana, tutachukua hatua na mtaona ni hatua gani ambazo tutachukua ili kuhakikisha vitendo kama hivi ndani ya hifadhi havifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala la kusafirisha wanyama na wale Maafisa wa Wizara na kutaka kujua ni hatua gani zilichukuliwa. Napenda kusema kuwa hili ni suala ambalo lilifanyiwa kazi kabla ya sisi hatujaingia Wizarani na tumekuta kazi iliyofanyika katika suala hili ni kazi nzuri sana. Wamelifanyia kazi nzuri na tumefika mahala pazuri kabisa ambapo hatua madhubuti zitachukuliwa kuhusu wale maafisa ambao walikuwa wamehusishwa moja kwa moja au kwa njia nyingine na kashfa hii ya kutoroshwa kwa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kuwa hatua tutachukua na ningeomba Waheshimiwa Wabunge kwa niaba yenu tunataka tuchukue hatua ambazo mtaziona zinaridhisha kwa mujibu wa Wizara. Maana kila kitu kitakuwa ni *open* na tufikie mahala tuanze kuzungumzia mambo mengine ya maendeleo, tuanze kuzungumzia mambo mengine ya kuona Wizara itajiweka katika nafasi ipi katika masuala ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie ahadi. Kuhusu ahadi za Serikali, Wizara iliahidi kuipatia Wilaya ya Chunya gari la doria kutoka Idara ya Maliasili kutimiza ahadi iliyotolewa hapa Bungeni mwaka jana. Niseme kuwa hili linafanyiwa kazi na karibu tunafikia utekelezaji mzuri katika jambo hili. Kwa hiyo, ahadi iliyotolewa hapa Bungeni bado ipo na

tunaifanyia kazi ili kuona kuwa Wilaya ya Chunya lile gari waliloahidiwa kwamba linakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utekelezaji wa ahadi ya Wizara kuchangia mifuko 150 ya simenti na nondo 20 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la mto Mbezi kule Ruvu. Hii ahadi inatekelezwa na mara tukishaanza mwaka huu wa fedha niseme kuwa hii ahadi tuliyotoa itatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala juu ya uteuzi wa Bodi na watu wamesema kuwa katika Bodi wanaoteuliwa wengine hawana sifa, wengine wanateuliwa kwa sababu ya kufahamiana na kadhalika. Haya maneno ni kweli yamekuwepo lakini ninataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kuwa tutakwenda sisi maana ninaona kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea na kupunguza kelele tutakwenda kwa utaratibu mwingine ambapo hizi Bodi tutakuwa tunazitangaza kwenye magazeti, kwenye redio na *television* na tutakuwa tunatoa vigezo kuwa tunataka watu wa aina gani, watu ambao watakuwa na sifa, sisi tutatazama na ninadhani hiyo itatupunguzia haya maneno na hizi kero ambazo zimekuwa zikijitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hoja za migogoro ya mipaka nimekwishalizungumzia na nimekwishasema kuwa kitu kikubwa ambacho nimewaomba Waheshimiwa Wabunge ni kuwa Wizara imeunda Tume ambayo ni kama kikosi kazi ambacho

kinazunguka nchi nzima. Nirudie tu kuwa iko Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo ni Wizara yangu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Halmashauri za Wilaya husika. Hii timu kama nilivyosema awali kuwa itazunguka, italeta maoni lakini baada ya hapo tutakwenda na sisi pia na mkumbuke Waheshimiwa Wabunge kuwa ni matatizo ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu sana siyo matatizo ambayo yapo kwa mwaka mmoja, miwili ama mitatu yamekuwepo kwa muda mrefu na niseme kuwa hayatachukua muda sana lakini tutafanya kila jitihada, kwa hiyo, nisijenge matumaini kuwa majibu tutayapata hapohapo, tutakwenda hatua kwa hatua ili tuhakikishe kuwa tunakwenda vizuri katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi na usimamizi wa misitu. Katika suala misitu yamejitokeza mengi. Kumekuwa na suala la mgao kwa maana ya vibali vinavyotolewa, kumekuwa na suala la kuhusisha wale ambao wanazunguka yale maeneo ambayo misitu hii inavunwa ili kuhakikisha na wao wananufaika. Mimi ninadhani nitakuwa mtu wa ajabu sana nikisimama hapa na kusema kwamba zile jamii ambazo zinazunguka hifadhi hizi hawatahusishwa au kupata faida, ni lazima wahusishwe na wahusishwe kwa sababu za msingi. Wao hata kama likitokea balaa lolote na Mwenyezi Mungu apishe mbali lakini wakati mwingine yanatokea hata Wabunge mmeongea, ikitokea balaa la moto watu ambao wanahusika wakiwa wa kwanza ni wale watu wanaozunguka lile eneo. Kwa hiyo, hapa ni suala la ujirani mwema lakini siyo ujirani mwema wa maneno tu upo ujirani mwema wa kuweza kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako kuwa yale maeneo na vile vijiji ambavyo mmezungumza na hata vigezo ambavyo tumeweka viko tofauti. Kuna Mbunge amezungumza hapa kuwa katika vigezo ambavyo tumeweka tumesema lazima mtu au watu wawe na misumeno ya kukatia ama wawe na *workshop,* hivyo vyote ni muhimu ni lazima tujiwekee vigezo. Lakini siyo jambo ambalo tunalitarajia kuwa watu katika vijiji watakuwa na vitu kama hivyo, kwa hiyo kunakuwa na mtizamo tofauti. Kikubwa ninataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa hilo tutalifanya na tutazidi kuhimiza kuwa suala la ujirani mwema, suala la maelewano mema ni lazima lizingatiwe katika shughuli zote za hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na Serikali kusimamia uhifadhi, lakini wahifadhi wakuu ni wale watu ambao wapo katika maeneo. Iwe ni katika wanyamapori, iwe ni katika misitu, lakini wao ndiyo wahifadhi wakuu na wadau wakuu ambao hatuwezi kwa vyovyote vile kama tukitaka kufanikisha tukawaacha wasiweze kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala la uendelezaji wa ufugaji wa nyuki. Suala hili limekuja katika sura mbili, sura ya kwanza imekuja kwamba, katika mabadiliko ya mfumo ndani ya Wizara inaonekana kwamba *department* ambayo ilikuwa inashughulikia masuala ya nyuki, uzalishaji wa asali na nta, ni kama limesahauliwa au ni kama limeachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Wabunge na kuwatoa hofu kwamba, hili ni eneo moja kubwa sana na tunaamini kwamba, ni eneo mkombozi na tunaamini kabisa ni eneo ambalo linaweza likanufaisha vijana wa Kitanzania walio wengi. Ipo haja ya kuweka nguvu kubwa sana na ukitazama uwekezaji kwa maana ya kusema kwamba mitaji siyo mikubwa sana kiasi hicho, ni mitaji ambayo Wizara itafanya kila jitihada kuhamasisha hata watu wengine wenye uwezo ndani ama nje ya nchi hata *NGOs* waweze kusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, hatuwezi tukalipuuza na hatuwezi tukaliondoa. Maana yake kumekuwa na dhana ya kusema kwamba, nguvu imewekwa katika upande wa misitu na kuonesha kwamba ndiyo yenye umuhimu, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika *structure* ambayo tunaitengeneza sasa hivi tutahakikisha kwamba linapata nafasi. Naomba Wabunge mtuamini katika hilo na niwahakikishie kwamba tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa hapa naomba pia Wabunge na ninyi pia muwe wabunifu kwa maana ya kusema kwamba, tushirikiane na Wizara kuona ni njia gani tunaweza tukachukua. Mnaweza kuwa mna mawazo pia siyo kwamba Wizara peke yake ndiyo inaweza kuwa na *monopoly* ya mawazo. Sisi tunaweza tuka-*facilitate,* lakini wananchi kwa ujumla na Wabunge wao hasa wanaweza kuja na mawazo katika sekta hii ya uvunaji wa asali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano dumu dogo la nusu lita la asali hapa Tanzania wanauza shilingi elfu kumi. Lakini hilo hilo kwa bei yake kule nje inakwenda mpaka dola 40, 50 mpaka hata dola 60 inategemea. Lakini pia wapo watu ambao wanaamini kwamba asali ambayo tunazalisha sisi ina uasilia fulani, halafu siyo kama zile ambazo zimepita katika *process* mbalimbali. Kwa hiyo, Wabunge ambao mnatoka katika maeneo hayo mlango wetu umefunguliwa, uko wazi, mngekuja tukashirikiana, tukapeana mawazo na kuona ni vipi tunaweza kusaidia katika kutengeneza ajira katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amezungumzia masuala ya utalii, kuna hili suala ambalo limejitokeza, naona Mheshimiwa Naibu Waziri hakupata nafasi ya kulijibu kwa undani sana, nalo ni suala la *concession* ambazo wanalipa hoteli za kitalii. Suala hili tutalitazama kwa undani sana na tutashirikiana na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunataka kupanua mjadala kuhusisha na wadau mbalimbali. Yapo mahoteli ambayo yanalipa *concession fee* kwa *TANAPA* kwa makubaliano ambayo wamekuwa nayo na *TANAPA*. Zipo hoteli ambazo hazilipi lakini hazizidi wawekezaji watatu na hao ndiyo kidogo wamekuwa wagumu na ndiyo wamekimbilia Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya kila jitihada ya kuona kwamba, kesi ambayo ipo Mahakamani kuhusu suala la *concession* inatolewa. Hapo niseme

kwamba, hatukufanikiwa, shabaha ilikuwa ni kulitoa suala hili Mahakamani. Kwa hiyo suala lipo Mahakamani na tunadhani litakaposikilizwa watatazama kila upande unaleta nini pale mezani. Kwa hiyo ule mhimili ambao unahusika mimi sitaki kuingia huko, wao watalitazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watakapokuwa wamemaliza shughuli za Kimahakama itabidi kwa kweli nasi tuingie tulitazame. Kwa sababu watu wengi wanalalamika kwamba baadhi ya hawa watu wanazo hoteli katika zile mbuga, unakuta wanachaji wakati mwingine mpaka dola elfu moja kwa siku moja, wengine mpaka dola elfu moja na mia tano na kadhalika. Lakini unakuta kitu ambacho wanalipa kama *concession* inakuwa ni kidogo sana. Inakuwa ni kitu ambacho ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya na nchi zingine, kidogo kuna tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajaribu kujenga msimamo tunangoja hili suala likitoka Mahakamani. Suala la *concession* msifikiri kwamba, sisi tumelifumbia macho, hapana. Ni suala ambalo tunafanya kila jitihada kuona kwamba tunakwenda sawa kwa sababu hatutaki Watanzania wadhulumiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na masuala ambayo yamezungumziwa juu ya Bodi ya Ngorongoro kwamba wamejipangia safari za kwenda sijui wapi. Mheshimiwa Telele alizungumzia juu ya Tume ambayo ilikuwa imewekwa na Waziri kutazama masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Tume imefanya kazi yake na imeleta ripoti kwa Waziri kama ilivyotakiwa na niseme tu kwamba, kwa sasa hivi kwa hali tuliyokuwa nayo ni Waziri kuzingatia yale mambo ambayo yametokana na Tume hiyo na yote tutayafanyia kazi. Maana yake kitu kikubwa hapa ni kwamba Bodi hii imebakiza mwezi mmoja inamaliza muda wake. Kwa hiyo, sidhani kama itakuwa jambo la maana sana tuanze kuzungumza kwamba hii Bodi tunafanyaje, muda wa Bodi hii unakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunafanya ni katika kutazama wakati tunatengeneza Bodi mpya itabidi tuzingatie Tume imesema nini, wadau wamesema nini, lakini kubwa zaidi Wabunge katika mawazo yenu ambayo mmetoa. Nataka niwahakikishie kwamba si mbaya sana kiasi hicho na tuhuma ambazo mmezitoa kuhusu wafanyakazi wa Ngorongoro ambao baada ya muda mchache wamekuwa na utajiri mkubwa, wamekuwa na majumba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Wabunge kwamba ni jambo ambalo tunalifanyia kazi na hatuwezi tukalipuuza kwa sababu ni tuhuma zipo. Naomba mtuamini kwamba, hatua za awali tumeshaanza kuzifanya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yupo Mbunge hapa jana wakati anazungumzia suala la Ngorongoro alikuwa radhi atoe hata nyaraka za Serikali, alitaka atoe barua ambayo imetoka kwa Katibu Mkuu wa

Wizara ya Maliasili na Utalii ikienda kwa uongozi wa Ngorongoro.

Waheshimiwa Wabunge *please*! hii nawaomba, mimi sikatai, lakini nilivyolichukulia ni kwamba, ndani ya Ngorongoro atakuwepo mtu ama watakuwepo watu ambao badala ya kufuata utaratibu unaostahiki wanaona wakikimbilia kwa Wabunge na wakawapelekea nyaraka zetu sisi ndani ya Serikali, wanaamini kwamba Wabunge wakija hapa wataweka *pressure* kwa Serikali. Nasema *the Government does not work in that way!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niiweke wazi tena kwa nia nzuri, Wizara yangu tupo *open* na tupo *transparent*. Lakini mtumishi yeyote akikimbia kwenda kwa Mbunge kwa matarajio kwamba eti kuna mambo yamefanyika ndani ya Wizara, kwa hiyo Mbunge aje hapa aanze kuni-*attack* mimi. Nasema kwangu *it is not acceptable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo siyo utaratibu na niko radhi Mbunge akipokea taarifa kama hiyo aniite pembeni aniambie Waziri kuna kitu kama hiki ndani ya Wizara yako unasemaje? Lakini aje ndani hapa na nyaraka kutoka katika Wizara yangu aseme kwamba anakuja kunitisha. Mimi nasema huo wakati umekwisha, *please*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa nia nzuri, kwa hiyo kitendo cha Afisa ama Maafisa ndani ya Ngorongoro kwenda kuchukua nyaraka za ofisi na ambayo ni *communication* ilikuwa imekwenda kweli

kule Ngorongoro na ni kweli zilikuwepo wakazipeleka kwa Wabunge na Wabunge wanakuja ndani ya Bunge kusema, kwa kweli haya ni mambo ambayo hayawezi yakavumilika na hayawezi yakakubalika. Kwa hiyo hilo suala tutalitazama kwa *merits* zake, lakini hatutalitazama kwa mujibu wa *pressure* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nataka niwahakikishie kwamba tutafanya uchunguzi ndani na itakapobainika Afisa ndani ama wale Maafisa ambao wametoa zile nyaraka ndani, nataka nikuhakikishie na Bunge lako Tukufu sitasita kuchukua hatua kwa sababu huo siyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ilitolewa na Hotuba ya Upinzani kwamba Waziri anadhoofisha Idara ya Wanyamapori na kusema kwamba, zipo nafasi za kukaimu. Waheshimiwa Wabunge vitu vingine tuzungumze, Waziri nipo hapa, unaweza kuja ukaniuliza. Vipi inakuwa katika Idara fulani ndani ya Wizara yako zipo nafasi zimechukua muda huu, maana huenda zipo sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Waziri ambaye atapenda maeneo yake ndani ya Wizara yazorote. Ni nzuri lakini kusema kwamba Waziri ameshiriki katika kuzorotesha, mimi *charges* kama hizo nazikataa si za kweli na niseme kwamba matatizo katika Idara ya Wanyamapori yametokea kutokana na wanyama wale ambao walisafirishwa na vitu vingine na kadhalika, ambayo mimi nasema hiyo ni historia tusiende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunatengeneza mifumo mizuri, tutawawekea Maofisa wazuri ndani ya Idara ambao ni wachapakazi ambao nina uhakika wataweza kufanya mambo ambayo tutakwenda nayo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo ya Malikale, suala hili limezungumzwa na Wabunge mbalimbali kusema kwamba, viongozi wa kihistoria akina Mkwawa na wengine ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza vivutio vya utalii katika maeneo kama hayo. Nataka niwahakikishie kwamba hayo tutayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja nyingi ambazo zimetolewa, lakini niseme kwamba, tutafanya kila jitihada, hoja zote ambazo sikuzijibu hapa au Naibu Waziri hakujibu hapa tutawajibu kwa maandishi bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ya Maliasili na Utalii iko wazi wakati wowote, muda wowote. Liko jambo lolote naomba mje tuzungumze, mje tubadilishane uzoefu na ndiyo shabaha yenyewe. Lakini haya mambo mengine kuja kushtukizana sidhani kama ni jambo jema, hilo tunaweza tukalifanya kama kumekuwa na ukaidi ama kuna mambo ambayo hayakufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wabunge kwa ujumla wenu, sikujibu hoja zote, lakini tutawajibu

kwa maandishi, nimejaribu kueleza zile ambazo nimeziona ni muhimu zifanyike, lakini nataka niwambie kwamba nia ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ili nisipigiwe kengele ya pili, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif.1001 - *Admin & HR Management*… … Sh. 4,210,563,864,000/=

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kwanza. Nakumbuka vizuri katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine, nilimwomba sana Waziri aje na Kauli kuhusu mgogoro wa wananchi wa Nzasa Chanika na Msitu wa Kazimzumbwi ambao umedumu kwa muda mrefu. Lakini pia kauli ilitoka kwa Waziri wa Ardhi kwamba mpaka unaotakiwa kutumika ni ule mpaka wa mwanzo, lakini mpaka sasa hivi wananchi wanaendelea kunyanyaswa na Watendaji pamoja na Polisi wa Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atoe tamko sasa kwamba, je, katika Wizara yake na Serikali hiyo moja, wanatumia mpaka ule ule ambao Serikali ambayo ndiyo hiyo hiyo yenye Wizara ya Ardhi imeamua kwamba ndiyo mpaka sahihi au wao wanatumia mpaka wa pili, ili wananchi waweze kujua hatma ya maisha yao katika eneo hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo suala na hoja aliyoleta Mheshimiwa Mwaiposa mimi nataka kumwambia kwa kweli ni hoja ambayo inafanyiwa kazi vizuri sana. Alikwenda Naibu Waziri katika maeneo hayo, lakini pia niseme kwamba takribani wiki tatu zilizopita alikwenda Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, alikwenda Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, ilikwenda timu pale, Wizara mbalimbali lakini pia alikwenda Mkuu wa Mkoa, alikuwepo Mkuu wa Wilaya takribani kama wiki tatu. Wakazungumza na wananchi na niseme kwamba, sasa tuko katika utaratibu wa kulifanyia kazi tuone ile kauli ya Wizara ya Ardhi na ule msimamo uliokuwa msimamo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi niseme kwamba, Mheshimiwa Mwaiposa suala ulilosema ni suala ambalo Serikali inashughulika nalo. Niseme takribani kama wiki tatu zilizokwisha, viongozi wa Wizara yetu na katika ngazi ya Makatibu Wakuu alikuwepo Katibu Mkuu wangu, alikuwepo Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, alikuwepo Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, alikuwepo Katibu Mkuu wa TAMISEMI, wote wamekwenda, lakini na Mkuu wa Mkoa wa Pwani na

viongozi wengine na maoni ya wananchi ambao walikuwepo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuko katika huo utaratibu na nataka nimhakikishie katika siku ambazo hazitakuwa nyingi na nina uhakika kabla hatujamaliza Bunge hili kutakuwa na tamko rasmi la Serikali kuhusu hili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru. Jamani swaumu kumi la mwisho hili.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wasamalia wema wakati tofauti walikamata meno ya Tembo Kilwa na wakapeleka katika Kituo cha Polisi, jumla ya meno hayo yalikuwa ni 70 mwaka 2007, kesi namba nne ilikuwa ni meno ya tembo 46 mwaka 2007, pia kesi namba 277 meno ya tembo 10 yakapelekwa, mwaka 2008 kesi 298 meno 10, mwaka 2008 pia namba ya kesi 541 meno ya tembo manne (4) yakapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha ajabu meno ya tembo haya hivi sasa wale waliopeleka kesi wasamalia wema ni kwamba meno ya tembo haya yametoweka katika Kituo cha Polisi na wanaambiwa upelelezi haujakamilika wakati wao wenyewe ndio waliopeleka meno hayo ya tembo kwenye Kituo cha Polisi cha Kilwa. Naomba maelezo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo kwa kuwa umeniambia tumelichukua, tutazungumza na Mambo ya Ndani kujua Polisi

wamekwama wapi ama nini hasa kinakwamisha hili, kwa sababu hiyo sasa itakuwa ni Wizara nyingine tofauti. Lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hilo tumelichukua na tutajaribu kutazama limekwama wapi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kwa upana juu ya suala zima la Kanuni ya kifuta machozi ambayo imetungwa tarehe 24 Machi, 2011. Nikazungumzia jinsi ambavyo hii kanuni yaani imeleta matatizo makubwa sana wakati wa fidia kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, ng'ombe akikamatwa na mnyamapori, anafidiwa kwa sh. 50,000. Sasa nikawa najiuliza hivi kwa dunia ya leo kuna ng'ombe wa sh. 50,000 kweli? Lakini mbuzi sh. 25,000, kondoo 25,000, punda 25,000. Nafikiri kwamba Waziri aangalie hii kanuni haiwasaidii Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wale wananchi ambao wamepakana na hifadhi kutoka eneo la hifadhi mpaka mita 500 hawalipwi chochote, wakati huo hawa wananchi wamewekwa na Sheria ya Vijiji ya mwaka 1974. Kwa hiyo, a napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali, ni kwa nini wametunga kanuni kandamizi kama hii kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Pauline Gekul kwamba, kwanza Serikali imepokea hoja hizi kwa Wabunge wengi sana na tumekubaliana

katika Wizara kuweza kuzipitia upya kanuni hizi. Huku kuzipitia upya kutatupa nafasi ya kuangalia ni wapi wananchi wanaonewa au fidia ni ndogo sana ili ziweze kuboreshwa kulingana na wakati.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, Serikali sikivu.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Sheria namba 5 kifungu 31(7) cha Sheria Kuu za Wanyamapori zinaipa uwezo *AAs* kutangaza na kuingia mikataba na wawekezaji katika vitalu vya utalii kwa kushirikisha Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sheria hiyo iweze kutekelezeka, ni lazima iende sambamba na kanuni zitakazoandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau. Tarehe 7 na tarehe 9/5/2012 Muungano wa Jumuiya ya dola hii ulitoa tangazo la kukaribisha wawekezaji kama sheria inavyotaka. Tarehe 16/5, Wizara ilisitisha tangazo hili kwa sababu kanuni zilikuwa bado hazijatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 15/6/2012 kanuni zimetoka, lakini kila Muungano unapokwenda kwenye Ofisi ya Waziri inaambiwa kanuni hizo hazijatoka. Kuchelewa kwa kanuni hizo kutasababisha Muungano kushindwa kupata muda mzuri wa kutafuta wawekezaji na hatimaye tunaweza tukaja kupata wawekezaji wa kupachikwa. Kwa hiyo, nataka nijue kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, je, kanuni hizo zimeshatoka na

kama zimetoka Muungano utaruhusiwa lini ili uweze kuendelea na mchakato?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent. Ni kwamba kanuni zimeshatoka. Mchakato mzima kati ya *AA* katika *WA* ya kwake na mwekezaji ni ruhusa, wanaweza kuanza mazungumzo wakati wowote. Sasa sijui imetokea nini ama wapi kapata taarifa hizi, lakini kanuni zimekwishatoka na utaratibu umekwishaanza.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza mwanamichezo David Bekham alitembelea Liberia mara baada ya vita kwa lengo la kuijenga nchi ile. Kitendo kile cha David Bekham kuingia Liberia kulisababisha watalii wengi sana kumimika katika nchi ile na fedha ikapatikana nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kama haitoshi, David Bekham alipojiunga na *Real Madrid Spain* alisababisha watalii wengi sana kumimika *Spain* na kusababisha kupata fedha nyingi kupitia hiyo. Je, Serikali iko tayari kushirikiana na *Victoria Foundation* kuwaalika watu mashuhuri kama hao duniani ili waje waitembelee Tanzania wawavute na watalii wengine kutoka Mataifa mbalimbali kuja kutembelea vivutio tulivyonavyo hapa nchini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kamata na Serikali kwanza iko tayari kabisa kushirikiana na *Victoria Foundation* kuweza

kuwaalika na kuwakaribisha hawa watu maarufu kwa sababu ni namna pekee tunaweza tukachochea utalii wetu kwa kuwatumia wao. Niseme sisi wenyewe tuko tayari kwenda mpaka uwanja wa ndege kusaidia kuwapokea. (*Makofi*)

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru utalii *College* na National *College of Tourism* naona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hamna fedha zozote zilizotengwa iwapo kuna fedha kwa ajili ya uendeshaji kwenye kitabu cha *volume II*. Sasa ningetaka kujua wenzetu wa Kenya wana *Nairobi College of Tourism* ambayo inatoa *product* nzuri sana na sisi huku Tanzania tumeona wahudumu wetu ni waoga, hawana *confident* na wengi wanaochukuliwa ni wale ambao wamefeli *form four* ndio wanakwenda kufanya hizi *hospitality course*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kujua Serikali mna mkakati gani ili na sisi tuweze kuwa na ma-*graduate* watakaoweza kufanya hizi *course* tuweze kushindana na wenzetu wa Kenya, fedha mtatoa wapi kwa sababu kwenye fedha za maendeleo hakuna chochote kilichotengwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Owenya mwaka huu Chuo chetu cha Utalii hakijawekewa fedha za *development*. Lakini chuo hiki katika mkakati mpana wa Wizara tunapanga kuendelea kukiwekea fedha za *development* katika mwaka ujao wa fedha. Tunategemea vile vile kama Mheshimiwa Mbunge anavyofahamu hiki ndio chuo

ambacho kimepangiwa kuwa na umahiri katika tasnia ya upishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wapishi wachache sana katika hoteli zetu na tunaamini kwamba kitakuwa ni chuo kinara kwa upishi katika eneo letu la Afrika Mashariki. Mkakati mzima wa Wizara kama nilivyosema ni kuhakikisha tunaongeza na tunatumia mbinu mbadala kuhakikisha kuwa hiki chuo kinaendelea.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilivyosimama nikachangia, nimechangia kuhusu majengo ya kale, lakini nimeangalia sijaona mahali popote palipopangwa fedha yoyote ya kutengeneza haya majengo. Sasa nataka kumuuliza Waziri haya majengo yatajengwa na nini? Naomba jibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msabaha hili suala tuko pamoja. Tumetazama bajeti ilivyo, kwa kweli tumeona lazima kuna mambo mengine tutayapa fedha, lakini kuna mengine ambayo itabidi tujinyime. Hata hivyo, tumefungua milango ya mazungumzo na baadhi ya mashirika nje ya nchi na tuna uhakika kwamba tutakavyokwenda yataweza kuzaa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matarajio na mategemeo hayo ili tusikae tu kusubiri kutoka katika Bajeti ya Serikali lakini tutumie njia nyingine za kuwahusisha watu wengine ambao kwa kweli ni wadau wakubwa katika mambo kama hayo. Hiyo ndio

ambayo tunafanya na nataka nikuhakikishie katika hili *sentiment* zangu na zako hazijapishana, tuko pamoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kanuni za uanzishwaji wa maeneo ya Hifadhi za Jamii *WMA* zinaainisha wazi kwamba, wananchi ndio watakuwa wahifadhi wakuu wa maeneo yale na watawezeshwa na Serikali katika kusimamia matumizi ya maeneo hayo na kwamba Serikali itatoa ushauri wa kitalaam pale unapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa nini Serikali kwenye maeneo ambayo tayari wameshaanza kutumia matumizi yao, wameshaanza kuweka wawekezaji inachukua asilimia 55 ya mapato yao na kuwaachia wananchi asilimia 45 tu kinyume na kanuni inavyotamka? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kauli ya Mheshimiwa Mbunge Sakaya. Lakini kama kweli nimemsikia vizuri anasema kwamba, eti *WMAs* wanabaki asilimia 45, mapato mengine yanakwenda katika Serikali Kuu si sahihi, kwa sababu mapato yaliyokuwa mengi takribani karibu 55 inabaki katika *WMAs*, ile nyingine itabidi tuitazame lakini ndio utaratibu ulivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, nasema kama hapa kuna hitilafu, nitakuonesha hasa ni mgao gani unakwenda, nani anapata kiasi gani kutoka kwa wenye *WMA,* lakini tunakuja pia katika Serikali Kuu na tutakuja katika idara

ya wanyamapori. Lakini makusanyo yaliyokuwa makubwa yanabaki katika *WMA*. Tatizo ambalo limekuwepo Mheshimiwa Mbunge, limekuwa ni katika makusanyo na marejesho.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Kwebe.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi ni Dkt. Kebwe siyo Kwebe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii. Wakati nachangia kwa mazungumzo nilizungumzia suala la manunuzi. Manunuzi haya kwa kweli ni kero ni maudhi na kwa kweli yanajenga chuki. Haiwezekani wawekezaji na wafanyabiashara wengine wanachukua bidhaa zikiwemo samaki, kwa mfano kutoka Ziwa Victoria wanapitishwa hapa Serengeti, wanapelekwa Arusha, halafu samaki hao hao wanatolewa Arusha kuja hoteli za Serengeti. Huo si utaratibu mzuri. Je, Mheshimiwa Waziri ana kauli gani juu ya hili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na hili jambo la Mheshimiwa Kebwe, siwezi nikalitolea kauli kwa sababu mpaka nipate ukweli na undani wa suala lenyewe. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba, nitazungumzia naye anieleze hili tatizo limekaa namna gani halafu kama kuna mambo ambayo yana hitilafu tutaweka sawasawa.

**MWENYEKITI:** Basi mkutane.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya migogoro mingi ya mipaka katika maeneo ya Jimbo la Mpanda Vijijini, Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu ambako kuna Vijiji takribani 10 vina mgogoro juu ya *WMAs*. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kumaliza mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Kakoso ya migogoro inakwenda sambamba na tamko letu ambalo Mheshimiwa Waziri alilitoa kwamba tuna maeneo mengi ambayo kuna migogoro katika *WMAs* na kwa sababu tumeandaa Tume kubwa na huru katika Serikali, tutahakikisha kwamba, Tume hii inafika katika eneo la vijiji hivi vya Mpanda na wanatuletea mapendekezo ili tuhakikishe kwamba mgogoro huu unakwisha kabisa.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza jinsi tatizo hili la uwindaji haramu lilivyo la kidunia na kwamba labda kuna nchi zenye matatizo makubwa zaidi kuliko hata Tanzania. Kwa mfano, *South Africa* mpaka sasa hivi tunavyozungumza hapa, mwaka huu wamepoteza faru 245 wakati sisi faru watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mazingira ya wafanyakazi katika kuwalinda hawa wanyama ni magumu sana na hatujayazungumzia. Wafanyakazi wa Hifadhi wanapambana na wanyama wakali,

wanapambana na nyoka, mashimo, mishale ya wawindaji na ambao hata wakiuawa hatuwasemei wakati tunawatetea wale wauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wanakutana na matatizo ya kutengwa na jamii zao kwa sababu wanaishi maeneo ya mbali. Sasa mashirika haya na idara hii inashindwa kutoa huduma nzuri kwa wafanyakazi na kuwawezesha kufanya kazi vizuri ili kuwalinda hawa wanyama. Serikali imekuwa ikiombwa na Waheshimiwa Wabunge hapa iondoe lile gawio la bilioni 10 ili kuweza kuboresha vitendea kazi. Naomba kauli ya Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaungana kabisa na Mheshimiwa Dkt. Kamani kwamba moja ujangili na mtandao wa ujangili ulioko duniani unazidi kuwa mkubwa. Wanyama wengi hususan tembo wanaendelea kuuawa na kutoroshwa katika masoko haya makubwa na hili tatizo linazidi kuwa kubwa sana katika nchi yetu. Ni kweli vile vile kwamba hali ya wafanyakazi katika mapori yetu na mapori yetu ya akiba siyo nzuri. Majangili hawa wanatumia mpaka silaha za kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, Serikali itaanzisha mara moja *Tanzania Wildlife Authority* ambayo itakuwa na mamlaka ya moja kwa moja ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato na kupanga mishahara na stahili za wafanyakazi hawa, kuajiri tasnia

hii ya maaskari wetu na kuhakikisha kwamba tuna ikama inayotosheleza mahitaji. (*Makofi*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kama ambavyo nilikuwa nimechangia kwenye mchango wangu wa maandishi kumekuwa na malalamiko sana kwa Watanzania wanaofanya kazi katika hoteli za kitalii ambao wengi wao vijana wamekuwa wakipata manyanyaso. Lakini pia wamekuwa wakikosa fursa ya kupata zile ajira za *star*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kujua Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi kwa sababu tatizo hili ni kubwa, imejipanga vipi kuhakikisha vijana wa Kitanzania wananufaika na ajira ambazo zinapatikana katika hoteli za kitalii? Malalamiko haya ni kwa pande zote mbili kati ya Tanzania Bara na Visiwani.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hili la ajira na utaratibu wote mzima alivyozungumzia Mheshimiwa Ester Bulaya, niseme kwamba, tunajipanga kwa maana ya kusema kwamba yale maeneo ambayo ni mtambuka, ambayo yanahusu Wizara mbili, tatu, nne, tano, tunao utaratibu wa kuweza kuzungumza na kupanga mikakati hii. Najua ana uchungu kuhusu mambo ya vijana, kwa hiyo, hilo tumelipokea na tutalifanyia kazi kuona vipi tunakuza ajira za vijana katika maeneo yetu.

**MWENYEKITI:** Vijana wa Tanzania wanaweza. Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchago wangu wa maandishi, niliuliza kuhusiana na Sera na mkakati wa utalii Dar es Salaam, hususani kuhusiana na pori la akiba la Pande ambalo liko kwenye Jimbo la Ubungo pamoja na Jimbo la Kawe linalogusa maeneo ya Msumi, Makabe, Kibesa, Mpigi Magoye kwa Jimbo la Ubungo na maeneo ya Mbompo, Mwabepande na mengineyo kwa upande wa Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, kwenye mikutano iliyopita ya Bunge, mwaka 2011, nilipendekeza kwa maana ya mkakati wa utalii na maliasili Dar es Salaam, pori hili liweze kugeuzwa kuwa kitovu cha utalii kama ilivyo Nairobi *National Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kauli ya Waziri kwa sababu kuachiwa muda mrefu kwa pori hili, kumeligeuza sasa kuwa pori la mateso, mauaji na tishio kwa usalama kwa wananchi wanaozunguka na matukio mengi sana yamejitokeza, matukio ya kwenye kesi ya Zombe, Dkt. Ulimboka. Hivi karibuni tena kuna mtu mwingine ameuawa kwenye pori lile na tishio la usalama sana kwenye maeneo yanayozunguka. Sasa naomba kauli ya Serikali ni lini Serikali italigeuza pori hili kutoka kuwa pori la mateso na mauaji na kuwa kivutio cha maliasili na utalii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mnyika kwa ajili ya mkakati wa

kuendeleza utalii katika Jiji letu la Dar es Salaam na kwamba pori hili la Pande, hatuwezi kabisa tukaliruhusu likaendelea kuwa pori la unyanyasaji na la mateso kwa mtu yeyote yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Wizara kwa kushirikiana na *TTB* kuratibu mkakati huu ambao wadau wote akiwepo Mheshimiwa Mnyika na Wabunge wa Dar es Salaam watashirikishwa ili tuhakikishe; moja, tunalipandisha hadhi hili pori ili liweze kusaidia utalii wa Dar es Salaam kama vile ambavyo tungependa wananchi wa Dar es Salaam na maeneo mengine waende Saadani. Lakini pili, tunaazimia vile vile kuongeza utalii wa Dar es Salaam kwa upande wa boti na mambo ya kale kama tulivyozungumza.

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Katika mchango wa Mheshimiwa Waziri katika kuwajibu Waheshimiwa Wabunge umesema kwamba, tayari kuna Tume ambayo imeundwa ambayo inatembelea katika nchi nzima kuweza kuratibu mipaka na kuweza kuelimisha wananchi katika maeneo hayo ya Hifadhi. Je, sasa Mheshimiwa Waziri, hiyo Tume iliyoundwa kuzungukia eneo hilo ni lini itafika Wilaya ya Kondoa kwenda kutatua mgogoro ambao uko unajiendeleza sana katika eneo la Mkongonero?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi pia nimechangia kwamba, Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Kondoa ni moja ya kivutio cha

watalii kama ilivyokuwa zamani, watalii wengi walikuwa wanaingia katika Wilaya ya Kondoa kwenda kuona kwenye michoro ile ya mapango ambayo sasa hivi imeshaanza kufutika. Je, ni lini Serikali itaweza kuitangaza Wilaya ya Kondoa ni moja ya kivutio ambacho kinaweza kuingizia rasilimali katika nchi yetu ya Tanzania?

**MWENYEKITI:** Swali linajieleza na jibu lake ni fupi tu. Karibu!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja ambazo ametoa Mheshimiwa Mbunge Bi. Moza nimwambie tu kwamba, hiyo Tume imekwishajipangia, ratiba sitoijua ni lini inakuja, lakini kweli Kondoa inakuja. Lakini kama unasema lazima ije mapema, basi nikuhakikishie tutakavyotoka nitatazama ratiba yao imekaa namna gani na tutatazama kama inaweza ikaja mara moja ikalitazama tatizo hilo ili kuona kwamba tunaweza tukapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la kuhusu kutangaza Kondoa, hiyo ni wajibu wetu kwa sababu mahali popote ambapo kuna vivutio na tukiweka mikakati ambayo ni mizuri, hatuna budi isipokuwa kutangaza ili kuweza kupata watalii wengi.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua kuhusu Sera za Uhaulishaji wa Misitu iliyoko katika ya Miji au makazi kwa kuwa katika Jimbo la Iringa Mjini kuna msitu wa

Kyesakilolo. Ule msitu kwa kweli sasa hivi ni kero na Halmashauri yetu imeshaleta barua muda mrefu sana kwamba ule msitu uhaulishwe, lakini hakuna majibu yoyote. Ningependa kujua kuhusu Sera za Uhaulishaji.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala ambalo ameliuliza Mheshimiwa Kabati, ni kwamba, yako maeneo ambayo yanaanguka moja kwa moja chini ya Wizara, sasa hivi tumefunua *TFS* ambayo ndiyo itakuwa inashughulikia masuala ya misitu, lakini pia iko misitu ambayo iko chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili suala niseme kwamba, itabidi tuzungumze na kumhakikishia Mheshimiwa Kabati, kama kweli itakuwa Wizara yangu inahusika ama itakuwa ni Halmashauri, lakini vyovyote itakavyokuwa tutazungumza kuhakikisha kwamba hili pori, mmoja atakuwa mmiliki kuhakikisha kwamba linakuwa salama kwa watu na hasa watu wa Iringa Mjini.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba, hizi Sera za hoteli hizi za mpito kwa maana ya kwamba hoteli ambazo zinakuwa zikimaliza malengo yake zinakabidhi umiliki kwenye hoteli zingine, zimekuwa zikiwapa shida sana wafanyakazi ambao ni wazawa wa Tanzania. Kwa mfano, iliyokuwa Sheraton na sasa hivi imekuwa Serena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni matatizo makubwa pale ambapo umiliki unapotaka kubadilisha

wafanyakazi wale ama walikuwa wako kwenye ajira ya mkataba ama sijui ni moja kwa moja maana mimi sielewi. Lakini wale wanakuja na wafanyakazi wao wakati wananchi wetu wa Tanzania wanapoteza ajira zao. Kwa hiyo, nilitaka kujua hii Sera inasema kuhusu hizi hoteli za mpito? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata ni kweli, wafanyakazi wengi sana wametuona sisi Wizarani na wameendelea kulalamikia hiki anachokisema cha kubadilika kwa wamiliki. Lakini Wizara inaangalia mambo mawili katika mchakato huu ambao umetokea kuwa kama tabia kwamba hoteli inakaa muda fulani, inanunuliwa. Kwa hiyo, tunachotaka kuhakikisha cha kwanza ni kodi zote za Serikali katika kubadilishana yale manunuzi, lazima ziwe zimelipwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tuna utaratibu ambao unamruhusu mnunuaji wa hoteli anunue pia na haki ya wale wafanyakazi wanaofanya kazi katika mmiliki wa awali na tutahakikisha kwamba tunaendelea kushirikiana na hizi taasisi, kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu, waajiriwa wetu wa ndani hawanyanyasiki.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu ambao naona umeleta tafrani kidogo, nimezungumzia sana kuhusu majangili pamoja na kwamba imeleta shida katika yule aliyeonekana ametajwa ni Mwenyekiti wa CCM na jana kwa bahati sielewi ni kitu

gani kilitokea, tulijaribu kuleta mabadiliko kabla Bunge halijaanza, bado nasisitiza kwamba mmoja wapo wa wale majangili ambaye nilimtaja wa Karatu anaitwa Lazaro na ukitaka ushahidi tutaleta na ni Mwenyekiti wa Kitongoji. Lakini swali langu ninalotaka kusema...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Msigwa nenda kwenye hoja.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ninayotaka kusema pamoja na kuwataja wote hao majangili, Wizara inasemaje pamoja na wengine wote tuliowataja, Wizara inasemaje kuhusu kukabiliana na ujangili huu ambao nimeutaja?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimjibu Mheshimiwa Msigwa. Msigwa *you know you are a friend of mine*, sasa unaposema Lazaro, Lazaro Nyalandu, Lazaro nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hata *Court of Law* watauliza, huwezi ukasema tu, lazima utataja fulani, fulani, fulani. Lakini hiyo tuiache, la msingi ni kwamba Wizara imejiandaa na Serikali imejiandaa. Hili ni jambo kubwa na ni jambo zito. Tunapambana na wale wenye macho, hawaambiwi ona, kazi zinafanyika na hii naisema *with passion* kwa sababu, Mheshimiwa Msigwa ni mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku nne kabla hatujaanza suala hili katika Bunge hili, tulikutana na Kamati, tulipokutana na Kamati, mazungumzo yaliyokuwa katika Kamati, halikuwa suala lingine, lilikuwa suala la ujangili, hii ni siku tatu, wale ambao ni Wabunge wamo ndani wanajua. Kwa hiyo, mkakati mzima tuliueleza katika kikao hicho, sasa sioni tatizo liko wapi Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Katika mchango wangu nimeongelea suala zima la umuhimu wa sekta ya misitu na nyuki, lakini katika muundo mpya, sekta hii au kitengo hiki muhimu sana ambacho kinatiliwa mkazo na watu wengi kimewekwa sasa chini ya Kurugenzi ya Sera na Mipango na chini ya Mkurugenzi Msaidizi wa kitengo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri au Naibu, haoni kwamba kitendo cha kuweka kitengo hiki muhimu sana katika kitengo cha Sera na Mipango ambacho kimsingi wahusika wana uweledi na ni wataalam sana wa misitu na nyuki kitapelekea kutokupata fedha au kutoonekana kabisa katika utekelezaji? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu tu Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba, hoja hii inayogusa Idara ndogo ya Nyuki imeficha *prominently* katika majadiliano na sisi tumesema tunalichukua, tuliangalie kimuundo ili tuhakikishe kwamba Idara ya Nyuki inapewa sehemu yake kutokana na umuhimu wake. *(Makofi)*

**MHE. MAHAMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Wilaya ya Mufindi kuna mgogoro mkubwa sana kati ya maliasili pamoja na wananchi na Vijiji, wananchi wanalalamika kwamba Serikali imechukua ardhi bila kufuata utaratibu. Lakini kuna ardhi ambayo haijaendelezwa na iko nyingine ambayo wananchi wameingia, wameanza kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba nisikie tamko la Serikali, kwa nini wasiiache ile ardhi ambayo haijaendelezwa kwa wananchi na ile ambayo wameshaiendeleza tayari wananchi, kwa nini wasiwaachie?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Mheshimiwa Mgimwa kwa kweli nimelisikia na tumekuwa tunalisikia na ndiyo maana nimesema na narudia pale pale, haki lazima itatendeka na nimesema si Wizara wala si Serikali itafanya kitu chochote ambacho kitakuwa ni kwa maudhi kwa wananchi ama kitakuwa ni bugudha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala kweli lipo, ile Tume ambayo tumeiweka, ambayo inahusu Wizara mbalimbali, Ardhi ikiwemo, Maliasili ikiwemo, Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwezo, TAMISEMI, wote tutafanya kazi hii, ni kiasi afanye subira tu, tutafanya kazi hii kwa shabaha ya kuhakikisha kwamba hii migogoro ya ardhi kati ya maliasili, wananchi na Vijiji inapata suluhu ambayo inakuwa ni ya kudumu.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilinukuu takwimu za mwaka 2009 ambazo nafikiri hazitofautiani sana na sasa hivi zinazoonesha kwamba, zaidi ya asilimia 65 ya aina ya utalii unafanyika kwa utaratibu wa *package arrangements* na hii inasababisha zaidi ya nusu ya fedha zibakie nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui Mheshimiwa Waziri anaweza akatuelezea ni mkakati gani ambao Serikali inao wa kuhakikisha kwamba unashajihisha wawekezaji wa ndani ili kupunguza wimbi kubwa la fedha za utalii kubakia nje?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara yetu inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa kwamba, ukweli ni kwamba fedha nyingi sana katika biashara hii ya utalii bado zinabaki nje kutokana na wawekezaji wakubwa kuwa wako nje. Hii ikiwa ni pamoja na *tour operators* wakubwa wanafanya *booking* moja kwa moja kutoka nje, fedha zinazoletwa nchini ni zile za *operations* tu na kulipa *Park fees* na *hotels* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mchakato ambao tulisema katika *speech* yetu tutaofanya, ni kuhakikisha kwamba, tunafanya mawili, moja tunaboresha na tunaimarisha wawekezaji wetu wa ndani, tunaweka sababu za makusudi za kuhakikisha kwamba *tour operators* wetu wana nguvu sio tu kwamba kuweza kuwa na wageni wao wenyewe,

lakini ikiwa ni pamoja na wao kwenda katika masoko kama soko la Afrika Mashariki. Jitihada hizi zitamlenga mwekezaji wa ndani na tutafanya kila linalowezekana kuwajengea uwezo.

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu nilitaka kujua pamoja na kwamba Waziri ametueleza kwamba, wameunda *something like* Tume kufuatilia wachimbaji wa dhahabu katika Mbunga ya Serengeti eneo la Kilimofedha, lakini nataka kujua tarehe 23 mwezi wa tatu mwaka huu, kuna Maafisa wa Polisi, *OCD* wa Mgumu, Afisa Usalama wa Taifa na dereva kwa kutumia gari la Polisi walikamatwa na wananchi wengine watano. Lakini cha ajabu wananchi watano ndiyo walishtakiwa, wakapelekwa Mahakamani, lakini hao Maafisa wa Polisi wenyewe hawakushtakiwa. Nataka kujua ni kwa nini?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri, kama ni la kwenu, kama ni la Uhamiaji semeni tu sio la kwenu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mashataka liko kwenye Idara ya Mahakama na Jeshi la Polisi, lakini nimjibu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuchimba madini katika Hifadhi ya Taifa, ni ku-*cross red line* katika uhifadhi. Wizara imejipanga ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wahusika ambao ni kweli walikamatwa, alikamatwa *OCD* na Afisa mwingine wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba walipokamatwa walifikishwa katika vyombo vya Sheria

na maamuzi sasa tumeyaachia vyombo vya Sheria juu ya mustakabadhi wa mambo yao. Lakini tunaendelea kusisitiza kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, jambo hili tutalitolea maamuzi makubwa na magumu katika kipindi kifupi ili tuweze kukomesha kabisa mtu yeyote ambaye hata anafikiria kichwani kwake kwamba anaweza aka- *cross,* akaenda kwenye hifadhi akachimba madini. Tutamkamata, tutawakamata wanaomsaidia, tutawakamata wanaoshirikiana naye, tuhakikishe kwamba tumetoa somo kubwa kwa watu wanaotuhujumu.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru Mheshimiwa Waziri, nakushukru sana na kwa wale ambao hawajakamatwa habari ndiyo hiyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2) sasa tunaingia kwenye *guillotine*.

**Fungu 69- Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … Sh.1,884,158,200/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning…* Sh. 1,673,528,240/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit*… … … … … … …Sh. 394,141,600/=
Kif. 1005 - *Internal Audit*… ... … … Sh. 597,313,800/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*… … … … … … … Sh. 629,925,960/=
Kif. 1007 - *Legal Unit*… … … … … Sh. 308,288,100/=
Kif 1008 - *Management Information System*… … … … … … … Sh. 620,045,800/=
Kif 2001 - *Wildlife*… … … …. Sh. 19,445,772,454/=
Kif. 3001 - *Forestry and Beekeeping* Sh.16,379,659,487/=
Kif. 4001 - *Tourism*… … … … … … Sh.12,477,646,240/=
Kif. 4002 - *Antiquities Unit*… … …Sh.5,916,148,255/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 69- Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* Sh. 127,000,000/=
Kif. 2001 - *Wildlife* … … … … … … Sh. 3,902, 000,000/=
Kif. 3001 - *Forestry and Beekeeping*...Sh. 8,683,682,000/=
Kif. 4001 - *Tourism* … … … ... ... ..Sh. 0/=
Kif. 4002 - *Antiquities Unit* … Sh. 12, 712, 682,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MALISILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha makadirio ya matumzi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2012/2013 kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Nachukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako kwa kazi nzuri mlioifanya na tunategemea mafanikio makubwa sana kwenye uendeshaji wa Wizara hii. Nina tangazo moja tu.

Naomba kuwatangazia kuwa Mheshimiwa Vita Kawawa ambaye ni Katibu Mkuu wa *APNAC*, anaomba kuwatangazia Wabunge wote wanachama hai wa *APNAC* wanaalikwa katika semina ya *social accountability* itakayofanyika kesho jumapili tarehe 12/08/2012 saa nne na nusu katika Ukumbi wa *New* Dodoma *Hotel*.

Vile vile kwanza nataka kuchukua nafasi hii kuwapongeza wale wote waliofanya mafunzo wiki ya unyonyeshaji, imeonesha namna gani akinababa wanatakiwa kuwasaidia akinamama katika kuwapa lishe bora ili waweze kunyonyesha vizuri watoto wao. Lakini kuna angalizo limetolewa, akinababa msile vyakula ambavyo si vyenu, mnatakiwa kuwaachia watoto wadogo waweze kunyonya. *(Kicheko/Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo

wako kupitia Kanuni ya 68(7) kwamba: “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika aweze kutoa ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa wakati Waziri Mheshimiwa Kagasheki anawasilisha mchanganuo wa bajeti na ni tabia imezuka hasa inatumiwa na Mheshimiwa Lukuvi vile vile ambayo naihesabu mimi kama ni *personal assassination,* kwa sababu mara nyingi wakizungumza, wanahusisha kujibu hoja na Uchungaji, sasa nilitaka nipate Mwongozo wako...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaongea kwa sauti)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

**MWENYEKITI:** Wewe zungumza na Kiti.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate Mwongozo wako kwa sababu mimi hapa nimesimama hapa kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani na siko mimi hapa kumpeti Waziri, *I am doing my job*, inawezekana katika uwasilishaji au uendeshaji kuna *mistake* ambazo zinaweza zikawa zimetokea ambazo kwa mujibu wa Sheria hata Chama chenyewe cha Mapinduzi huwa kinaleta *addendum* ambayo na mimi nasema nilileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza ni kwamba, ni halali kuni- *assassinate personally* na kuniambia mimi ni muongo wakati yeye mwenyewe hata ukiangalia hata kwenye picha, anam- *shake* mkono Balozi wa Uingereza. Picha zipo zimeonesha, magazeti yameonesha. Amesimama hadharani na kuniambia mimi mwongo na kuhusisha na Uchungaji ambao uchungaji sipewi na mtu yeyote humu ndani, sio suala la kisiasa, ni suala langu la nje, nataka nipate Mwongozo wako.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana. Waheshimiwa *order*. Nakushukuru sana Mheshimiwa Msigwa. Kanuni hiyo hiyo ukimalizia mstari wa mwisho, tatu inasema taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa. Mwongozo wako nitautoa baadaye. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru wote kwa michango mizuri na ambayo itajenga Taifa letu. Sina matangazo mengine, naomba kuliahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.05 mchana Bunge lilihairishwa Mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 13 Agosti, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*